# USAWIRI WA MOTIFU ZA KIMAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE: UHAKIKI WA KIEKOLOJIA

**MARY KANYUA NJERU**

**Tasnifu hii Imewasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**SEPTEMBA 2022**

# UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo la Mwanafunzi**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada au stashahasda katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi……………………………………Tarehe…01/09/2022…

Mary Kanyua Njeru
AD12/38559/18

**Idhini ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi……………………………………Tarehe 01/09/2022

Prof. John M. Kobia
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi……………………………………Tarehe…1/9/2022……

Dkt. Dorcas M. Musyimi
Chuo Kikuu cha Chuka

## HATILINZI

©2022

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuchapisha, kuhifadhi kwa mfumo wowote au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa, Mzee Agostino Njeru na Mama Agera Cianjoka Njeru kwa mapenzi yao ya dhati na kujitoa mhanga kunielimisha licha ya changamoto nyingi maishani. Kwa mume wangu mpendwa Kanali Micheni Dennis Kinoti na watoto wangu Shantelle Makena na Shanell Lulu; Nyinyi ni mihimili muhimu katika maisha yangu. Kwa heshima na kumbukumbu za marehemu ndugu zangu; Kaka John Ndeke Njeru na dada Fridah Karegi Njeru, wandani na washauri wangu tangu utotoni. Natamani sana kuwa mngekuwepo kushuhudia mafanikio yangu! Mungu azilaze roho zenu pema peponi.

## SHUKURANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema, busara, maarifa na nguvu za kuendeleza kazi hii tangu mwanzo hadi tamati. Kukamilika kwa kazi hii ni ushahidi tosha kuwa hakika yote yanawezekana kwa jitihada na imani. Shukurani za dhati na maalumu ni kwa wasimamizi wangu Prof. John M. Kobia na Dkt. Dorcas M. Musyimi kwa kunipa mwongozo wa kitaaluma, kunishauri, kunikosoa na kunielekeza katika hatua zote za uandishi wa tasnifu hii. Mchango wenu hauwezi kupuuzwa kamwe. Namshukuru kwa njia ya kipekee Mkuu wa Idara ya Fani katika Chuo Kikuu cha Chuka Dkt. Christine Atieno kwa kunishauri na kunitia shime kila nilipokosa matumaini nilipokuwa nikifanya utafiti huu.

Nawashukuru pia wahadhiri wenzangu katika Chuo Kikuu cha Chuka, hasa Dkt. Allan Mugambi na Dkt. Onesmus Ntiba kwa kunishauri na kunihimiza kuukamilisha utafiti huu. Namshukuru Bw. Enock Matundura kwa mchango wake hasa kunifaa kwa vitabu vya marejeleo na makala mengine muhimu niliyohitaji katika kipindi cha utafiti wangu. Wazazi wangu wapendwa Mzee Agostino Njeru na Agera Njeru, nawashukuru kwa kunilea na kujitoa mhanga kunielimisha hadi chuo kikuu licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi maishani. Siwezi kamwe kuwasahau ndugu zangu Albert Murithi na Margret Kabunge kwa kufuatilia kila hatua niliyopiga katika utafiti huu. Kwa dadangu mpendwa Dorothy Kagendo, Mola aendelee kukubariki kwa kusimama nami katika maombi, kunishauri, kunitia shime na muhimu zaidi kuwashughulikia wanangu kila niliposafiri kufanya utafiti wangu.

Mume wangu mpendwa Kanali Micheni Dennis Kinoti anastahiki shukurani za pekee kwa kunifadhili kwa hali na mali licha ya majukumu mengi yaliyomkabili. Aidha, uchochezi wake chanya ulinipa ari ya kuendelea na utafiti huu. Ningependa pia kuwashukuru wanangu Shantelle Makena na Shanell Lulu kwa kunipa wakati mtulivu na kunitia shime kila nilipokosa matumaini. Kwa wazamifu wenzangu; Bw. Reuben Mwilaria na Bi. Faith Muthoni, mchango wenu katika kazi hii hauwezi kupuuzwa. Mwisho, ningependa kutoa shukrani za dhati kwa wote walionifaa kwa namna moja au nyingine katika masomo na utafiti huu. Nyote nawaombea baraka za Mwenyezi Mungu.

## IKISIRI

Suala la mabadiliko ya tabianchi limeibua mijadala katika viwango vya kitaifa na kimataifa. Kwa msingi huu, kazi mbalimbali za kifasihi zimebuniwa kwa kuangazia uharibifu wa mazingira asilia, athari zake na mwito wa kuhifadhi mazingira. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza motifu za kimazingira zinazojitokeza katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Msisitizo ulikuwa kuangazia jinsi wasanii wa matini hizi wamesawiri uharibifu wa mazingira, kuonyesha matatizo yanayotokana na uharibifu huo pamoja na athari zake. Hii ni kwa sababu fasihi huwasilisha hali, maingiliano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira. Hivyo, ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayokumba jamii yoyote ile. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza jinsi motifu za kimazingira zilivyosawiriwa katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege, kujadili jinsi mtindo ulivyotumika kusawiri motifu za kimazingira katika tamthilia teule na hatimaye kutathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia iliyoasisiwa na Glotferty (1996). Nadharia hii hujikita katika uchambuzi wa kazi za kifasihi kwa kuonyesha uhusiano na utegemeano baina ya binadamu na mazingira. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ambapo uteuzi wa sampuli wa kimakusudi ulitumiwa kuteua matini teule. Data ya utafiti ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa matini teule, ikapangwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti na kuchanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya uhakiki wa kiekolojia. Baadaye, data ilifasiriwa kwa kutumia mbinu elezi. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa tamthilia teule za Kiswahili zilizochunguzwa zimeangazia masuala mbalimbali ya kimazingira pakiwemo chanzo cha uharibifu wa mazingira, athari za uharibifu huo pamoja na kubainisha njia ambazo zinaweza kutumika katika uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu unatarajiwa kuwa na manufaa kwa wasomi na wahakiki wa fasihi kwa kuangazia suala la motifu za kimazingira kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia. Vilevile, umetoa mchango katika uwanja wa fasihi mazingira kwa kuongezea suala la motifu za kimazingira. Isitoshe, utafiti huu ni muhimu kwa washikadau wote wa masuala ya kimazingira Barani Afrika na ulimwengu kwa jumla.

## ABSTRACT

The issue of climate change has recently elicited intense debate in both national and international forums. In this regard, many current literary works are focusing on environmental degradation, its effect, and the call for environmental conservation. This study investigated how environmental motifs are portrayed in the selected Kiswahili plays by Said Ahmed Mohamed and Timothy Arege. Literature is an important tool to educate and enlighten the wider public about their problems. Based on this, the emphasis was put on how Said Ahmed Mohamed and Timothy Arege in their selected Kiswahili plays focused on the environmental degradation, its effects and ways of conserving the environment. The specific objectives for the study were; to investigate how the environmental motifs have been portrayed in the selected Kiswahili plays, discuss how the stylistic devices have been used to portray environmental motifs and to evaluate the place of environmental motifs in environmental conservation as portrayed by writers of selected Kiswahili plays. The study was guided by Ecocriticism theory that was founded by Glotferty (1996), which analysis the literary works by examining the relationship and the interdependence between human beings and the physical environment. The research was carried out in the library where the selected Kiswahili plays were read. The researcher purposively selected two plays by Said Ahmed Mohamed and two plays by Timothy Arege for the study. Data was collected through close-textual reading of the selected texts focusing on different environmental motifs as portrayed by writers of the selected texts. Data analysis was done in descriptive prose based on the tenets of ecocriticism theory and categorized in reference to the three objectives guiding the study. The research findings indicated that the selected Kiswahili plays that were analyzed focused on various environmental issues such as environmental degradation and its impacts as well as indicating ways in which the environment can be conserved. This study is expected to be useful to literature scholars and critics by bringing to light the issue of environmental motifs in the context of ecocriticism theory. It also adds to the existing knowledge on environmental literature as well as benefiting environmental stakeholders and environmentalists in Africa and the world at large.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** ........ **ii**

**HATILINZI** ........ **iii**

**TABARUKU** ........ **iv**

**SHUKURANI** ........ **v**

**IKISIRI** ........ **vi**

**ABSTRACT** ........ **vii**

**YALIYOMO** ........ **viii**

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ **xiii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Usuli wa Mada ........ 1

1.2 Suala la Utafiti ........ 4

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 5

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 5

1.6 Upeo wa Utafiti ........ 6

1.7 Maelezo ya Istilahi ........ 6

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI** ........ **7**

2.1 Utangulizi ........ 7

2.2 Uharibifu wa Mazingira na Athari zake ........ 8

2.3 Uhifadhi wa Mazingira ........ 9

2.4 Fasihi Mazingira katika Fasihi ya Ulimwengu ........ 11

2.5 Fasihi Mazingira katika Fasihi ya Kiafrika ........ 15

2.6 Fasihi Mazingira katika Fasihi ya Kiswahili ........ 16

2.7 Dhana ya Motifu katika Fasihi ........ 18

2.8 Motifu za Kimazingira katika Fasihi ........ 19

2.9 Yaliyoandikwa kuhusu Tamthilia Teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege ........ 20

2.10 Muhtasari wa Tamthilia Teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege ........ 22

2.11 Misingi ya Kinadharia ........ 23

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ... 28**
3.1 Utangulizi ... 28
3.2 Eneo la Utafiti ... 28
3.3 Uteuzi wa Sampuli ... 29
3.4 Ukusanyaji wa Data ... 29
3.5 Uchanganuzi wa Data ... 29
3.6 Uwasilishaji wa Data ... 30
3.7 Maadili ya Utafiti ... 30

**SURA YA NNE: USAWIRI WA MOTIFU ZA KIMAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE ... 31**
4.1 Utangulizi ... 31
4.2 Motifu ya Maji ... 31
4.2.1 Umuhimu wa Maji ... 32
4.2.2 Chanzo cha Uhaba wa Maji ... 35
4.2.2.1 Uongozi Mbaya ... 36
4.2.2.2 Ukataji wa Miti ... 37
4.2.2.3 Ubadilishaji wa Mikondo ya Maji ... 40
4.2.3 Athari za Uhaba wa Maji ... 42
4.2.3.1 Milipuko ya Magonjwa ... 42
4.2.3.2 Kuathirika kwa Elimu ... 43
4.2.3.3 Biashara ya kuuza Maji ... 45
4.2.3.4 Kupungua kwa Viwango vya Usafi ... 46
4.2.3.5 Athari za Kiuchumi ... 47
4.2.3.6 Kuzuka kwa Mizozo ... 48
4.3 Motifu ya Magonjwa ... 50
4.3.1 Kemikali kutoka kwenye viwanda ... 50
4.3.2 Uchafu ... 52
4.3.3 Wasiwasi na Hofu ... 53
4.4 Motifu ya Ukame ... 56
4.4.1 Chanzo cha Ukame ... 56
4.4.1.1 Mabadiliko ya Tabianchi ... 56
4.4.1.2 Ongezeko la Joto Duniani ... 59

4.4.1.3 Kuasi Ujadi ........................................................................61
4.4.1.4 Ukataji wa Miti ........................................................................64
4.4.1.5 Tamaa ya Viongozi ........................................................................66
4.4.1.6 Unyakuzi wa ardhi ........................................................................68
4.4.2 Athari za Ukame ........................................................................70
4.4.2.1 Kukauka kwa Mimea ........................................................................70
4.4.2.2 Uhaba wa Chakula ........................................................................71
4.4.2.3 Umaskini ........................................................................72
4.4.2.4 Kudidimia kwa Maliasili ........................................................................74
4.4.2.5 Kuathirika kwa Masomo ........................................................................74
4.5 Motifu ya Njaa ........................................................................75
4.6 Motifu ya Kifo ........................................................................80
4.6.1 Ukosefu wa Chakula ........................................................................81
4.6.2 Kula Chakula Kibovu ........................................................................82
4.6.3 Kiangazi ........................................................................83
4.6.4 Kemikali ........................................................................84
4.7 Hitimisho ........................................................................86

**SURA YA TANO: MTINDO KATIKA USAWIRI WA MOTIFU ZA KIMAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE ........................................................................86**
5.1 Utangulizi ........................................................................86
5.2 Jazanda ........................................................................87
5.2.1 Jazanda ya Mpya ........................................................................87
5.2.2 Jazanda ya Janga la Werevu ........................................................................88
5.2.3 Jazanda ya Unajisi ........................................................................90
5.2.4 Jazanda ya Jipu ........................................................................92
5.2.5 Jazanda ya Ugonjwa wa Kristy ........................................................................93
5.2.6 Jazanda ya Majira ya Utasa ........................................................................95
5.2.7 Jazanda ya Ndoto ya Kato ........................................................................96
5.3 Kinaya ........................................................................97
5.4 Taswira ........................................................................99
5.5 Majazi ........................................................................101
5.6 Nyimbo ........................................................................106

5.7 Kejeli ........ 108
5.8 Ushairi ........ 110
5.9 Chuku ........ 111
5.10 Tashbihi ........ 113
5.11 Sitiari ........ 115
5.12 Mbinu Rejeshi ........ 117
5.13 Hitimisho ........ 118

**SURA YA SITA: MOTIFU ZA KIMAZINGIRA NA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE ........ 119**

6.1 Utangulizi ........ 119
6.2 Motifu ya Safari ........ 119
6.2.1 Safari ya Siki ........ 120
6.2.2 Safari ya Mpya ........ 121
6.2.3 Safari ya Wawakilishi wa Kijiji ........ 123
6.3 Motifu ya Ujadi ........ 123
6.3.1 Itikadi na Miiko ........ 124
6.3.2 Matambiko ........ 125
6.4 Motifu ya Elimu ........ 128
6.4.1 Somo la Mazingira katika Mitaala ya Elimu ........ 128
6.4.2 Elimu kupitia Vyombo vya Habari ........ 130
6.4.3 Elimu kwa Umma ........ 134
6.5 Motifu ya Umoja ........ 135
6.5.1 Kufanya Maandamano ........ 135
6.5.2 Uundaji wa Sheria za Mazingira ........ 138
6.5.3 Mijadala kuhusu Mazingira ........ 140
6.5.4 Kufufua Misitu ........ 142
6.6 Motifu ya Uzalendo ........ 144
6.6.1 Busara na Kristy ........ 144
6.6.2 Mpya na Bi Subira ........ 145
6.6.3 Lulu ........ 147
6.7 Motifu ya Mapinduzi ........ 149
6.8 Hitimisho ........ 153

**SURA YA SABA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........... 153**
7.1 Muhtasari .......... 153
7.2 Hitimisho .......... 154
7.3 Mapendekezo ya Utafiti Kwa Jumla .......... 158
7.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye .......... 159

**MAREJELEO .......... 160**
**VIAMBATISHO .......... 171**
Kiambatisho I: Kibali cha Utafiti .......... 171
Kiambatisho II: Idhini ya Utafiti .......... 172

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ASLE:** | Associaciation for the Study of Literature and Environment |
| **NACOSTI:** | National Commission for Science, Technology and Innovation. |
| **NEMA:** | National Environment Management Authority. |
| **UN:** | United Nations |
| **UNCCC:** | United Nation Climate Change Confererence. |
| **UNDP:** | United Nations Development Programme. |
| **UNEP:** | United Nations Environment Programme. |
| **UNFCCC:** | United Nations Framework Convention on Climate Change. |
| **UNICEF:** | United Nation Children Fund. |
| **WHO:** | World Health Organization. |

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzingira kiumbe katika maisha yake. Yanaweza kuwa ya asili kama vile misitu, milima, maziwa, mabonde, mito, na bahari. Vilevile, yanaweza kutokana na uvumbuzi wa binadamu kama vile majengo na viwanda (Sera ya Kitaifa ya Mazingira, 2012). Katika mazingira yoyote yale, kila kiumbe ana haki ya kuwa na mazingira yanayoboresha afya njema. Isitoshe, binadamu kote ulimwenguni hutegemea kwa namna moja au nyingine bidhaa na huduma kutokana na mazingira.

Mazingira ni muhimu katika uundaji wa mandhari ya kifasihi. Hii ni kwa sababu huipa kazi ya sanaa usanii na ujumi wake. Kulingana na Buell (2005), sitiari nyingi za kifasihi huzalika kutokana na mazingira ya msanii. Mawazo ya Buell (keshatajwa) yanashabihiana na ya Sangili (2015) anayetambua kuwa baadhi ya misamiati katika kazi za sanaa hasa fasihi hutokana na miti, wanyama, wadudu na mito. Kwa hivyo, ari ya kuthamini mazingira kwa wanajamii inaweza kukuzwa kupitia kazi za fasihi zinazohusu mazingira.

Licha ya kuwa mazingira asilia ni sehemu muhimu katika maisha ya wanadamu pamoja na viumbe wengine duniani, mwanadamu ameyaweka katika hali ya hatari hasa kupitia ongezeko la viwanda na uvumbuzi katika nyanja za kiteknolojia. Shughuli za binadamu kama vile ukataji wa miti, uchafuzi wa mazingira baharini na nchi kavu na uchafuzi wa hewa, ni baadhi ya vizingiti vinavyotishia kuangamiza mazingira asilia duniani (UN, 2011). Aidha, tangu ukombozi katika nchi nyingi hasa za Afrika Mashariki, juhudi nyingi za kimaendeleo zimechangia pakubwa katika uharibifu wa mazingira. Hii imetokana na njia mbovu za ukulima, ukataji ovyo wa miti, kuwa na idadi kubwa ya mifugo na utupaji ovyo wa taka (DeMott, 2018).

Athari za uharibifu wa mazingira kama vile vifo, milipuko ya magonjwa, uhaba wa maji, ukame pamoja na mabadiliko ya tabianchi zimekuwa dhahiri katika jamii na kusababisha dhiki kuu katika mataifa mengi duniani (Maathai, 2009). Aidha, masuala ya kimazingira yameibua hisia na mijadala ya kitaifa na kimataifa miongoni mwa

wanasayansi, wanamisitu, utawala pamoja na wanaharakati wengine wa kimazingira. Ili kukabiliana na athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira kama vile ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi, vyombo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa vinabuni mbinu na sera za uhifadhi wa mazingira. Miongoni mwa washikadau wakuu katika harakati hizo ni Umoja wa Mataifa chini ya UNEP na UNFCCC (Nabeta, 2011). Katika kiwango cha kimataifa, mwaka wa 2010 kulikuwa na mkutano wa *United Nation Climate Change Conference* (UNCCC) uliofanyika nchini Mexico. Katika mkutano huo, suala la ongezeko la joto duniani na jinsi ya kukabili athari zake lilijadiliwa. Mwaka wa 2009, kulikuwa na mkutano wa *Copenhagen Climate Change Conference* ulioangazia miaka sita ya mabadiliko ya hali ya anga na jinsi yalivyosababisha mafuriko na athari zake. Aidha, walitambua kuwa uharibifu wa mazingira ni mojawapo ya changamoto zinazokumba dunia ya sasa hivi.

Juhudi za kuangazia masuala ya mazingira kwa muda mrefu zimekuwa zinahusisha wanaharakati wa kimazingira, wanasayansi mazingira, wanamisitu pamoja na serikali kuu za mataifa mbalimbali duniani (Garrard, 2004). Hii ina maana kwamba hoja na ushahidi wa sayansi asilia kuhusu uharibifu wa mazingira na athari zake vimepewa nafasi kubwa kuliko hoja za sayansi za jamii kama Historia, Anthropolojia, Lugha na Fasihi. Akieleza kuhusu asili ya fasihi mazingira, DeMott (2018) anatambua kuwa kabla ya uwanja huu kuibuka, matatizo ya kimazingira yalikuwa yakishughulikiwa na wanasayansi. Hivyo, uwanja huu uliibuka kama juhudu za kuhusisha sanaa mbalimbali katika uhifadhi wa mazingira.

Kwa mujibu wa Rueckert (1978), uwanja wa fasihi mazingira unachukua mwelekeo wa kimwingilianotaaluma kwa kuhusisha falsafa kimazingira, usomi wa mandhari, mapisi kimazingira, nyanda na sehemu za dunia na kuoanisha na sanaa mbalimbali. Aidha, Rigby (2002) anafafanua fasihi mazingira kwa kusema kuwa, uwanja huu huwa na kusudi la kuleta mageuzi ya kijamii na kimazingira kupitia fasihi. Kwa hivyo, kando na mazingira asilia, huhusisha mandhari yaliyojengwa na binadamu pamoja na mahusiano yake na utamaduni. Kwa mujibu wa Sabula na Sangili (2019), fasihi mazingira ni uwanja ulioendelezwa na Glotfelty na Fromm (1996) pamoja na Buell (1996) miaka ya 1990 walipozindua tena uwanja wa fasihi mazingira katika fasihi za lugha ya Kiingereza huko Marekani. Vilevile, wanatambua kuwa uwanja wa fasihi mazingira

unachukua mkabala wa kimazingira katika masuala ya kifasihi hasa kwa kuchanganua maudhui ya kiekolojia na jinsi wahusika wanavyohusiana na ekolojia. Kinachodhihirika ni kwamba fasihi mazingira ni usomaji wa matini za kifasihi unaoegemea kwenye masuala ya kimazingira.

Uhifadhi wa mazingira ni suala linalohitaji kila mtu kujukumika. Kwa sababu hii, wanafasihi wamebuni uwanja wa fasihi mazingira ili kujihusisha katika harakati hizi. Kutokana na msingi huu, Glotfelty na Fromm (1996) wanadai kuwa vita dhidi ya uharibifu wa mazingira vinafaa kuwajumuisha hata wanafasihi. Aidha, Ojomo (2011) anaeleza kuwa njia mojawapo ya kutatua suala la uharibifu wa mazingira ni kuhusisha fasihi ambayo inamulika maovu yanayofanyiwa mazingira. Maoni ya Bulaya na Mhango (2020) yanaafikiana na madai hayo kwa kusema kuwa, matatizo yanayotokana na uharibifu wa mazingira yanaweza kudhibitiwa kwa kutumia mafunzo na elimu ipatikanayo katika fasihi simulizi na andishi. Kwa hivyo, pana umuhimu wa watunzi na wasomi wa kazi za kifasihi kushika usukani ili kuhusika na kuchangia katika utatuaji wa matatizo ya kimazingira.

Fasihi ya Kiswahili ni mojawapo ya fasihi ambazo zimehusika katika maudhui na mitindo ya utunzi inayomulika jamii ya sasa (Sabula na Sangili, 2019). Miongoni mwa maudhui ambayo yanashughulikiwa na kupewa kipaumbele ni suala la mazingira. Maelezo haya yanaafikiana na yale ya Wesonga na wenziwe (2020) wanaodai kuwa, waandishi wa fasihi wamejihusisha katika kuangazia matatizo ya kimazingira ili kuwasilisha uhalisia wa jamii. Jinsi mazingira yanavyobadilika ndivyo fasihi inavyoendelea kubadilika kimaudhui huku ikichukua dhima mpya ya kusawiri uharibifu wa mazingira, athari zake na njia za kuhifadhi mazingira ili kuepuka majanga. Hii inatokana na sababu kuwa fasihi ni nyenzo mojawapo ambayo inaweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii yoyote ile. Aidha, fasihi inaakisi kikamilifu masuala ya jamii ilimoibuka. Kwa hivyo, inaweza kutumika katika kusuluhisha matatizo ya kijamii. Mambo haya ndiyo yalichochea utafiti huu kwa kuchunguza jinsi ambavyo masuala ya kimazingira yamejitokeza katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Katika uchunguzi wa kazi za kifasihi, mtindo ni elementi muhimu ambayo hurejelea jinsi ambavyo mtunzi wa kazi za kisanaa hutumia lugha kujieleza, kukuza na kuwasilisha maudhui kwa wasomaji wa kazi hizo (Wafula, 1999). Maelezo haya yanaafikiana na yale ya Wamitila (2003) anayesema kwamba, motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi ni miongoni mwa elementi muhimu za kimtindo ambazo mchanganuzi wa matini za kifasihi anapaswa kuchunguza. Hivyo, matumizi ya motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege ndiyo yanayojenga msingi wa utafiti huu, ili kuchunguza jinsi ambavyo motifu hizo zimekuza suala la mazingira kama vile uharibifu wa mazingira, athari za uharibifu huo na njia za kuhifadhi mazingira.

Dhana ya motifu hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya kifasihi (Wamitila, 2003). Huweza pia kutumiwa kuelezea elementi fulani ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi fulani. Wamitila (keshatajwa) anatoa mfano wa motifu ya kifasihi `wawapi? ` katika utungo wa *Al-Inkishafi* wa Sayyid Nassir. Motifu hii ya `wawapi`inakuwa muhimu katika utungo huo kwa kuwa inakuza na kuendeleza maudhui muhimu ya kutokuepukika kwa kifo pamoja na mpito wa maisha. Kutokana na maelezo ya Wamitila (keshatajwa), ni dhahiri kuwa dhana ya motifu inaweza kutumiwa kama msingi wa kuhakikia kazi za kifasihi. Kwa msingi huu, utafiti huu ulijikita katika usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege ili kuchunguza jinsi motifu mbalimbali zilivyotumika kuendeleza masuala ya kimazingira..

### 1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege pamoja na kufafanua muktadha halisi ambao umetumiwa na watunzi hawa kama malighafi ya kazi zao. Motifu ni kati ya vipengele muhimu katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, hususan katika uchambuzi wa vipengele vinavyokuza maudhui ya kazi hizo. Utafiti huu umechochewa na ufahamu kwamba, matumizi ya motifu katika kazi za kifasihi humwezesha msomaji kung`amua mawazo makuu na dhamira ambazo msanii anajaribu kuzionyesha ili aweze kuitafsiri kazi ya sanaa kwa ufasaha zaidi. Kutokana na athari za uharibifu wa mazingira zilizo dhahiri katika jamii, waandishi wa tamthilia teule wamejumuisha matumizi ya motifu

za kimazingira katika kazi zao kwa lengo la kuliweka wazi suala hili. Kwa msingi huu, mtafiti alichunguza jinsi ambavyo waandishi wa tamthilia teule wamesawiri masuala ya kimazingira kiubunifu kupitia matumizi ya motifu.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

i. Kuchunguza jinsi motifu za kimazingira zinavyosawiriwa katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.
ii. Kujadili jinsi mtindo ulivyotumika kusawiri motifu za kimazingira katika tamthilia teule.
iii. Kutathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Motifu za kimazingira zimesawiriwa vipi katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege?
ii. Mtindo umetumika vipi katika kusawiri motifu za kimazingira kwa mujibu wa tamthilia teule?
iii. Motifu za kimazingira zina mchango gani katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una manufaa kwa wahakiki na wasomi wa fasihi kwa kuwa umepanua uelewa wa suala la motifu za kimazingira kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia. Vilevile, umetoa mchango katika uwanja wa fasihi mazingira kwa kuongezea suala la motifu za kimazingira. Hivyo, utachochea tafiti za baadaye katika fasihi mazingira kwa kuzingatia mkabala mwingine tofauti. Zaidi ya hayo, una manufaa kwa msomaji kwa kuwa mtafiti alimfafanulia muktadha halisi ambao umetumiwa na watunzi kuzitungia kazi zao.

Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yana manufaa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili; kwa kuwa mtafiti alichambua matini teule kwa kuangazia jinsi ambavyo wasanii wa

matini hizo wamesawiri motifu za kimazingira. Hivyo, ulinganishaji wa matini hizo ulimwezesha mhakiki kuweka kazi ya mwandishi mmoja katika muktadha wa maandishi mengine. Kwa kufanya hivyo, mtafiti alitoa kauli zilizojengwa katika misingi imara kuhusiana na masuala ya kimazingira.

Utafiti huu pia ni muhimu kwa watafiti na wasomi wa Kiswahili. Sababu ni kwamba, Kiswahili kinazidi kupewa umuhimu katika taasisi tofauti kote ulimwenguni, ambapo fasihi ya Kiswahili inaweza kutumiwa kutatua matatizo ya kijamii kama zilivyo sayansi nyinginezo za kijamii. Vilevile, utafiti huu utatumiwa kutathmini upya hatua za kuchukuliwa ili kujenga mustakabali endelevu wa mazingira. Isitoshe, matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa washikadau wote wa masuala ya kimazingira Barani Afrika na ulimwengu kwa jumla.

### 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia. Uhakiki wa tamthilia teule uliangazia jinsi watunzi wa tamthilia teule wamesawiri motifu za kimazingira na jinsi walivyotumia mtindo kusawiri motifu za kimazingira. Aidha, mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira ulichunguzwa. Matini zilizohakikiwa katika utafiti huu ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009), *Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). Tamthilia hizi ziliteuliwa kwa kuwa zinahusu masuala ya kimazingira kama maudhui yake makuu, hivyo kuafiki mada ya utafiti huu. Isitoshe, utafiti ulijikita katika nadharia ya uhakiki wa kiekolojia iliyoasisiwa na Glotferty (1996) ili kuafiki madhumuni ya utafiti huu.

### 1.7 Maelezo ya Istilahi

**Ekolojia** : Ni mimea, viumbehai na mazingira wanamoishi.

| | | |
|---|---|---|
| **Fasihi mazingira** | **:** | Ni uwanja mpya unaochipuka katika karne ya ishirini kama juhudi za sanaa za kuunga mkono utetezi wa uhifadhi wa mazingira. |
| **Uhakiki wa kiekolojia** | **:** | Ni uchambuzi wa kazi za kifasihi kwa kujikita katika vipengele vya uhusiano na utegemeano baina ya binadamu na mazingira. |
| **Maliasili** | **:** | Madini, misitu au maji yanayotokana na maumbile, ambayo hupatikana katika mazingira. |
| **Mazingira** | **:** | Mazingira yanahusisha vitu vyote vinavyosaidia kuendelea kuwepo kwa maisha ya wanadamu na viumbe wengine. |
| **Mazingira asilia** | **:** | Ni viumbe hai na visivyo hai ambavyo vimetokea kiasili duniani. |
| **Motifu za kimazingira** | **:** | Ni mawazo au miundo katika kazi za fasihi yanayojirudiarudia, ambayo hutumiwa na wasanii katika kazi zao ili kufafanua masuala ya kimazingira. |
| **Ufeministi Kiekolojia** | **:** | Ni mtazamo wa uhakiki ambao huangalia jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika harakati za utetezi wa mazingira au uharibifu wake. |

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilijumuisha uhakiki wa maandishi ambayo yanahusiana na mada ya utafiti. Katika kufanya hivyo, mtafiti alipitia maandishi kuhusu masuala ya kimazingira, dhana ya motifu na fasihi mazingira kwa jumla. Lengo lilikuwa kupata maandishi ambayo

yalibainisha na kuweka wazi pengo la utafiti huu. Hivyo, masuala yafuatayo yaliangaziwa: suala la uharibifu wa mazingira na athari zake, uhifadhi wa mazingira, fasihi mazingira katika fasihi ya ulimwengu, fasihi mazingira katika fasihi ya Kiafrika, fasihi mazingira katika fasihi ya Kiswahili, dhana ya motifu katika fasihi, motifu za kimazingira katika fasihi, yaliyoandikwa kuhusu tamthilia teule na muhtasari wa tamthilia teule. Hatimaye, misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu ilibainishwa ili kutolea utafiti mwelekeo wa kitaaluma.

## 2.2 Uharibifu wa Mazingira na Athari zake

Si wanafasihi pekee waliojihusisha na masuala ya kimazingira. Wasomi, wanamisitu, wataalamu na wanaharakati wa kimazingira pia wameshughulikia suala hili. Ufafanuzi wao wa masuala ya kimazingira unadhihirisha kuwa suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mtu ulimwenguni kote. Katika utafiti wake, Nankhuni (2004) alichunguza athari za uhaba wa maliasili kwa ubora wa mtoto nchini Malawi. Kutokana na utafiti wake, ubora wa mtoto ulipimwa kupitia mahudhurio na maendeleo yake shuleni pamoja na afya ya watoto wachanga. Matokeo ya utafiti wa Nankhuni (keshatajwa) yalibaini kuwa, mahudhurio na maendeleo ya watoto shuleni yaliathirika kupitia kuongezeka kwa kazi zilizohusiana na uhaba wa maliasili kama vile kuni na maji. Zaidi ya hayo, utafiti wake ulibaini kuwa, afya ya watoto iliathiriwa na uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa. Utafiti wa Nankhuni (keshatajwa), ulinufaisha kazi hii katika kuchunguza athari za uharibifu wa mazingira hasa kwa watoto wachanga. Hata hivyo, utafiti huu ni wa kifasihi ambapo mtafiti alichunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Uharibifu wa mazingira umeleta madhara makubwa, si tu kwa jamii bali katika mataifa yote duniani. Hali hii inadhihirika kupitia mabadiliko ya tabianchi, kukithiri kwa viwango vya joto duniani katika baadhi ya sehemu duniani, kuongezeka kwa ukame hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki, mafuriko, vifo vya wanyama na wanadamu, kuchipuka kwa magonjwa na ukosefu wa maji safi miongoni mwa madhara mengine (UNFCCC, 2009). Maelezo hayo yalikuwa muhimu katika kazi hii kwa kuweka wazi athari za uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, utafiti huu ni wa kifasihi ambapo mtafiti

alichunguza athari mbalimbali za uharibifu wa mazingira kama zilivyosawiriwa na watunzi wa tamthilia teule.

Wanaharakati wa kimazingira pia wamehusika katika kupambanua athari za uharibifu wa mazingira. Maathai (2009) anatambua kuwa rasilimali asilia zingali zinaharibiwa kupitia shughuli za binadamu kwa kupuuza afya bora ya mazingira. Hivyo, kuenea kwa jangwa kupitia ukataji wa miti kunaathiri vyanzo vya maji, nyanja za kufugia na mashamba kwa ajili ya kilimo na kuchangia katika uchamkaji wa chakula wa dharura. Isitoshe, kubadilika kwa taratibu za mvua hasa kutokana na mabadiliko ya tabianchi kote ulimwenguni kunatishia maisha ya Waafrika wengi ambao wangali wanategemea ardhi kwa mahitaji yao ya kimsingi. Utafiti huu ulihusu usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Kiswahili, ambapo suala la uharibifu wa mazingira liliangaziwa kwa kina ili kuweka wazi athari zake katika maisha ya binadamu pamoja na viumbehai wengine.

Athari za uharibifu wa mazingira ni dhahiri katika ulimwengu tunamoishi. Utafiti wa Rice (2020) kuhusu athari za uharibifu wa mazingira unadhihirisha kuwa tangu karne ya 19, viwango vya halijoto vimeongezeka kwa asilimia kubwa kote ulimwenguni. Hii inadokeza kuwa viwango vya joto duniani katika mwongo mmoja uliopita (2010-2019) viliongezeka kuliko wakati mwingine wowote kwa muda wa miaka elfu kumi na miwili iliyopita. Kutokana na uhalisia wa athari za uharibifu wa mazingira katika ulimwengu wa sasa, utafiti huu ulilenga kuangazia jinsi watunzi wa tamthilia teule wamesawiri athari hizo na njia za kuyahifadhi mazingira.

## 2.3 Uhifadhi wa Mazingira

Katiba ya Kenya (2010), inatambua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ambapo sura ya tano inahusu Ardhi na Mazingira. Kwa mujibu wa katiba hii, serikali ya Kenya uhakikisha matumizi, usimamizi na uhifadhi wa mazingira na maliasili unadumishwa. Vilevile, uhakikisha usawa katika ugavi wa fidia zinazopatikana. Aidha, halmashauri ya *The National Environment Management Authority of Kenya* (NEMA) iliasisiwa mwaka wa 2002. Madhumuni ya NEMA ni pamoja na kusimamia na kuratibu shughuli za kimazingira. Isitoshe, hutumika kama kiungo kikuu cha kitaifa cha kutekeleza sera za kimazingira katika sekta zote katika nchi. Katika utafiti huu, mtafiti alichunguza

mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira ili kubaini mchango wa fasihi ya Kiswahili katika suala hilo kama zilivyo sayansi nyingine za kijamii.

Utafiti wa Gachuru (2010) kuhusu athari za elimu ya kimazingira miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari ulibaini kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya elimu ya mazingira na uhifadhi wa mazingira. Isitoshe, alichunguza kiwango cha ufahamu wa wanafunzi hao kuhusu hali ya sasa ya masuala ya mazingira inayoathiri mataifa mengi ulimwenguni likiwemo taifa la Kenya. Aidha, alilenga kuchunguza kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana za kimsingi kuhusu mazingira kama vile uhifadhi na udhibiti wa uharibifu wake. Matokeo ya utafiti wa Gachuru (keshatajwa) yalibaini kuwa kuhusisha elimu ya kimazingira katika mitaala ya elimu huwa na athari chanya katika uhifadhi wa mazingira miongoni mwa wanafunzi. Utafiti huo ni muhimu katika kuchunguza njia mbalimbali za uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, utafiti huu ni wa kifasihi ambapo mtafiti alitathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

Juhudi za uhifadhi wa mazingira zinabainika kupitia wanaharakati wa kimazingira kama vile Wangari Maathai aliyeanzisha muungano wa *Green Belt movement* mwaka wa 1977. Kupitia muungano huo, Wangari Maathai alihusisha wanawake katika upanzi wa miti. Zaidi ya hayo, serikali ya Kenya imeendeleza Sera ya Mazingira (2012) kama njia ya kushirikisha umma katika uhifadhi wa mazingira. Miongoni mwa mambo mengine, inalenga kuimarisha mchango wa umma katika kufanya maamuzi kama njia moja inayohitajika kwa ajili ya maendeleo endelevu. Vilevile, imeanzisha mazingira ya pamoja katika uhifadhi wa rasilimali za asili kwa sababu ya uhusiano uliopo na shughuli kuu za kiuchumi. Katika kazi hii, mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira lilikuwa jambo muhimu ambalo lilichunguzwa ili kuonyesha jinsi fasihi ya Kiswahili inavyohusika katika uhifadhi wa mazingira

Suala la ulinzi na utunzaji wa mazingira limepewa umuhimu na dharura katika mfumo wa kimataifa hasa kufuatia kongamano la Umoja wa Mataifa la Stockholm la 1972 kuhusu mazingira. Nasong`o (2018) anatambua kwamba azimio hilo la Stockholm liliweka kanuni 26 na kuweka mazingira katika utambuzi wa kimataifa. Hivyo, ukawa mwanzo wa mjadala baina ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea kuhusu uhusiano

baina ya ukuaji wa kiuchumi, uchafuzi wa hewa na maji na ustawi wa watu kote ulimwenguni. Kutokana na umuhimu unaopewa suala la mazingira na wataalamu mbalimbali wa kitaifa na kimataifa, utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa tamthilia ya Kiswahili katika kuangazia suala la uhifadhi wa mazingira.

Juhudi za serikali ya Kenya za kukabiliana na uharibifu wa mazingira vilevile zinadhihirika kupitia hatua ya kuondoa watu walioishi ndani ya msitu wa Mau kiharamu. Isitoshe, serikali imehusika katika ubomoaji wa majengo yaliyo karibu na mito ili kurudishia mazingira hadhi (Obara, 2018). Zaidi ya hayo, Shughuli za Mazingira ni somo lililoanzishwa katika mtaala mpya wa elimu (CBC) nchini Kenya mwaka wa 2017. Somo hili ni la lazima katika viwango vya gredi ya kwanza hadi ya tatu, ambapo shughuli kama vile kupanda miti na kuitunza ni miongoni mwa shughuli muhimu. Kwa hivyo, lengo kuu la somo hili ni kuwapa wanafunzi uelewa na maarifa ya kimsingi kuhusu mabadiliko ya tabianchi (Murikira, 2019). Wanafasihi nao wamejihusisha katika uwanja wa fasihi mazingira ili kuchangia katika harakati za uhifadhi wa mazingira. Hivyo, utafiti huu ulichunguza jinsi watunzi wa tamthilia teule za Kiswahili wamesawiri suala la mazingira ili kuonyesha uhusiano baina ya shughuli za binadamu na mazingira yake.

### 2.4 Fasihi Mazingira katika Fasihi ya Ulimwengu

Utafiti wa Quick (2004) ulioegemea katika uhakiki wa kiekolojia ulichochewa na baadhi ya mawazo ya kimsingi ya mazingira. Moja kati ya mawazo hayo ni kwamba, kwa sababu ya ukuaji wa idadi ya watu na maendeleo ya kiteknolojia katika miaka mia chache iliyopita, kasi na kiwango cha mabadiliko ya mazingira ni makuu na yasiyo endelevu. Kwa msingi huu, utafiti wa Quick (keshatajwa) ulikusudia kuonyesha maadili tata ya mazingira pamoja na kutathmini upya makubaliano muhimu ya kwamba, riwaya za kusini za Cormac McCarthy zinadhihirisha udhanaishi au falsafa ya kinihilisti. Utafiti wa Quick (keshatajwa) ulibaini kwamba, suluhisho la matatizo ya kimazingira halipo katika maendeleo zaidi ya kiteknolojia bali katika mabadiliko ya kimsingi katika jinsi binadamu hujiona kama sehemu ya asili. Utafiti wa Quick (keshatajwa) ulichangia katika kazi hii kwa kuwa uliangazia athari za maendeleo ya kiteknolojia kwa mazingira. Kando na teknolojia, kazi hii ilichunguza athari za shughuli

nyinginezo za binadamu kwa mazingira na kutathmini njia za kusuluhisha athari hizo, kwa mujibu wa tamthilia teule.

Uhusiana baina ya binadamu na mazingira umekuwa malighafi kwa waandishi na wahakiki wa fasihi. Haya yanadhihirika kupitia kwa kazi ya Massey (2009), ambaye alihakiki kazi teule za fasihi nchini Australia. Alichunguza jinsi ambavyo kazi hizo zinajenga tungo zenye masuala ya kiekolojia na kuwatolea wasomaji viwango vya maudhui ya kiekolojia katika itikadi za kimazingira za kisasa. Aidha, alishughulikia jinsi ambavyo kazi teule zinabainisha athari hasi za binadamu kutawala mazingira. Matokeo ya utafiti yalithibitisha kuwepo kwa matatizo yanayotokana na mahusiano ya binadamu na mazingira na hivyo kupendekeza njia za kushughulikia matatizo ya kisasa ya mazingira. Utafiti wa Massey (keshatajwa) ulijenga msingi wa kazi hii kwa kuwa ulionyesha umuhimu wa mazingira kama malighafi ya waandishi wa kazi za fasihi. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika tamthilia ya Kiswahili ili kuchunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Haja ya kubadili mitazamo ni muhimu ili kutatua matatizo ya kimazingira. Isitoshe, mwito wa kubadili uhusiano wa binadamu na mazingira huhimiza kubadili si tu jinsi wanavyotumia rasilimali za mazingira bali pia jinsi wanavyowaza na kuhisi kuhusu mazingira yao (Sexton, 2012). Katika utafiti wake, Sexton (keshatajwa) aliangazia uwakilishaji wa mazingira katika fasihi ya Marekani kati ya mwaka 1835 na 1945. Utafiti wake unadokeza kuwa kazi za sanaa hudhamiria kubadilisha uhusiano kati ya binadamu na mazingira yake hasa kwa kubadili mielekeo yao kuhusu mazingira hayo. Utafiti wa Sexton (keshatajwa) ulifaa kazi hii hasa katika kuangazia umuhimu wa fasihi katika kusuluhisha matatizo ya kijamii. Miongoni mwa matatizo hayo ni uharibifu wa mazingira. Tofauti na kazi ya Sexton (keshatajwa), utafiti huu ulichunguza nafasi ya motifu za kimazingira katika uwanja wa fasihi mazingira.

Uhakiki wa kiekolojia wa kisasa lazima ukumbatie maono ya kilimwengu ambayo ni pamoja na utunzaji wa mazingira wa kimataifa, haki za kijamii na wajibu wa binadamu ambao unavuka mipaka ya taifa, kabila, misimamo ya kisiasa na kiakili, tabaka na jinsia. Haya yalibainika kutokana na utafiti wa Njiru (2015) aliyechunguza jinsi

ambavyo haki za kimazingira, majanga na mambo mengine huingiliana na teknolojia, elimu na vitendo na nadharia ya kisasa ya ulimwengu katika kazi teule za Margret Atwood, Leslie Silko, Barbara Kingslover, Ruth Ozeki, Starhawk na waandishi wengine. Hivyo, riwaya teule katika utafiti wake zilitathmini jinsi ambavyo mataifa na jamii mbalimbali zinapaswa kutumia mbinu za ulimwengu na mawazo ya kiekolojia katika kutambua, kujadili na kupambana na uzalishaji wa kaboni, mabadiliko ya tabianchi pamoja na vitisho vinavyotokana na masuala mengine ya kimazingira na kiteknolojia. Kazi ya Njiru (keshatajwa) ilinufaisha utafiti huu katika utambuzi wa njia mbalimbali za kupambana na athari za uharibifu wa mazingira. Tofauti na utafiti wa Njiru uliojikita katika riwaya za Kingereza, kazi hii iliangazia motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Kiswahili za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Iheka (2015) alichunguza jinsi kazi za kifasihi za kiafrika husawiri, kukosoa na kutoa maono mbadala juu ya matatizo ya ekolojia kama vile uchafuzi wa mafuta katika Delta ya Naija na utupaji ovyo wa taka zenye sumu katika maji ya Kiafrika. Hivyo, utafiti wake ulisisitiza mahusiano baina ya binadamu na wasio binadamu katika ekolojia ya Kiafrika. Utafiti wa Iheka (keshatajwa) ulibaini kwamba, kutokana na uwezekano wa uhalisia wa ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi, elimu ya baadaukoloni inapaswa kutilia maanani athari za kiekolojia si tu za ukoloni na ubeberu bali pia za upinzani wa baadaukoloni. Utafiti wa Iheka (keshatajwa) ulinufaisha kazi hii katika utambuzi wa athari za kikoloni katika mazingira ya Kiafrika. Hata hivyo, kazi hii ilijikita katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kwa kuchunguza jinsi walivyosawiri athari za shughuli za binadamu kwa mazingira.

Uhusiano baina ya ardhi ya baadaukoloni na binadamu uliangaziwa na Alia (2017) alipochunguza jinsi ambavyo kwa pamoja huunda mazingira. Utafiti wake ulihusu uhakiki kiekolojia wa kibaadaukoloni wa binadamu, wanyama na ardhi. Alijikita katika matini kutoka tamaduni mbalimbali zifuatazo: *Things Fall Apart* na Chinua Achebe, *The Hungry Tide* na Amitav Ghosh, *Remnants of the First Earth* na Ray A. Young Bear Pamoja na *Ceremony* na Leslie Mamon Silko. Alitumia rasilimali zilizosawiriwa katika matini hizi kutambua thamani, haki na imani kuhusiana na asili na ardhi katika kila utamaduni pamoja na athari za uharibifu wa asili hizo kwa binadamu. Utafiti wa Alia (keshatajwa) unasisitiza haja ya kukumbatia tofauti za watu kwa misingi mbalimbali

katika kuzuia ubaguzi wa mazingira pamoja na mawazo ya Ulaya au yale ya kibinafsi ambayo yanaweza tu kuwa chanzo cha kuchochea matatizo ya kimazingira yaliyopo. Utafiti wa Alia (keshatajwa) ulichangia kazi hii katika kuangazia imani na tamaduni mbalimbali kuhusu mazingira zilizolenga kuzuia uharibifu wa mazingira. Tofauti na utafiti wa Alia, kazi hii ilipiga hatua zaidi kwa kuchunguza jinsi ambavyo uasi wa imani na tamaduni kuhusiana na asili zimechangia katika uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

Malnati (2017) alichunguza fasihi na filamu za sanaa kwa kuangazia kazi teule za fasihi kutoka maeneo mawili ya kijiografia; Kaskazini Magharibi mwa Pasifiki na Kusini mwa Italia. Utafiti wake ulilenga kuchunguza athari za uharibifu wa mazingira kama ilivyosawiriwa katika kazi teule za fasihi. Aligundua kuwa fasihi ina uwezo wa kuwakilisha kikamilifu ulimwengu halisi hasa katika matatizo ya kimazingira na kijamii. Hivyo, hutekeleza wajibu muhimu katika kutatua masuala hayo. Vilevile, alibainisha kuwa, kuhusisha masuala ya udhalimu wa kimazingira na uwakilishi wake katika sanaa kunaweza kumulika sehemu za kawaida za uharibifu wa kijamii, kiuchumi na kimazingira. Kwa hivyo, katika baadhi ya masuala, fasihi inaweza kutoa jibu ambalo haliwezi kupatikana kwingineko. Utafiti wa Malnati (keshatajwa) ulikuwa muhimu katika kazi hii kwa kuwa uliweka msingi wa mchango wa fasihi katika kuangazia na kusuluhisha masuala ya kijamii likiwemo suala la kimazingira. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga kuangazia jinsi ambavyo watunzi wa tamthilia teule za Kiswahili wamesawiri motifu za kimazingira ili kuweka wazi matatizo yanayotokana na uharibifu wake na namna ya uhifadhi wa mazingira

Utafiti wa Tan (2019) ulijikita katika uchambuzi wa kiekolojia wa riwaya za kubuni za hali ya hewa za mwanzo wa miaka ya sitini za J.G Ballard kwa mtazamo wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia. Kutokana na utafiti wake, ilibainika kwamba uharibifu wa ardhi unaweza kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu hasa kupitia ukuaji wa viwanda. Hivyo, hata ingawa kazi teule katika utafiti wa Tan (keshatajwa) ni za kubuni, zina uhalisia na uhalali katika ulimwengu wa sasa. Hii inatokana na sababu kwamba, mabadiliko ya tabianchi ni suala zito ambalo limekuwa likijadiliwa katika kiwango cha kitaifa na kimataifa tangu miongo miwili iliyopita. Utafiti wa Tan (keshatajwa) ulichangia kazi hii katika kutambua jinsi ambavyo baadhi ya shughuli za binadamu

huchangia katika uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, kazi hii ilijikita katika tamthilia teule za Kiswahili katika kuchunguza chanzo cha uharibifu wa mazingira na mtazamo wa waandishi wa tamthilia hizo katika uhifadhi wa mazingira hayo.

**2.5 Fasihi Mazingira katika Fasihi ya Kiafrika**

Methali za kiekolojia hudhihirisha utajiri wa utamaduni wa jamii. Utafiti wa Fortress na Onwuka (2014) kuhusu methali za kiekolojia za Yoruba ulibaini kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya methali za Kiyoruba na ekolojia unaosaidia katika uhifadhi wa mazingira. Hata ingawa utafiti wa Fortless na Onwuka (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa vile uliegemea katika fasihi simulizi, uliifaa kazi hii katika maelezo ya kimsingi kuhusu suala la ekolojia na mazingira. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika fasihi andishi ambapo ulishughulikia motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Fasihi simulizi inaweza kuwa chanzo cha kusawiri suala la mazingira katika jamii. Adugna (2014) alitafiti kuhusu usawiri wa mazingira katika fasihi simulizi kwa kutathmini methali za Oromo. Aligundua kuwa methali za Kioromo hubeba maadili yanayosaidia katika uhifadhi wa mazingira. Hivyo, huwezesha wanajamii kuishi kwa ushirikiano na viumbe wengine. Isitoshe, methali hizi huhimiza wanajamii kuwa waadilifu katika utunzaji wa mazingira. Utafiti wa Adugna (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa kuwa uliangazia fasihi simulizi hasa utanzu wa semi, ili kubainisha nafasi yake katika uhifadhi wa mazingira. Licha ya kuwa kazi hii ilijikita katika fasihi andishi hasa kupitia utanzu wa tamthilia, kazi ya Adugna (keshatajwa) ilikuwa muhimu katika kufafanua umuhimu wa fasihi kwa jumla katika uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Utetezi wa uhifadhi wa mazingira umeathiriwa pakubwa na utamaduni wa jamii kwa kuwa katika jamii husika, uhifadhi wa mazingira huoanishwa na imani za kidini. Haya yalithibitika kupitia utafiti wa Maleya (2016) katika Riwaya ya Ole Kulet ya *Vanishing Herds & the Hunter*. Aidha, alibaini kuwa kuna mwelekeo tofauti kuhusu uhifadhi wa mazingira kati ya Waafrika na Wamarekani. Hii ni kwa kuwa Wamarekani huoanisha mazingira na suala la uchumi ilhali Waafrika huoanisha utunzaji wa mazingira na imani

za kidini. Utafiti wa Maleya (keshatajwa) uliifaa kazi hii katika kueleza uhusiano baina ya fasihi na ekolojia. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika utanzu wa tamthilia ya Kiswahili. Hivyo, ulichunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule.

Kuna uhusiano wa karibu kati ya fasihi na mazingira. Haya yanathibitika kupitia utafiti wa Wu (2016), aliyeshughulikia uhakiki wa kiekolojia wa Kiafrika huku akiangazia nchi ya Nigeria. Alichunguza riwaya sita za waandishi wa Kiafrika kutoka nchi ya Nigeria. Utafiti wake ulibaini kuwa, ili kueleza uhusiano uliopo kati ya fasihi ya Kiafrika na mazingira ni bora kuhakiki fasihi ya Kiafrika kwa jumla. Vilevile, aligundua kuwa fasihi ya Kiafrika ina mchango katika kumulika athari za uharibifu wa mazingira na kufafanua jinsi ya kuyahifadhi mazingira. Hata ingawa utafiti wa Wu (keshatajwa) uliangazia suala la mazingira kwa kuegemea katika utanzu wa riwaya, ulikuwa muhimu katika maelezo ya kimsingi kuhusu fasihi mazingira. Kazi hii ilijikita katika tamthilia ya Kiswahili kwa kuchunguza nafasi yake katika uwanja wa fasihi mazingira kwa mujibu wa tamthilia zilizoteuliwa.

**2.6 Fasihi Mazingira katika Fasihi ya Kiswahili**

Suala la fasihi mazingira katika fasihi ya Kiswahili limetafitiwa na Vierke (2007) aliyeangazia suala la mwanamke kuhusishwa na mazingira. Alibainisha jinsi mwanamke mwenye asili ya uswahilini anavyolinganishwa na baadhi ya mimea kama vile pilipili (kwa ukali wake), maua (urembo wake unaofifia haraka) na hata minazi kwenye utendi wa *Utumbuizo wa Mjemje* na shairi la *Mtambuu. Aidha*, Alionyesha jinsi mazingira asilia yalivyo na umuhimu katika jamii ya Waswahili na hasa walipotunga ushairi wa kale. Utafiti wa Vierke (keshatajwa) ulikuwa tofauti na huu kwa vile ulijikita katika suala la mazingira katika ushairi wa Kiswahili, ilhali kazi hii ilijikita katika utanzu wa tamthilia ya Kiswahili kwa kuangazia jinsi watunzi wa matini teule wamesawiri suala la mazingira.

Riwaya ya Kiswahili imetafitiwa kuonyesha jinsi inavyounga mkono suala la uhifadhi wa mazingira. Utafiti wa Sabula (2014) ni mojawapo ya tafiti hizo ambao uliangazia nafasi ya mwanamke katika uhifadhi wa mazingira kupitia riwaya ya *Nakuruto*. Katika utafiti wake, Sabula (keshatajwa) aliangazia changamoto anazopitia mwanamke katika kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia mkabala wa fasihi ya Ufeministi wa Kiekolojia.

Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, mwanamke ana nafasi kubwa katika kubadili tabia za kijamii kuhusu mazingira yake. Utafiti wa Sabula (keshatajwa) uliifaa kazi hii katika kuangazia nafasi ya kila mwanajamii katika uhifadhi wa mazingira. Hata hivyo, kazi hii ilikuwa tofauti kwa kuwa ilijikita katika utanzu wa tamthilia ya Kiswahili. Hivyo, mtafiti aliangazia usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule kwa kuegemea katika mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Fasihi ya Kiswahili imedhihirisha kuwepo kwa maendeleo ya kisanii katika utunzi. Haya yanatokana na utafiti wa Ong`utte (2014) uliohusu uhakiki wa suala la uhifadhi wa mazingira katika tanzu teule za fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya. Alichunguza jinsi masuala ya mazingira yalivyojitokeza katika vitabu vitatu vya fasihi ya Kiwahili. Vitabu vitatu kutoka tanzu tatu za fasihi ya Kiswahili vilivyochapishwa mwanzoni mwa Milenia Mpya vilihakikiwa kwa mkabala wa uhakiki kimazingira. Vitabu hivyo ni riwaya ya *Babu Alipofufuka*, tamthilia ya *Kifo Kisimani* na mashairi kutoka diwani ya *Bara Jingine*. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa uharibifu wa mazingira ni bayana katika jamii, jambo ambalo limeangaziwa na watunzi wa fasihi ya Kiswahili. Vilevile, utafiti ulibainisha kuwa wasanii wa kazi teule za fasihi walipotunga kazi zao, walilenga kuburudisha, kuzindua na kutabiri hali ya baadaye ya mazingira kwa jamii. Utafiti wa Ong`utte (keshatajwa) ulinufaisha kazi hii katika kufafanua mchango wa fasihi ya Kiswahili kwa jumla katika kusawiri masuala ya mazingira. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika tamthilia ya Kiswahili ambapo mtafiti alichunguza motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Fasihi ya Kiswahili imeanza kujitokeza kama mojawapo ya fasihi zinazotetea mazingira. Katika utafiti wake, Sangili (2015), alichunguza nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika uwanja wa fasihi mazingira. Alichunguza jinsi wasanii wa tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili wanavyohusika kiuchanganuzi katika uwanja wa fasihi mazingira. Utafiti wa Sangili (keshatajwa) ulibaini kuwa viongozi katika serikali huchangia kwa kiwango kikubwa katika uharibifu wa mazingira kwa namna mbalimbali. Utafiti wa Sangili (keshatajwa) ulikuwa tofauti na kazi hii kwa vile ilishughulikia motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege, ili kuchunguza jinsi walivyosawiri mazingira kwa mkabala wa

uhakiki wa kiekolojia. Hata hivyo, utafiti wake ulinufaisha kazi hii katika maelezo kuhusu chimbuko la uwanja wa fasihi mazingira na mawanda yake.

Maudhui ya utunzaji wa mazingira yanaangaziwa kwa kiwango kikubwa na watunzi wa fasihi ya watoto. Bulaya na Mhango (2020) walichunguza ujitokezaji wa maudhui ya utunzaji wa mazingira katika hadithi kutoka fasihi ya watoto ya Kiswahili. Walibaini kuwa athari za uchafuzi wa mazingira zinagusa makundi yote ya kijamii pakiwemo watoto. Kwa hivyo, mapambano dhidi yake yanapaswa kuwa jumuishi bila kujali jinsia, umri, elimu, mamlaka au hata uwezo wa kiuchumi alionao mtu. Utafiti wao uliifaa kazi hii katika uelewa wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika utanzu wa tamthilia ya Kiswahili ili kuchunguza jinsi motifu za kimazingira zilivyosawiriwa katika tamthilia teule kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Masuala ya kimazingira yanaendelea kuzungumziwa katika nyanja mbalimbali. Haya yanatokana na utafiti uliofanywa na Wesonga na wenziwe (2020). Walishughulikia nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya teule za K.W Wamitila kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisia. Walitambua kuwa fasihi haijaachwa nyuma katika mjadala kuhusu mazingira. Aidha, waligundua kuwa fasihi ya Kiswahili ina uwezo wa kuangazia masuala ya mazingira jinsi yalivyo katika jamii halisi. Utafiti wao ulinufaisha kazi hii katika kuelewa nafasi ya fasihi katika kuangazia masuala ya kijamii kama vile suala la kimazingira. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika tamthilia ya Kiswahili ili kuchunguza mchango wake katika kuangazia masuala ya kimazingira.

### 2.7 Dhana ya Motifu katika Fasihi

Masoud (2015) alichunguza matumizi ya motifu ya nambari katika ngano za Ki-pemba. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa matumizi ya motifu ya nambari yana dhima kubwa katika fasihi hususan fasihi simulizi. Aidha, uchunguzi ulibaini kuwa kuna uhusiano wa karibu baina ya miktadha mbalimbali ya jamii za Wapemba ambayo huhusisha matumizi ya nambari na jinsi inavyojitokeza katika ngano zao. Utafiti wa Masoud (keshatajwa) ulihusiana na kazi hii kwa kuwa ulijikita katika suala la motifu na kuonyesha umuhimu wa matumizi yake katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui

katika fasihi. Hata hivyo, tofauti ni kwamba utafiti huu ulijikita katika fasihi andishi ambapo mtafiti alichunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Utafiti wa Njoki (2018) ulichanganua motifu za yatima katika fasihi andishi ya watoto. Utafiti wake ulilenga kubainisha mambo yanayochangia watoto kuwa yatima kwa mujibu wa hadithi teule za fasihi ya watoto. Vilevile, utafiti ulimwezesha kuelewa changamoto zinazowakumba watoto yatima katika jamii pamoja na kuonyesha jinsi mtoto yatima anavyokabiliana na changamoto zinazomkumba. Utafiti wa Njoki (keshatajwa) ulinufaisha kazi hii katika kuelewa namna kipengele cha motifu kinaweza kutumika kama mtindo katika kazi za fasihi ili kufafanua maudhui ya mwandishi. Tofauti na utafiti huo, kazi hii ilijikita katika motifu za kimazingira katika tamthilia teule ili kuchunguza namna Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege wametumia motifu za kimazingira kusawiri uharibifu wa mazingira, athari zake na namna ya kuyahifadhi mazingira.

Gakii (2019), alichunguza mwingilianomatini katika utenzi wa *Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwepo na mwingilianomatini katika mitindo mbalimbali pakiwemo motifu za tanzia na motifu za usaliti. Kutokana na utafiti wake, motifu hizo zilitumika kama mtindo wa waandishi wa kusawiri maudhui kama vile tamaa, ukosefu wa maadili katika jamii na changamoto zinazowakumba wanaharakati wa ukombozi. Kazi ya Gakii (keshatajwa) ilinufaisha utafiti huu katika uelewa wa namna motifu mbalimbali zinaweza kutumika kama mtindo ili kusawiri maudhui katika fasihi. Tofauti na kazi yake, utafiti huu ulichunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

## 2.8 Motifu za Kimazingira katika Fasihi

Baadhi ya wasomi na watafiti wa kifasihi wamezungumzia suala la motifu kama mtindo unaoweza kuwasilisha masuala ya kimazingira. Katika utafiti wake, Nyamsenda (2015) alichunguza ushujaa wa shujaa wa motifu za safari na msako katika ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Utafiti wake ulibaini kuwa motifu za safari na msako zinaweza kutumika katika kuelezea utamaduni, falsafa, imani, jiografia, historia,

maisha na mazingira ya Waikizu. Utafiti wa Nyamsenda (keshatajwa) unahusiana na kazi hii katika kuchunguza motifu mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kufafanua masuala ya kijamii pakiwemo mazingira. Kando na kuwa utafiti wake ulijikita katika kipera cha ngano katika fasihi simulizi, ulitofautiana na kazi hii kwa kuwa mtafiti alijikita katika motifu mbalimbali za kimazingira zilizotumika kueleza suala la mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Kwa mujibu wa Nyamsenda (2015), riwaya ya *Bustani ya Edeni* ya Emmanuel Mbogo (2002) imetawaliwa na motifu za safari na msako. Kwa mfano, "Pasta Yona anatoka kuelekea kwenye kilele cha mlima cha Golgotha". Motifu za Safari na msako wa Pasta Yona zinajitokeza katika harakati ya kupambana na uchafuzi wa mazingira. Hatimaye kiwanda cha `*Sagasaga Chemical Industry*` kinafungwa. Maelezo hayo yalinufaisha kazi hii katika kuelewa namna suala la uchafuzi wa mazingira linaweza kufafanuliwa kupitia motifu mbalimbali. Hata hivyo, utafiti huu uliangazia motifu za kimazingira ambazo zimetumiwa na waandishi wa tamthilia teule ili kusawiri hali ya mazingira kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Kane (2016) anaeleza aina mbili za motifu katika `*The Pearl*` ya John Steinbeck ambazo ni taswira za asili na nyimbo za Kino. Anafafanua kuwa mwandishi Steinbeck anatumia taswira za asili kuonyesha jinsi mhusika Kino alivyo na uhusiano wa karibu na ulimwengu asilia unaomzunguka. Isitoshe, anaeleza kuwa bila manufaa kutokana na maliasili, Kino na aila yake wasingekuwa na chochote. Maelezo ya Kane yalifaa utafiti huu katika kuelewa jinsi ambavyo kipengele cha motifu kinaweza kutumiwa kuonyesha jinsi binadamu huhusiana na kuathiriana na mazingira asilia. Utafiti huu nao ulipiga hatua katika kuangazia motifu za kimazingira kama zilivyosawiriwa katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

## 2.9 Yaliyoandikwa kuhusu Tamthilia Teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege

King'ora (2014) alichunguza utendaji katika tamthilia za *Sudana* (Mazrui na Njogu, 2006*)* na *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011). Alibaini kuwa tamthilia hizo zimezingatia kigezo kikuu katika matini za kidrama ambao ni uwezo wa kuwasilisha jukwaani. Aliendelea kubainisha jinsi vipengele hivi vinavyofanikisha uwasilishaji wa

ujumbe kwenye jukwaa. Hata ingawa utafiti huu ulishughulikia utendaji katika tamthililia ya *Kimya Kimya Kimya* kwa kutumia nadharia ya Utendaji, uliifaa kazi hii katika kuelewa uwasilishaji wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ambayo ni mojawapo ya tamthilia teule katika kazi hii. Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Kiswahili za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege ambazo ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*), Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015).

Vipengele vya usimulizi ni muhimu katika kusimulia hadithi na kuwasilisha maudhui na dhamira katika tamthilia kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi hasa hadithi fupi na riwaya. Khamis (2015) alishughulikia usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* kwa kuongozwa na nadharia ya naratolojia. Matokeo ya utafiti wake yalithibitisha kuwepo kwa usimulizi katika uwasilishaji wa tamthilia. Kazi ya Khamis (keshatajwa) iliufaa utafiti huu katika kuelewa mtindo ambao Arege ametumia katika kuwasilisha maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya.* Tofauti na kazi ya Khamis (keshatajwa), kazi hii ilijikita katika usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule.

Tamthilia za Arege hudhihirisha matumizi ya lugha kwa ubunifu na hivyo kuleta ujumi katika maudhui anayowasilisha. Haya yanathibitika kupitia kwa utafiti wa Oiko (2017) aliyeshughulikia mtindo katika tamthilia za Arege ambazo ni *Kijiba cha Moyo, Mstahiki Meya* na *Chamchela.* Aidha, utafiti wake ulibainisha kuwa Arege ametumia mtindo wa kinaya ili kuwakejeli Waafrika walioufuata ukoloni mamboleo kikasuku. Kazi ya Oiko (keshatajwa) iliufaa utafiti huu katika uchambuzi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* kwa kuelewa mtindo wa Arege katika uwasilishaji wa maudhui yanayohusiana na mazingira. Hata hivyo, kazi hii ilijikita katika usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Utafiti wa Haji (2018) kuhusu uhalisia wa utabaka katika tamthilia za *Janga la Werevu* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* za Said Ahmed Mohamed ulionyesha kwamba, utabaka unaojitokeza zaidi katika tamthilia hizo teule ni ule wa kiuchumi, kisiasa, kiitikadi na utabaka wa hali na hadhi. Aidha, utafiti wake ulibaini kuwa, baadhi ya

athari za utabaka ni pamoja na mizozo katika jamii, umaskini na ufisadi. Utafiti wa Haji (keshatajwa) ulikuwa muhimu katika kazi hii hasa katika uchambuzi wa maudhui ya kimazingira katika tamthilia ya *Janga la Werevu* (Mohamed, 2011). Kando na tamthilia ya *Janga la Werevu*, kazi hii ilichunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Kiswahili za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*)*, *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015).

Omoga (2018) aliangazia mwananchi wa kawaida kama mdhulumu wa maslahi yake katika tamthilia za *Kilio cha Haki*, *Amezidi* na *Mstahiki Meya*. Utafiti wa Omoga (keshatajwa) ulionyesha kuwa wananchi wa kawaida wamekuwa wakichangia katika dhuluma dhidi yao huku wakiwalaumu viongozi wao. Vilevile, ilibainika kwamba mwananchi anaweza kujiepusha kutokana na dhuluma kupitia ufahamu wa haki zake, kwani ana uwezo wa kuhakikisha kuwa viongozi wanaongoza kwa kujali masilahi ya wote. Katika utafiti huu, mtafiti alichunguza usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Kiswahili za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Kwa hivyo, kazi ya Omoga (keshatajwa) ilisaidia katika kuangazia mchango wa wananchi wa kawaida katika kusababisha uharibifu wa mazingira hasa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* na jinsi anavyoweza kuepuka uharibifu wa mazingira asilia.

## 2.10 Muhtasari wa Tamthilia Teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege

Kwa muhtasari, tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2015) inahusu uongozi wa Mstahiki Meya ambaye kando na kuendesha baraza kwa njia mbovu, anazingatia ushauri wa baadhi ya madiwani na marafiki wake wa karibu ambao wanampotosha. Matokeo ni kuzorota kwa miundo msingi na huduma muhimu za umma, kama vile matibabu, elimu na usafi wa mazingira.

Katika tamthilia ya *Janga la Werevu*, (Mohamed, 2011) Bamkuu na Bimkuu wanamiliki vipande vikubwa vya ardhi ya umma. Aidha, wanafweka misitu na kuanzisha mashamba makubwa ya pareto, chai na kahawa. Matokeo ya ufyekaji wa misitu ni kukosekana kwa maji, hali inayowaangamiza wananchi. Isitoshe, wanafungua biashara ya kuuza maji wanayosomba katika chemchemi za maji za misitu ya wananchi. Maji yanakuwa adimu kupatikana katika kila pembe ya nchi isipokuwa nyumbani kwao tu. Hata hivyo, mambo yanabadilika wakati binti zao, Busara na Kristy wanaungana na waandamanaji kulalamikia haki yao ya kupata maji safi.

Kadhalika, tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011*)*, inaangazia Bw. Binafsi, kiongozi anayetumbukiza nchi anayoongoza katika hali ya umaskini na njaa. Kupitia uongozi wake uliojaa ufisadi na ubinafsi, anageuza mali ya umma kuwa ya kibinasi. Hali hii inachangia katika kuzorota kwa hali za kimaisha za wananchi. Katika miaka hamsini baada ya kupata uhuru, wananchi wamekuwa kimya huku wakitarajia kuwa viongozi waliochagua watayajalia maslahi yao. Hata hivyo, hali ya mambo inaanza kubadilika baada ya kuzaliwa kwa Mpya, binti ya Bw, Binafsi na Bi. Shoo. Yeye anaongoza umma katika kuzungumza waziwazi kuhusu maslahi yao. Hatimaye, ndugu zake Mussa na Zanga wanajiunga naye katika kupinga uongozi dhalimu wa baba yao.

Tamthilia ya *Majira ya Utasa* (Arege, 2015) nayo inahusu jinsi Jumbe, kiongozi anayemiliki mashamba na viwanda vya maua anageuza nchi anayoiongoza kuwa tasa. Anaharibu mazingira kupitia mambo mbalimbali pakiwemo ufyekaji wa misitu, jambo linaloathiri vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, anaachilia kemikali hatari kutoka katika viwanda vya maua kupitia ardhini, mitoni hadi baharini. Vilevile, tamthilia hii inaangazia jinsi juhudi za wananchi waliozinduka na kuungana kwa kukerwa na uongozi potovu wa Jumbe zinaleta mwamko wa harakati za ukombozi.

### 2.11 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia iliyoasisiwa na Glotferty (1996). Nadharia hii ilianza huko Marekani kwa lengo la kuwahusisha wanafasihi katika utetezi wa mazingira, kufuatia mabadiliko ya tabianchi ambayo yalisababishwa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika sehemu mbalimbali ulimwenguni (Heise, 2008). Hivyo, mchakato wa uhakiki wa kiekolojia ulizuka kutokana na nia ya kuyaboresha mazingira yaliyoangamia, na kuimarisha jinsi mazingira yalivyoathiriwa na binadamu; masuala ambayo hayakutimika kupitia kwa sayansi, ila kupitia uandishi na kazi za kifasihi.

Kwa mujibu wa Barry (2013), makala ya Karl Kroeber (1974), "Home at Grasmere" ndiyo yalikuwa ya kwanza kutumia dhana ya ekolojia katika uhakiki wa kifasihi. Kwa maoni ya Barry (keshatajwa), licha ya kuwa tapo hili lilizuka miaka ya tisini, makala

ya Rueckert (1978) *Literature and Ecology: An Experiment in Ecocriticism* yaliweka msingi uwanja wa uhakiki wa kiekolojia. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa uhakiki wa kiekolojia ulibainika katika tafiti za kifasihi kuanzia miaka ya sabini. Kimsingi, Nadharia ya uhakiki wa kiekolojia huchambua kazi za kifasihi kwa kujikita kwenye vipengele vya uhusiano na utegemeano baina ya binadamu na mazingira.

Baada ya makala ya Rueckert yaliyoweka msingi wa uhakiki wa kiekolojia, muongo mmoja baadaye mnamo mwaka wa 1989, Glen A. Love alipendekeza matumizi ya `Uhakiki wa Fasihi ya Kiekolojia`. Aidha, Glen Love aliongoza kundi la wasomi wachanga ambao walikutana mwaka wa 1992 na kuanzisha Chama cha Taaluma ya Fasihi na Mazingira (ASLE).  Lengo kuu la chama hiki lilikuwa kukuza mabadilishano ya mawazo na habari zilizohusu fasihi na utafiti wa kimwingiliano taaluma wa kimazingira. Hivyo, walitilia maanani uhusiano uliopo baina ya binadamu na ulimwengu asili (Glotferty, 1996). Chama hiki kilikua kwa kasi na kupanuka kutoka uegemezi katika uandishi wa asili hadi kwenye mtazamo mpana zaidi wa aina mbalimbali za tafiti za kifasihi kutoka kote duniani.

Nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inasisitiza kwamba utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Glotferty, 1996). Kimsingi, utamaduni unahusu namna watu wanavyoishi katika maisha yao ya kila siku. Vilevile, uhakiki wa kiekolojia huchunguza jinsi ambavyo binadamu, utamaduni na mazingira huathiriana. Kwa msingi huu, utafiti huu ulichunguza jinsi utamaduni huathiri uhusiano uliopo baina ya binadamu na mazingira anamoishi kama ilivyobainika katika tamthilia teule za Kiswahili.

Glotfelty na Fromm (1996) wanafafanua fasihi ya ekolojia kama uhusiano baina ya kazi ya kifasihi na ekolojia. Uwanja huu unachukua mtazamo wa kiardhi kwa masuala ya kifasihi ya ekolojia. Aidha, Uwanja huu upo mintarafu ya wanadamu kujadili, kuandika na kuchanganua diskosi mbalimbali kuhusu mandhari, sehemu za dunia, viumbe hai, maliasili na uzuiaji wa uchafuzi katika viwanda. Nadharia ya uhakiki wa kiekolojia iliufaa utafiti huu katika kufafanua jinsi watunzi wa tamthilia teule za fasihi ya Kiswahili walivyosawiri motifu za kimazingira kwa kuangazia njia za uharibifu wa mazingira, athari zake na namna ya kuyahifadhi.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, binadamu, mazingira na viumbe wengine huhusiana kwa namna ya kutegemeana na kukamilishana. Kwa msingi huu, Tarton na Henwood (2002), wanaeleza kuwa mfumo ekolojia ni namna ya maisha katika eneo fulani ambapo viumbe wa aina mbalimbali hutegemeana kwa chakula ama hifadhi au vyote kwa pamoja. Wanaendelea kusema kuwa mfumo huu wa maisha hushirikisha viumbe wote waliopo katika eneo husika, kuanzia wale wakubwa hadi wale wadogo wasioonekana kwa macho. Aidha, watu wote katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea wanategemeana kupata ustawi kutokana na shughuli zinazofanywa katika ekolojia. Kwa kuzingatia mtazamo huu, utafiti huu ulieleza jinsi ambavyo shughuli za binadamu zinaweza kuweka mazingira asilia katika hali endelevu ya uharibifu na kusababisha madhara mengi, kwa mujibu wa tamthilia teule.

Rigby (2002), anaeleza ekolojia kama mfumo unaotazama jinsi mwanadamu kando na kufaidika kutokana na mazingira na maumbile asilia anasababisha uchafuzi wa mchanga, hewa na maji. Vilevile, mwanadamu anachangia katika kuharibu uhai asilia wa mimea na wanyama na kutishia msingi wa uhai unaotegemewa na jamii za kibinadamu. Hata hivyo, kimsingi matatizo ya kimazingira ni ya kisayansi. Kwa hivyo, mijadala mingi kuhusu matatizo hayo huhusisha zaidi wanahewa kuliko watunzi wa fasihi au hata wahakiki wa kazi ya kifasihi. Ndiposa Garrard (2007), anasema kuwa masuala haya ya kimazingira yanaweza kuwasilishwa kwa jamii kupitia fasihi kwa kuwa ndio huingiliana pakubwa na utamaduni wa jamii. Kwa msingi huu, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia.

Uhakiki wa kiekolojia huelezea mitazamo tofauti tofauti ya fasihi, na utofauti huu ni mojawapo ya nguvu zake (Quick, 2004). Upana wa kimitazamo ya utafiti katika uhakiki wa kiekolojia ni dhihirisho la kuwepo na nyanja nyingi ndani ya ekolojia yenyewe. Hivyo, kukubalika kwa mitazamo tofauti ya kiutafiti si ishara ya ushindani miongoni mwa wahakiki wa kiekolojia bali ni hali ya kudhamini suala la ekolojia kuwa kiini ndani ya kazi za kifasihi. Maoni ya Quick (keshatajwa) kuhusu uhakiki wa kiekolojia yanaafikiana na yale ya Alia (2017) anayedai kwamba, uwiano kati ya fasihi, utamaduni na ekolojia unaahidi si tu kuchangia katika uboreshaji wa kimwingilianotaaluma katika

taaluma inayohusika, bali pia kuwezesha muda mrefu zaidi wa mitazamo ya ubunifu inayovuka mipaka ya mwelekeo mmoja wa uhakiki. Kufanya hivyo kutasaidia katika kutathmini upya umuhimu wa masomo ya kitamaduni na yale ya kifasihi yenye mabishano mengi ndani ya jamii ya sasa pamoja na utambuzi wa umma.

Kwa mujibu wa Catrine na Sylvia (2006), juhudi za kuunganisha uhakiki wa kiekolojia na sayansi pia zimethibitika kufaulu, ambapo wataalamu wa kihistoria wanachunguza uhusiano uliopo baina ya sayansi ya asili ya karne ya tisini na waandishi kama vile Henry David, Thoreau na Thomas Hardy. Isitoshe, hivi karibuni wahakiki wa kiekolojia wa Marekani wameongeza umakini katika suala la `Fasihi ya haki ya Kimazingira`ambapo waandishi wa Kirumi wa Magharibi ya Kusini na wazawa wa Marekani kutoka maeneo mengi ni maarufu.

Heise (2008), anaeleza kuwa ekolojia hutazama jinsi mifumo mbalimbali ya kimazingira inavyofanya kazi ili kukidhi maisha na jinsi mifumo hii inavyoharibiwa na kusababisha vifo vya mimea na wanyama. Anaendelea kusema kuwa ekolojia imo katika hatari ya maangamizi kutokana na matendo ya binadamu. Matendo kama vile: ukataji wa miti, ujenzi wa nyumba katika mahali oevu, kuongezeka kwa teknolojia haribifu za kisasa pamoja na ukosefu wa uongozi mwafaka katika masuala ya ekolojia yamesababisha mitandao ya viungahai kudhoofika. Matokeo ya matendo haya ni kuongezeka kwa viwango vya joto, magonjwa kuzidi, vifo kukithiri na mazao katika jamii kupungua na kusababisha njaa. Athari hizi zinatatiza maisha ya binadamu na maendeleo endelevu. Mtazamo huu uliongoza utafiti huu katika kuangazia athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matendo ya binadamu katika shughuli zao za kila siku, kama zinavyodhihirika katika matini zilizoteuliwa katika utafiti huu.

Kwa mujibu wa Culler (2011), uhakiki wa kiekolojia unahusu usawiri wa mazingira katika fasihi na mabadiliko katika maadili kuhusiana nayo, hasa kuhamasisha wanajamii kuhusu kubadilisha mielekeo na mienende yao kuhusu mazingira. Maelezo ya Culler (keshatajwa) yanaafikiana na yale ya Buell (2005) kuwa kazi za kimazingira ni lazima zionyeshe mambo ambayo husababisha madhara makubwa kwa jamii na kuonyesha njia mbadala za kuponya jamii. Kutokana na maelezo hayo, utafiti huu

ulitathmini nafasi ya tamthilia ya Kiswahili katika kutatua matatizo ya kimazingira kwa mujibu wa tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege.

Mulokozi (2017) anaeleza kuwa uhakiki wa kiekolojia ni mkabala wa uchambuzi wa kazi za fasihi ambao huchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na mazingira. Hivyo, mkabala wa kiekolojia katika uchambuzi wa kazi za fasihi huchukulia mazingira kama suala la msingi katika uhakiki wake. Kutokana na mhimili huu, mtafiti alihakiki matini teule za fasihi ya Kiswahili kwa kuangazia uhusiano uliopo baina ya mazingira na matini hizo, kwa kuchukulia masuala ya kimazingira kama ya msingi. Kwa kuongozwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, mtafiti alichunguza kwa kina athari za uhusiano baina ya binadamu na mazingira katika matini teule.

Kutokana mitazamo mbalimbali kuhusu nadharia ya uhakiki wa kielekolojia, mihimili ifuatayo inajitokeza:

i. Binadamu, mazingira na viumbe wengine huhusiana kwa namna ya kutegemeana na kukamilishana.
ii. Utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana.
iii. Mwanadamu anasababisha uchafuzi wa mazingira kupitia vitendo vyake licha ya kufaidika kutokana na mazingira hayo.
iv. Uhakiki wa kiekolojia unahusu uhamasishaji wa wanajamii kuhusu kubadilisha mielekeo na mienendo yao kuhusu mazingira.
v. Kazi za kimazingira lazima zionyeshe njia mbadala za kuponya jamii kutokana na athari za uharibifu wa mazingira.

Mhimili wa kwanza ulitumika katika kuonyesha jinsi ambavyo binadamu, mazingira na viumbehai wengine hutegemeana na kukamilishana hivi kwamba, uharibifu wa mazingira unaweza kuathiri mfumo wote wa ekolojia hasa kwa sababu ya mahusiano haya. Mhimili wa pili nao ulitumika katika kuonyesha jinsi ambavyo shughuli za kitamaduni za binadamu kama vile matambiko yanahusiana na ulimwengu halisi ambamo binadamu anaishi. Kwa hivyo, mhimili huu ulitumika kuchunguza jinsi ambavyo baadhi ya shughuli za kitamaduni za binadamu zilikusudiwa kuhifadhi mazingira yake.

Kadhalika, mhimili wa tatu ulikuwa muhimu katika kuangazia jinsi ambavyo shughuli za binadamu kama vile ukataji wa miti, utupaji ovyo wa taka, uendeshaji wa magari na ujenzi wa viwanda unasababisha uharibifu wa mazingira. Uharibifu huu huathiri binadamu, mimea pamoja na viumbehai wengine. Katika kuangazia mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira, mhimili wa nne na wa tano ulitumika. Hivyo, mihimili hii ilisaidia katika kuangazia dhima ya tamthilia teule kama kazi za kimazingira ambazo zilikusudia kuhamasisha jamii kuhusu mielekeo na mienendo yao kuhusu mazingira. Vilevile, kutathmini njia mbadala za kukomboa mazingira yaliyoharibiwa hasa kutokana na vitendo vya binadamu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliangazia mbinu za utafiti zilizotumiwa kwa lengo la kudhihirisha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Hatimaye, mtafiti alitoa maelezo kuhusu maadili ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Ulihusisha uhakiki wa tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Maktaba iliyotumika kufanyia utafiti huu ni ile ya Chuo Kikuu cha Chuka. Mtafiti alisoma kwa kina tamthilia teule ambazo ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009), *Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). Pamoja na usomaji wa tamthilia teule, mtafiti alisoma vitabu na matini mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti ili kupata uelewa wa kina kuhusu mada. Matini hizi pia zilimwezesha mtafiti kupanua maarifa na uelewa wake kuhusu masuala ya kimazingira kama vile chanzo cha uharibifu wa mazingira, athari za uharibifu huo pamoja na jinsi ya kuyahifadhi mazingira. Vilevile, mtafiti alisoma na kuaua tasnifu, makala, majarida na maandishi mengine yaliyohusiana na masuala ya mazingira pamoja na misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu mtandaoni.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulichanganua tamthilia za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege zinazosawiri suala la mazingira. Hivyo, uteuzi wa kimakusudi ulitumika kuteua *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*), Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). Tamthilia hizo zilipatikana kwa kuteua na kusoma tamthilia mbalimbali zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Baada ya kusoma, mtafiti alibaini kuwa watunzi hawa wameonyesha uhamaji wa kimakusudi wa kimaudhui na mtindo katika tamthilia hizo teule. Hivyo, aliteua tamthilia zilizokuwa na upekee wa maudhui na mtindo ambao ulibainisha motifu za kimazingira; suala ambalo lilichunguzwa katika utafiti huu. Tamthilia teule ziliwezesha kutimiza malengo ya utafiti huu ambayo yalikuwa kuchunguza jinsi motifu za kimazingira zinavyosawiriwa katika tamthilia teule, kujadili jinsi mtindo ulivyotumika kusawiri motifu za kimazingira katika tamthilia teule na kutathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

### 3.4 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulihusisha kwa kiasi kikubwa data za msingi kutokana na usomaji wa matini teule. Vitabu teule katika utafiti huu vilisomwa kwa kina ili kupata data iliyotegemewa. Tamthilia zilizoteuliwa katika utafiti huu ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*), Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015), ambazo zilichunguzwa ili kupata data katika vigezo vya maudhui na fani. Katika kigezo cha maudhui, masuala yaliyochunguzwa ni usawiri wa motifu mbalimbali za kimazingira pamoja na kutathmini mchango wa motifu hizo katika uhifadhi wa mazingira. Kuhusiana na kigezo cha fani, data ilipatikana kwa kubainisha na kujadili mitindo iliyotumiwa na watunzi wa tamthilia teule katika usawiri wa motifu za kimazingira kama vile taswira na jazanda. Kwa hivyo, data ilikusanywa kuambatana na maswali ya utafiti.

### 3.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyopatikana kupitia kusoma *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*), Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015) ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti.

Maneno, sentensi na aya ambazo zilikuwa na ujumbe kuhusiana na madhumuni ya utafiti ziliangaziwa na kisha kunukuliwa na kuchanganuliwa. Baadaye, maelezo ya kina yalitolewa ili kujibu maswali maalumu ya utafiti. Mtafiti aliongozwa na mihimili mikuu ya nadharia ya uhakiki wa kiekolojia katika kuchanganua data. Data iligawanywa katika makundi matatu kwa kuzingatia madhumuni matatu ya utafiti huu. Kundi la kwanza liliangazia usawiri wa motifu za kimazingira kwa mujibu wa tamthilia teule. Hivyo, motifu mbalimbali za kimazingira zilibainishwa pamoja na kuchunguza jinsi waandishi wa tamthilia teule walivyozisawiri. Kundi la pili lilibainisha na kujadili jinsi mtindo ulivyotumika katika kusawiri motifu za mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule. Katika kufanya hivyo, mtafiti alibainisha mbinu za lugha mbalimbali zilizotumika na kufafanua jinsi zilivyofanikisha usawiri wa motifu za kimazingira. Kundi la tatu nalo lilitathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira. Hivyo, mtafiti alichunguza masuala yaliyoonyesha juhudi za uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

### 3.6 Uwasilishaji wa Data

Utafiti huu ulizingatia uwasilishaji wa kimaelezo wa data iliyokusanywa na kuchanganuliwa kuhusiana na motifu za kimazingira katika tamthilia ya Kiswahili. Baada ya kuhakiki matini teule, mtafiti alitoa uamuzi wake kuhusiana na motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia. Hivyo, alijikita katika usawiri wa motifu za kimazingira, mitindo mbalimbali katika usawiri wa motifu za kimazingira na mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

### 3.7 Maadili ya Utafiti

Ili kuhakisha kuwa utafiti huu ulizingatia suala la maadili, mtafiti aliomba idhini ya kufanya utafiti wake kutoka Chuo Kikuu cha Chuka na kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Aidha, mtafiti alihakikisha kuwa data aliyotoa ilikuwa ya kweli na iliongozwa na madhumuni ya utafiti. Vilevile, data iliyokusanywa ilitokana na kazi zilizoteuliwa; ambazo zilisomwa kwa makini na kuchanganuliwa kwa mtazamo wa uhakiki wa kiekolojia. Zaidi ya hayo, mawazo ya wasomi wengine yaliyorejelewa katika kazi hii yalinukuliwa ipasavyo ili kuepukana na suala la wizi wa mawazo.

# SURA YA NNE

# USAWIRI WA MOTIFU ZA KIMAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE

## 4.1 Utangulizi

Madhumuni ya kwanza katika utafiti huu yalikuwa kuchunguza jinsi motifu za kimazingira zinavyosawiriwa katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Tamthilia zilizochanganuliwa ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*), Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). Usawiri wa motifu za kimazingira ulifafanuliwa kwa kuchunguza mtazamo wa watunzi wa tamthilia hizo kuhusu mazingira kwa kuangazia motifu mbalimbali zinazojitokeza na namna zilivyosawiriwa. Vipengele vya motifu vilivyozingatiwa ni motifu ya maji, motifu ya magonjwa, motifu ya ukame, motifu ya njaa na motifu ya kifo.

## 4.2 Motifu ya Maji

Kwa mujibu wa Maganga (2019), mwanadamu, wanyama, mimea na ndege kwa ujumla huhitaji maji katika maisha yao ya kila siku. Aidha, anaeleza umuhimu wa maji kama vile kutumika katika kutibu magonjwa mengi pakiwemo msongo wa mawazo na ugonjwa wa kisukari, kutumika kupikia, kulimia, kusafishia pamoja na kutumika kama makazi ya wanyama wengine wa majini na viumbe hai mbalimbali waishio majini. Motifu ya maji ni kipengele kilichojitokeza katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege kama njia ya watunzi hawa ya kueleza kiubunifu umuhimu wa maji katika jamii, chanzo cha uhaba wa maji na vilevile athari za uhaba wa maji.

### 4.2.1 Umuhimu wa Maji

Maji yamesawiriwa na watunzi wa tamthilia teule kama kiungo muhimu katika maisha ya kila siku. Kutokana na mazungumzo ya wahusika katika tamthilia hizo, ni wazi kwamba bila maji ni muhali uhai kupatikana. Katika *Majira ya Utasa*, umuhimu wa maji unadhihirika kupitia mfano ufuatao:

> Mbawazi: Naona basi tutakuja kuangamizwa na hii njaa. Ardhi tunayo lakini kumbe *haizai bila maji.*
> Bi Siwa: Kila kitu hutegemea maji mama. *Maji ni uhai.*
> Mbawazi: Naona hali hii ikiendelea tutakuja kufa na kuwa karamu ya tai na fisi (Uk 6)

Mazungumzo baina ya wahusika Mbawazi na Bi Siwa yanaonyesha kuwa maji ni uhai kwa sababu kila kitu kinayategemea. Kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa*, ardhi yao haizai kutokana na ukosefu wa mvua. Hii ndio maana Mbawazi anasema kuwa wao wana ardhi lakini haizai bila maji. Matokeo ya kukosekana mvua ni kiangazi na njaa, hali inayosababisha vifo vya binadamu na viumbe hai wengine. Majanga haya yanatokana na kile Njiru (2015) anachoita `udhalimu wa mazingira`, ambapo binadamu wamechangia katika ukosefu wa mvua kupitia baadhi ya vitendo vyao kama vile ufwekaji wa misitu. Kadhalika, mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* anasawiri maji kuwa kitu muhimu na kitakatifu kuliko kitu kingine chochote. Katika mfano ufuatao, mhusika Mwendawazimu anasema:

> Mwendawazimu: Pamoja na hayo, nadhani tumekuwa tukimkariri Kinjeketile bila kumfahamu. Tumekuwa tukimkariri na kukejeli *maji yake ya uhai* bila kufahamu maneno yake… Hebu tujiulize tunajua maana ya ndani ya maji ya uhai aliyopendekeza Kinjeketile? pia katika *Vita vya Majimaji,* maji yalikusudiwa *kuchochea haja ya kuvinjari* hata kama kuna kifo mbele ya wanaoonewa. Hata kama kifo kinawakabili (Uk 4-5)

Kupitia nukuu hili, Mwendawazimu anasema kwamba kauli ya Kinjeketile ni fumbo linalotilia mkazo umuhimu na utakatifu wa maji. Akisisitiza kuhusu umuhimu wa maji, Mwendawazimu anarejelea muktadha wa *vita vya Majimaji* kwa kusema kuwa maji yalikusudiwa kuchochea haja ya kujithamini na kujiamini hata kama kifo kiliwakabili

waliohusika. Kando na utakatifu wa maji, mfano uliotolewa pia unayasawiri maji kuwa na manufaa katika kuwapa watu matumaini na ujasiri. Licha ya maji kusawiriwa kuwa chanzo cha uhai, mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* anaangazia hali ambapo binadamu amevunja miiko na itikadi zilizolenga kuhifadhi maji. Matokeo ya ukaidi wa binadamu ni kukauka kwa maji kwenye visima, hali ambayo imesababisha madhara mengi. Hali hii inathibitishwa na utafiti wa Kisanji (2013) kuhusu uhusiano baina ya miiko na mazingira katika jamii ya Wabungu, Tanzania. Alibaini kuwa uvunjaji wa baadhi ya miiko katika jamii ulisababisha ukaukaji wa maji katika mito na kwenye chemichemi na hata mvua kukosa kunyesha. Hivyo, mwandishi wa tamthilia hii anasisitiza haja ya watu kuzingatia utamaduni wa jamii. Hii ni kwa sababu utamaduni wa jamii na mazingira uhusiana na kuathiriana moja kwa moja (Glotfelty, 1996).

Aidha, umuhimu wa maji katika kuwapa watu ujasiri unadhihirika katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ambapo maji ya kisima yanawapa watu ujasiri wa kuzungumza hadharani. Wao walikuwa wamenyamaza kimya kwa miaka mingi huku wakiangamia kutokana na majanga mengi yaliyowakabili likiwemo tatizo la ukosefu, njaa na maradhi. Mpya anathibitisha haya kwa kusema:

> Mpya: Nitazameni mimi mtoto wa Afrika. Mimi ninayeshika kiamo kilichosafishwa kwa moshi wa vifuu. Kiamo cha *kutekea maji ya ujasiri*. Hili ndilo tambiko letu. Tambiko la uhai wa nchi zetu. *Tambiko la kusema ukweli bila ya kuhofu wala kuogopa*. Tazameni wananchi, *nakunywa maji ya ujasiri* kwa niaba yangu na niaba yenu. Tazameni nikisafisha hofu na woga wangu na natumai woga wenu pia. (Uk 23)

Mhusika Mpya ni binti ya Bw. Binafsi na Bi. Shoo ambaye anawakilisha kizazi kipya kinachofundishwa kutatua matatizo kwa kutumia masikio na midomo yao. Kutokana na maneno yake, tambiko la kuyanywa maji ya ujasiri linawapa watu uwezo wa kusema ukweli bila hofu. Aidha, Mpya anawakumbusha wananchi kuwa anakunywa maji hayo kwa niaba yake na wao. Hii ina maana kwamba wakati umefika wa kuyatilia maanani baadhi ya mambo ya jadi yaliyokuwa na manufaa kama vile matambiko. Kama anavyoeleza Glotfelty (1996), utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana. Hivyo, utamaduni kuhusu matambiko ni jambo lililokuwa na umuhimu wake katika jamii iliyoangaziwa na mtunzi wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*. Vilevile, inadhihirika kwamba, dhima iliyojikita katika matambiko yaliyohusisha maji

yalilenga kulinda na kutunza mazingira na maliasili. Ndiposa mwandishi anahimiza umuhimu wa kuyatunza mazingira ili kuzuia ukaukaji wa maji ambayo yalitumiwa katika shughuli muhimu za kijamii kama vile matambiko.

Maji ni maliasili ya nchi ambayo yanastahili kumfaidi kila mwananchi. Hata hivyo, baadhi ya viongozi wanachangia katika kuharibu vyanzo vya maji kwa sababu za kibinafsi. Katika *Janga la Werevu*, Busara anasema:

> Busara: Eeh, Baba! Ikiwa watu hawana maji hata ya kunywa tunadhani watakubali maji yawe yetu peke yetu? *Maji ni maliasili ya nchi hii. Ni mali ya wananchi* kwa sababu tofauti na shaba na dhahabu, *maji ni uhai wao*. Wakikosa maji hawana uhai. Lakini wengi hatuna dhahabu lakini tunaishi. Kila mwananchi anastahiki kufaidika na maji hata kama hawana pesa. Hata kama mtu mwingine atatoa gharama za kuhudumia kazi ya kuweka mabomba. (Uk 28)

Busara ni binti ya Bamkuu na Bimkuu aliye katika chuo kikuu. Anawakosoa wazazi wake wanapodai kuwa wao wana haki ya kutumia maji watakavvyo kwani yanatokana na visima walivyochimba kwa kutumia pesa zao wenyewe. Kwa mujibu wa Wirth (1945), katika jamii yoyote ile, mamlaka yote yamo mikononi mwa wachache ambao huamua vipi, lini na ni nani anafaa kufaidika kutokana na rasilimali. Ndiposa Busara anawakumbusha wazazi wake kuwa maji ni hazina ya uhai wa kila mja, kwa hivyo wananchi wote wana haki ya kuyafaidi. Kama inavyodhihirishwa na Waweru (2019), Machi 22 ni siku maalum ya kimataifa iliyotengwa ili kuadhimisha umuhimu wa maji duniani kila mwaka. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa muungano wa kimataifa (UN) ndio mwasisi wa siku hii malengo yake yakiwa kuangazia kuwepo kwa maji safi. Vilevile, siku hii inatumika katika kuhamasisha watu kuhusu haja ya kulinda vyanzo vya maliasili hii muhimu.

Kando na maji kuwa muhimu katika maisha ya binadamu, wanyama pamoja na mimea, tamthilia ya *Janga la Werevu* inathibitisha kuwa hata vifaa vingine vitumiwavyo na binadamu vinahitaji maji ili kutekeleza shughuli inayokusudiwa ipasavyo. Dondoo zifuatazo zinashadidia:

Busara: Hallo, hallo!... Tuna mgonjwa mahututi. Enh! Gari la wagonjwa halina maji kwenye *redieta*? Sasa si muweke maji kwenye hilo *redieta* tu… Ala! Mnasema hamna hata tone moja la maji? (Uk 34)

Busara: Mnaona? *Hata gari huhitaji maji. Hata ndege, hata roketi, hata roboti*. Tazameni, *maji yamekuwa adimu na ghali kuliko petrol*? Magari yetu sisi lakini yana petrol na maji pia. Haya, haraka tumbebe Kristy tumtie garini mwetu, tumpeleke hospitali…haraka. Labda tukio hilo la ugonjwa wa Kristy ndilo lililoleta kitendawili cha maji tunachotegewa. Ndilo fumbo tunalotakiwa kulifumbua kama lile fumbo la uhai wa maji. (Uk34)

Nukuu hizi ni ushahidi fika kuwa uhaba wa maji katika jamii iliyosawiriwa na mtunzi wa *Janga la Werevu* umeathiri kila pembe ya nchi. Kwa mujibu wa Nabeta na Ongutte (2014), nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inadokeza kwamba kila binadamu ameathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira bila kujali tabaka, mifumo ya kiuchumi na mielekeo ya kisiasa au ya kitaaluma. Hii ndio maana Busara anapopiga simu hospitalini ili wapate msaada wa gari la wagonjwa wakati dadake Kristy anaugua, anaaarifiwa kuwa gari hilo halina maji, kumaanisha kwamba hata hospitalini kuna uhaba wa maji. Hivyo, Busara anaposema kwamba hata gari, ndege, roketi na roboti huhitaji maji, anasisitiza kuhusu umuhimu wa maji katika kila shughuli, ambapo kila binadamu ameathiriwa na uhaba wake. Kuongezeka kwa matumizi ya maji kunadhibitishwa na habari za Umoja wa Mataifa (UN, 2020) kwa kueleza kuwa matumizi ya maji yameongezeka mara sita katika karne iliyopita na kwamba yanaongezeka kwa kiwango cha asilimia moja kila mwaka. Hivyo, ni muhimu kuongeza uwekezaji katika vyanzo vya maji na miundombinu ya maji yenye afya na kuboresha ufanisi wa matumizi yake.

### 4.2.2 Chanzo cha Uhaba wa Maji

Kwa mujibu wa Marshall (2011), watu wanaoishi nchini Kenya ni takriban milioni arobaini. Idadi ya watu milioni kumi na saba ya watu hawa hawapati maji safi. Kadhalika, anasema kuwa suala la uhaba wa maji kwa muda mrefu nchini Kenya limesababishwa na hali ya kiangazi cha mara kwa mara, usimamizi mbovu wa usambazaji wa maji, uchafuzi wa maji yanayopatikana na kuongezeka kwa mahitaji ya maji kunakotokana na ongezeko la idadi ya watu. Katika tamthilia teule, mambo

mbalimbali yamejitokeza kuwa chanzo cha kukosekana kwa maji. Mambo hayo ni pamoja na uongozi mbaya, ukataji miti, na ubadilishaji wa mikondo ya maji.

#### 4.2.2.1 Uongozi Mbaya

Watunzi wa tamthilia teule wamesawiri hali halisi ya uhaba wa maji katika jamii kwa kuonyesha chanzo cha kukosekana kwa maji. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mbinu mbovu za utawala wa Meya wa jiji la Cheneo unasababisha kukosekana kwa maji Cheneo nzima. Mfano ufuatao unashadidia:

> Siki: Hali ikibadilika mshahara nao utakuja…
> Waridi: Kama itabadilika si hivi karibuni. Sitaki kufanya kazi isiyoninufaisha mimi au watu wengine. Mwenyewe unaona *hospitali ilivyo chafu. Hakuna maji ya kutosha*. umetwaliwa na nzi. Ni hatari hata kwetu sisi. (Uk 36)

Mazungumzo baina ya daktari Siki na Waridi yanadhihirisha kwamba hali ni mbaya katika mji wa Cheneo chini ya uongozi wa Mstahiki Meya. Kutokana na hali mbaya ya mazingira ya kufanyia kazi, wafanyikazi wanashindwa kuvumilia. Hii ndio maana Waridi ambaye ni nesi katika zahanati mojawapo katika Cheneo, anamwambia Siki kuwa hawezi kuendelea kufanya kazi isiyomnufaisha yeye wala watu wengine. Kando na kulipwa mishahara duni, hakuna vitu vingi vya kimsingi hospitalini kama vile maji na dawa. Ndiposa Waridi anakiri kuwa hospitali ni chafu kwa sababu ya uhaba wa maji, hali inayohatarisha maisha ya wagonjwa na wafanyikazi. Athari za uongozi mbaya zinazosawiriwa na mtunzi wa *Mstahiki Meya* zinaafikiana na matokeo ya utafiti wa Sangili (2015) yaliyobaini kuwa, viongozi ndio wahusika wakuu katika kusababisha uharibifu wa mazingira. Haya hutokana na ufisadi, ubinafsi na unyakuzi wa ardhi ya umma miongoni mwa mambo mengine.

Hata ingawa ufahari na ubadhirifu wa viongozi ni mojawapo wa chanzo cha majanga yanayokabili jamii, viongozi wanaofaidika kutokana na rasilimali za umma wanaikana hali inayokabili watu na kukataa kwamba kuna balaa. Mwandishi wa *Janga la Werevu* anaangazia hali hii kupitia Mwendawazimu anayesema:

> Mwendawazimu: Naam, sasa balaa zote hizo zinaonekana waziwazi. Tunaziona kwa macho yetu. Hatuna haja kuzifasiri kwa kubahatisha. Hakuna haja ya

> kuzipigia ramli ili tuzione. Balaa zimeenea**.** *Lakini wenye kufaidika bado wanakataa kwamba kuna balaa. Wanafumba macho na kuziba masikio. Wanaamua kuukimbia ukweli. Wanaikana historia na majilio yake. wanaepuka majukumu yao***.** Wanapinga maneno matakatifu yenye msingi wa kuishi na kuwepo. (Uk 10)

Viongozi wanaosawiriwa katika dondoo hili ni wale wasiojali masilahi ya wananchi. Kama anavyosema Slovic (2008), uhakiki wa kiekolojia hauwezi kutenganishwa na masuala ya kisiasa pamoja na uhalisia wa mambo mengineyo kote ulimwenguni. Hii ni kwa sababu lugha, fasihi, mawazo na asili bila shaka huingiliana. Ili kufichua maovu yanayotendwa na viongozi kutokana na unafiki wao, mhusika Mwendawazimu anasema kwamba watu wachache katika jamii wanaofaidika na rasilimali za umma, wanafumba macho na kuziba masikio huku wakiukimbia ukweli na uhalisia wa balaa iliyopo inayosababishwa na uharibifu wa mazingira. Hivyo, wanaepuka majukumu yao ya kuwashughulikia wananchi waliowachagua. Kutokana na mfano huu, imebainika kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* anawakashifu viongozi wabadhirifu ambao hawajali madhara ya vitendo vyao kwa wananchi waliowachagua. Kama inavyodokezwa na ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN, 2006), watu bilioni moja nukta moja duniani wanakosa maji safi ya kunywa na wengine bilioni mbili nukta sita hawana njia ya kujipatia hata maji ya kujisafisha. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, matatizo hayo yanasababishwa na utawala mbaya, rushwa na ukosefu wa vitega uchumi. Hivyo, ni dhahiri kuwa utawala mbaya kama unavyosawiriwa na watunzi wa tamthilia teule unaweza kuwa chanzo cha uhaba wa maji.

#### 4.2.2.2 Ukataji wa Miti

Watunzi wa tamthilia teule wamebaini kuwa ukataji wa miti ni chanzo kikuu cha kukosekana kwa maji. Ukataji wa miti unaobainika katika tamthilia hizi unaendelezwa ama na viongozi au watu wachache walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi katika jamii zinazohusika. Katika *Janga la Werevu*, mfano ufuatao unathibitisha:

> Bamkuu: Look! Tazama ukurasa wa tatu wa gazeti la *Mazingira*… Wanasema watachukua ardhi, mashamba na viwanja

vyetu vyote vya *Msitu wa Uma* bila ya fidia. Kosa letu ni lipi lakini?

Bimkuu: Kwani kuna kosa? Si basi tu. Eti *wanasingizia kukatwa miti ndio chanzo cha kukauka maji!* Wanasahau kwamba *tulifyeka msitu kwa jasho letu na gharama zetu* kwa maslahi ya nchi hii. Tukaanzisha mashamba makubwa ya chai, pareto na kahawa na kutoa ajira kwa wafanyakazi. Tukazalisha vyakula na mazao ya biashara. Kuna ubaya gani? … (Uk 26)

Katika mfano uliotolewa, Bamkuu anashangazwa na habari katika gazeti la *Mazingira*. Kwa mujibu wa gazeti hilo, inasemekana kuwa ardhi, mashamba na viwanja vyao vyote vya msitu wa uma vingetwaliwa bila ya fidia. Aidha, Bimkuu anadai kuwa wao walifyeka misitu hiyo kwa maslahi ya nchi yao. Hii ni kwa sababu baada ya kuanzisha mashamba makubwa walizalisha vyakula na mazao ya biashara pamoja na kutoa ajira kwa wafanyakazi. Kutokana na mazungumzo hayo, ni dhahiri kuwa kukosekana kwa maji kumesababishwa na ukataji wa miti kiholela kwa manufaa ya kibinafsi. Kwa mujibu wa Bookchim (2007), binadamu wamekuwa na uwezo wa kudumisha uhusiano wa amani kati yao na mazingira ya asili. Hata hivyo, wamefanya kinyume ambapo hatua kwa hatua wameharibu kile ambacho kingekuwa umoja wa kipekee kati yao na mazingira. Kinachodhihirika hapa ni kwamba, licha ya binadamu kuwa na uwezo wa kuhifadhi mazingira ili kuzuia madhara yanayotokana na uharibifu wake, vitendo kama vile ukataji wa miti vimechangia katika kuzorotesha hali ya mazingira ambamo binadamu anaishi.

Katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, wahusika mbalimbali wanakutana ili kuzungumzia matatizo yanayowakabili. Baada ya kunyamaza kimya kwa muda mrefu tangu kupata uhuru, wengi wao wameanza kuzungumza kwa ujasiri ili kutetea maslahi yao. Katika mfano ufuatao, Bi. Subira anasema:

Bi. Subira: Mchakato ndio huu uliotuleta hapa. Huwezi kujikomboa kama husemi. Lazima useme. Siku hizi hapa petu watu wanafanya wapendavyo. *Miti inakatwa ovyo*, watu wanajenga nyumba au makazi bila ya vibali. Ardhi na viwanja vya watu vinachukuliwa kwa nguvu. Watu wanachafua mazingira kila eneo. (Uk 59)

Miongoni mwa matatizo yanayowakabili watu katika jamii iliyosawiriwa ni uchafuzi wa mazingira kama inavyodokezwa na Bi. Subira. Aidha, anatambua kuwa ukataji ovyo wa miti umechangia katika baadhi ya matatizo yanayowakumba. Haya yote yanatokana na tamaa na ubinafsi wa kiongozi mkuu Bw. Binafsi ambaye hayajali maslahi ya walio wengi katika jamii. Kama juhudi za kuepuka athari za uharibifu wa mazingira zinazotokana na ubinafsi, Alia (2017) anasema kwamba `tumejipoteza wenyewe kwa kuchagua ubinafsi juu ya kila kitu kinachotuzingira`. Utambuzi huu ni hali ya upatanisho wa mtu binafsi na mazingira yake. Hivyo, huu ni wito wa kuacha ubinafsi miongoni mwa wanajamii hasa viongozi ili kuokoa mazingira yaliyoharibiwa, kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*. Kadhalika, tamthilia ya *Majira ya Utasa* inasisitiza ukataji wa miti kuwa chanzo cha ukosefu wa maji kama inavyojitokeza katika mazungumzo yafuatayo:

> Bi Siwa: Majuzi ilikuwa habari tofauti na hii. Sasa tuiamini gani?
> Siwa: Kwani ilikuwa habari gani?
> Bi Siwa: Kwamba *uhaba wa maji umetokana na misitu kukatwa kiholela* na chemchemi za maji kuharibiwa…
> Siwa: Aliyepinga hilo nani? Uyasemayo wewe yamekuwa yakisemwa kwa muda sasa. Na kwa kweli si siri tena. Yote yalianza kwa wenyewe hao *kujigawia ardhi ambayo ilikuwa mwiko watu kujitwalia***.** Mengine haya yamefuatia baadaye. (Uk 25)

Haya ni mazungumzo baina ya Siwa na mke wake Bi Siwa. Wanazungumza kuhusu hali inayowakabili katika jamii hasa uhaba wa maji baharini na chanzo cha kutonyesha kwa mvua. Kutokana na maneno ya Bi Siwa, ni wazi kwamba hali hiyo inazungumziwa na wanajamii wengi ili kutafuta suluhu la tatizo hilo. Hii ndio maana baadhi ya wanajamii washatambua kuwa ukataji wa misitu ni mojawapo ya chanzo cha ukosefu wa mvua kwani miti ni chemchemi za maji. Kwa upande wake, Siwa anamuunga mkewe mkono kwa kusisitiza kuwa matatizo ya kimazingira yalianza wakati viongozi walipoanza kujigawia ardhi ambayo ilikuwa mwiko watu kujitwalia.

Kwa mujibu wa Alia (2017), Uhakiki wa kiekolojia humpa mtu nafasi ya kuelewa utamaduni wa asili na mazoea yao ili kulinda urithi wa asili na ule wa mababu zao. Hii inadokeza kwamba, iwapo yeyote ataenda kinyume na sheria ya ardhi

iliyotengwa, basi yeye pamoja na jamii nzima itaadhibiwa na asili. Katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi, viongozi wameenda kinyume na sheria ya kutojigawia ardhi iliyokuwa na mwiko. Kutokana na kitendo hiki, jamii nzima imeadhibiwa kupitia mvua kutonyesha, jambo ambalo limesababisha uhaba wa maji.

Hali ya uharibifu wa mazingira kupitia vitendo vya binadamu inasisitizwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inayodokeza kuwa, kando na kufaidika kutokana na mazingira, mwanadamu anachangia katika uchafuzi wa mchanga, hewa na maji (Rigby, 2002). Hali hii inahatarisha maisha ya binadamu pamoja na viumbehai wengine. Kadhalika, jambo hili linathibitishwa na Matheka (2018) anayesema kuwa wataalamu wa mazingira wanaonya kwamba, ukataji wa miti kiholela hasa nchini Kenya kunaangamiza misitu, kukausha vyanzo vya maji na kuathiri hali ya hewa. Hivyo, ni muhimu mazingira kulindwa ili kuepuka majanga zaidi yanayotokana na uharibifu wa mazingira, hasa ukataji wa miti.

#### 4.2.2.3 Ubadilishaji wa Mikondo ya Maji

Tamaa na ubinafsi wa baadhi ya viongozi katika jamii unasababisha ubadilishaji wa mikondo ya maji huku wakiyaelekeza katika mashamba yao. Matokeo ni uhaba wa maji unaoathiri kila mwanajamii pamoja na viumbe wengine. Katika tamthilia ya *Janga la Werevu*, mfano ufuatao unashadidia:

> Busara: Nasi tumekaa tutwe tu, tukifisidi, tukidhulumu mazingira, tukilaumu wengine na kuibia umma hadharani. Mbona maharamia, *Developers na Real Estates Developer* wanaochipuka na kuangusha miti na kufyeka misitu na *kugeuza safari za mikondo ya maji* huku wakijenga majumba marefu marefu na viwanda vinavyotiririsha uchafu kwa mikondo hiyo ya maji. (Uk 33)

Kutokana na maneno ya Busara, ni dhahiri kuwa kuna baadhi ya wanajamii wanaobadili mikondo ya maji huku wakiwanyima watu wengine nafasi ya kuyafaidi. Licha ya kuwa maji ni maliasili ya umma, ni wazi kwamba watu hasa walio na ushawishi mkubwa katika jamii wanashiriki katika unyakuzi wa ardhi ya umma pakiwemo sehemu za misitu. Baada ya kufyeka misitu hiyo wanabadili mikondo ya maji ili kuyaelekeza katika mashamba yao, kama wanavyofanya Bamkubwa na Bimkubwa. Kadhalika,

tamthilia ya *Majira ya Utasa* inaangazia hali ambapo watu wenye ushawishi mkubwa kama vile Jumbe wanabadili mikondo ya maji hadi katika mashamba yao. Mazungumzo yafuatayo baina ya Siwa na Bi Siwa yanathibithisha:

> Bi Siwa: Hata nasikia baadhi ya watu wakisema kiwango cha maji huko baharini kiko chini sana. Hata wanasema eti uhaba wa maji umesababishwa na akina Jumbe…
>
> Siwa: Uyasemayo ni kweli. Lakini ni zaidi ya hivyo. Jumbe ni unyoya tu. *Wapo vigogo haswa ambao wamebadili mikondo ya maji hadi mashambani mwao* na kutunyima sisi haki ya kupata kuyafaidi. (Uk 24-25)

Mazungumzo haya yanathibitisha kuwa kiwango cha maji baharini kiko chini sana. Vilevile, imebainika kuwa si Jumbe tu aliyesababisha uhaba wa maji bali wapo `vigogo` ambao wamebadili mikondo ya maji hadi mashambani mwao. Siwa anapotaja `vigogo` anawarejelea watu wanaotambulika katika jamii na walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi. Kwa mfano, mhusika Jumbe anamiliki viwanda vya maua ambapo amewaajiri wafanyikazi wengi. Aidha, mahali palipo na viwanda palikuwa ni msitu wa umma uliofyekwa. Vilevile, maji yanayotumiwa kwenye viwanda hivyo yametokana na ubadilishaji wa mikondo ya maji na kuyaelekeza kwake bila kuwajali watu wengine. Akieleza kuhusu nafasi ya uhakiki wa kiekolojia, Njiru (2015) anasema kuwa, kuunganisha uhakiki wa kimazingira na haki ya kimazingira huwawezesha wasomi kuchunguza jinsi ambavyo makundi yaliyotengwa yanatishiwa na uchafuzi wa mazingira, siasa na ubaguzi wa kimazingira. Hii itawezesha uelewa wa jinsi walio wachache katika jamii wananyimwa haki ya kufaidi kutokana na rasilimali ya umma kama vile maji. Hali hii inadhihirika katika tamthilia ya *Majira ya Utasa* ambapo watu wachache wanabadili mikondo ya maji kwa manufaa ya kibinafsi huku wanajamii wengine wakikosa maji hata ya matumizi ya kimsingi.

Hatua ya kubadilisha au kusimamisha mikondo ya maji ya mito inaweza kuwa na athari nyingi kama vile kupunguza maji yanayowafikia watu wanaoishi upande wa chini wa mito hiyo (UNESCO, 2006). Ripoti hii inaafikiana na uchunguzi wa Mulwa na wenziwe (2021), uliobaini kuwa, licha ya kuwa maeneo ya vyanzo vya maji yanatoa huduma muhimu za kiuchumi nchini Kenya, shughuli mbalimbali kama vile mbinu mbovu za ukulima pamoja na ufyekaji wa misitu husababisha uharibifu wa vyanzo hivyo. Aidha, vyanzo hivi vimeharibiwa kupitia uvamizi wake na binadamu kama vile

ubadilishaji wa mikondo ya maji kwa sababu ya shughuli za kilimo. Matokeo yake ni athari hasi kwa jamii pakiwemo uhaba wa maji na matatizo ya kiafya. Hivyo, ni muhimu kulinda vyanzo vya maji ili kuzuia uhaba wa maji hasa kwa kuepuka mambo yanayochangia katika kusababisha uhaba wake, jambo ambalo linasisitizwa na watunzi wa tamthilia teule.

### 4.2.3 Athari za Uhaba wa Maji

Katika karne ya sasa, wasiwasi mkuu uliopo ni kuhusu athari za mabadiliko ya anga kwa mazingira, kwa mfano uhaba wa maji (Qatium, 2020). Uhaba huu wa maji umekuwa dhahiri katika kila pembe ya dunia na kutatiza shughuli nyingi. Kama inavyosisitizwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inayoongoza utafiti huu, binadamu, mazingira na viumbe wengine huhusiana kwa namna ya kutegemeana na kukamilishana. Hii ndio maana shughuli mbalimbali za binadamu zinaweza kuchangia katika uharibifu wa mazingira anamoishi na kumwathiri pamoja na viumbe wengine. Matatizo yanayotokana na uhaba wa maji yamesawiriwa na watunzi wa tamthilia teule ili kuliweka suala hili wazi. Athari zinazojitokeza ni kama vile milipuko ya magonjwa, kuathirika kwa elimu, biashara ya kuuza maji, kupungua kwa viwango vya usafi, athari za kiuchumi na kuzuka kwa mizozo.

#### 4.2.3.1 Milipuko ya Magonjwa

Uhaba au ukosefu wa maji safi unaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mhusika Tatu anasema:

> Tatu: Bwana Meya hilo hatutalifuata. Mgomo wetu utaendelea. Uonavyo hali ni hii. Uvundo huu utawazuia watu kuingia hata mjini. Kumbuka vyoo vinatusubiri sisi wafanyikazi kuvisafisha. *Majitaka yanatusubiri sisi kuyashughulikia. Bado kidogo na kipindupindu hakitakuwa tishio tena bali hali halisi.* (Uk 72)

Tatu ni mmoja kati ya wawakilishi watatu wa wafanyakazi katika mji wa Cheneo unaoongozwa na Mstahiki Meya. Anatamka maneno haya wakati yeye na wawakilishi wa wafanyakazi wenzake wapomtembelea Mstahiki Meya katika afisi yake. Sababu kuu ya kumtembelea ni kumweleza kuhusu hali mbovu ya wafanyakazi pamoja na kumtahadharisha kuhusu tishio la mgomo wa wafanyakazi wote iwapo angeendelea

kupuuza masilahi yao. Kutokana na maneno ya Tatu, uhalisia wa uhaba wa maji ni dhahiri katika mji wa Cheneo. Hii ndio maana Tatu anasema kuwa majitaka yameenea kote mjini na kuwa endapo hali itaendelea hivyo, milipuko ya magonjwa kama vile kipindupindu haitakuwa tishio tena bali uhalisia. Kwa mujibu wa Scholerberg (2007), udhalimu wa mazingira unaonekana kama mchakato ambao huzuia uwezo wa watu pamoja na jamii zao kutenda kazi kikamilifu kupitia hali duni za kiafya, uharibifu wa maisha ya kiuchumi na kitamaduni pamoja na vitisho vya mazingira vya jumla vilivyoenea. Kwa kutambua athari za uchafuzi wa mazingira, Tatu anasisitiza ya kwamba kuna hofu ya milipuko ya magonjwa kote katika Cheneo. Jambo hili litaathiri si tu afya za wanajamii, bali pia mifumo ya kiuchumi.

Usafi wa mazingira kama unavyoelezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO, 2021), ni mbinu za kuzuia upanuzi wa maradhi hasa kwa kudhibiti majitaka na kinyesi pamoja na kupanga kuhusu upatikanaji wa maji safi. Vilevile, ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN, 2021) inathibitisha kwamba, ukosefu wa maji safi na salama unaweza kuwa chanzo cha kusambaa kwa magonjwa kama kipindupindu. Kadhalika, ripoti hiyo inasema kwamba watoto walio dhaifu sana wako katika hatari mara nne zaidi kufariki dunia kama watakosa maji safi na salama ikilinganishwa na watoto waliozaliwa katika mazingira ambamo maji safi yanapatikana. Hivyo, kutokana na mtazamo wa mwandishi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya*, upatikanaji wa maji safi na salama ni njia mojawapo ya kuimarisha uhai.

#### 4.2.3.2 Kuathirika kwa Elimu

Uhaba wa maji ni tatizo ambalo limeathiri viwango vya elimu kwa mujibu wa tamthilia teule. Hii inatokana ama na muda mrefu unaotumiwa na wanafunzi kwenda kutafuta maji katika mito au baadhi ya shule kufungwa na watoto kusalia nyumbani bila matumaini ya kurejea shuleni. Katika *Janga la Werevu*, Kristy anasema:

> Kristy: Baba, baba, baba, mama, mama, mama, *huu sasa ni mwezi wa sita maji hayapatikani chuoni kwetu. Yamekatika moja kwa moja.Yameyoyoma kabisa kabisa. Hayatoki tena Mabombani.* Mjadala wetu chuoni unaelezea kuwa vyanzo vya maji vimekauka. Na kisha tunatabiri kwamba litazuka balaa la watu kugombana na kupigana vita kwa nia ya kuhodhi peke yao maji ya taifa zima… (Uk 31)

Uhalisia wa uhaba wa maji chuoni unadhihirika kupitia maneno ya Kristy ambaye ni mwanafunzi katika chuo kikuu. Kama inavyodokezwa na Njiru (2015), kila binadamu anastahili kuhusishwa katika mambo na mijadala kuhusu michakato ya kiteknolojia na kimazingira. Hii ni kwa sababu kila mja ameathiriwa na mambo hayo. Maneno ya Mhusika Kristy yanathibitisha kuwepo na mijadala ya wanafunzi kuhusu athari za uharibifu wa mazingira. Anawaeleza wazazi wake jinsi hali ilivyo chuoni na kuwa mijadala yao chuoni inadokeza kuwa, uhaba wa maji unatokana na kukauka kwa vyanzo vya maji. Aidha, wanatabiri kuwa ikiwa hali ingeendelea hivyo, huenda likazuka balaa la watu kugombana na kupigana vita kwa sababu ya uhaba wa maji. Hali kadhalika, tamthilia ya *Majira ya Utasa* inaangazia jinsi uhaba wa maji unaosababisha njaa unaweza kuathiri elimu. Hali hii inajitokeza kupitia mfano ufuatao:

> Mbawazi: Sasa *karibu unatimia mwaka tangu kufungwa shule. Bado hakuna dalili kwamba karibuni hali itabadilika nasi kurejea*. Tutakaporudi tutakuwa hata hatuwezi kujuana. Tutakuwa ni vinyanya na vibabu vinavyokwenda kwa mikongojo. Tutakuwa tumekwisha kuzeeka.
>
> Bi Siwa: Hilo lisikutie wasiwasi. Muhimu ni kuwa na moyo. Wanasema ujana wa moyo unashinda ujana wa umri… (Uk 8)

Katika mazungumzo baina ya Mbawazi na mamake Bi Siwa, ni dhahiri kuwa Mbawazi ana wasiwasi mwingi kuhusu hatima ya masomo yake. Kutokana na maneno yake, inabainika kuwa shule zimefungwa kwa muda mrefu kutokana na makali ya njaa inayotokana na ukosefu wa mvua. Zaidi ya hayo, anafafanua kuwa hakuna matumaini yoyote ya kurejea shuleni kwa sababu hakuna dalili za hali kubadilika. Athari za uhaba wa maji katika elimu ni tatizo ambalo linakabili wanafunzi wengi duniani. Kama anavyoeleza Etyang (2021), shule nyingi nchini Kenya zinakabiliwa na changamoto za uhaba wa maji hasa katika kaunti ya Turkana. Anatoa mfano wa Shule ya Upili ya wavulana ya Kerio na Shule ya Upili ya wasichana ya Nakurio ambao hawapati muda wa kupumzika baada ya masomo. Badala yake, huenda mitoni kutafuta maji kwa ajili ya kunywa, kufua na kuoga. Kando na kuhatarisha maisha yao wanapopitia katika maeneo yaliyo na wanyama hatari, afya yao pia inaathirika kutokana na maji chafu yapatikanayo katika mto wa Kerio. Kutokana na changamoto zinazowakabili wanafunzi kwa sababu ya uhaba wa maji, ni muhimu kwa serikali pamoja na mashirika

yasiyo ya serikali kuhusika katika kuibua mbinu mwafaka za kukabiliana na hali ya uhaba wa maji shuleni ili kuzuia madhara zaidi.

#### 4.2.3.3 Biashara ya kuuza Maji

Licha ya kuwa maji ni maliasili ya umma, uhaba wa maji umesababisha baadhi ya wanajamii kuyatumia kama vitega uchumi. Katika tamthilia ya *Janga la Werevu,* Busara anasema:

> Busara: Lakini mama *watu wanasumbuka sana kwa uchache na ukosefu wa maji*. Na sisi tunafanya nini? Tunafanya dhambi kubwa. Sikiliza huko nje maji yanavyomwagwa ovyo kwa kuosha magari mengi tuliyonayo wakati wengine hawana hata tone moja la maji ya kunywa. *Pia tumefungua biashara ya maji tuliyosomba katika chemchemi za maji za misitu ya wananchi*. Na miongoni mwetu hata maji machafu ya sumu tunawauzia watu kuharibu siha zao na kuwaua. (Uk 27)

Busara anayatamka maneno haya akimwambia mamake anayepinga madai kuwa kukatwa kwa miti ni chanzo cha kukauka kwa maji. Habari hizo zimechapishwa katika gazeti la Mazingira, jambo ambalo haliwafurahishi wazazi wa Busara; Bamkuu na Bimkuu. Kutokana na maneno ya Busara, inabainika kuwa baada ya wazazi wake kunyakua ardhi ya umma na kuharibu chemchemi za maji za misitu ya wananchi, wanaanzisha biashara ya kuuza maji kwa bei ghali hasa kwa sababu maji yamekuwa adimu kupatikana. Kama anavyoeleza Heise (2008), uhakiki wa kiekolojia huangazia jinsi vitendo mbalimbali vya binadamu huweka mazingira katika hali ya hatari, jambo ambalo husababisha mitandao ya viungauhai kudhoofika. Hii ndio maana Busara anakashifu vitendo vya wazazi wake kwa kuwaeleza kuwa wao ndio wamesababisha hali mbaya ya ukame unaoshuhudiwa kote katika jamii yao. Kadhalika, Kutokana na uhaba wa maji, baadhi ya watu katika jamii wanayatumia kama vitega uchumi. Mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anathibitisha haya kupitia mhusika Lulu katika dondoo lifuatalo:

> Lulu: Usiseme hivyo Jumbe. Watu wananung`unika na kukulaumu wewe.
> Jumbe: Kuhusu nini?
> Lulu: …kuhusu mambo kadha. Moja kati ya hayo ni kwamba wewe na wenzako *mmechukua sehemu za vyanzo vya maji*

> *na kuzigeuza kuwa vitega uchumi vyenu.* Kuna fununu kuwa nyinyi ndio mliosababisha kiangazi hiki… (Uk 38)

Mfano uliotolewa unaonesha kuwa licha ya wanajamii kutambua umuhimu wa maji, kunao wachache ambao wanayatumia kama vitega uchumi huku wakiwanyima wenzao haki ya kuyafaidi kwa matumizi yao ya kimsingi. Hali hii inachangia katika kusababisha kiangazi na hatimaye njaa isiyokadirika. Kwa mujibu wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, matatizo ya kiekolojia hutokea pale ambapo shughuli za kibinadamu zinapoharibu uwezo wa kawaida wa dunia kuwezesha uendelevu wa mifumo ya kiekolojia (Glotferlty, 1996). Hivyo, ni wazi kwamba baadhi ya vitendo vya binadamu kama vile kuharibu vyanzo vya maji kunasababisha uhaba wa maji. Matokeo yake ni watu wachache kuanzisha biashara za kuuza maji ambayo ni rasilimali ya wananchi wote.

#### 4.2.3.4 Kupungua kwa Viwango vya Usafi

Maji yanapokosekana au kupungua, viwango vya usafi navyo hudidimia. Kama inavyodokezwa na ripoti ya WHO (2021), watoto wadogo wana hatari kubwa zaidi kuliko watu wengine ya kudhurika na maji machafu, ukosefu au uchafu wa vyoo na mazingira machafu. Mwandishi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* ameangazia hali ambapo viwango vya usafi vimepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na uhaba wa maji kama ifuatavyo:

> Siki: Hali ikibadilika mshahara nao utakuja…
>
> Waridi: Kama itabadilika si hivi karibuni. Sitaki kufanya kazi isiyoninufaisha mimi au watu wengine. Mwenyewe unaona *hospitali ilivyo chafu. Hakuna maji ya kutosha*. *Usafi umetwaliwa na nzi*. Ni hatari hata kwetu sisi. (Uk 36)

Mazungumzo baina ya Waridi na Siki ambao ni wahudumu katika hospitali mojawapo katika mji wa Cheneo, yanatufafanulia hali mbaya ya viwango vya uchafu katika hospitali. Waridi anaposema kuwa `usafi umetwaliwa na nzi`, anatupa taswira ya jinsi uchafu wa kila aina ulivyotapakaa kote hospitalini, mahali panapotarajiwa kudumisha viwango vya juu vya usafi. Hali hii inatokana na ukosefu wa maji kote Cheneo. Hivyo, ni kinaya kwamba kuna uchafu wa kupigiwa mfano katika hospitali, mahali ambapo panatarajiwa kuwatibu wagonjwa hata walioathirika kutokana na magonjwa yanayohusiana na uchafu. Akieleza kuhusu

uhakiki wa kiekolojia, Heise (2008) anadokeza kuwa ekolojia hutazama jinsi mifumo ya kimazingira inavyofanya kazi ili kukidhi maisha na jinsi mifumo hii inavyoharibiwa kupitia vitendo vya binadamu. Vitendo vya binadamu ambavyo Heise (keshatajwa) anarejelea ni kama vile ukataji wa miti, ujensi wa viwanda pamoja na uongozi mbaya. Vitendo hivi vinavyochangia katika uharibifu wa mazingira vinadhihirika wazi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kupitia vitendo vya Meya. Matokeo yake ni uhaba wa maji katika mji wa Cheneo.

#### 4.2.3.5 Athari za Kiuchumi

Kwa mujibu wa waandishi wa tamthilia teule, uhaba wa maji unaweza kuathiri uchumi wa nchi yoyote ile. Hii ni kwa sababu maji huhitajika katika takribani kila shughuli za kiuchumi. Katika *Mstahiki Meya*, mazungumzo yafuatayo yanathibitisha:

> Gedi: Ni…ni habari za duru za kuaminika Mstahiki. Tena kuna madai kuwa *wageni wanaogopa kuwa huenda ugonjwa wa kipindupindu ukazuka.* Wanaogopa mkurupuko wa kipindupindu maana *mji mzima hauna maji*.
> Meya: Lakini kwangu yapo maji safi.
> Gedi: Labda, lakini *mahoteli hayana maji* yanayoweza kufikia viwango vya kimataifa. Sasa hivi mahoteli *yananunua maji kutoka mtoni* ambayo yanasombwa na punda. (Uk 77)

Wageni wanaotarajiwa kufika Cheneo wanaogopa kuwa huenda ugonjwa wa kipindupindu ukazuka, maana mji mzima hauna maji safi. Kuingia kwao kuna manufaa kwa baraza kwa sababu wanatarajiwa kuleta misaada ya aina mbalimbali. Hii ndio sababu Meya ana wasiwasi mwingi anaposikia kuwa kuna fununu kwamba wageni hao huenda wakose kuingia Cheneo. Isitoshe, Gedi anamwambia Meya kwamba mahoteli ambayo yangetumiwa na wageni hayana maji safi. Kwa hivyo, yananunua maji kutoka kwenye mito. Sarver (1994) anatambua haja ya uhakiki wa kiekolojia kushughulikia masuala muhimu ya kimazingira katika jamii ya sasa. Kwa maoni yake, njia mojawapo ni kutathmini upya utafiti katika kazi za kifasihi ambazo maudhui yake makuu ni mazingira. Sababu ni kwamba, uharibifu wa mazingira ulio dhahiri katika jamii umekuwa na athari nyingi katika kila shughuli za kijamii, pakiwemo afya, elimu na uchumi.

Hivyo, kama inavyosawiriwa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, uharibifu wa mazingira unaosababisha ukosefu wa maji safi pia unaweza kutatiza shughuli nyingi za kijamii hasa uchumi wa nchi. Hali hii inaweza kuthibitishwa na ripoti ya Umoja wa Kitaifa (UN, 2019), inayodokeza kwamba ukuaji wa uchumi katika maeneo ambako kuna maji yaliyoharibiwa vinapungua kwa theluthi moja kwa sababu ya athari mbaya dhidi ya afya, kilimo na mfumo wa ekolojia. Kadhalika, ripoti hiyo imeonya kwamba bila hatua za haraka, viwango vya maji vitaendelea kuzorota na kuathiri afya ya binadamu, kupunguza uzalishaji wa chakula na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi. Kwa hivyo, kutokana na mtazamo wa mwandishi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya*, uhaba, ukosefu au uchafuzi wa maji una athari hasi katika ukuaji wa kiuchumi wa nchi yoyote ile.

#### 4.2.3.6 Kuzuka kwa Mizozo

Uzukaji wa mizozo inayosababishwa na uhaba wa maji unashadidiwa katika tamthilia ya *Janga la Werevu.* Katika tamthilia hii, Mohamed (2011) anafafanua jinsi wanajamii kutoka sehemu mbalimbali wanang`ang`ania maji machache yanayopatikana katika chemchemi mojawapo ya wananchi. Jambo hili linajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Mwanamke I: Ala! Itakuwaje bwana wewe ututangulie na sisi tulifika mwanzo hapa? Utatokaje huko nyuma kuja kutusimamia mbele na kuzipinga zamu zetu? Sisi pia tunataka maji.
>
> Mwanamume II: Hapana cha mbele wala cha nyuma hapa. Mimi nimetamba misitu yote hapa nchini kutafuta maji kwenye vyanzo vya maji. Na kote huko hakuna maji. Kuna kiu tu kwa sisi tusio na maji. Labda wale watu wakubwa walio na visima vya maji. …nakwambia kwa hivyo, usizungumze fujo, *maana fujo ya maji hapa petu imeanzishwa zamani. Tena zamani sana…Tokea mwanzo ukitaka kujua, maji yamefanyiwa fujo na wenye nguvu. Na mpaka sasa maji yanaambatana na fujo* inayosababishwa na wenye nguvu… (Uk 16-17)

Maneno ya Mwanamume II anapomjibu Mwanamke I wakati analalamika wanapoteka maji, yanadhihirisha kuwa fujo ya maji ilianza zamani sana. Aidha, anamfafanulia kuwa maji yamefanyiwa fujo tokea zamani na wenye nguvu. Kwa mtazamo wa Mwanamume II, maji yanaambatana na fujo hadi sasa na hakuna dalili za fujo hiyo

kufika mwisho. Kwa mujibu wa Njiru (2015), uhakiki wa kiekolojia haufai kupiga vita tu majanga ya kiekolojia bali pia kukuza uwezo wa binadamu wa kuishi kwa amani na watu wengine pamoja na viumbe wasio binadamu. Kama inavyobainika kupitia mfano uliotolewa, uhaba wa maji unazua mizozo miongoni mwa wanajamii, jambo ambalo mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* anaangazia ili kuliweka wazi.

Isitoshe, imebainika kwamba kiu cha maji kimewaathiri tu wananchi wa kawaida hasa kwa sababu `watu wakubwa` wanavyo visima vya maji katika jamii zao. `Watu wakubwa` katika muktadha huu ni viongozi na watu wengine walio na ushawishi mkubwa katika serikali. Mfano uliotolewa unathibitisha kwamba, uharibifu wa mazingira wakati mwingine una misingi yake katika mambo ya kiuchumi na kisiasa. Hii ndio maana Carter (1999) anasisitiza kuwepo na mabadiliko makubwa katika namna binadamu anavyoaini na kupambana na matatizo ya kimazingira ya leo yanayosababishwa na mambo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.Vilevile, hali ya vurugu kutokana na uhaba wa maji inajitokeza kupitia maneno ya Mwendawazimu anapotongoa kishairi kama ifuatavyo:

> Mwendawazimu: …*Tunaanza kupigana kila mahali. Watu wanagombea maji kila hali.* Sisi si mwanzo wala wa pili. Wengi wamevuka hapa duniani na waliobaki hali taabani. *Tumo sote tunasukumana na maji mengi tena hakuna.* Yameyeyuka tokea jana… (Uk 22)

Mwendawazimu anadokeza kwamba uhaba wa maji ulianza zamani, hali ambayo inawafanya watu kugombana na kusukumana kila mmoja akitaka kupata maji. Kupitia maneno yake, inabainika pia kuwa maji yamekauka katika kila pembe ya dunia, ndiposa watu wamo taabani kwa sababu ya kukosa maji. Miongoni mwa mambo ambayo yameendelea kusababisha vurugu juu ya maji baina ya mataifa ya Marekani na miongoni mwa nchi mbalimbali duniani, ni kuongezeka kwa idadi ya watu na ongezeko la joto duniani (Wendorf, 2021). Mtaalamu huyu anaendelea kusema kuwa `vita vya maji` huelezea mizozo baina ya nchi, mataifa au makundi kuhusu haki ya kupata rasilimali ya maji hasa maji safi. Hii inatokana na umuhimu wa maji safi katika kilimo, uzalishaji wa umeme na kwa ajili ya kunywa. Kwa hivyo, vurugu hutokea wakati

ambapo mahitaji ya maji yanazidi usambazaji wake. Hivyo, ni muhimu kulinda vyanzo vya maji ili kuepuka vurugu kuhusu rasilimali hii.

### 4.3 Motifu ya Magonjwa

Waandishi wa tamthilia teule wametumia motifu ya magonjwa kusawiri athari za uharibifu wa mazingira. Uchanganuzi wa tamthilia hizo umebaini chanzo na aina mbalimbali za magonjwa. Aidha, mwingiliano wa kimaudhui katika tamthilia hizi teule unadhihirisha uzito wa suala hili la uharibifu wa mazingira hasa kutokana na madhara yake. Kwa mtazamo wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, mwanadamu anasababisha uchafuzi wa mazingira kupitia vitendo vyake licha ya kufaidika kutokana na mazingira hayo. Hivyo, imebainika kuwa baadhi ya vitendo vya binadamu vimesababisha madhara kama vile magonjwa. Katika tamthilia teule, magonjwa yanayoathiri wanajamii yamesababishwa na mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo yaliyobainika kuwa chanzo cha magonjwa ni: Kemikali kutoka kwenye viwanda, uchafu, wasiwasi na hofu na uchafuzi wa hewa.

#### 4.3.1 Kemikali kutoka kwenye Viwanda

Madhara ya kemikali kutoka kwenye viwanda vya maua yameangaziwa kwa mapana na marefu hasa katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*. Dondoo lifuatalo linathibitisha:

> Jumbe: …watu wamekufa kwa kukohoa. Na yapo magonjwa mengi ya kukohoza. Kuna Bird flu, Swine flu, Tuberculosis, AIDS, na mengine mengi. Kwa kutofahamu mambo wao wanafikiri kuwa maua yanaua. Mbona maua tuliyopanda majumbani mwetu yasituue?
>
> Mebo: Usitufanye wajinga bwana Jumbe. Tunajua fika kuwa maua yenyewe hayana taabu. *Shida ni kemikali hatari zinazotumiwa katika vibanda vya maua. Unaona ninavyokohoa?* Ajira uliyonipa ilifaa nini? Imenifaa hili kaburi la taratibu huku wewe ukistarehe. (Uk 73)

Mhusika Mebo alikuwa mwajiriwa wa zamani katika vibanda vya maua vya Jumbe. Yeye pamoja na mzee Dosho wanaenda kwa Jumbe ili kumweleza madhila yanayowakabili wanajamii kutokana na vitendo vyake. Kutokana na maneno ya Mebo, imebainika kuwa kemikali kutoka kwenye vibanda vya maua imesababisha ugonjwa wa kukohoa. Mebo aliyekuwa mwajiriwa wa Jumbe ni miongoni mwa watu walioathiriwa

na kemikali, jambo linalothibitishwa na kikohozi chake cha mara kwa mara wanapoendelea na mazungumzo. Vilevile, kemikali kutoka kwenye vibanda vya maua imesababisha ugonjwa wa ngozi. Ili kumweleza Jumbe uhalisia wa madhara ya kemikali kutoka kwenye vibanda vyake vya maua, Mhusika Dosho anasema:

> Dosho: …Na si hayo tu, tuna mzigo mkubwa kuwalea wagonjwa wa kemikali. Afadhali hili la kukohoa. *Wapo walioliwa na kemikali ngozi zao zikabaki nyama. Zimekunwa hadi ya kutokunika tena. Ni nyama zenye madonda.* Tunajua wanasubiri kifo ingawa hatuna ujasiri wa kuambiana hivyo. Machozi ya wanaume hutoka kwa nadra. Na yatokapo lipo jambo kubwa… (Uk 76)

Mfano uliotolewa unafafanua uhalisia wa madhara ya kemikali zinazotumiwa katika vibanda vya maua vya Jumbe. Kutokana na maneno ya Dosho, imebainika kwamba mbali na ugonjwa wa kukohoa, kemikali pia imesababisha ugonjwa wa ngozi ambapo waathiriwa wanajikuna na ngozi zao kusalia vidonda tupu. Kwa mujibu wa Tan (2019), athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira bado zinabaki kuwa mambo ya kimsingi yanayosababisha tishio la wazi kwa vizazi vijavyo. Kutokana na dondoo lililotolewa, ni wazi kwamba vizazi vya baadaye ndivyo vimo katika hatari zaidi ya maangamizi kutokana na athari za kemikali kutoka kenye viwanda. Hili linathibitishwa na maneno ya Dosho anaposema kuwa wao wana mzigo mkubwa kuwalea wagonjwa wa kemikali. Hii ina maana kwamba wengi waliougua ugonjwa wa ngozi ni watoto, ambao ni tegemeo la kizazi cha mwanadamu.

Maelezo haya yanashadidiwa na utafiti wa Mutua (2020) anayedai kuwa wanasayansi wametambua uharibifu wa mazingira unaoendelezwa na shughuli za binadamu, kama vile kuachilia kemikali hatari kwenye vyanzo vya maji kama mojawapo ya chanzo cha milipuko ya majanga na maradhi. Hii ndio maana mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* ameangazia athari za uharibifu wa mazingira kwa lengo na kuchochea kila mja kuhusika katika uhifadhi wake. Hata hivyo, mwandishi wa *Majira ya Utasa* anaonyesha kuwa iwapo tahadhari zinazostahili zinachukuliwa na waajiri hasa katika hema za maua, magonjwa yanayotokana na kemikali yanaweza kuzuiliwa. Akithibitisha madai haya, Mhusika Mebo anasema:

Mebo: Si kweli. Wala hiki si kifua kikuu. Kingekuwa ndicho, singetaka kutangamana nanyi maana naelewa hatari iliyoko. Tuliisha kufanyiwa uchunguzi. Sisi tuliopata ugonjwa huu tumeelezwa na madaktari kuwa ni kwa sababu ya kemikali katika hema za kukuza maua. *Tahadhari zinazostahili hazikuchukuliwa na mwajiri wetu.* (Uk 43)

Mebo anatamka maneno haya wakati yeye pamoja na wawakilishi wa kijiji wenzake wanapokutana ili kujadili na kutafuta suluhu la hali ngumu inayowakabili watu. Katika mazungumzo haya, Mebo anawafafanulia wenzake kuwa ugonjwa wa kifua aliougua umesababishwa na kemikali zinazotumika katika hema za kukuza maua. Kwa mujibu wa Dickens na Fielding (1988), maendeleo ya kiteknolojia hayastahili kusababisha uharibifu wa aina yoyote kwa asili pamoja na vipengele vyake vyote. Hii ina maana kwamba, maendeleo ya kiteknolojia yanafaa kuboresha maisha ya binadamu, wala si kuyaharibu kwa kuchangia katika kudidimia kwa afya yao kama inavyojitokeza katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*.

Hata hivyo, mfano uliotolewa unaonyesha kinyume chake ambapo wafanyakazi katika viwanda vya maua vya Jumbe wameangamizwa na kemikali zinazotumika humo. Jambo hili linathibitishwa na mhusika Mebo anapokiri kwamba baada ya uchunguzi, madaktari wameeleza kuwa sababu ya kuathiriwa na kemikali ni mwajiri wao kutochukua tahadhari zinazostahili katika hema hizo. Kwa hivyo, imebainika kwamba Arege katika *Majira ya Utasa* anawaonya waajiri ambao wanahatarisha maisha ya wafanyikazi wao kwa kutochukua tahadhari zote zinazostahili ili kuhakikisha usalama wa wafanyikazi wao.

**4.3.2 Uchafu**

Uchafu ni mojawapo ya chanzo cha magonjwa kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Katika tamthilia hii, kuna hofu ya mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu hasa kwa sababu ya uchafu wa kila aina uliotapakaa kila sehemu ya Cheneo. Katika mfano ufuatao, maneno ya Tatu yanathibitisha:

Tatu: Bwana Meya hilo hatutalifuata. Mgomo wetu utaendelea. Uonavyo hali ni hii. *Uvundo huu utawazuia watu kuingia hata mjini*. Kumbuka vyoo vinatusubiri sisi wafanyikazi kuvisafisha. *Majitaka yanatusubiri sisi kuyashughulikia. Bado kidogo na kipindupindu hakitakuwa tishio tena bali hali halisi*. (Uk 72)

Tatu anayatamka maneno haya wakati yeye pamoja na wawakilishi wa wafanyikazi wenzake Medi na Beka wanaenda ofisini mwa Meya, ili kulalamikia maslahi ya wafanyikazi ambayo hayajashughulikiwa. Kutokana na maneno ya Tatu, wafanyikazi wamegoma ambapo wamesitisha kutekeleza usafi jijini. Kama anavyosema Tatu, uvundo umeenea kote jijini, vyoo havijasafishwa na vilevile majitaka hayajashughulikiwa. Hii ndio maana kuna uwezekano mkubwa wa kuzuka kwa kipindupindu. Hali ya uchafu katika miji ina uhalisia katika jamii, jambo ambalo limechangia katika milipuko ya magonjwa hasa kutokana na majitaka, kinyesi na taka za viwandani. Kutokana na athari za kiafya zinazotokana na uchafu mijini, Bennett (2001) anatoa wito wa fasihi na elimu ya kimazingira kukuza kile anachoita `uhakiki wa kiekolojia wa kijamii` ambao unachukulia uharibifu wa mazingira ya mijini kwa umakini sawa na inavyochukulia uharibifu wa mazingira ya asili. Kwa kufanya hivyo, hali za kiafya za kila mja zitaimarika. Kama anavyosema Khamis (2018), mojawapo kati ya magonjwa yanayohusishwa na umaskini na uchafu ni ugonjwa wa kipindupindu. Kadhalika, anasema kuwa mlipuko wa ugonjwa huu ni mojawapo wa changamoto zinazokabili nchi zinazoendelea hasa kutokana na kutokuwa na uhakika wa kupata maji safi na salama, pamoja na kutokuwa na mazingira safi kwa ujumla. Kwa hivyo, kunahitajika juhudi nyingi za serikali na mamlaka zake kuhimiza wananchi kupambana na ugonjwa huu.

### 4.3.3 Wasiwasi na Hofu

Ugonjwa mwingine unaoathiri watu kwa mtazamo wa waandishi wa tamthilia teule unatokana na wasiwasi na hofu. Katika tamthilia ya *Janga la Werevu*, mhusika Busara anaeleza kuhusu ugonjwa huu kwa kusema:

> Busara: Mbona mama ugonjwa huu umeingia na kutawala kila kipembe hapa petu. Na wala hauhusiani na uchawi au ushirikina. Watu wanauita *ugonjwa wa maji matakatifu.* Ugonjwa mpya. *Unawaingia hasa vijana ugonjwa huu, hasa wale wenye ari na nchi yao*. Kusema kweli ugonjwa huu unatishia kulimaliza taifa zima, maana vijana wa leo ndio wajenzi wa nchi wa kesho. (Uk 41).

Kutokana na mfano uliotolewa, kuna ugonjwa mpya unaoitwa ugonjwa wa *Maji Matakatifu*. Kama anavyoeleza Busara, huu ni ugonjwa ambao unawaingia vijana

wazalendo walio na hamu ya kukomboa nchi yao kutokana na uharibifu wa mazingira. Hivyo, inaelekea kuwa Kristy ameugua ugonjwa huu, ndiposa wauguzi wengi wamejaribu kumtibu bila mafanikio. Vilevile, Busara anasema kwamba ugonjwa huu unaotokana na wasiwasi na hofu unatishia kumaliza taifa kwa sababu walioathirika zaidi ni vijana, ambao ndio wajenzi wa kesho. Hii ina maana kwamba, vijana wanadhihirisha uzalendo wa kweli kwa taifa lao kwa kujitokeza katika kupiga vita udhalimu unaofanyiwa mazingira. Kwa mujibu wa Garrard na Murphy (1998), ni lazima watu waanze kuwaza kwa namna tofauti kuhusu akili, miili na utambulisho wao kwa sababu ya majanga ya kimazingira. Kwa maoni ya Garrard na Murphy (keshatajwa), namna hii mpya ya kuwaza inapaswa pia kukuza maadili ya kiekolojia, usikivu na uraia kwa sayari endelevu. Uraia wanaozungumzia ndio unadhihirishwa na mtunzi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* kupitia vijana kama Kristy na dadake Busara.

Ushirikishwaji wa vijana katika vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi unashadidiwa na ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN, 2021). Kutokana na ripoti hiyo, mkutano wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi COP26 uliokuwa mjini Glasgow, Scotland ulijikita pia na mada ya ushirikishwaji wa vijana na umma katika kuhakikisha janga hili la mabadiliko ya tabianchi ambalo limeathiri mamilioni ya watu duniani linakomeshwa. Kadhalika, vijana walitoa wito kwa viongozi kutekeleza kwa vitendo ushirikishwaji wa vijana katika vita dhidi ya janga hilo. Hivyo, ni wazi kwamba vijana wenyewe katika kila pembe ya dunia wana ari ya kushiriki katika harakati ya kuyaokoa mazingira yaliyoharibiwa kupitia vitendo mbalimbali vya binadamu. Hata ingawa ugonjwa unaosababishwa na hofu, wasiwasi na hasira unawaathiri vijana kwa kiwango kikubwa, Daktari wa akili anaeleza aina mbili za hofu, wasiwasi na hasira kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Daktari wa akili: Hofu, wasiwasi na hasira tunazo sote. Lakini kila mmoja kwa namna yake. kwanza *kuna wale ambao wana hofu, wasiwasi na hasira kama Kristy. Hawa wana hofu ya dunia na ulimwengu kuangamia.*Kisha kuna wale wanaoishi kwa kusindika kemikali na madawa ya manufaa na yenye madhara, wale wanaochakata mafuta ya petroli, wale wanaotengeneza magari, meli na ndege wanaoendeleza viwanda vyenye kutoa hewa chafu na haribifu, wale wanaojaza uchafu wenye sumu kwenye meli na kuutupa mbali na

| | |
|---|---|
| | makwao, wale wanaohodhi ardhi kubwa kubwa na kutema misitu na machaka na kukata miti ili kupata mbao au kuni za kupikia au kuchimba madini na maliasili za kutumia... |
| Kristy*:* | *Enhe?* |
| Daktari wa akili: | Pengine *hawa wana hofu ya kupoteza mapato yao yanayozalisha wingi wa mijipesa na kupoteza nguvu zao.* Hawa wana wasiwasi na wanakwenda na hasira za chini kwa chini. *Wana hofu ya vuguvugu linaloendelea duniani kila pahala.* Hawa ni wachache lakini wana nguvu kubwa… kwa hivyo, uchafuzi na ukeketaji wa dunia na ulimwengu una manufaa kwao. (Uk 54-55) |

Katika dondoo lililonukuliwa, Daktari wa akili anaeleza kuwa kila mwanajamii ana hasira, wasiwasi na hofu lakini kila mmoja kwa namna yake. Anatoa mfano wa watu kama vile Kristy kwa kusema kuwa wao wana hofu ya dunia na ulimwengu kuangamia. Kisha anaeleza wengine ambao wanaishi kwa kusindika kemikali na madawa ya manufaa na yenye madhara, pamoja na kutekeleza vitendo vingine vinavyochangia katika uharibifu wa mazingira. Kutokana na mtazamo wa Daktari wa akili, pengine hawa wana hofu ya kupoteza mapato yao yanayozalisha pesa nyingi kwa manufaa yao na familia zao. Hivyo, wana wasiwasi kutokana na vuguvugu la mabadiliko linaloendelea kila pahala.

Vuguvugu hili ndilo Tan (2019) analozungumzia anaposema kuwa, uhakiki wa kiekolojia husisitiza kuwepo na maono ya jamii ambayo imeangamizwa na athari za shughuli za kibepari. Shughuli za kibepari zinazoendelezwa na Bamkuu na Bimkuu kama inavyobainika katika *Janga la Werevu* ni pamoja na uuzazi wa maji kwa manufaa ya kibinafsi. Kadhalika, imebainika kuwa watu wa aina hiyo ni wachache katika jamii ila wana nguvu nyingi. Katika *Janga la Werevu*, Bamkubwa na Bimkubwa wanawakilisha watu wa kundi hili la pili ambao uchafuzi na ukeketaji wa dunia na ulimwengu una manufaa kwao. Kwa hivyo, kutokana na mtazamo wa mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu*, wanajamii wengi hasa vijana wana ari ya mwamko mpya ambapo wana ari ya kukomboa mazingira yaliyoharibiwa kutokana na vitendo vya watu wachache katika jamii hizo.

### 4.4 Motifu ya Ukame

Ukame ni hali ya hewa ya sehemu fulani inayofanya pakose maji ya kutosha kwa muda mrefu. Ukame unatokea pia pale ambapo watu na kilimo wanategemea maji kwa umwagiliaji na vyanzo vya maji vinakauka, hali ambayo inahatarisha uhai wa mimea, wanyama na watu (Riccardo, 2017). Kwa mujibu wa Wanjohi (2010), suala la ukame limeanza kupata umakini mwingi kwa sababu ya kuongezeka kwa hivi karibuni kwa marudio na makali yake. Mathalani, ni mwanzo wa maafa ya polepole yanayoaminika kuwa chanzo cha kimsingi cha baa la njaa kwa ajili ya uharibifu wa mazao. Katika kuangazia jinsi ambavyo watunzi wa tamthilia teule wamesawiri motifu ya ukame, mambo yaliyozingatiwa ni chanzo na athari za ukame.

#### 4.4.1 Chanzo cha Ukame

Uchanganuzi wa tamthilia teule ulibainisha mambo mbalimbali ambayo yalisababisha ukame ulioathiri wanajamii. Miongoni mwa mambo yaliyobainika ni mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la joto duniani, kuasi ujadi, ukataji wa miti, tamaa ya viongozi na unyakuzi wa ardhi.

##### 4.4.1.1 Mabadiliko ya Tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi yanahusu kuwepo na mabadiliko ya muda mrefu ya viwango vya joto na mielekeo ya hali ya hewa. Mabadiliko haya yanaweza kutokana na sababu za kiasili, lakini tangu karne ya kumi na nane, shughuli mbalimbali za binadamu zimekuwa chanzo kikuu cha mabadiliko ya tabianchi (UN, 2021). Kadhalika, athari za mabadiliko ya tabianchi zinaonekana katika dunia yote katika uhalisia wake na kwa namna inayohatarisha maisha. Kwa msingi huu, watunzi wa tamthilia teule wameangazia suala hili ili kuonyesha madhara yake na namna ya kulitatua. Watunzi wa tamthilia teule wamedhihirisha jinsi ambavyo mabadiliko ya tabianchi ni mojawapo ya chanzo cha ukame. Katika *Majira ya Utasa*, dondoo lifuatalo linashadidia:

Jumbe: Mazingira yamekuwepo tangu siku za mababu wa mababu zetu. Leo mnaanza kudai kuwa mtayaokoa! Si mchezo huo?

Lulu: Siku zao mababu hali haikuwa hivi. Mazingira hayakuwa na tatizo. Hii ni ishara tosha. Miaka ya nyuma ulikuwa huwezi kuwa hivi. Leo hii *huwezi tena kuvaa shati ndani kwa sababu ya joto*. Huwezi kukaa ndani bila kuuacha mlango wazi au kutumia pangaboi. Unaona sasa? *Hewa*

> *safi imechafuliwa na gesi. Hatuwezi kutabiri hali ya anga maadamu, leo kiangazi kesho masika*. (Uk 79)

Katika dondoo hili, Lulu anamweleza mumewe Jumbe kuwa mabadiliko ya tabianchi yanayoshuhudiwa hayakuwepo katika siku za mababu zao. Anamweleza haya kwa kumtolea mfano wa joto kubwa lililo dhahiri katika jamii yao. Kutokana na maneno ya Lulu, imebainika kuwa imekuwa vigumu kutabiri hali ya anga kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kiangazi na masika vilevile. Kutokana na ongezeko la joto duniani pamoja na mabadiliko ya tabianchi yaliyo dhahiri katika jamii, uhakiki wa kiekolojia unahitaji kuangazia kwa umakini athari za kiekolojia Iheka (2015). Aidha, imebainika kuwa chanzo cha mabadiliko hayo ni hewa iliyochafuliwa na gesi. Kama inavyodhihirishwa na ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN, 2021), majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa yanashuhudiwa kila uchao katika sehemu mbalimbali za dunia, ikiwemo mvua nyingi, mafuriko, ukame mbaya ambao mara nyingi huchangia kutokea njaa. Kwa hivyo, kupunguza gesi chafuzi zinazochangia katika madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ni moja ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa. Kadhalika, hali ya mabadiliko ya tabianchi imesawiriwa na mwandishi wa *Janga la Werevu* kama ifuatavyo:

> Mwendawazimu: …Tazama *ukame unavyoenea na kunywa kila tone la maji ya vidimbwi, mito na maziwa*. Tazama jinsi ukame unavyosakarisha viumbe. Tazama vilele vya *milima ya barafu na maeneo ya theruji ya pola ya Kaskazini na pola ya Kusini inavyoyeyushwa na kutishia kufurisha maji ya pwani na bahari na kufikia visiwa.* Angalia fukwe na ardhi tambarare zinavyofunikwa na maji. Tazama ukame na ukavu unavyokithiri barani Afrika…*Na kama si ukame basi mafuriko yanayomfunika binadamu mwenyewe na kuharibu mali zake…* (Uk 12)

Mfano uliotolewa unaonyesha jinsi Mwendawazimu alikuwa akieleza hadhira kuhusu hali inayowakabili kutokana na uharibifu wa mazingira. Kutokana na maneno yake, ni wazi kwamba ukame umekita mizizi na kuathiri watu kote barani Afrika. Isitoshe, anafafanua jinsi ambavyo imekuwa muhali kutabiri hali ya anga kwa kusema kuwa kumekuwa na nyakati za ukame na vilevile mafuriko yanayomfunika binadamu mwenyewe na kuharibu mali zake. Mwendawazimu anaposema hivyo, anaonyesha

jinsi ambavyo watu katika maeneo mengi duniani wameathirika kutokana na vitendo vya kuharibu mazingira licha ya kunufaika kutokana na mazingira hayo. Jambo hili linashadidiwa na mtazamo wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia kuwa, licha ya kunufaika kutokana na mazingira, mwanadamu anasababisha uchafuzi wa mchanga, hewa na maji (Rigby, 2002).

Akieleza kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi, Maathai (2009) anasema kuwa mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kubwa katika kupunguza umaskini na kuafikia malengo ya Umoja wa Mataifa ya Milenia (MDGs). Aidha, Maathai (keshatajwa) anatambua kwamba mojawapo kati ya malengo manane ya maendeleo ya Milenia yaliyotarajiwa kutimizwa kufikia mwaka 2015 ni kuhakikisha uendelevu wa kimazingira. Kutokana na mtazamo wake, kutimia kwa kila lengo kati ya malengo hayo manane, kulitegemea kwa kiasi kikubwa afya ya mfumo wa ekolojia. Hata hivyo, jambo hili halikupewa umakini unaostahili. Kwa hivyo, kutokana na dondoo zilizonukuliwa, imebainika kwamba mabadiliko ya tabianchi ni mojawapo ya chanzo cha ukame ambao umekuwa na athari nyingi katika kila pembe ya dunia. Kwa upande mwingine, kuna watu katika jamii ambao bado hawaelewi kuhusu mabadiliko ya tabianchi, wala kujua chanzo cha majanga yanayowakabili na kuathiri hali zao za maisha. Jambo hili linasawiriwa na mwandishi wa *Majira ya Utasa* kama ifuatavyo:

> Bi Siwa: Wanasema eti haya yote yanatokana na mipango mibaya na ubinafsi. Lakini *mimi nafikiri ni kwa sababu ya dhambi.* Ulimwengu una dhambi nyingi na Mungu nionavyo amekasirika. *Padre alisema hii ni moja kati ya mambo yanayoonyesha kuwa dunia inakwisha*. Siku ya kiyama inakaribia. (Uk 7)

Katika mfano huu, Bi Siwa anasema kwamba majanga yanayowakabiri yanatokana na dhambi zilizo katika ulimwengu. Kwa maoni yake, majanga hayo yanaweza kuepukika iwapo watu wangetubu dhambi zao. Aidha, padre ambaye anawakilisha viongozi wa kidini anawahakikishia waumini kuwa kuwepo kwa majanga kama vile ukame na mafuriko ni mojawapo ya dalili za kukaribia kwa siku ya kiyama. Maneno ya wahusika hawa ni dhihirisho tosha kuwa watu wengi katika jamii bado hawajui chanzo cha masaibu yanayowakabili. Kwa mujibu wa Curry (2011), ulimwengu mzima unahitaji elimu ya kiekolojia katika viwango vyote ili maadili ya kimazingira yawekewe msingi

katika mifumo ya chakula, mabadiliko ya tabianchi, nishati, maendeleo endelevu, uharibifu wa mazingira, biashara ya kaboni na ushirikiano katika uwajibikaji. Kwa kufanya hivyo, watu wote kote ulimwengu watakuwa na uelewa wa chanzo na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hivyo, watahusika na kuchangia katika kusuluhisha matatizo yanayotokana na uharibifu wa mazingira.

Kama inavyoelezwa na Simel (2015), katika jamii yoyote ile, familia zilizo maskini ndizo zilizo katika hatari zaidi ya kuathiriwa na mabadiliko hasi ya tabianchi. Sababu kuu ni kuwa hawajui chanzo chake na pia hali zao za kimaisha zinawafanya washindwe kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayojitokeza kila uchao. Hivyo, ni muhimu kwa wananchi kuelimishwa kuhusu mabadiliko ya tabianchi pamoja na namna ya kukabiliana na athari zake.

#### 4.4.1.2 Ongezeko la Joto Duniani

Watunzi wa tamthilia teule wameangazia hali ya ukame unaotokana na ongezeko la viwango vya joto duniani. Kutokana na mazungumzo ya wahusika katika tamthilia ya *Majira ya Utasa* (Arege, 2015), inadhihirika kuwa ukame unaoshuhudiwa haujakuwepo nyakati za jadi. Hii ina maana kwamba, hali imekuwa ikizorota kila uchao hasa kutokana na joto kali linalowakabili watu. Mazungumzo yafuatayo baina ya Kato na Hori yanathibitisha:

> Kato: *Joto hili halijawahi kushuhudiwa tangu tutie fahamu.* Ndani hapakaliki na nje ni mfano wa tanuu. Huu ni mwaka wa hari.
>
> Hori: Kiangazi cha namna hii sijakiona mimi. *Nimekuwa nikizisikia hadithi za mbali huko***.** Hadithi za Sahara na Kalahari. Si hapa kwetu. *Viwango hivi vya joto vinaweza kukuyeyusha ubongo* ikiwa utalifanyia ushindani.
>
> Kato: Makubwa haya! Maisha yetu yamekuwa ni dhiki kwa dhiki. (Uk 65)

Katika mazungumzo hayo, Kato anamwambia Hori kuwa viwango vya joto vinavyowakabili havijawahi kushuhudiwa katika jamii yao. Aidha, Hori anakiri kwamba, kwa muda mrefu amekuwa akisikia habari kuhusu kuongezeka kwa viwango vya joto katika sehemu tofauti kama vile Sahara na Kalahari bali si hapo kwao. Hii inamaanisha kwamba janga hili limeenea hadi katika jamii wanamoishi. Kutokana na

hali hii, maisha yao yamekuwa katika dhiki kuu ya njaa iliyosababishwa na ukame. Kama inavyodhihirika katika Mwongozo wa Mabadiliko ya Tabianchi (PSI, 2020), hali ya joto inazidi kuongezeka kwa kasi. Kwa mfano, mwezi Juni 2019 ulikuwa ni mwezi wenye joto kubwa zaidi kuwahi kutokea. Aidha, katika bara la Afrika, mwaka 2019 ulikuwa mwaka wa tatu wenye joto zaidi kuwahi kurekodiwa (baada ya mwaka 2016 na 2010).

Kadhalika, kati ya 2010 na 2019, India ilirekodiwa kuwa na karne yenye joto zaidi tangu takwimu kuanza kukusanywa mnamo mwaka 1901. Kwa hivyo, ongezeko la joto duniani lililo na uhalisia katika dunia ya sasa linasababisha madhara mengi pakiwemo moto katika mapori na mvua zisizotabirika ambazo huleta ukame wa muda mrefu unaoathiri ulinzi wa chakula. Hivyo, watunzi wa tamthilia teule wameliangazia suala hili kwa kuonyesha madhara yake ili lishughulikiwe na washikadau wote wanaohusika. Kando na kuangazia uhalisia wa ongezeko la joto duniani, watunzi wa tamthilia teule wameonyesha athari zinazotokana na jambo hili. Katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*, dondoo lifuatalo linashadidia:

> Lulu: Si uongo. *Sehemu za huko Arctic zenye theruji nyingi ajabu zimeanza kupoteza kiasi kikubwa cha theruji yake kutokana na global warming…*
> Jumbe: *Arctic* si maeneo ya huko uzunguni?
> Lulu: Ni huko huko.
> Jumbe: Yanatuhusu vipi?
> Lulu: Yanatuhusu kiasi chake. *Muyeyuko wa theruji utaleta ongezeko la maji baharini na hiyo hatari kwa wakazi wa pwani maana maji yatapasua kingo zake za kawaida na kuvuka nchi kavu*. (Uk78-79)

Katika mazungumzo yaliyodondolewa, Lulu anamweleza mumewe Jumbe kuhusu athari za ongezeko la joto. Anamfafanulia jinsi ambavyo sehemu za *Arctic* zimeanza kupoteza kiasi kikubwa cha theruji yake kutokana na ongezeko la joto duniani. Hivyo, muyeyuko huo wa theruji utasababisha kuongezeka kwa maji baharini, jambo ambalo ni hatari kwa wakazi wa pwani kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa maji hayo kupasua kingo zake za kawaida na kuvuka nchi kavu. Akieleza kuhusu nafasi ya uhakiki wa kiekolojia katika kusuluhisha matatizo ya mazingira, Njiru (2015) anasema kwamba, ni lazima watu wote wakumbatie hali halisi ya majanga ya kiekolojia pamoja na rasilimali zilizoharibiwa na kudidimia kila uchao. Hali ya kuukimbia uhalisia wa

athari za uharibifu wa mazingira inadhihirika katika mfano uliotolewa wakati Jumbe anamwambia mkewe Lulu kuwa, tishio la mafuriko haliwahusu wao bali linahusu watu wa huko uzunguni. Ndiposa Lulu anamweleza jinsi ambavyo hayo yote yanawahusu wao pia, ili kwa pamoja wachangie katika kuleta suluhisho.

Uhalisia wa athari za ongezeko la joto duniani unadhihirika kupitia mafuriko yaliyoshuhudiwa katika nchi za Ujerumani na Ubelgiji tangu miaka ya 1950, ambako watu zaidi ya 150 waliripotiwa kufa. Aidha, ilibainika kuwa chanzo cha mafuriko hayo ni mvua kubwa iliyosababisha maji ya mito kufurika na kumwagika nje ya kingo zake, jambo ambalo lilisababisha uharibifu mkubwa katika eneo hilo huku baadhi ya vijiji vikiangamizwa kabisa. Hivyo, wataalamu wa kimazingira wanaonya kwamba majanga yanayotokana na mafuriko yataendelea kutokea hasa barani Ulaya iwapo suala la mabadiliko ya tabianchi halitashughulikiwa kama jambo la dharura. (BBC NEWS, 17/07/2021)

#### 4.4.1.3 Kuasi Ujadi

Uasi wa baadhi ya mambo ya jadi umekuwa mojawapo ya chanzo cha ukame katika jamii. Hali hii imebainika kupitia uchanganuzi wa tamthilia teule kwa mtazamo wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia. Katika *Janga la Werevu*, uasi wa mambo ya jadi umeangaziwa na mwandishi wa tamthilia hiyo kama ifuatavyo:

> Kristy: Lakini mama, *kwa nini sisi Waafrika tunazidharau jadi zetu hata zikiwa nzuri?*
> Bimkuu: Kwa sababu jadi maana yake ni kupitwa na wakati, na kuupuuza wakati ni kupiga ngumi ukuta.
> Busara: Lakini si kweli kwamba kila siku mtu akipiga ngumi ukuta huumiza mkonowe…mimi nadhani kwamba *wahenga wetu hawakuwa wendawazimu kuweka itikadi zilizoambatana na matambiko ili kuilinda misitu yetu*. Na kulinda misitu yetu ni kulinda uhai wa miti, wanyama, wadudu na sisi wenyewe. (Uk 38)

Ujumbe unaojitokeza katika mazungumzo haya baina ya Busara, Kristy na mama yao Bimkubwa ni kwamba Waafrika wanadharau jadi zao hata zikiwa nzuri. Sababu kuu ni kwamba, jadi hizo zinachukuliwa kuwa zimepitwa na wakati kama anavyosema Bimkuu. Hata hivyo, kinachodhihirika kupitia maneno ya Busara ni kwamba si kila jambo la jadi ambalo limepitwa na wakati, kwani huenda lina manufaa katika jamii ya

sasa. Busara anatoa mfano wa itikadi zilizoambatana na matambiko kwa kusema kuwa zililenga kulinda misitu.

Kwa kurejelea wazo la Buell (1995) kuhusu sheria ya kwanza ya ekolojia ya mfumo ekolojia kwamba "kila kitu kimeunganishwa na kila kitu kingine", wahakiki wa kiekolojia wanashikilia kuwa, utamaduni wa binadamu umeshikamana na ulimwengu halisi kwa kuathiri asili, nayo asili ikiuathiri utamaduni huo. Kutokana na maneno ya Busara, itikadi ya jamii yake iliyoambatana na matambiko iliwekwa na wahenga ili kulinda asili kama vile misitu. Athari za kuasi itikadi hiyo zinajitokeza wakati hatua ya kufyeka misitu ilisababisha kukosekana kwa mvua. Hivyo, ni wazi kwamba, matambiko hayo yalikusudiwa kulinda uhai wa miti, wanyama, wadudu na binadamu wenyewe. Kwa upande wake, mwandishi wa *Majira ya Utasa* anaangazia hali ambapo uasi wa ujadi umekuwa chanzo cha ukame kupitia mfano ufuatao:

> Siwa: Kuna nini?
> Hori: Luvea hii. Dalili tosha
> Dosho: Ndipo hapa.
> Hori: Hii *luvea* ndiyo *iliyotumiwa kwenye madhabahu tangu jadi*. *Ndiyo iliyowaunganisha wazee wetu na mizimu*. Na siku zote ilikuwa yasimikwa kuangalia juu. Si chini ilivyo hivi. Unaona? Wameiziba kinywa. Haiwezi kupumua. Kushindwa kwake kupumua kunaua mkondo wa mawasiliano baina yetu na wao. Kumbe tulitengwa na wazee wetu zamani bila sisi kufahamu! (Uk 50)

Ujadi unaodhihirika katika dondoo hili unahusu utoaji wa kafara kwa wazee huko mlimani. Hata hivyo, imebainika kwamba madhabahu yaliyotumiwa tangu jadi kwa ajili ya shughuli za utoaji kafara yaliharibiwa na Jumbe na wafanyikazi wake. Aidha, imebainika kwamba `luvea` iliyotumiwa tangu jadi ambayo iliwaunganisha wazee na mizimu pia imeharibiwa, hivyo kuifanya ishindwe kupumua. Jambo hili linatinga mkondo wa mawasiliano baina ya wanajamii na wazee. Kwa mujibu wa Glotferty (1996), utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana. Kutokana na mtazamo huu, wanajamii katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi wa *Majira ya Utasa* wanaathirika kutokana na kiangazi kinachodhaniwa kuwa kimetokana na uasi wa ujadi unaoambatana na matambiko ya utoaji wa kafara kwa wazee.

Ujumbe unaobainika kupitia dondoo hili ni kwamba, kutengwa na wazee kumekuwa chanzo cha matatizo yanayowakabili watu katika jamii iliyosawiriwa, kama vile janga la ukame. Kwa mujibu wa Assumpta (2011), matambiko katika jamii nyingi za kiafrika za jadi yalihusu shughuli za utoaji wa kafara na sadaka kwa mwenyezi mungu, miungu au mahoka, mizimu au pepo hasa wakati wa kusalia miungu. Vilevile, Masebo (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa matambiko hayo yalikuwa muhimu katika jamii hizo za kiafrika za jadi katika utatuzi wa matatizo yaliyowakabili wanajamii kama vile magonjwa, vifo, vita, kukosa watoto, mafuriko na pia ukame.

Kadhalika, Shemboko (2020) anaeleza umuhimu wa matambiko katika jamii za kiafrika kwa kusema kwamba yalijenga imani kama chombo cha kutatulia matatizo ya kijamii. Hivyo, jamii huongozwa katika kupambana na matatizo mbalimbali yanayoikabili. Shemboko (keshatajwa) anatoa mfano wa jamii ya Wasambaa, Tanzania ambapo janga la ukame lilidhibitiwa kupitia mwiko uliohusishwa na misitu na mito. Kwa hivyo, sehemu za misitu na mito zilichukuliwa kuwa maalumu za kufanyia matambiko ili kuzuia janga hilo. Watunzi wa tamthilia teule wameonyesha kuwa masuala ya kijadi kama vile matambiko na utoaji wa kafara katika jamii ni muhimu katika kuzuia au kusuluhisha matatizo yao.

Licha ya umuhimu unaohusishwa na shughuli za kijadi katika kuzuia majanga kama vile janga la mafuriko na ukame, watunzi wa tamthilia teule wameonyesha kuwa shughuli hizo zimepuuzwa katika jamii ya sasa. Hivyo, imebainika kwamba maendeleo ya sayansi na teknolojia na hamu ya kutaka kuishi kulingana na wakati, ni miongoni mwa mambo ambayo yamewafanya waafrika kuasi utamaduni wao na kufuata tamaduni za kigeni. Katika *Janga la Werevu*, dondoo lifuatalo linathibitisha:

| | |
|---|---|
| Bimkuu: | Aaa, Busara binti yangu, *katika karne hii bado unataka utambike?* |
| Busara: | Kwa nini nisitake kutambika? Nina sababu gani? |
| Bimkuu: | *Hatutaki kuachwa nyuma katika dunia hii ya sayansi na Hi-tech!* |
| Busara: | Hutaki kuachwa nyuma na *u-dotcom*. Je, *Hi-tech* na *u-dotcom* havina madhara hata kidogo? Busara ya kuishi husema kwamba kila zuri huzungukwa na mabaya na kila baya huzungukwa na mazuri. |
| Busara: | Tatizo ni kwamba *tunatazama ukale na matambiko yake kijuujuu tu. Hatuzamii ndani kuchunguza kina cha falasafa* na maana ya matambiko. (Uk 38-39) |

Kutokana na mtazamo wa Bimkuu katika dondoo hili, suala la matambiko limepitwa na wakati katika karne hii. Kwa maoni yake, kutambika ni dhihirisho la watu waliobaki nyuma katika dunia ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hata hivyo, Busara anamweleza kwamba kila jambo linalodhaniwa kuwa zuri pia linaweza kuwa na madhara yake. Kumaanisha kuwa hata hayo maendeleo ya sayansi na teknolojia yanaweza kuwa na madhara yake. Hii ndiyo maana wahakiki wa kiekolojia wanadokeza kwamba, suluhisho la matatizo ya kimazingira halipo katika maendeleo zaidi ya kiteknolojia, bali wanapendekeza mabadiliko katika jinsi ambavyo binadamu hujiona kama wao ni sehemu ya asili (Quick, 2004). Hivyo, ni muhimu kuchunguza kina cha falsafa na maana ya matambiko badala ya kutazama ukale na matambiko yake kijuujuu.

#### 4.4.1.4 Ukataji wa Miti

Kwa mujibu wa Maathai (2009), misitu hujumuisha asilimia 31 za ardhi ya dunia. Hata hivyo, kwa sababu ya ukataji miti, idadi hii inapungua haraka. Hivyo, inakadiriwa kuwa kila mwaka hekta milioni 10 za misitu duniani hupotea ambapo hekta milioni 3.9 hupotezwa barani Afrika. Kama inavyoangaziwa na watunzi wa tamthilia teule, ukataji wa miti umekuwa chanzo cha majanga pakiwemo janga la ukame. Katika mfano ufuatao, mwandishi wa *Majira ya Utasa* anaangazia madhara ya ukataji wa miti:

> Kato: Hata madhabahu?
> Hori: Madhabahu gani? Hamna hata unyasi uliosimama. Mavumbi tu. Watu waliisha kujitwalia wakaikata miti. Tunasikia baadhi waliiuza ng`ambo. Kuna wakati Mebo alisema kuwa *miti iliuzwa na wakubwa* kufanyia kampeni. Walipoona limebaki shamba tupu, wakaamua kulifanyia shughuli za kilimo. Sasa *matokeo yake haya, kiangazi* (Uk 60)

Katika mfano uliotolewa, mhusika Hori anamweleza Kato kuhusu chanzo cha kiangazi kinachoshuhudiwa katika jamii yao. Kutokana na maneno yake, ni wazi kwamba ukataji miti ovyo unachochewa na mambo mbalimbali pakiwemo upanuzi wa mashamba ya kilimo, utengenezaji wa mbao, uchomaji makaa, pamoja na kukosekana kwa miundo mwafaka ya usimamizi. Kupitia dondoo hili, imebainika kwamba viongozi walikata miti kiholela na kuiuza ili kufanyia kampeni. Zaidi ya hayo, walitumia sehemu

zilizokatwa miti kwa shughuli za kilimo kwa manufaa ya kibinafsi. Matokeo ya ukataji miti ni kiangazi kinachoshuhudiwa.

Kama anavyoeleza Maathai (Keshatajwa), rasilimali asilia zingali zinadhulumiwa kupitia shughuli za binadamu kwa kupuuza afya bora ya mazingira. Maelezo ya Maathai (keshatajwa) yanaafikiana na kauli ya Bookchin (2007) anaposema kuwa, binadamu wamekosea asili yao hasa kwa kuiharibu vibaya kupitia shughuli zao. Hivyo, kuenea kwa jangwa kupitia ukataji wa miti kunakoathiri vyanzo vya maji, nyanja za kufugia na mashamba kwa ajili ya kilimo na kuchangia katika uchamkaji wa chakula wa dharura, ni miongoni mwa shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira, ambazo Bookchin (keshatajwa) anazungumzia. Kando na kuwa chanzo cha ukame, hali ya kuharibu misitu kupitia ukataji wa miti inaweza kuhatarisha maisha ya binadamu kama inavyosawiriwa na mtunzi wa *Majira ya Utasa*:

> Kato: Kweli hiyo milio ya fisi? Ajabu ya fisi kulia mchana
> Hori: Na hawapo mbali. *Makao yao msituni wamepanda Mimea. Hakuna tena maficho ya wanyama waliowawinda*. Sasa watatula sisi.
> Kato: Kama ni kweli hivyo ulivyosema, *ina maana tumevamia makao yao.* Sasa naona lililobaki ni sisi kuwawinda kuupigania uhai wetu nao wakituwinda kupata chakula. (Uk 66)

Kinachodhihirika kupitia dondoo hili ni kwamba watu wamevamia makao ya wanyama msituni. Hii ni kupitia ufyekaji wa misitu kwa ajili ya kilimo, hivyo kuharibu makazi ya wanyama wengine waliowawinda wanyama hao. Kwa mujibu wa Alia (2017), mazingira ni ushirikiano wa asili na utamaduni, binadamu na wasio binadamu pamoja na viumbe hai na visivyo hai. Hii ina maana kwamba, iwapo binadamu atavuruga mfumo wa kawaida wa ekolojia kwa namna yoyote, ataathiri si mazingira ya asili tu bali mfumo wote wa ekolojia pakiwemo wanyama, viumbehai na visivyo hai. Kama inavyodhihirika katika dondoo lililotolewa, athari ya tendo la ufyekaji wa misitu ni kuwa wanyama sasa wanaweza kuvamia makazi ya watu, hali inayohatarisha maisha yao, kama inavyoelezwa na mhusika Hori. Kwa upande wake, Kato anashauri kuwa kutokana na hatari iliyopo, inabidi waanze kuwawinda wanyama ili kuokoa maisha yao, kwani hata nao wanyama wanawawinda kwa ajili ya kupata chakula. Kadhalika, mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* ameangazia hali ambapo baadhi ya vitendo

vinavyofanywa na viongozi vinahatarisha maisha ya wananchi. Hii ndio maana Bi. Subira anawaeleza wenzake kuhusu hali inayowakabili kama ifuatavyo:

Bi. Subira: Kwani kumezidi tu? *Kunafufurika na kujaa maovu hapa petu.*
Bi. Mgeni: Nini cha mno lakini?
Bi. Subira: Nchi imekaa kama msitu wa watoro. *Umejaa wahalifu wanaotafuna watu na kumeza. Afadhali hao masimba na mafisi wanaohujumu na kula viumbe.* (Uk 58)

Ujumbe unaojitokeza katika dondoo hili ni kwamba jamii iliyoangaziwa imejaa kila aina ya uovu. Hii ndio maana Bi. Subira anasema kwamba kumejaa wahalifu `wanaotafuna watu na kuwameza`. Kumaanisha kwamba miongoni mwao kuna watu wasiojali athari za matendo yao, ndiposa watu wanaumia. Vilevile, ni dhahiri kwamba makazi ya wanyama hatari yamevamiwa kupitia vitendo vivyo hivyo vya kutojali. Matokeo ni kwamba hao wanyama wanahujumu na kula viumbe, hasa kwa sababu hawana mahali pa kujificha. Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, binadamu, mazingira na viumbe wengine huhusiana kwa namna ya kutegemeana na kukamilishana (Tarton na Henwood, 2002). Kwa kuzingatia mtazamo huu, imebainika kwamba tendo la kuvamia makazi ya wanyama, limeharibu pia sehemu ambazo wanyama wanaowawinda hujificha. Hivyo, kuna hatari ya binadamu na viumbehai wengine kuliwa na wanyama hatari. Kutokana na athari zinazohusiana na ukataji ovyo wa miti, hatua za dharura zinahitajika ili kutunza bayoanuai ya misitu wakati ambapo kudidimia kwa misitu kunaendelea kwa kiwango cha kutisha duniani. (UNEP, 2020).

#### 4.4.1.5 Tamaa ya Viongozi

Ukame uliokithiri katika jamii umesababishwa na tamaa ya viongozi ya kujilimbikizia mali pamoja na ujinga wa kutotambua athari za matendo yao. Jambo hili ni dhahiri katika jamii ambapo viongozi wanawahadaa wananchi kuwa wangewashughulikia masilahi yao ili waweze kuchaguliwa. Baada ya kuchaguliwa, wao hunyakua mali ya umma huku wakijifaidi wao wenyewe pamoja na marafiki wao wa karibu. Mtunzi wa *Majira ya Utasa* amesawiri hali hii kupitia maneno ya mhusika Hori kama ifuatavyo:

Kato: Kama ni kweli hivyo ulivyosema, ina maana tumevamia makao yao. Sasa naona lililobaki ni sisi kuwawinda kuupigania uhai wetu nao wakituwinda kupata chakula.

Hori: …tumefikia hali ambapo tunawazika watu wetu eti kwa sababu ya njaa. Njaa iliyosabibishwa na ukame. *Ukame! Ukame waliousababisha wanadamu. Labda kwa tamaa, labda kwa ujinga…* (Uk 66)

Kupitia dondoo hili, inaelekea kuwa mtunzi wa *Majira ya Utasa* anawalaumu viongozi ambao wanachangia katika kuharibu mazingira kwa sababu ya tamaa yao. Kiongozi Jumbe anawakilisha viongozi wa kiafrika ambao kutokana na tamaa yao walivamia maeneo ya misitu. Matokeo ya uvamizi huo ni kukosekana kwa mvua na hatimaye athari zisizokadirika kama vile njaa kutokana na kiangazi pamoja na kuongezeka kwa viwango vya joto. Katika *Janga la Werevu*, mwandishi anaangazia hali ambapo tamaa ya viongozi inawafanya wakate miti na kufyeka mapori bila kufahamu madhara ya matendo yao kwa mazingira. Katika mfano ufuatao, Mwakilishi wa mabwanashamba anasema:

Mwakilishi wa Mabwanashamba: Lakini tunyang`anywe kwa nini na sisi ardhi tunaifanyia kazi ya kuzalisha na kuinua uchumi wa taifa? Tunakata miti na kuuza mbao. *Tunafyeka mapori na kupanua mashamba makubwa ya kuzalisha chakula na mazao ya biashara yanayoingiza pesa za kigeni;* chai, kahawa, bhangi… (Uk 71)

Ujumbe unaojitokeza katika mifano iliyotolewa ni kwamba, kichocheo kikubwa cha ufyekaji wa mapori ni kupanua mashamba makubwa ya kuzalisha chakula na mazao ya biashara kwa sababu ya tamaa ya pesa za kigeni. Zaidi ya hayo, imebainika kuwa ni kutokana na tamaa ya viongozi ambapo walinyakua ardhi ya umma ili kuweza kujitajirisha wao wenyewe. Matokeo ya vitendo hivi ni kuangamiza umma kupitia athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira, kama vile janga la ukame. Kwa mujibu wa Easterlin (2012), mabadiliko ya kiekolojia na majanga hubadili namna watu hufikiria kuhusu wao wenyewe, binadamu wengine na asili isiyo binadamu. Kwa msingi huu, wahakiki wa kiekolojia wanasisitiza haja ya kuwepo na mabadiliko kuhusu namna watu wanavyowaza na kujiona kama wao ni sehemu ya mazingira, ili kuweza kuyahifadhi. Utafiti wa Sangili (2015) unashadidia maelezo haya kwa kutambua kuwa

viongozi katika serikali ya nchi huchangia kwa kiwango kikubwa katika uharibifu wa mazingira kwa namna mbalimbali pakiwemo tamaa na hali ya kutojali athari za vitendo vyao.

Hali ya kutojali na unafiki wa viongozi imesawiriwa na watunzi wa tamthilia teule. Licha ya kuwa viongozi waliochaguliwa ni wenyeji wa jamii husika, hawajali maslahi ya wananchi waliowachagua baada ya kuchukua hatamu za uongozi. Arege anaangazia hali hii katika *Majira ya Utasa* kama ifuatavyo:

> Deka: Ni upangaji mikakati tu.
>
> Bi Siwa: Kila mwaka kuna vikao vya namna hii kuhusu mikakati hiyo hiyo. *Miezi mitatu iliyopita kiangazi hiki kilipoanza kutuparuza kwa kucha zake, kikao cha kutafuta ushauri na kuandaa mikakati kiliandaliwa.* Sote tunajua maazimio yake. mangapi yalifuatwa kutuauni? (Uk 15)

Katika dondoo hili, maneno ya Bi Siwa yanatoa ushahidi kuwa kiangazi ambacho kimeathiri watu wengi katika jamii kimekuwepo kwa muda. Licha ya viongozi kuandaa vikao vinavyolenga kutafuta ushauri na kuandaa mikakati ya kusuluhisha janga la kiangazi, maazimio ya vikao hivyo hayafuatwi. Kutokana na mfano huu, Jumbe anawakilisha viongozi wanafiki katika jamii ambao huwahadaa wananchi kuwa wanawashughulikia huku wakichukua nafasi hiyo kujifaidi wenyewe. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba mtunzi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anawashutumu viongozi wa aina hii ambao wanazidisha hali inayokumba wanajamii badala ya kutafuta suluhisho.

#### 4.4.1.6 Unyakuzi wa ardhi

Suala la ardhi ni jambo ambalo huibua hisia kali miongoni mwa watu katika kila pembe ya dunia. Kwa mujibu wa M`ngaruthi (2015), unyakuzi wa msitu wa Mau nchini Kenya ni tendo linaloshadidia madhara yanayotokana na unyakuzi wa ardhi ya umma. Hii ilitokana na sababu kuwa eneo lililozunguka msitu huo lilikosa mvua ya kutosha kutokana na vitendo vya viongozi wa kisiasa.  Hali hiyo ya ukame ilisababisha uhaba wa maji na chakula kwa wakazi wa eneo hilo pamoja na mifugo wao. Mtunzi wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* anashadidia maoni ya mtafiti huyu kwa kusawiri hali ya unyakuzi wa ardhi kama ifuatavyo:

Bi. Subira: Mchakato ndio huu uliotuleta hapa. Huwezi kujikomboa kama husemi. Lazima useme. Siku hizi hapa petu watu wanafanya wapendavyo. Miti inakatwa ovyo**.** Watu wanajenga nyumba au makazi bila ya vibali. *Ardhi na viwanja vya watu vinachukuliwa kwa nguvu***.** Watu wanachafua mazingira katika kila eneo**.** Uchafu umejaa uchafu wa kila aina. (Uk 59)

Kinachodhihirika katika mfano huu ni kwamba viongozi wanatenda kila aina ya maovu bila kujali, pakiwemo unyakuzi wa ardhi na viwanja vya watu kwa kutumia nguvu. Zaidi ya hayo, mazingira yanachafuliwa katika kila eneo la jamii iliyosawiriwa. Kama anavyofafanua Alia (2017), uhakiki wa kiekolojia huangazia namna ambavyo uhusiano baina ya binadamu na mazingira unaendelea kuzorota kama matokeo ya ubepari, kiburi na mielekeo hasi kuhusu mazingira. Tendo la unyakuzi wa ardhi ni mojawapo ya vitendo vya kibepari na kiburi kutokana na viongozi kama inavyobainishwa na maneno ya Bi, Subira katika mfano uliotolewa. Kutokana na athari za vitendo hivyo, wananchi wanaamua kuzungumza kuhusu matatizo yao kwa kutambua kuwa huwezi kujikomboa kama husemi. Hivyo, majanga yanayowakabili watu yanawalazimu kukashifu mfumo mzima wa uongozi dhaifu ambao unawatumbukiza katika maafa yasiyokadirika. Kando na janga la ukame, unyakuzi wa ardhi unaweza kuwa chanzo cha masaibu mengi yanayowakumba waathiriwa. Kauli hii imeshadidiwa na mtunzi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* katika dondoo hili:

Mwakilishi wa Mabwanashamba: Tulipwe fidia. Lazima tulipwe nguvu zetu

Mwananchi 1: Mtakubali wananchi? Mtakubali?

Kundi lililobaki: Hatukubali, hatukubali… *Tuko hapa kambini kwa siku. Siku zimekuwa majuma, nayo majuma yamekuwa miezi, miaka na kisha mikaka*. Kila siku hadi kila siku juhudi. Eti kundi la wakubwa linafanya juhudi! *Nasi tuko mahemani tunaumia kwa baridi. Wakimbizi wa ndani, dhuluma, ahadi.* Ahadi tupu zitatufaidi nini? (Uk 71)

Taswira inayobainika katika dondoo hili ni kuhusu uhalisia wa madhila yanayowakumba waathiriwa wa unyakuzi wa ardhi. Imebainika kuwa baada ya ardhi yao kunyakuliwa, wao hulazimika kuishi kambini bila kupata usaidizi wowote. Wao hukaa katika mahema huku wakiumia kwa baridi. Hivyo, wanakua wakimbizi wa ndani

katika nchi yao wenyewe. Viongozi katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi wanawakilisha viongozi wa kisiasa katika mataifa mbalimbali ambao huwapa wakimbizi wa ndani ahadi za kila aina kuhusu utatuzi wa matatizo yao, lakini hazitimizwi. Kwa mujibu wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC, 2014), tangu Kenya kupata uhuru mwaka wa 1963, kumeshuhudiwa ukimbizi wa ndani mara kwa mara uliochochewa na siasa, ukabila na mizozo inayohusiana na suala la ardhi pamoja na maafa na miradi ya kimaendeleo. Aidha, Njeru (2018) alibaini kuwa wakimbizi wa ndani anbao hukimbilia sehemu mbalimbali hasa mijini kwa sababu ya mizozo ya ardhi hukabiliwa na matatizo mengi pakiwemo ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na malazi. Kwa hivyo, suala hili limewekwa wazi na mtunzi wa *Janga la Werevu* ili masilahi ya wakimbizi yaweze kushughulikiwa na serikali ya nchi kama vile kupewa ardhi na fidia ya pesa.

### 4.4.2 Athari za Ukame

Kwa mujibu wa Magharibi (2017), ukame unaweza kuwa na madhara mengi kama vile ya kiafya, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Uchunguzi wa tamthilia teule katika utafiti huu umedhihirisha kwamba watunzi wa tamthilia hizi wameliangazia suala la ukame na kubainisha athari zake katika jamii.

#### 4.4.2.1 Kukauka kwa Mimea

Uchunguzi wa tamthilia teule umebaini kuwa, kuendelea kwa ukame kwa muda mrefu kunaweza kusababisha kuungua na kukauka kwa mimea, jambo ambalo linasababisha baa la njaa miongoni mwa watu wanaotegemea kilimo kwa ajili ya chakula. Hali hii inathibitishwa na mwandishi wa *Janga la Werevu* kupitia mfano ufuatao:

> Busara: …kila siku *tunasoma kwenye magazeti juu ya tatizo la ukame na mazao kuungua na kukauka*. Tunasoma magazetini, na kusikia redioni na kuona kwa macho runingani. *Tunaona hata watoto wakinywa shii ya ng`ombe ili kunusuru uhai wao. Tumeona wanawake wakitafuna magome na kuguguna miti kupata japo mate wameze.* (Uk 28)

Ujumbe unaojitokeza katika mfano uliotolewa ni kwamba tatizo la ukame ni janga ambalo linaangaziwa katika vyombo vya habari pakiwemo magazetini, redioni na kwenye runinga. Hii inatokana na athari zake kama vile kusababisha mazao kuungua na kukauka, jambo ambalo limechangia katika ukosefu wa chakula. Kwa sababu ya

uhaba wa chakula, Busara anasema kwamba hali hiyo ni mbaya kiasi cha kwamba watoto wanakunywa *shii* ya ng`ombe huku wanawake wakitafuna magone na kuguguna miti ili kunusuru uhai wao. Kutokana na athari nyingi za uharibifu wa mazingira ambazo zinaibua misisimko mikali miongozi mwa wanajamii, uhakiki wa kiekolojia unasisitiza kuhusu haja ya kuweka asili na mazingira ya asili katika umakini wa umma kupitia uchunguzi wa kina katika diskosi za kifasihi, utamaduni maarufu na falsafa (Alia, 2017). Hii ni hatua mojawapo katika kusuluhisha athari hizo hasa kwa kuhamasisha umma kuhusu chanzo chake. Uhalisia wa athari hii ya ukame unashadidiwa na utafiti wa Gichure (2017) uliobaini kuwa wakaazi wa kaunti ya Makueni kwa muda mrefu wamekabiliwa na ukame mkali kiasi cha kuifanya mimea yao kukauka, licha ya wao kupanda mimea iliyo na uwezo wa kustahimili makali ya ukame. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba uharibifu wa mazingira unaosababisha ukame unaathiri pia mimea, hivyo kusababisha ukosefu wa chakula.

#### 4.4.2.2 Uhaba wa Chakula

Kuna ushahidi wa kutosha kutokana na tamthilia zilizohakikiwa katika utafiti huu kuwa muda mrefu wa kukosekana kwa mvua unasababisha ukame. Matokeo yake ni uhaba wa chakula kwa binadamu pamoja na viumbehai wengine. Mtunzi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anathibitisha hayo kupitia mfano ufuatao:

> Deka: Usitie shaka. Hapa panatosha kabisa. Wewe unapashuku bure tu. Mnaendelea vipi muda huu wote?
> Bi Siwa: Tunashukuru tumejaliwa uhai. *Tatizo ni hii njaa iliyozidi.*
> Deka: Si mbaya sana hali. Wajua ni *kwa sababu ya msimu huu mrefu wa kiangazi*. (Uk 9)

Kile ambacho mtunzi anasisitiza hapa ni kwamba msimu mrefu wa kiangazi umesababisha njaa kwa sababu mimea waliyopanda katika mashamba yao haikumea, au ilikauka kutokana na mvua kutonyesha. Taswira ya uhaba wa chakula kutokana na kiangazi inaweza kushadidiwa na matokeo ya utafiti wa Simel (2015). Simel (keshatajwa) alibaini kuwa ukame na baa la njaa ni majanga ambayo yameathiri wakazi wa kaunti ya Kitui kwa muda wa muongo mmoja uliopita. Kutokana na maafa hayo, wakazi hao wameteseka sana hasa kutokana na uhaba wa chakula, jambo ambalo limefanya hali yao ya maisha kuwa ngumu. Hivyo, ni wajibu wa serikali kuibua njia

mbadala za kuhifadhi chakula miongozi mwa jamii zinazoathiriwa na ukame ili kuepuka baa la njaa.

Kwa upande mwingine, mtunzi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* ameangazia hali ambapo ukosefu wa lishe bora unaweza kusababisha madhara mengi kwa afya ambapo wanaoathirika zaidi ni watoto wadogo. Baadhi ya madhara hayo yanajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Siki: Tatizo… *la utapiamlo lipo*.
> Waridi: Hilo pia watatuletea sisi hapa? Mpaka sasa wapo watu wasioelewa *umuhimu wa lishe bora*?
> Siki: Kuwepo wapo. Lakini hata katika wanaofahamu, *wapo wasiomudu lishe ya aina yoyote.* Wengi wa watu wetu bado wanaishi kwa kupapatisha. (Uk 6)

Dondoo hili linatoa ithibati kuwa ukosefu wa lishe bora huhatarisha maisha hasa ya watoto kwa kusababisha madhara ya aina mbalimbali. Katika mazungumzo baina ya Waridi na Siki ambao ni wauguzi katika zahanati mojawapo katika Cheneo, Siki anamthibitishia Waridi kuwa licha ya mtoto wa miaka mitatu kudhuriwa na chakula kibovu alichopewa, alikuwa pia na tatizo la utapiamlo. Kwa mujibu wa Tan (2019), Fasihi inazingatiwa kuwa nyenzo mwafaka ya kuleta utambuzi wa mabadiliko katika ekolojia ambayo ingawa ni kwa njia isiyo ya moja kwa moja, inaweza kusaidia na kuchangia katika kubadilisha hali za kijamii na kisiasa. Hali za kijamii ni pamoja na hali za kiafya na za kiuchumi ambazo zinaweza kuimarika kupitia uhifadhi wa mazingira. Vilevile, imebainika kuwa licha ya baadhi ya watu kufahamu umuhimu wa lishe bora, wengi wao hawamudu lishe ya aina yoyote. Hii ndio maana daktari Siki anasema kwamba watu wengi wanaishi kwa kupapatisha. Hivyo, ni wazi kwamba mwandishi anawashutumu viongozi ambao hawawezi kuwasaidia wananchi kutimiza mahitaji yao ya kimsingi kama vile chakula, hasa kwa kudhibiti njia zinazochangia katika hali mbaya ya umaskini.

#### 4.4.2.3 Umaskini

Kwa mujibu wa Maathai (2009), kilimo nchini Kenya kama ilivyo katika mataifa mengi barani Afrika hutegemea mvua wala si mifumo ya unyunyiziaji mashamba maji.

Hivyo, mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri mifumo ya mvua huathiri pia kilimo cha kibiashara pamoja na kile cha kujikimu. Vilevile, Maathai (keshatajwa) anatambua kwamba wakulima wadogo wanaofanyia kazi mchanga ulioharibiwa ni miongoni mwa watu walio maskini zaidi nchini Kenya. Mtunzi wa *Majira ya Utasa* anashadidia maoni haya kwa kusawiri hali ya umaskini kama ilivyo katika dondoo lifuatalo:

> Bi Siwa: Kupata *dhiki na nyingi tabu*, Ni nini yake hasa sababu, *Hali ngumu waja kutusibu*, Ni lipi kosa tulilotenda? *Kutufanya hivi kama ng`onda* ana nyofu leo kuwa pinda?
> Deka: Hodi huku! Wenyewe mpo ndani?
> Bi Siwa: Tupo. Pita ndani. Kumbe ni wewe shemeji! Ajabu hii. Siku hizi ni vigumu kupata wageni…
> Deka: Asante shemeji.
> Bi Siwa: Karibu keti. *Kiti chenyewe hiki cha aibu lakini usijali shemeji*. (Uk 9)

Dondoo hili linaashiria kuwa watu wanakabiliwa na hali ya umaskini. Haya yanathibitika kutokana na wimbo wa Bi Siwa anapoeleza jinsi walivyo na dhiki na taabu nyingi. Katika wimbo wake, Bi Siwa anafafanua namna ambavyo hali ngumu ya maisha inawasibu na kuwafanya kuishi kwa mashaka mengi. Kadhalika, imebainika kwamba hali inayowakabili wanajamii haiwezi kutabirika, jambo linalodhihirika wakati Bi Siwa anaposema kwamba `jana nyofu leo kuwa pinda`. Kwa kusema hivyo, Bi Siwa anarejelea hali ya mabadiliko ya tabianchi ambayo imebadili misimu hasa nyakati za mvua na kiangazi. Kwa mujibu wa Tan (2019), watu wametambua makali na dharura ya ongezeko la joto duniani pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na hali halisi ya majanga haya, hatua madhubuti zinafaa kuchukuliwa ili kupindua majanga haya ya kiekolojia.

Katika dondoo lililotolewa, Bi. Siwa anarejelea athari za majanga yanayowasibu katika jamii kwa kusema kuwa wao wanapitia dhiki na taabu nyingi. Isitoshe, taswira ya hali ya umaskini inadhihirika wakati Bi Siwa anampa Deka `kiti cha aibu` kukalia. Kiti chenyewe ni kikuukuu, jambo ambalo ni ishara ya ufukara uliokithiri. Kama inavyodokezwa na Maathai (2009), ukame hudhoofisha matarajio ya kutokomeza njaa na umaskini uliokithiri. Hivyo ni muhali kutimiza lengo hili la kwanza katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG).

#### 4.4.2.4 Kudidimia kwa Maliasili

Maliasili ni vitu vinavyotokana na maumbile kama vile misitu, maji na madini. Aghalabu maliasili ya nchi huchangia katika utajiri wa nchi husika. (Maathai, 2006). Katika dondoo lifuatalo, mtunzi wa *Majira ya Utasa* anaangazia hali ambapo ukame umechangia katika kudidimia kwa maliasili ya nchi. Katika mfano ufuatao, Bi Siwa anasema:

> Bi Siwa: Watoto saba katika kipindi hiki?
> Siwa: Ugumu uko wapi?
> Bi Siwa: Mwenyewe unaona hali ilivyo. Utahitaji kweli kuelezwa? *Mali asili zetu zinazidi kudidimia siku baada ya siku na maisha kuzidi kuwa magumu!* Afadhali enzi za babu zetu. (Uk 2)

Katika dondoo hili, Bi Siwa anapinga wazo la mumewe la kupata watoto saba. Sababu anayoitoa ni kwamba ni vigumu kuwalea watoto wengi kiasi hicho hasa kutokana na kudidimia kwa maliasili ambazo huipa nchi utajiri mkubwa. Aidha, Bi Siwa anasema ya kwamba katika enzi za mababu zao hali ya maisha haikuwa ngumu, ndiposa watu waliweza kupata na kuwalea watoto wengi. Kile mwandishi anasisitiza hapa ni kwamba, uharibifu wa mazingira unaosababisha ukame unachangia pakubwa katika kudidimia kwa maliasili za jamii, jambo ambalo hufanya hali za maisha za wanajamii kuwa ngumu. Kutokana na hatari inayotokana na mabadiliko ya tabianchi, Njiru (2015) anasema kuwa wakati umefika wa kuunda na kutekeleza hatua za kiteknolojia, kisiasa, kiuchumi na zile za kisheria ili kukabiliana na chanzo na athari za majanga ya kimazingira. Hivyo, ni wajibu wa serikali kuunda sera madhubuti zinazolinda maliasili za taifa ili kuhakikisha ya kwamba hali za maisha ya wananchi zimeboreshwa.

#### 4.4.2.5 Kuathirika kwa Masomo

Katika hali ngumu ya ukame, kunao uwezekano wa elimu ya watoto kuathiriwa. Hii ni kwa sababu ya wazazi na pia serikali kukosa kuhimili na kudhibiti makali ya njaa. (Maathai, 2009). Maoni ya Simel (2015) yanaafikiana na haya kwa kudokeza kuwa janga la ukame linapotokea, watoto hulazimika kuacha masomo kwa sababu ya njaa. Arege katika *Majira ya Utasa* anashadidia maoni ya watafiti hawa kwa kuangazia athari za ukame kwa masomo kama inavyojitokeza katika mfano huu:

Jumbe: …Watu wana watoto wengi ambao hawawezi kuwakimu. Mara ngapi tumewaambia kuwa waache kuzaana kama panya? Rasilimali zetu haziwezi tena kuitosheleza idadi ya watu. *Watoto hawaendi tena shule. Unaona*?

Lulu: Hayo si kweli Jumbe. Tatizo la njaa halitokani na uhaba wa rasilimali wala kuzaa kwa watu. La! *Watoto hawaendi shule kwa sababu ya njaa hii iliyosababishwa na ukame.* Na hili ndilo ninalokuomba uliangalie wewe kiongozi wao. (Uk 37)

Haya ni mazungumzo baina ya Lulu na mumewe Jumbe ambaye ndiye kiongozi katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi. Katika mazungumzo yao, Lulu anamwambia Jumbe kuwa watoto hawaendi shule kwa sababu ya njaa iliyosababishwa na ukame. Hivyo, anamshauri Jumbe kama kiongozi wa jamii hii aliangalie suala hilo. Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, mwanadamu amesababisha uharibifu wa mazingira kupitia vitendo vyake (Rigby, 2002). Hivyo, uharibifu huu umekuwa na athari mbalimbali pakiwemo kuathiri masomo ya watoto. Maathai (2009) anasisitiza kwamba katika muktadha wa janga la ukame nchini Kenya, serikali haiwezi kuwa na matumaini ya kuafikia Elimu ya Msingi kwa Wote kama ilivyo katika Malengo ya Mendeleo ya Milenia (MDG). Kwa hivyo, mwandishi analiweka suala hili wazi ili liweze kushughulikiwa kupitia mikakati inayofaa.

### 4.5 Motifu ya Njaa

Baa la njaa barani Afrika na ulimwenguni kwa jumla linaongezeka kwa kiwango cha kutisha. (Reid, 2021). Miongoni mwa mambo yaliyobainika kuwa chanzo cha baa hili la njaa ni pamoja na janga la COVID 19, vita, ukame, matatizo ya kiuchumi na mabadiliko ya tabianchi. Isitoshe, Reid (keshatajwa) anadokeza kuwa, kufikia mwaka wa 2019, watu milioni mia mbili na hamsini katika Afrika nzima walikuwa wamekabiliwa na njaa, idadi ambayo ni takriban asilimia ishirini ya idadi ya watu wote. Uchanganuzi wa tamthilia teule umebaini chanzo kikuu cha baa la njaa kuwa kiangazi na umaskini unaosababishwa na miundo mibovu ya utawala. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mwandishi anafafanua haya kupitia mfano ufuatao:

Siki: Watu wetu wana shida. Wengine *wanakufa kwa njaa kwa sababu hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi.* Hata sembe na sukuma vinawatoa jasho kuvitia mezani.

Meya: Uongo!

Siki: Kweli. Ni jana tu kitoto kidogo *kimenifia mkononi mwangu kwa njaa na ugonjwa.* (Uk 11)

Kilicho dhahiri kutokana na dondoo hili ni kwamba wanajamii wamekumbwa na njaa hivi kwamba wengine wanakufa. Hii ni kwa sababu hawawezi kumudu mahitaji yao ya kimsingi. Kwa hivyo, ni wazi kwamba watu wamekumbwa na njaa kutokana na umaskini unaosababishwa na mbinu za utawala zisizowafaidi wananchi. Katika dondoo lililotolewa, Meya anawakilisha viongozi katika jamii ambao hutekeleza kila aina ya maovu bila kujali athari za matendo yao kwa wananchi waliowachagua. Kwa msingi huu, Arege anasawiri chanzo cha baa la njaa inayowakumba watu ili kuwapa changamoto viongozi wabinafsi katika jamii. Kando na umaskini, mwandishi wa *Majira ya Utasa* anarejelea hali ambapo kiangazi cha muda mrefu kimesababisha njaa ambayo imeathiri binadamu pamoja na viumbehai wengine. Mfano ufuatao unathibitisha:

| | |
|---|---|
| Deka: | Habari za njaa tunazo lakini si kama hizi unazonipa. Hizi za mizoga si za kweli. |
| Bi Siwa: | Sisi basi hizi zimekuwa ni habari za kawaida. Kila mtu anazijua. *Watoto wa mzee Mona juzi wamepatikana wakila mzoga wa ng`ombe. Hata afadhali wao. Wapo wanaokula mizoga iliyovunda*. (Uk 10) |

Dondoo hili linaashiria kuwa hali ya ukame imesababisha njaa ambayo imeathiri watu pamoja na wanyama. Kutokana na maneno ya Bi Siwa, watu wameathirika kiasi cha kula mizoga ya ng`ombe, jambo ambalo linahatarisha hata afya yao. Kama sehemu ya uwajibikaji wa kiekolojia, binadamu wanapaswa kuepuka aina zote za mashaka ya kiekolojia. Hivyo, ni lazima wakubali ukweli ulio wazi na uhalisia wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na majanga mengineyo ya kiekolojia na kiteknolojia, ili kukabiliana nayo (Njiru, 2015). Katika dondoo lililotolewa, mhusika Deka ambaye ni Rafiki wa karibu wa kiongozi Jumbe anakana uhalisia wa makali ya njaa inayotokana na mabadiliko ya tabianchi, ili kuuficha udhaifu ulio katika uongozi wa Jumbe. Lakini ukweli ulio wazi ni kwamba watu pamoja na wanyama wanakufa kwa sababu ya njaa kama anavyoeleza mhusika Bi Siwa.

Uhalisia wa makali ya njaa unashadidiwa na ripoti ya Sauti ya Amerika (VOA, 31/12/2021) kuhusu maafa ya ukame na njaa Barani Afrika. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mamilioni ya watu barani Afrika hawana uwezo wa kupata chakula cha kutosha.

Somalia ni miongoni mwa mataifa Barani Afrika ambayo yako ukingoni mwa janga la njaa. Nchini Kenya, serikali imetangaza ukame kuwa janga la taifa. Eneo la Kaskazini Mashariki mwa nchi ya Nigeria linakabiliwa na utapiamlo, na njaa imekwishatangazwa katika baadhi ya sehemu za Sudan Kusini. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa maisha ya watu wengi yako katika hatari ya maangamizi kutokana na ukame ikiwa uharibifu wa mazingira hautakomeshwa.Hata ingawa watu wengi wamekabiliwa na baa la njaa, mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* ameonyesha kwamba si kila mtu ameathirika, bali ni yakhe hasa wasiokuwa na ajira. Mfano ufuatao unathibitisha:

> Bw. Binafsi: …Fumbueni macho muone jinsi *ukosefu, njaa na maradhi yalivyojaa dunia nzima. Tazameni majirani. Hawana cha kutegemea. Lakini kwenu vimejaa vitu tele vya manufaa. Mnakula mnachokitaka*. Mnavaa mnavyopenda. (Uk 34)

Bw. Binafsi ni kiongozi katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi. Katika dondoo hili, anawaeleza watoto pamoja na mke wake kuhusu madhila yanayowakabili watu katika jamii isipokuwa hapo kwao nyumbani. Anawafafanulia jinsi ambavyo ukosefu, njaa na maradhi yalivyojaa dunia nzima hata kwa majirani wao. Maneno ya Bw. Binafsi yanadhihirisha ubinafsi alionao kiongozi huyu, ambaye anategemewa na wananchi waliomchagua. Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, ni lazima binadamu ajiepushe na ubinafsi, ubaguzi wa rangi unaopotosha na mabishano ya kijinsia ili kuweza kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira (Njiru, 2015). Kinachodhihirika hapa ni kwamba mtunzi anawashutumu viongozi ambao wanajali masilahi ya familia zao huku wananchi wanaowategemea wakiendelea kuteseka.

Ingawa watunzi wa tamthilia teule wanawalaumu viongozi wanafiki na wabinafsi wasiojali, umma pia unalaumiwa kwa kunyamaza kimya licha ya kujua chanzo cha majanga yanayowakumba. Katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, mwandishi anaeleza:

> Bw. Taja: …Nafasi yetu imepotezwa. Hatusemi tukasikilizwa na mataifa mengine. *Sisi kazi ni kukubali majanga ya wenzetu. Kila siku tunaunga mkono vita vya wenzetu. Vita vya ukandamizaji*. Vita vya maslahi ya watu wengine. Mara vita vya kupigana na magaidi, mara vita dhidi ya silaha za kinyukilia, kisha vita vya ukombozi

> dhidi ya…sasa tunatakiwa tutoe ardhi zetu kulima vyakula vya watu wengine…*wanaendeleza dhana ya zimwi likujualo, nasi tuko kimya*…(Uk 60-61)

Katika mfano huu, mtunzi anashikilia kuwa wananchi pia wanapaswa kulaumiwa kwa majanga yanayowakumba likiwemo janga la ukame na baa la njaa. Hii ni kwa sababu wao wanakubali kupotoshwa na viongozi bila kuuliza swali lolote. Wao wanaunga mkono kila jambo linalopendekezwa na viongozi hata kama linaangamiza wenzao. Hili ni dhihirisho tosha la ujinga wa umma ambao wanawatukuza viongozi wanaowadhulumu. Ndiposa mwandishi anamtumia mhusika Mpya ambaye analeta mwamko mpya katika jamii na kuzindua umma kuhusu haja ya kusema waziwazi bila woga. Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, kazi za kimazingira zinapaswa kuonyesha njia mbadala za kuponya jamii kutokana na athari za uharibifu wa mazingira (Buell, 2005). Hivyo, imebainika kwamba uzidushi wa umma ni njia mbadala ambayo inaweza kutumiwa kutetea mazingira yanayoharibiwa.

Kutokana na baa la njaa, chakula kimekuwa ghali kupatikana. Mohamed anasawiri hali hii katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* kama ifuatavyo:

> Bi Subira: …Ardhi zinauzwa au zinakodishwa kwa miaka mia mbili. *Chakula kimekuwa ghali kupatikana. Kila mtu analia njaa, njaa, njaa na mashamba tunayo. Hivi leo tunaagiziwa vyakula vya GMO`s kwa ajili ya kuzima fujo za matumbo yetu.* Na wanaoagiza ni walewale walioyarithi mashamba yenye rutuba na wasiyoyalima. Ni walewale wenye kuunda sheria za kumaliza njaa huku wakitilia mbolea njaa na ukata… (Uk 59-60)

Katika mfano uliotolewa, Bi Subira anaeleza kuhusu masaibu yanayowakumba watu katika jamii. Anaeleza jinsi ambavyo kila mtu analia njaa licha ya kuwa wao wana mashamba. Hii inamaanisha kwamba huenda uharibifu wa mazingira umesababisha mazao yao kuharibika, jambo ambalo limechangia katika uhaba wa chakula. Aidha, imebainika kwamba viongozi wanachukua ardhi ya wananchi kwa manufaa ya kibinafsi. Kadhalika, viongozi hao wanawaagizia wananchi chakula cha *GMO`s,* ambacho kinaweza kudhuru afya yao. Hivyo, mwandishi anawashutumu viongozi wanafiki ambao licha ya kuunda sheria za kumaliza majanga yanayowakumba wananchi, ndio wanaozidisha hali hiyo huku wakijifanya kuwa wanawashughulikia.

Baada ya kushindwa kuhimili makali ya njaa, kilichosalia ni wananchi kuomba na kutegemea chakula cha msaada kutoka kwa serikali na mashirika mengine. Hata hivyo, mara kwa mara misaada hiyo huwa haiwafikii waathiriwa. Arege anasawiri hali hii katika *Majira ya Utasa* kama ifuatavyo:

> Bi Siwa: Atafanya nini? Wajua si kama nyinyi mnaofaidi kwa hao wakubwa. *Misaada haifiki huku. Na tukiifuata hiyo misaada huko inakofika mara nyingi utarudi bila kitu*.
>
> Deka: Siku hizi si kama zamani. Hali ya uchumi imekuwa ngumu ingawa *bado kipo kiasi kidogo cha misaada. Serikali na mashirika wamepunguza kiwango cha misaada*. Wanataka watu kuanza kubuni mikakati ya kujitegemea wenyewe. (Uk 13)

Maneno ya Bi Siwa katika dondoo hili yanabainisha wazi kuwa misaada ya chakula ambayo hutolewa ili kuwafaidi wananchi, wakati mwingine huwa haiwafikii. Deka anawakilisha watu walio na uhusiano wa karibu na viongozi ambao ndio hufaidika kutokana na chakula cha misaada ya wananchi. Hali hii ni kisababishi cha mipaka ya kitabaka baina ya maskini na matajiri kuendelea kuwa mipana kila uchao. Nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inadokeza kuwa, watu wote wameathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na uharibifu wa mazingira bila kujali tabaka, hali ya kiuchumi, siasa au hata viwango vya elimu (Nabeta na 0ngutte, 2014).

Katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa*, viongozi wanajitenga na wananchi huku wao wakiendeleza shughuli zinazochangia katika kuharibu mazingira. Hali ya kutojali umma inajitokeza wakati hata vyakula vya misaada haviwafikii wananchi, bali viongozi wanaficha ili wavitumie katika kufanya biashara. Ili kuficha ufisadi wa viongozi, Deka anamtetea Jumbe kwa kusema kuwa serikali na mashirika wamepunguza kiwango cha misaada. Huu ni ufisadi wa viongozi ambao mtunzi wa *Majira ya Utasa* anakashifu. Hivyo, ni wajibu wa kila mtu kuhusika katika uhifadhi wa mazingira bila kujali tofauti hizi za kijamii.

Hata ingawa marafiki wa karibu wa viongozi wanajaribu kuficha maovu ya viongozi huku wakiwahadaa wananchi kuwa wanashughulikiwa, imebainika kwamba uongo huu huwa wa muda tu. Hii ni kwa sababu wananchi wanapogundua ila za viongozi hao

hawana budi kuzifichua hadharani ili waweze kusikilizwa. Katika *Majira ya Utasa*, mhusika Kato anasema:

> Kato: Iwe *tamaa ama ujinga au chochote kingine kiwacho.* Ninaanza kushawishika kuwa karibu tutahitaji kwenda kumwona Jumbe kwa lazima. *Tumeomba kuonana naye vya kutosha huku watu wetu wanakufa*. Si viwanda hatari, si uangamizaji wa vyanzo vya maji, *si kwa kuiba misaada ambayo ingetupa tumaini la kuiona kesho*. Na yeye *anafikiri sisi hatuyajui yote haya*. (Uk 67)

Ujumbe unaodhihirika hapa ni kwamba wakati umefika ambapo baadhi ya wanajamii wamegundua maovu wanayofanyiwa na viongozi. Ndiposa Kato anashutumu maovu kama ya wizi wa vyakula vya misaada, ambavyo kwa maoni yake vingewapa tumaini la kuiona kesho. Kwa hivyo, kile ambacho mtunzi anasisitiza hapa ni kwamba maovu ambayo viongozi huwatendea wananchi hayawezi kufichika daima. Akieleza umuhimu wa uhakiki wa kiekolojia katika kupambana na uhalifu na majanga ya kiekolojia, Schatz (2012) anadai kwamba, wahakiki wa kiekolojia wanaweza kutumia diskosi za fasihi katika kupambana na nguvu za kiserikali zinazosababisha uharibifu wa mazingira, hasa kwa kuhamasisha watu kuhusu haja ya kupigania maisha bora ya baadaye.

Kutokana na mtazamo huu, mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anathibitisha kuwa, wakati umefika ambapo wananchi wanaamua kurekebisha hali ya mambo kwa lazima ili kuinua hali zao za maisha. Uhalisia wa wizi wa chakula cha misaada unashadidiwa na ripoti ya Matheka (2021) inayoanika mbinu chafu ambazo maafisa wa serikali hutumia kuficha ufisadi huku wakisingizia kuwa wanalenga kusaidia maskini. Kadhalika, mara kwa mara hutumia hali ya ukame na mafuriko kutenga na kuomba misaada ya mabilioni ya pesa ambazo huwa zinaporwa huku waathiriwa wakiendelea kuteseka na hata kufariki kutokana na njaa na maradhi.

### 4.6 Motifu ya Kifo

Kifo ni tendo au uyakini wa kufariki; ni mwisho wa maisha; hatua ya mwisho ya kutoweka kwa ufanyikazi wa kimsingi wa viungo vya mwili vya mnyama au miti. Vilevile, kifo ni hali ya ufu; hali ya kutokuwa na maisha ama kutoweza kutekeleza shughuli yoyote (Odongo, 2014). Uchanganuzi wa tamthilia teule umebaini kuwa waandishi wamesawiri kifo kwa namna mbalimbali. Hivyo, waandishi hawa

wameangazia kwa kina chanzo cha vifo hivyo vinavyowakabili binadamu, wanyama pamoja na viumbehai wengine. Vifo vilivyosawiriwa katika tamthilia teule, vimesababishwa na mambo mbalimbali. Hivyo, kwa maoni ya waandishi wa tamthilia hizo, vifo vinaweza kusababishwa na njaa, kula chakula kibovu, sumu na kiangazi.

### 4.6.1 Ukosefu wa Chakula

Vifo kutokana na njaa vimetawala kwa mapana na marefu katika tamthilia teule. Mwingiliano katika usawiri wake unadhihirisha uzito wa suala la kifo kinachosababishwa na njaa kwa mtazamo wa watunzi wa tamthilia zilizoteuliwa katika utafiti huu. Katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*, dondoo lifuatalo linashadidia:

> Bi Siwa: Hali yenyewe ipo sana lakini ilivyo kawaida, Mwenye shibe hamjui mwenye njaa. Wewe leo umeshiba maana uko karibu na mamlaka. Na kwa kuwa umeshiba, kila mmoja ameshiba vilevile. Umesahau mara kwamba *nyanyako mwenyewe amekufa kwa hiyo hiyo njaa miaka mitatu iliyopita*?
>
> Deka: *Hata! Si kweli. Si kweli hata kidogo*. Nyanyangu amekufa kwa ugonjwa ila kwa kuwa alikufa wakati wa kiangazi watu walifikiri kuwa alikufa kwa njaa. (Uk 12)

Katika mfano huu, Bi Siwa anafichua unafiki wa viongozi na watu wenye uhusiano wa karibu na viongozi hao. Anamshutumu Deka kwa kujifanya kuwa hajui kuhusu njaa inayowakabili watu, kwani yeye pia ni mwenyeji katika jamii husika. Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba watu ambao hufaidika kutokana na serikali ni wale walio karibu na mamlaka tu, huku wananchi wa kawaida wakiangamia. Bi Siwa anamkumbusha Deka kuwa nyanyake mwenyewe alikufa miaka mitatu iliyopita kutokana na njaa, jambo ambalo Deka analikana. Hii ndio maana Glotfelty 2005) anasema kwamba ` tumefikia nyakati za mipaka ya kimazingira`. Kwa kusema hivyo, Glotfelty (keshatajwa) anarejelea wakati ambapo athari za matendo ya binadamu yameharibu mfumo wa msingi wa maisha katika Sayari. Kama inavyoshadidiwa na dondoo lililotolewa, vifo vinavyotokana na makali ya njaa ni dhihirisho la hali ya kufikia mipaka ya kimazingira ambayo Glotfelty (keshatajwa) anazungumzia.

Hali hii inashadidiwa na ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN, 2020) inayodokeza kwamba, idadi ya watu wenye njaa barani Afrika inaendelea kuongezeka, ikichochewa na uwepo

wa migogoro, mabadiliko ya tabianchi, kuzorota kwa uchumi na janga la COVID-19. Kadhalika, imeendelea kueleza kwamba njaa katika bara la Afrika imekuwa mwiba tangu mwaka 2013, na kuzorota zaidi kati ya 2019 na 2020 huku hali ikitarajiwa kuwa mbaya zaidi mwaka wa 2021. Hata hivyo, hakuna matumaini yoyote ya kupunguza njaa inayosababisha vifo. Kwa hivyo, ni muhimu kwa nchi kuwekeza katika kilimo na sekta nyinginezo zinazohusiana, na vilevile katika huduma za maji, afya na elimu ili kupunguza vifo vinavyosababishwa na njaa. Kwa kufanya hivyo, serikali ya Kenya itaweza kutimiza mojawapo ya Agenda Nne Kuu inayohusu usalama wa chakula kufikia mwisho wa mwaka wa 2022.

### 4.6.2 Kula Chakula Kibovu

Uhaba wa chakula unapotokea, waathiriwa huwa hawana budi kufanya kila wawezalo ili kupata chochote cha kujikimu. Matokeo ni kwamba huenda wanachokula kikadhuru afya yao na kusababisha vifo. Arege anaangazia hali hii katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Majira ya Utasa* kama ifuatavyo:

> Siki: Iwapo umefanya, yapo mengi ambayo hayakunyoka. Yanakungoja wewe na wenzako kuyanyoosha. *Watu hii leo wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu*! Watu wako ndugu Sosi. Watu unaowaongoza wewe. (*Mstahiki Meya*, Uk 12)
>
> Bi Siwa: Mizizi ndiyo. Inasaidia kusukuma siku kwa kupitiliza mara moja moja. Na wewe unafahamu. Na wewe si mgeni wa kuambiwa kuwa yenyewe hiyo mizizi haipatikani hivi hivi. Lazima kuitolea jasho. Tena nayo sasa imetushinda. *Huwa yanitia wasiwasi maana wakati mwingine inaweza kuua. Watoto wa jirani hivi majuzi wamekufa kwa kula hiyo mizizi.* Sasa tunaichelea. (*Majira ya Utasa*, Uk 13)

Dondoo zilizotolewa zinaonyesha jinsi ambavyo ukosefu wa lishe bora unaweza kuwafanya watu kula vyakula vinavyowadhuru na hata kusababisha vifo. Katika *Mtahiki Meya*, Siki anazungumzia kiongozi Meya ambaye uongozi wake mbaya umesababisha maangamizi kwa wananchi waliomchagua. Siki anamkumbusha kuwa watu anaowaongoza wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu, jambo ambalo anasema kwamba linahatarisha uongozi wa Meya kwa kuwa watu hao hawajaridhishwa na uongozi wake. Kadhalika, katika *Majira ya Utasa*, Bi Siwa anamweleza Deka ambaye ni mfanyakazi wa kiongozi Jumbe kuwa watu wanateseka kwa sababu ya njaa.

Hivyo, hali imekuwa mbaya kiasi cha wao kutegemea mizizi na matunda mwitu ambayo pia haipatikani kwa urahisi kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mifano iliyotolewa imebainisha wazi kuwa hali za kiuchumi kwa wananchi wa kawaida ni mbaya kiasi kwamba hawawezi kutimiza mahitaji yao ya kimsingi. Uhalisia wa vifo hasa vya watoto vinavyotokana na ukosefu wa lishe bora unashadidiwa na maoni ya Maathai (2009) anayesisitiza kwamba, serikali inapaswa kuwajibika na kujukumika ili kutafuta mbinu mbadala za kuhakikisha kuwa kuna uhifadhi wa chakula nchini. Hii ni kwa sababu ukosefu wa lishe bora uliokithiri unapunguza uwezekana wa kutimiza lengo la nne katika Malengo manane ya Maendeleo ya Milenia (MDG), ambalo linahusu upunguzaji wa vifo vya watoto vinavyohusishwa na ukosefu wa lishe bora.

### 4.6.3 Kiangazi

Uchanganuzi wa tamthilia teule umebainisha kuwa hali ya kiangazi husababisha vifo. Aidha, utafiti huu unaonyesha kuwa hali hiyo ya kiangazi katika jamii na hasa katika kiwango cha kitaifa imeanza kuchochea maudhui yanayohusu athari za uharibifu wa mazingira katika tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili, pakiwemo tamthilia. Mathalani, suala la kiangazi ndilo linaloangaziwa zaidi katika tamthilia za *Majira ya Utasa* na ya *Janga la Werevu.* Licha ya kuwa tamthilia hizi zimetungwa na watunzi tofauti, uhusiano wa jinsi ambavyo wamelisawiri suala la kiangazi ni dhihirisho tosha la uzito wa athari zake katika taifa na ulimwengu kwa jumla. Katika *Majira ya Utasa,* mfano ufuatao unathibitisha:

> Bi Siwa: Sasa mimi nitayajuaje mume wangu?
> Siwa: Wewe waona mchezo lakini mimi nionavyo ni kuwa *ni vigumu kupata watoto wawili wakaishi hadi kuwa watu wazima katika mazingira haya. Wamekufa watoto wangapi hapa kijijini kwa sababu ya hiki kiangazi?* Haina haja kuwataja maana haya wayajua wewe vizuri. Kwa nini tu… (Uk 27)

Katika dondoo hili, kilicho dhahiri ni kwamba hali ya kiangazi imesababisha madhara mengi katika jamii iliyoangaziwa na mwandishi. Siwa anapompendekezea mke wake Bi Siwa kuwa angetaka wapate watoto saba, mkewe anamkumbusha kuwa ni vigumu kuwalea hata watoto wawili katika mazingira hayo magumu. Kwa mujibu wa Tan (2019), mabadiliko ya tabianchi ni tishio kubwa hasa kwa vizazi vijavyo. Kwa maoni

yake, ardhi itaendelea kuwa suala muhimu la mabadiliko ya kimazingira isipokuwa hatua kubwa na ya kudumu ichukuliwe na mataifa mengi yaliyoendelea.

Kutokana na maneno ya Bi Siwa, watoto wengi wamekufa katika kijiji chao kwa sababu ya kiangazi. Hivyo, ni wazi kwamba wanaoathiriwa zaidi na kiangazi ni watoto. Hali ya kuathirika kwa watoto kutokana na njaa ni ishara ya tishio la kuwepo na vizazi vya baadaye ambavyo vinaweza kutegemewa. Hii ndio maana mwandishi wa *Majira ya Utasa* anaangazia suala hili ili liweze kushughulikiwa upya. Katika *Janga la Werevu,* mwandishi anasawiri vifo vinavyotokana na kiangazi kama ifuatavyo:

> Kicheko cha Mwendawazimu: Itazame Serengeti, siku hizi hainywishizwi tena. Kongoni wana hatihati. *Mamba wamekufa. Huwapati mwewe na bata, hawana bahati, hakuna waliobaki,* na waliobaki wamekonda kama ng`onda. (Uk 22)

Katika mfano huu, tunapata taswira ya athari za kiangazi hasa katika Serengeti ambapo wanyama wengi wamekufa. Vifo vya mamba vinadhihirisha kuwa maji ya mito yamekauka kutokana na kiangazi. Navyo vifo vya wanyama kama vile kongoni, mwewe na bata vinatoa ushahidi wa kuwa hata miti na mimea nyingine itumiwayo na wanyama kama chakula haipo tena. Kwa hivyo, ni wazi kwamba kiangazi hakiathiri binadamu tu bali pia wanyama wa aina mbalimbali. Kama inavyodokezwa na nadharia inayoongoza utafiti huu, uhakiki wa kiekolojia unahusu uhamasishaji wa wanajamii kuhusu kubadilisha mielekeo na mienendo yao kuhusu mazingira (Culler, 2011). Kwa msingi huu, waaandishi wa *Majira ya Utasa* na *Janga la Werevu* wanalenga kuhamasisha jamii kuhusu namna ya kuhifadhi mazingira ili kuzuia madhara yanayotokana na kiangazi.

### 4.6.4 Kemikali

Uhakiki wa tamthilia teule umebaini kuwa matumizi ya kemikali hatari katika viwanda husababisha vifo vya binadamu na wanyama. Katika *Majira ya Utasa*, madhara ya kemikali hizi yamekuwa dhahiri katika jamii hivi kwamba watu wameungana ili kulalamikia suala hili kwa viongozi.  Mwandishi amesawiri vifo vya wanyama kutokana na kemikali kupitia mfano ufuatao:

Siwa: Haya sikiliza. Siku za nyuma tulipotoka kwenda baharini, *tulikuwa tunawakuta samaki chekwa waliokufa wanaelea majini. Takriban wote wamebambuka bambuka! Wengi wamefura!* Wavuvi wenye utundu waliwapasua. Utumbo wa kila waliyempasua ulikuwa na vidonda vikubwa mfano wa kuchomeka huku wanatoa harufu ajabu.

Bi Siwa: Alaa! Na mlipata kugundua wanachomwa na nini?

Siwa: Sisi wavuvi tuna lipi tulijualo! (Uk 22-23)

Mfano uliotolewa unatupa taswira ya jinsi samaki wengi walivyokufa. Kutokana na maneno ya mvuvi Siwa, ni dhahiri kwamba samaki hao walisumishwa na kemikali iliyoachiliwa baharini kutoka kwenye viwanda vya maua vya Jumbe, jambo lililosababisha kifo chao. Hivyo, hii ni mojawapo ya sababu ya uhaba wa samaki baharini. Ushahidi zaidi wa vifo vinavyotokana na athari za kemikali unajitokeza katika mfano ufuatao:

Dosho: Sisi ni wajinga kwa kutazama mkiharibu mazingira yetu! Ni wajinga kwa kunyamaza watu wetu wanapolipwa pesa nane kwa jasho la kutwa! Sisi wajinga? *Sisi wajinga watu wetu wafa kwa hilo sumu la hema zenu. Ndiyo, sisi wajinga.Wajinga kwa kutazama tu mnaposumisha samaki wetu ambao hutuhasiri sisi hatimaye.*

Deka: Aliyewalazimisha watu kufanya kazi mashamba yetu ya maua nani? (Uk 53)

Katika mfano huu, Dosho analalamikia mazingira yao yaliyoharibiwa kupitia shughuli mbalimbali za viongozi. Kadhalika, vifo vya watu kutokana na matumizi ya kemikali katika mahema ya maua ni thibitisho la athari za uharibifu wa mazingira. Zaidi ya hayo, ni wazi kwamba hata samaki wameathiriwa na kemikali zizo hizo, jambo linalothibitishwa na Dosho anaposema kuwa samaki ambao huwahasiri hatimaye pia wamesumishwa na kemikali. Kinachodhihirika hapa ni kwamba watu wanaweza kufa kwa sababu ya madhara ya kemikali ya moja kwa moja au kupitia ulaji wa samaki waliosumishwa na kemikali hizo. Garrard (2007) anaeleza kwamba, teknolojia inaweza kuharibifu mazingira kwa namna ambayo huibua wasiwasi kwa umma, hasa kwa sababu ya majanga yanayotokana na athari za uharibifu huo. Wasiwasi wa wanajamii unabainika katika mfano uliotolewa, ambapo Dosho anahofu kwamba huenda kukawa na madhara zaidi kutokana na athari za kemikali iwapo hali haitabadilika. Ndiposa Dosho anamlaumu Deka pamoja na viongozi wengine kwa kuharibu mazingira.

Athari za kemikali kutoka kwenye viwanda kama vile vya maua, zinadhibitishwa na utafiti wa Maosi (2020). Alibaini kuwa, maisha ya samaki katika ziwa Nakuru yanakuwa hatarini kwa sababu wamiliki wa mashamba ya maua, hupulizia mimea yao kemikali kupita kiasi ambazo hatimaye husombwa na maji hadi ziwani. Hii ni hatari kwa ziwa Naivasha ambalo ndilo la kipekee linalotegemewa katika sehemu ya Mashariki ya Bonde la Ufa hasa katika uvuvi. Kwa hivyo, mwandishi wa *Majira ya Utasa* analenga kuhamasisha wanajamii kuhusu madhara ya kemikali zinazotumiwa katika viwanda mbalimbali pakiwemo vile vya maua, ili jambo hilo liweze kushughulikiwa.

### 4.7 Hitimisho

Sura hii imebainisha aina mbalimbali za motifu za kimazingira ambazo zimejitokeza katika tamthilia teule. Mbali na kubainisha motifu za kimazingira, mtafiti amechunguza jinsi ambavyo waandishi wa tamthilia teule wamezisawiri kwa lengo la kuangazia chanzo na athari za uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, uhakiki wa tamthilia teule umethibitisha kuwa, waandishi wametumia motifu hizo kuweka wazi kiubunifu matatizo ya kimazingira ambayo yameathiri watu katika kila pembe ya duniani.

# SURA YA TANO

# MTINDO KATIKA USAWIRI WA MOTIFU ZA KIMAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE

### 5.1 Utangulizi

Sehemu hii inashughulikia madhumuni ya pili ya utafiti huu ambayo ni kujadili jinsi mtindo ulivyotumika katika kusawiri motifu mbalimbali za kimazingira. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kurejelea tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege, ambazo ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*)*, *Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). Kwa mujibu

wa Wamitila (2003), dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Hivyo, uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha miongoni mwa nyingine. Kutokana na msingi huu, wasanii wa tamthilia teule wametumia mbinu mbalimbali katika kusawiri motifu za kimazingira. Mbinu zinazojitokeza katika tamthilia teule ni pamoja na jazanda, kinaya, taswira, majazi, nyimbo, kejeli, ushairi, chuku, tashbihi, sitiari na mbinu rejeshi.

## 5.2 Jazanda

Jazanda ni istilahi ambayo hutumiwa kuelezea sifa za matumizi ya picha katika kazi za kifasihi (Wamitila, 2003). Kwa hivyo, mbinu hii hutumiwa na waandishi katika kusawiri mambo mbalimbali ambayo ni fiche katika jamii. Waandishi wa tamthilia teule wametumia jazanda kama mtindo wao katika kusawiri motifu za kimazingira. Jazanda zilizobainika kutokana na uchanganuzi wa tamthilia hizo ni pamoja na jazanda ya Mpya, Jazanda ya janga la werevu, jazanda ya unajisi, jazanda ya jipu, jazanda ya ugonjwa wa Kristy, jazanda ya majira ya utasa *na* jazanda ya ndoto ya Kato.

### 5.2.1 Jazanda ya Mpya

Katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, mtunzi ametumia mhusika Mpya kijazanda. Mpya ni kitinda mimba wa Bi. Shoo na Bw. Binafsi. Licha ya kuwa Bw. Binafsi ni kiongozi aliyechaguliwa na wananchi katika jamii iliyosawiriwa, uongozi wake wa muda mrefu umekuwa wa kidhalimu. Ubinafsi wake umetumbukiza nchi anayoitawala katika matatizo mengi. Hata hivyo, kuzaliwa kwa mtoto wake Mpya kunaleta mwamko mpya katika jamii. Mwandishi anadhihirisha jambo hili kupitia mfano ufuatao:

| | |
|---|---|
| Mpya: | *Umeshafika…Umeshafika…Umeshafika wakati wa kusema ingawa mimi peke yangu sina uzito wa kusema.* Mimi msema pweke. Kusema ni haki ya uzawa kwa kila kiumbe, binadamu hata wanyama. Natamani siku moja kila mtu aseme atoe madukuduku yake. |
| Sauti Ndani ya Kisima: | Ishara njema…Ishara njema… Ishara njema… Njema, njema, njema, ishara njema. *Tulikutaraji. Sasa wakati umeshafika. Njoo uliyekuwa ukitarajiwa. Njoo uliyengojewa.* Njoo, njoo, njoo… |

Njoo polepole, njoo kwa uhakika, njoo
Tukunyweshe maji ya ujasiri…(Uk 20-21)

Ujumbe unaojitokeza katika mfano uliotolewa ni kwamba mhusika Mpya ndiye anawakilisha mwanzo wa harakati za ukombozi. Hii inatokana na maneno yake anaposema kwamba wakati wa kusema umeshafika. Aidha, anasema kwamba yeye ni msema pweke, hivyo anazindua umma kwa kuwaonyesha haja ya kuwa na umoja ili waweze kufaulu katika azma yao. Vilevile, ari ya kuwepo na mapinduzi dhidi ya utawala dhalimu inadhihirika wakati Mpya anaposema kuwa kusema ni haki ya uzawa wa kila kiumbe, binadamu au hata wanyama. Umuhimu wa kuzaliwa kwa mhusika Mpya unadhihirika pia kutokana na sauti ndani ya kisima katika mfano uliotolewa. Kutokana na sauti hiyo, inadhihirika kwamba kufika kwa Mpya ni ishara njema na kwamba ndiye aliyekuwa akitarajiwa ili kuanzisha harakati za kuikomboa jamii dhidi ya udhalimu pakiwemo uharibifu wa mazingira.

Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia iliyoongoza utafiti huu, uhakiki wa kiekolojia unahusu uhamasishaji wa wanajamii kuhusu kubadilisha mielekeo na mienendo yao kuhusu mazingira (Culler, 2011). Mhusika Mpya anahamasisha jamii kuhusu haja ya kutetea mazingira yao yaliyoharibiwa kupitia vitendo vya viongozi. Isitoshe, Mpya anawakilisha mwamko mpya katika jamii unaoongozwa na vijana. Umuhimu wa vijana katika harakati ya kuhifadhi mazingira unadhihirika kupitia ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN, 2020), kuhusu umuhimu wa vijana wa kiafrika katika majadiliano ya kimataifa kuhusu mazingira. Kutokana na ripoti hiyo, wakati umefika wa vijana Waafrika kuzungumza, kuhamasisha na kuchukua hatua katika michakato ya kimataifa kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi, hasa wakati tunapoingia muongo wa mwisho wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Kwa hivyo, ni wazi kwamba mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* amemtumia mhusika Mpya katika tamthilia hii ili kuonyesha nafasi ya vijana katika harakati ya uhifadhi wa mazingira.

### 5.2.2 Jazanda ya Janga la Werevu

Mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* ametumia kichwa `Janga la Werevu` kijazanda. Uchanganuzi wa data katika tamthilia hii umebaini kuwa watu wa jamii iliyosawiriwa na mwandishi wamekumbwa na majanga mengi ambayo yanatokana na

kuwafuata kiholela watu wanaojiita `werevu`. Katika mfano ufuatao, Mwendawazimu anatoa kejeli zake kwa hadhira huku akiwafafanulia chanzo cha masaibu yanayowakumba katika jamii. Anasema:

> Mwendawazimu: …Tazama *ukame na ukavu unavyokithiri barani Afrika… Na kama si ukame basi mafuriko yanayomfunika binadamu mwenyewe na kuharibu mali zake…* Angalia yanayotokea Pakistan, Haiti, China, Amerika ya Kusini Tazama hapa kwetu: Turkana, *budalangi*, vifo vya samaki ziwa-ni Naivasha, Rufiji, Kivu, Zambezi Nile… *Dunia tunaichafua wenyewe kwa kuwafuata wanaojiita werevu*; wale wanaojigamba kuwa wameendelea…(Uk 12-13)

Kupitia maneno ya Mwendawazimu, mwandishi anaeleza kuhusu matatizo yanayotokana na uharibifu wa mazingira, kama vile ukame na mafuriko yaliyo na athari kubwa kwa binadamu, mimea pamoja na viumbehai wengine. Aidha, maneno yake katika mfano huu ni ushahidi tosha wa majanga yanayowakabili watu katika kila pembe ya dunia pakiwemo Pakistan, Haiti, China, Amerika ya Kusini pamoja na Afrika. Haya yanathibitishwa na Sangili (2015) anaposema kuwa, athari za uharibifu wa mazingira ziko kote duniani. Anatoa mfano wa mataifa ya Afrika ambapo watu wanaaga kwa njaa, Asia watu wanakufa kutokana na kabobo za *Tsunami,* Marekani wanatilifiwa kutokana na mafuriko na vilevile Bara Uropa wanaathirika kutokana na mipigo ya joto kali. Hili ni dhihirisho la kwamba tishio la athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira linahusu kila binadamu kote ulimwenguni.

Kwa msingi huu, Glotferty na Fromm (1996) wanasema kwamba vita dhidi ya uharibifu wa mazingira ni jukumu la kila mtu kote ulimwenguni, kwani kila mja ameathirika. Ili kuonyesha uzito wa hali ya kutojali kwa baadhi ya wanajamii ambao wanachangia katika kuharibu mazingira, Mwendawazimu anatoa mfano wa vifo vya samaki vinavyoshuhudia ziwani Naivasha, Rufiji na Zambezi. Vilevile, Mwendawazimu anaeleza hadhira kuwa mambo hayo yote yanatokana na wanajamii wenyewe kwa kuwafuata wanaojiita `werevu`. Werevu katika muktadha huu ni wazungu ambao wanatumia mbinu za kisasa za uzalishaji mali, kama vile matumizi ya kemikali hatari kwenye viwanda vyao, ambazo zinachafua hewa pamoja na kuhatarisha maisha ya binadamu na viumbehai wengine.

`Werevu` pia unarejelea viongozi wa kiafrika wabinafsi ambao wanaharibu mazingira kupitia njia mbalimbali kwa manufaa yao wenyewe bila kujali athari za uharibifu huo. Wahusika Bamkuu na Bimkuu wanawakilisha viongozi katika jamii ambao wanatekeleza kila aina ya maovu kwa manufaa ya kibinafsi bila kujali umma, pakiwemo unyakuzi wa ardhi na ukataji wa miti unaosababisha uhaba wa maji katika taifa nzima. Hali hii inaweza kuthibitishwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia kuwa, mwanadamu anasababisha uchafuzi wa mazingira kupitia vitendo vyake licha ya kufaidika kutokana na mazingira hayo (Rigby, 2002). Ndiposa mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* anatahadharisha dhidi ya kufuata na kuiga mambo ya watu wengine kiholela bila kufikiria madhara yake.

### 5.2.3 Jazanda ya Unajisi

Hali ya unajisi imetumiwa na mwandishi wa *Janga la Werevu* kijazanda. Matumizi ya neno `unajisi` ili kuwakilisha aina mbalimbali za uharibifu wa mazingira inaonyesha uzito na kina cha uharibifu huo na athari zake kwa jamii. Hivyo, mwandishi wa tamthilia hii ameangazia aina mbili za unajisi ambazo ni unajisi wa maji na unajisi wa hewa. Licha ya kuwa maji ni muhimu katika shughuli za kila siku za binadamu, wanyama na mimea, vitendo mbalimbali vya binadamu vimesababisha uchafuzi na uhaba wake. Matokeo ni magonjwa, umaskini, njaa na vifo miongoni mwa madhara mengine. Kutokana na athari hizi, mwandishi anarejelea uchafuzi wa maji kama unajisi. Katika uk. wa 22, mwandishi anasema:

> Kiu za mwili na roho sasa zaongoza kwa uchache wa maji na maji yaliyopo yamejaa sumu za viwanda. Viwanda vya madawa, viwanda vya karatasi, viwanda vya kusafisha madini, mito imegeuka maji taka, *pwani na bahari zimenajisiwa.* (Uk 22)

Kinachodhihirika katika mfano uliotolewa ni kwamba kuna uhaba wa maji, hali inayosababisha kiu za mwili na roho pia. Licha ya kuwa na uhaba wa maji, yale machache yanayopatikana yamejaa sumu kutokana na viwanda vya madawa, vya karatasi na vya kusafisha madini. Isitoshe, mito na bahari zimegeuzwa maji taka kupitia huo uchafuzi. Kwa hivyo, maji `yamenajisiwa` kupitia shughuli mbalimbali za binadamu na kuachwa yakiwa na uchafu mwingi. Kwa mujibu wa Schlosberg (2007), binadamu anapokatiza, kufisidi au kunajisi uwezo wa kufanya kazi wa mfumo wa

ekolojia, huwa ni ukosefu wa haki si tu kwa binadamu bali pia kwa viumbe wengine ambao hutegemea uwezo wa mfumo wa ekolojia kwa utendakazi wao wenyewe.

Hali hii inaangazia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mazingira, ambayo Tarton na Henwood (2002) wanaeleza kuwa binadamu, mazingira na viumbe wengine huhusiana kwa namna ya kutegemeana na kukamilishana. Hivyo, mwandishi wa *Janga la Werevu* anasawiri hali ambapo uchafuzi wa maji unaweza kuathiri binadamu pamoja na viumbe wengine kwa lengo la kuweka wazi jambo hili, ili liweze kushughulikiwa na hatimaye kuepuka madhara zaidi. Akisisitiza kuhusu athari za kemikali kutoka kwenye viwanda, Abdallah (2013) anasema kwamba sumu za kemikali kutoka kwenye viwanda mbalimbali huathiri binadamu pamoja na viumbehai wengine hasa wale waishio majini, jambo ambalo husababisha vifo vya wanyama na magonjwa hatari kwa binadamu kama vile saratani. Kwa hivyo, kuna haja ya sheria na kanuni zinazosimamia viwanda kutumiwa na serikali ili kuhakikisha kuwa wanaomiliki viwanda wanatunza mazingira na kudhibiti kemikali zinazotumika. Katika *Janga la Werevu*, `Unajisi` wa hewa unabainika kupitia wimbo wa mhusika Mwendawazimu kama ifuatavyo:

> Sauti ya Mwendawazimu: Pwani na bahari zinafura. Ardhi zatishiwa kufunikwa, mafuriko yameenea na maafa yanatukamia. *Hewa imenajisiwa* nasi hatusikii, hatutaki kujua. Hatumaizi wala kufikiria. U wapi ubinadamu tulioumbiwa? (Uk 23)

Ujumbe unaojitokeza katika mfano uliotolewa ni kwamba `unajisi` wa hewa umesababisha maafa mengi. Mojawapo ya maafa hayo ni mafuriko ambayo yanatishia kufunika ardhi. Vilevile, imedhihirika kwamba mwandishi ametumia `unajisi` kuonyesha kuwa kitendo cha kuchafua hewa kinatendwa pasi kumaizi wala kufikiria athari za vitendo hivyo. Hivyo, mwandishi anaonyesha kuwa kitendo kama hiki ni kinyume na ubinadamu tulioumbiwa. Uhalisia wa athari za uchafuzi wa hewa unathibitishwa na Massoi (2021) anayeeleza kwamba, majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa yanashuhudiwa kila uchao katika sehemu mbalimbali za dunia, ikiwemo mvua nyingi, mafuriko na ukame unaosababisha njaa. Aidha, mtaalamu huyu anashikilia kuwa kupunguza gesi chafuzi zinazochangia katika madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ni njia mwafaka ya kutatua matatizo yanayotokana na uchafuzi huo. Kadhalika, upunguzaji wa gesi hizi chafuzi unatiliwa

maanani kupitia kutambuliwa kwake kama mojawapo ya malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs). Kwa hivyo, mwandishi wa *Janga la Werevu* ameyaeleza kiubunifu madhara ya uchafuzi wa hewa ili hatua mwafaka zichukuliwe na wote wanaohusika, kuhakikisha kuwa uchafuzi huo umesitishwa.

### 5.2.4 Jazanda ya Jipu

Kwa mujibu wa TUKI (2004), jipu ni uvimbe kwenye mwili utoao usaha. Mwandishi wa *Majira ya Utasa* ametumia dhana ya `jipu` kijazanda kama inavyojitokeza katika dondoo hili:

> Siwa: Tunajua kiini cha tatizo hili lakini bado tunasita. *Tunaliona jipu lakini tunaogopa kuliminya*. Auchaye uchungu wa jipu haishi kupumwa.
>
> Kato: Hatuwezi kuanza kufanya hayo katika kipindi hiki kigumu. Tungoje kwanza mpaka dhiki hii iishe. *Nalo jipu tuhakikishe kuwa limeiva sawasawa* kisha tulifanyie mbinu. Kwanza tufikirie kuhusu kunusuru maisha ya watu wetu. (Uk 41)

Katika muktadha huu, `jipu` linamrejelea kiongozi Jumbe ambaye anaaminika kuwa chanzo cha matatizo yanayowakabili watu katika jamii. Amekwenda kinyume na alivyowaahidi watu wakati wa kampeni za uchaguzi. Isitoshe, yeye pamoja na wenzake wamechukua sehemu za vyanzo vya maji na kuzigeuza kuwa vitega uchumi vyao. Kwa kufanya hivyo, Jumbe na wenzake wamewatia wananchi uchungu mkali kama vile wa jipu. Aidha, inaaminika kuwa wao ndio waliosababisha janga la kiangazi. Katika kikao cha wawakilishi wa kijiji, ni wazi kwamba watu wanajua chanzo cha kiangazi hicho, ila wanasita kumkabili Jumbe. Hii ndio maana Siwa anawaambia kuwa licha ya kuliona `jipu`, wanaogopa kuliminya.

Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, shughuli mbalimbali za binadamu husababisha uharibifu wa mazingira (Rigby,2002). Hali hii inaweza kuthibitishwa na Abdallah (2014) anayesema kuwa shughuli za kiuchumi za mwanadamu ni chanzo kikuu cha uharibifu wa vyanzo vya maji. Hivyo, vyanzo hivyo vimevamiwa kupitia shughuli za kilimo pamoja na ufugaji. Matokeo ni ongezeko la joto duniani, mafuriko, kuenea kwa jangwa na kukauka kwa mito. Ili kuepuka madhara

zaidi, ni wajibu wa serikali kuhakikisha ya kwamba sheria kama vile za usimamizi wa misitu, ardhi na mazingira zimezingatiwa.

### 5.2.5 Jazanda ya Ugonjwa wa Kristy

Ugonjwa wa mhusika Kristy katika tamthilia ya *Janga la Werevu* umetumika kijazanda. Ugonjwa wa ghafla unaomkumba Kristy unaweza kueleweka kama jazanda inayorejelea msisimko wa mabadiliko unaoleta hofu na hasira hasa miongoni mwa vijana. katika dondoo lifuatalo, Daktari wa akili anafafanua:

| | |
|---|---|
| Daktari wa akili: | Jambo hilo ndilo linaloweza kuwa sababu ya ugonjwa wako. *Uchafuzi wa hali ya hewa na mazingira…* |
| Kristy: | Mimi sina ugonjwa wowote. |
| Daktari wa akili: | Ndiyo, huna ugonjwa. *Una hofu na hasira.* |
| Kristy: | Hofu? |
| Daktari wa akili: | Hofu ndio inayokupa hasira na mtibuko wa akili. (Uk 51) |

Kinachodhihirika hapa ni kwamba sababu ya ugonjwa wa Kristy ni uchafuzi wa hali ya hewa na mazingira, ambao uko kila pahali katika dunia nzima. Kama anavyofafanua Daktari wa akili, matendo ya binadamu ya kila siku huharibu mashiko ya dunia anayoishi na inayompa nyenzo za kuishi. Matendo hayo yanaathiri ulimwengu mzima wa mbingu na ardhi. Na hayo humbana na kumpekecha mno na kuchimbua hofu na hasira akilini mwake. Kwa hivyo, Kristy ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu, anawakilisha vijana ambao wana hofu ya madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira, ambao wako tayari kushiriki katika harakati ya kukomesha uharibifu huo na hatimaye kuyaokoa mazingira. Wahakiki wa kiekolojia wanadai kwamba, ili kukabiliana na majanga ya kiekolojia, watu watalazimika kutathmini upya mawazo yao wenyewe, mtindo wao wa maisha, mahusiano, matarajio yao na desturi zao. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wawakilishi wema wa ardhi na rasilimali zake (Njiru, 2015). Mambo haya ndiyo mwandishi wa *Janga la Werevu* anayopendekeza kama inavyobainika katika mfano uliotolewa.

Verma (2016) anatambua umuhimu wa vijana kushiriki katika uhifadhi wa mazingira. Hii ni kwa sababu vijana ni viwakilishi vya vizazi vya baadaye vinavyotegemewa katika uendelezaji wa jamii. Kwa hivyo, matatizo yanayotakana na uharibifu wa

mazingira yanaweza kuwaathiri watoto na vijana kwa muda mrefu zaidi. Kadhalika, Verma (keshatajwa) anapendekeza kuwepo na elimu kuhusu mazingira na uhifadhi wake katika shule na vyuo vikuu ili kushirikisha vijana katika shughuli kama vile upanzi wa miti. Vilevile, mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) yanaweza kushirikisha vijana katika shughuli za kuhifadhi mazingira pamoja na kuhusishwa katika kuelimisha umma kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na namna ya kuyahifadhi.

Hata hivyo, kupona kwa Kristy kutokana na ugonjwa uliomkabili ni jazanda ya kupona kwa jamii na ulimwengu kwa jumla baada ya hatua za muda mrefu za kuhifadhi mazingira. Hatua hizo zilitokana na ushauri wa Mwendawazimu kuhusu tiba ya Kristy. Alipendekeza kurejeshwa kwa misitu ya wananchi katika hali iliyokuwa, hata ingawa kungehitajika muda mrefu na fedha nyingi mpaka misitu irudi na kutengenea tena. Kutokana na umuhimu wa kuhifadhi mazingira, Quick (2004) anasisitiza kwamba, mahitaji ya mazingira kwa jumla lazima yatambuliwe na kuchukuliwa kwa umakini sawa na siasa, uchumi na mahitaji ya kiteknolojia ya jamii. Hii ina maana kwamba, suala la uhifadhi wa mazingira linafaa kutambuliwa na serikali ya nchi ili pesa za shughuli hiyo zitengwe kwenye bajeti ya taifa, kama zinavyotengewa shughuli nyinginezo muhimu za kitaifa. Hivyo, ili kuponya ulimwengu, ni lazima kuifufua misitu yote ya wananchi na chemchemi za maji, kama inavyojitokeza katika *Janga la Werevu*. Hata ingawa ugonjwa wa Kristy ulikuwa wa ajabu na kuwahangaisha wazazi wake huku wakitafita tiba, maafikiano kuhusu chanzo na tiba ya ugonjwa wa Kristy yanajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Bimkuu: Aaaa, wakati umefika kwa wazazi na wazee kufunzwa na watoto wao wenyewe tuliowazaa. Tulifanya maasi na makosa mengi kwa nyingi zetu tamaa.
>
> Bamkuu: Uzuri ni kwamba vidonda vingi vya nchi yetu vimeshaanza kupona. Misitu inajirudi, vyanzo vya maji vinachemka tena. Miti na mimea inakua na kunawiri. Ndege na wanyama wengine wanatembea msituni na sisi sote tumesoma funzo letu na tunasimama kidete kutonajisi mazingira yetu…(Uk 79)

Mazungumzo haya yanatokea katika sherehe ya kupona kwa Kristy. Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba vijana kama vile Kristy na dadake Busara wamefaulu kuwafundisha wazazi wao kuhusu faida za utunzaji wa mazingira. Wamepata mafanikio makubwa baada ya muda mrefu wa juhudi hizo kama vile kurudi kwa misitu, vyanzo vya maji kuchemka tena, kukua na kunawiri kwa miti na mimea miongoni mwa

mafanikio mengine. Ndiposa Bimkuu anakiri kwamba yeye na wananchi wenzake walifanya maasi na makosa mengi kwa tamaa zao nyingi. Kwa hivyo, ni wazi kwamba mwandishi wa *Janga la Werevu* anautumia ugonjwa wa Kristy kama fumbo la kuonyesha namna ya kuyatunza mazingira.

### 5.2.6 Jazanda ya Majira ya Utasa

Katika *Majira ya Utasa***,** mwandishi ametumia kichwa cha tamthilia hii kama jazanda. Kwa hivyo, kinaweza kueleweka kama jazanda inayorejelea msimu au nyakati ambapo hakuna matumaini ya mazao au maendeleo yoyote kutokana na athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira, kama vile ukame unaosababisha njaa. Mfano ufuatao unathibitisha:

> Mbawazi: Naona basi tutakuja kuangamizwa na hii njaa. *Ardhi tunayo lakini kumbe haizai bila maji!*
> Bi Siwa: Kila kitu hutegemea maji mama. Maji ni uhai.
> Mbawazi: Naona hali hii ikiendelea tutakuja kufa na kuwa karamu ya tai na fisi. (Uk 6)

Katika mfano huu, Mbawazi ana hofu na wasiwasi mwingi kutokana na kiangazi cha muda mrefu ambacho kimesababisha njaa. Licha ya kuwa wana ardhi, hakuna mazao yoyote kwa sababu ya ukosefu wa mvua. Ndiposa mamake anamwambia kuwa maji ni uhai kwani kila kitu huyategemea. Ujumbe unaobainika hapa ni kwamba huu ni msimu ambao hali ya ukame imewakabili watu kiasi cha kusababisha njaa. Hivyo msimu huu unaweza kurejelewa kama \`msimu wa utasa\`. Kadhalika, mwandishi wa *Majira ya Utasa* anausawiri utasa kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

> Bibi: …Hadithi zetu zimebaki tu ngano za kale maana hakuna tena hadithi mpya za kuwapigia mifano wajukuu wetu. *Ni kipindi cha utasa. Ni majira ya ukame wa hadithi zetu wenyewe.* Labda tunaziogopa hadithi zetu. Hadithi za tulivyoishi na kushindwa kuchangia hadithi walizoacha wazee wetu. (Uk 83-84)

Matumizi ya maneno \`kipindi cha utasa\` katika mfano uliotolewa yanarejelea kipindi ambapo kuna uhaba wa kila kitu katika jamii, hali ambayo imesababishwa na ukame. Uchanganuzi wa data katika tamthilia hii umebaini kuwa kwa sababu ya hali ya ukame, hakuna elimu kwa sababu watoto hawaendi shule, wanyama wanakufa kwa njaa, mimea

inakauka, mito na bahari zinakauka hivi kwamba hata viumbe waishio humo wanaangamia na kufa. Taswira inayojitokeza hapa ni kwamba, hiki ni kipindi chenye matatizo mengi na hakuna matumaini ya hali kubadilika. Ndiposa Bibi anakiri kwamba hakuna tena hadithi mpya za kuwapigia mifano wajukuu wao. Hivyo, ni kipindi cha utasa wa kila aina. Akieleza kuhusu umuhimu wa mazingira katika uundaji wa mandhari ya kifasihi, Buell (2005) anasema kwamba mazingira ndiyo huipa kazi ya sanaa usanii na ujumi wake. Aidha, maoni ya Sangili (2015) yanaafikiana na ya Buell (keshatajwa) anapodai kuwa baadhi ya misamiati katika kazi nyingi za sanaa hutokana na miti, mito, wanyama na wadudu. Kwa hivyo, ni wazi kwamba uharibifu wa mazingira ambayo huipa kazi za fasihi usanii na ujumi wake, husababisha utasa wa fasihi hiyo, jambo ambalo mwandishi wa *Majira ya Utasa* anafafanua kupitia mhusika Bibi.

### 5.2.7 Jazanda ya Ndoto ya Kato

Ndoto ya mhusika Kato katika tamthilia ya *Majira ya Utasa* imetumika kijazanda. Ndoto hiyo inaweza kurejelewa kama ishara ya matumaini ya kubadilika kwa hali za maisha za wanajamii baada ya kufanya juhudi za kuhifadhi mazingira. Katika ndoto hiyo, Kato anaeleza:

> Kato: Nimeota nikitoka malishoni na punda wangu. Tena majira haya ya taabu. Nikiwa njiani kurejea, *mara punda wangu anazama katika shimo. Shimo refu.* Nimewaita watu tufanye maarifa ili tumtoe lakini wapi! Hakuna mwenye kauli ya kumwopoa maskini yule punda. Kwa hivyo tukaamua kumfunika kwa udongo ili kumsahau. *Lakini ajabu ni kuwa punda anafanya muujiza. Kila tukirusha mchanga ndani, yeye anaruka juu na kuukanyaga hadi mwishowe akatokea juu na kutoka nje* japo alikuwa mnyonge…(Uk 59)

Katika ndoto hii, kuzama kwa punda katika shimo lenye kina kirefu kunaweza kufananishwa na jinsi ambavyo wanajamii wametumbukia katika dhiki na taabu nyingi kutokana na kiangazi kilichowakabili. Hii inatokana na uharibifu wa mazingira ambao ulisababisha kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu. Matokeo ni njaa, vifo, mafuriko miongoni mwa majanga mengine. Hata hivyo, miujiza ya punda ya kuweza kutoka kwenye lile shimo ni ishara ya kuwa bado kuna matumaini ya kuibadili hali ilivyo hasa baada ya kutia bidii ili kuyaokoa mazingira yaliyoharibiwa.

Kadhalika, matumaini ya hali ya awali ya mazingira kurejeshwa inajitokeza kufikia mwisho wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* baada ya wananchi kufanya maandamano. Lengo lao kuu ni kutwaa ardhi yao iliyonyakuliwa na Jumbe ili waanze kujenga madhabahu kama hatua mojawapo ya kusitisha kiangazi. Aidha, katika ukurasa wa 82, mwandishi anatupa taswira ya mngurumo wa radi na upepo mkali baada ya maandamano ya wananchi. Hii inaweza kurejelewa kama ishara ya kunyesha kwa mvua, dalili ya kufaulu kwa wananchi katika azma yao ya kuhifadhi mazingira ili kukomesha kiangazi. Kwa hivyo, kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, kazi za kimazingira huonyesha matumaini ya kuiponya jamii kutokana na athari za uharibifu wa mazingira (Culler, 2011). Jambo hili linadhihirishwa wazi na mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa*.

**5.3 Kinaya**

Mbinu ya kinaya hutumiwa na waandishi kusawiri kinyume cha uhalisia wa mambo. Aidha, ni onyesho la kinyume cha matarajio kuhusu mkondo ambao matukio yanapaswa kuchukua. (Wamitila, 2003). Katika *Janga la Werevu*, uamuzi wa mwandishi wa kumtumia mhusika Mwendawazimu kuwazindua wanajamii kuhusu chanzo cha matatizo yanayowakabili ni kinaya. Mfano ufuatao unathibitisha:

> Mwendawazimu: Hakuna mjukuu, kitukuu, kilembwe, kilembwekeza, kinyinginya au kizazi hata kimoja ambacho kimechachamaa kama alivyochachamaa Kinjeketile na wafuasi wake wakati wa vita vya majimaji. Badala yake *tunaiga yasiyofaa kuigwa. Tunakiri. Tunakubali tu kila kitu kama watu tuliopoteza dira. Watu tuliopoteza mwelekeo. Tumegeuka mbumbumbu, mabubu au viziwi. Watu tusiozingatia*. (Uk 14)

Kinachodhihirika kutokana na maneno ya Mwendawazimu ni kwamba, yeye ndiye anayetambua kiini cha matatizo yanayowakabili wanajamii, ndiposa amechukua hatua ya kuwazindua. Ni kinaya kwamba Mwendawazimu ambaye kwa kawaida huwa ni mtu asiye na akili razini, anatoa kauli nzito kuhusu namna ya kuepuka matatizo yanayoikabili jamii yake. Anawaeleza wanajamii kuwa chanzo cha matatizo yao ni kuiga yasiyofaa kuigwa, kukubali tu kila kitu kama watu waliopoteza dira pamoja na kuwa watu wasiozingatia. Isitoshe, Ni kinaya kwamba Kristy aliyeugua ugonjwa

usioeleweka na kutibiwa na wauguzi wa aina mbalimbali bila mafanikio, anapona kutokana na fikra za Mwendawazimu. Ili kuthibitisha haya, Kristy anasema:

> Kristy: Naona nuru mpya. Naona nuru ambayo sijapata kuiona ndani ya maisha yangu yote. Naona nimepona. Najua nimepona. Nimepona mimi na najua wamepona watu wangu na taifa langu pia. *Kinyume cha mambo ni kuwa nimepona kwa fikra za mwendawazimu au tuseme fikra za mganguzi asiye na werevu lakini mwenye akili.* (Uk 80)

Katika sherehe ya kupona kwa Kristy, yeye anakiri kwamba amepona na alijua kuwa watu wake na taifa kwa jumla lilipona. Kupona kwake kulitokea baada ya miaka mingi ya juhudi za kufufua mazingira yaliyokuwa yameharibiwa. Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba, `werevu` unaweza kuzua janga. Hata hivyo, watu wanaoonekana wendawazimu huenda ndio wenye busara na hekima. Kama wanavyosema Bulaya na Mhango (2020), uhifadhi wa mazingira ni suala na jukumu la kila mwanajamii. Hii ina maana kwamba, kila mwanajamii ana nafasi yake katika uhifadhi wa mazingira kwani kila mmoja wao ameathiriwa na uharibifu wa mazingira hayo. Hata ingawa wazazi wa Kristy wanaonekana kumpuuza Mwendawazimu, hatimaye wanampongeza kwa kuwa mawazo yake ndiyo yanayomponya binti yao. Kwa hivyo, mchango na maoni ya kila mja katika jamii hayafai kupuuzwa, kwani yana umuhimu wake na huenda yakaleta suluhisho kwa matatizo ya kimazingira.

Katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, vuguvugu la ukombozi wa jamii dhidi ya utawala dhalimu wa Bw. Binafsi linaanzishwa na kuendelezwa na bintiye Mpya. Isitoshe, ndugu zake Zanga na Mussa pia wanaungana na umma katika kutetea maslahi ya wanajamii wote, wakiongozwa na Mpya. Hiki ni kinaya kwa sababu katika hali ya kawaida, inatarajiwa kuwa watoto wangewaunga mkono wazazi wao katika kila hali kwani wao pia wanafaidika kutokana na mali yao. Dondoo lifuatalo linashadidia:

> Sauti ya Mpya: Sasa wanaojua ni wengi kuliko wasiojua.
> Mussa: Kumbe kweli wanaojua ni wengi kuliko wasiojua.
> Zanga: Sasa nimeshajua.
> Mussa: Sasa tumeshatambua. (Uk 55)

Mazungumzo haya baina ya Mpya, Mussa na Zanga ni idhibati ya maafikiano yao ya kuungana na umma ili kuleta mabadiliko katika nchi yao, hasa kwa kupiga vita utawala dhalimu unaoendelezwa na baba yao Bw. Binafsi. Kupitia mhusika Mpya, wananchi wengi wameelimishwa ili waweze kutambua kiini cha matatizo yao. Hii ndio maana Mpya anawaambia ndugu zake kuwa sasa wanaojua ni wengi kuliko wasiojua. Hivyo, hawakuwa na budi pia kujiunga na wananchi wengine katika harakati hizo. Kama inavyofafanuliwa na Schlosberg (2007), haja kuu ya uhakiki wa kiekolojia si tu katika kushughulikia watu binafsi bali pia uwezo na utendakazi wa jamii kwa jumla. Jambo hili linaonyesha kuwa masilahi ya umma ni muhimu zaidi kuliko masilahi ya mtu binafsi. Aidha, mchango wa vijana katika vuguvugu la kuleta mabadiliko pakiwemo uhifadhi wa mazingira, unadhihirika wazi kupitia wahusika Mpya, Mussa na Zanga, jambo ambalo mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* analiweka wazi.

## 5.4 Taswira

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), taswira ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Aidha, Wamitila (keshatajwa) anafafanua namna mbili za ujitokezaji wa taswira katika kazi za fasihi kwa kueleza kuwa, taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za kiishara ambazo huunda picha inayoashiria jambo fulani au imeficha ujumbe. Waandishi wa tamthilia teule wametumia taswira kusawiri hali na athari za mazingira kwa namna mbalimbali. Katika *Janga la Werevu*, athari za uhaba wa maji uliosababishwa na uharibifu wa mazingira unashadidiwa na dondoo lifuatalo:

| | |
|---|---|
| Mwanamke IV: | *Jamani mnanikaba mpaka nakosa pumzi, mtaniua*! |
| Mwanamume V: | Wewe kosa tu hizo pumzi. Nani kwani anajali? |
| Mwanamke IV: | We… wewe… unajifanya mwanamume sana, si Ndio? Ngoja basi utaona nguvu za mwanamke wa kisasa zikoje… |
| Mwanamume V: | *Wewe… umenisukuma mpaka umenifanya matone yangu machache ya uhai*. |
| Mwanamke IV: | Uhai? |
| Mwanamume V: | Hujui kwamba maji ni uhai? |
| Mwanamume VI: | Wewe unafikiri upo arusini hapa? *Haya ni mapambano kamili bwana*! |
| Mwanamume V: | Mapambano ya kweli tusiyoyafanya sisi ndiyo yepi? |

Mwanamume VI: Ya kupambana na wale walioisababisha hali hii. *Wale waliosababisha vianzo vya maji kukauka*. (Uk19)

Taswira inayojitokeza katika dondoo lililotolewa inaangazia wanajamii kutoka sehemu mbalimbali wakigombania maji kutoka chemchemi ya maji ya wananchi. Kinachodhihirika hapa ni kwamba kumekuwa na uhaba wa maji katika kila pembe ya jamii iliyoangaziwa na mwandishi, ndiposa watu wanagombana na kusukumana ili muradi wapate machache yanayopatikana. Hii ndio maana Mwanamke IV analalamika kwamba amesukumwa hadi akamwaga matone machache aliyokuwa amefaulu kuchota. Njiru (2015) anapoeleza kwamba haki ya kimazingira inapaswa kukuza uwezo wa watu pamoja na viumbe wengine kuishi kwa amani, anarejelea athari za mizozo inayosababishwa na uhaba wa rasilimali, kama inavyojitokeza katika mfano uliotolewa. Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba, licha ya kuwa maji ni uhai, yamekuwa haba kupatikana. Chanzo cha uhaba huu kama inavyodhihirika katika mfano uliotolewa ni kuharibiwa kwa mazingira kulikosababisha vyanzo vya maji kukauka.

Hali hii inashadidiwa na utafiti uliofanywa na shirika la umoja wa mataifa linaloshughulika na mazingira (UNEP). Kutokana na utafiti huo, sababu mojawapo ya uhaba wa maji safi katika nchi nyingi za Afrika ni kuanza kutoweka kwa uasili wa vyanzo vya maji ikiwemo kukauka kwa ziwa Chad, na kuharibika kwa sehemu ya ukanda wa mto Nile. (UN, 2010). Hivyo, ni dhahiri kwamba uhaba wa maji unaweza kuzua vurugu na vita miongoni mwa wanajamii. Ili kuafikia shabaha mojawapo ya malengo ya maendeleo ya milenia ambayo ni kuondokana na shida ya kukosa maji safi ya kunywa kwa wakazi katika mataifa mbalimbali duniani na hasa barani Afrika, ni muhimu kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji kama jambo la dharura. Katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*, mwandishi analeta taswira ya athari za kemikali hatari zinazotumiwa katika viwanda vya maua vya Jumbe. Hali hii inathibitishwa na mfano ufuatao:

Siwa: Haya sikiliza. Siku za nyuma tulipotoka kwenda baharini, tulikuwa *tunawakuta samaki chekwa waliokufa, wanaelea majini. Takriban wote wamebambuka bambuka! Wengi wamefura*! Wavuvi wenye utundu waliwapasua. Utumbo wa kila waliyempasua *ulikuwa na vidonda vikubwa*

*vikubwa mfano wa kuchomeka huku wanatoa harufu ajabu*.
(Uk 23)

Siwa anatamka maneno haya anapomweleza mke wake sababu ya uhaba wa samaki baharini walikokuwa wakitegemea kwa uvuvi wao. Kutokana na maneno yake, ni wazi kwamba samaki wengi wameaga kutokana na sumu za kemikali huko baharini. Vidonda vikubwa kama vile kuchomeka vilivyopatikana katika utumbo wa kila samaki aliyepasuliwa, ni idhibati tosha ya kwamba chanzo cha vifo vya samaki hao ni kuchomwa na kemikali. Mwandishi anatumia taswira ya samaki wengi waliokufa na kuelea majini ili kuonyesha madhara na hasara kubwa itokanayo na uharibifu wa mazingira kupitia kemikali kutoka kwenye viwanda. Ili kudhibiti na kuzuia madhara ya kemikali kwa mazingira, ni muhimu kwa serikali kuhakikisha kuwa sheria za usimamizi wa kemikali za viwandani zinazingatiwa (Carter, 1999). Zaidi ya hayo, serikali inaweza kuweka jitihada katika kuelimisha umma na makundi mbalimbali kuhusu usimamizi bora wa kemikali, ili wapate uelewa juu ya madhara ya kemikali hizo.

### 5.5 Majazi

Kwa mujibu wa Wangari (2019), mbinu ya majazi katika fasihi hujitokeza pale ambapo tabia za wahusika zinaambatana na majina yao halisi. Kwa upande wake, Wamitila (2003) anaeleza majazi kuwa mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi au kutuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Aidha, majazi huhusisha pia majina ya mahali au mandhari. Akieleza umuhimu wa majazi, Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa mbinu hii ina uzuri wa kuwa inamsaidia msomaji kuweza kuifahamu tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi. Vilevile, mwandishi anaweza kuitumia mbinu hii kuuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahusu wahusika fulani pamoja na mwelekeo wa hadithi nzima. Hata hivyo, Wamitila (keshatajwa) anaeleza kuwa mbinu ya majazi ina udhaifu wa kutomshirikisha msomaji katika uamuzi wa wasifu wa mhusika na badala yake humlazimu kuridhika na maoni ya mwandishi. Uchanganuzi wa tamthilia teule ulibainisha majina mbalimbali ya wahusika ambayo ni ya kimajazi. Majina hayo ni Busara, Mpya, Bw. Binafsi na Lulu.

Katika tamthilia ya *Janga la Werevu*, jina la mhusika Busara ni la kimajazi. Hii ni kwa sababu mwandishi amemsawiri kama msichana mwenye maarifa yaliyomwezesha

kuamua na kutenda mambo yalivyofaa. Idhibati ya busara ya mhusika huyu inajitokeza katika mfano ufuatao:

> Bimkuu: Hatutaki kuachwa nyuma katika dunia hii ya sayansi na *Hi-tech!*
> Busara: Hutaki kuachwa nyuma na *u-dotcom*. Je, Hi-tech na u-dotcom havina madhara hata kidogo? *Busara ya kuishi husema kwamba kila zuri huzungukwa na mabaya na kila baya huzungukwa na mazuri.*
> Busara: Tatizo ni kwamba tunatazama ukale na matambiko yake kijuujuu tu. *Hatuzamii ndani kuchunguza kina cha falsafa na maana ya matambiko.* (Uk 39)

Katika dondoo hili, Busara anamweleza mamake Bimkuu kuhusu manufaa ya matambiko katika uhifadhi wa mazingira. Mamake anaposema kuwa matambiko ni ujadi uliopitwa na wakati, Busara anamfafanulia kuwa itikadi zilizoambatana na matambiko zililenga kulinda misitu, hivyo kulinda uhai wa miti, wanyama, wadudu na binadamu. Kwa mujibu wa Alia (2017), mazingira kwa jumla ni ushirikiano wa asili na utamaduni, binadamu na wasio binadamu pamoja na viumbe hai na vile visivyo hai. Hii ina maana kwamba, ni vigumu kutenganisha mazingira na utamaduni wa jamii. Busara anafahamu umuhimu wa utamaduni wa jamii katika uhifadhi wa mazingira. Ndiposa anasema kuwa tatizo la watu ni kutazama ukale na matambiko yake badala ya kutazama ndani kuchunguza kina cha falsafa na maana ya matambiko. Kauli za Busara ni dhihirisho la maarifa ya hali ya juu aliyonayo kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na namna ya kuyahifadhi.

Akieleza kuhusu umuhimu wa matambiko katika jamii hasa za kiafrika, Shemboko (2020) anasema kuwa matambiko hujenga imani kama chombo cha kutatulia matatizo ya jamii husika. Kadhalika, matambiko huiongoza jamii katika mapambano dhidi ya matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii husika. Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana. Kwa hivyo, kupitia mhusika Busara, mwandishi anaelekeza kwenye mtazamo wake kuhusu ujadi ulioambatana na matambiko kama njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira asilia.

Jina la mhusika Mpya katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* vilevile ni la kimajazi. Kuzaliwa kwa mhusika huyu kunaleta upya wa mambo mbalimbali katika jamii husika kama vile kuleta mwamko mpya na mapinduzi katika jamii baada ya miaka mingi ya kunyamaza kimya. Umuhimu wa Mpya unadhihirika katika mfano ufuatao:

| | |
|---|---|
| Sauti: | Nani huyo? Nani anayethubutu kuangusha chuma nchi hii? |
| Mpya: | *Kikaango cha chuma kimeangushwa hatimaye!* |
| Sauti: | A-a, Bi Mpya, *hapa kwenu watu hawasemi waziwazi wala hawasemi kwa Kelele*. Hawaruhusiwi kufanya hivyo! |
| Mpya: | *Mimi nimeanza*. |
| Sauti: | Wewe nani? |
| Mpya: | Mimi mwananchi. Mimi mzalendo. Mimi mkereketwa. |
| Sauti: | Hapana, wewe ni raia wa familia hii inayoongoza nchi. Wewe ni mtoto wa Mzee Binafsi, babako na Bi Shoo, mamako. (Uk 27-28) |

Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba Mpya ndiye wa kwanza kuzungumza waziwazi tena kwa kelele, jambo ambalo halikuruhusiwa katika jamii yake. Hii inadokeza kuwa uongozi wa wazazi wake ni wa kidikteta. Anapohojiwa na Sauti anasema kwamba, ingawa watu wamekuwa wamenyamaza kimya, yeye ndiye ameanza kuzungumza kwa niaba ya jamii yake. Kama inavyodhihirika kupitia Sauti, Mpya ni mtoto wa Bw. Binafsi na Bi Shoo, ambao ndio viongozi wa jamii husika. Kinachobainika hapa ni kuwa mhusika huyu ndiye wa kwanza kushutumu na kuonyesha kutoridhishwa na uongozi wa wazazi wake. Hivyo, analeta upya wa mawazo na mtazamo kuhusu haja ya kuweka mahitaji ya jamii mbele kuliko yale ya kibinafasi.

Isitoshe, mchango wa Mpya katika kuikomboa jamii yake dhidi ya utawala dhalimu ni dhihirisho la kuwa suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mtu katika jamii. Mpya anawakilisha vijana katika jamii ambao wanaweza kuzua mambo mapya yanayoweza kuikomboa jamii nzima kutokana na udhalimu wa viongozi wa kisiasa. Aidha, kufaulu kwa Mpya katika kuelimisha umma na hatimaye kuikomboa jamii ni ushahidi tosha ya kwamba yote yanawezekana kwa juhudi na kuchukua hatua. Hali hii inaafikiana na maoni ya Sangili (2015) anayesisitiza kwamba suala la uhifadhi wa mazingira linahitaji kila mja kujukumika bila kujali umri, kabila wala jinsia. Kwa hivyo, ni wazi kwamba inawezekana kuyarejesha mazingira katika hali yake ya awali

muradi tu hatua mwafaka zichukuliwe pamoja na kutia bidii katika kuelimisha umma kuhusu njia za kuyahifadhi mazingira hayo.

Ubinafsi ni tabia ya mtu kujali maslahi yake mwenyewe na kupuuza ya wengine. (Kamusi ya Karne ya 21,2011). Mwandishi wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* amemsawiri mhusika Bw. Binafsi kama kiongozi mbinafsi ambaye alijali maslahi yake na familia yake tu bila kujali umma uliomchagua. Ubinafsi wake unadhihirika katika mfano ufuatao:

> Bi. Subira: Hivi leo tunaagiziwa vyakula vya *GMO*`s kwa ajili ya kuzima fujo za matumbo yetu. Na *wanaoagiza ni wale wale walioyaridhi mashamba yenye rutuba na wasiyoyalima. Ni wale wale wenye kuunda sheria za kumaliza njaa na ukata. Majoka ya midimu hayo*… maeneo ya bahari kubwa yanakondishwa kwa makampuni ya kutoka nje ili wavue samaki wetu… (Uk 59-60)

Kupitia kwa maneno ya Bi. Subira katika mfano uliotolewa, ubinafsi wa viongozi unadhihirika wazi. Wananchi wamekumbwa na matatizo mengi kama vile njaa, ila viongozi hawafanyi chochote cha kuwasaidia. Ubinafsi wa Bw. Binafsi unadhihirika kupitia kwa unyakuzi wa ardhi ya umma yenye rutuba, kukodisha maeneo ya bahari kubwa kwa makampuni kutoka nje kwa manufaa yake binafsi, badala ya umma kufaidika kwa kuvua samaki. Licha ya kuwa Bw. Binafsi ndiye anayechangia katika kusababisha njaa kwa wananchi anaowaongoza, anaunda sheria zinazonuia kumaliza njaa na ukata, lakini haziwafaidi wananchi kwa vyovyote vile kwani haja yake ni kunufaisha familia yake.

Isitoshe, yeye anaficha ubinafsi wake kwa kuwaagizia wananchi vyakula vya GMO`s bila kujali madhara ya vyakula hivyo kwa afya ya wananchi. Kama anavyoeleza Tan (2019), uhakiki wa kiekolojia unasisitiza kuhusu haja ya kuinuka dhidi ya sheria na sera ambazo huchochea mabadiliko ya tabianchi ambayo yatasababisha majanga makuu ya kiekolojia. Bw. Binafsi ni mfano wa viongozi ambao huficha maovu yao katika uundaji wa sheria ambazo haziwafaidi wanajamii. Hivyo, wanajamii wanapaswa kuwakabili viongozi wa aina hii ili kuhakikisha ya kwamba masilahi yao yanashughulikiwa ipasavyo. Bw. Binafsi anawakilisha viongozi wengi wa kisiasa ambao ni wabinafsi hivi

kwamba huwahadaa wananchi kuwa, baada ya kuchaguliwa wangeshughulikia mahitaji yao ipasavyo. Kinyume na matarajio ya umma, baada ya kuchaguliwa ubinafsi wao hujitokeza wazi, ambapo wao huanza kujihusisha katika uporaji wa mali ya umma bila kujali watu waliowachagua.

Sifa hizi za viongozi wabinafsi zinadhihirika pia kutokana na utafiti wa M`Ngaruthi (2015) aliyebaini kwamba, wanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru ni wabinafsi kiasi cha kupanga njama za kuwaibia wananchi wanaotarajiwa kuwatetea. Hivyo, wanasawiriwa kama viongozi wenye ila wasiojali umma bora tu wajinufaishe, hasa kwa kupora mali ya umma. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* amemtumia mhusika Bw. Binafsi ili kuleta taswira ya sifa za viongozi wabinafsi ambao hawajali maslahi ya wananchi wanaoongoza, ili kuwakashifu viongozi wa aina hiyo katika jamii.

Katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*, jina Lulu limetumika kimajazi. Neno lulu lina maana ya kito cha thamani kinachotokana na chaza wa baharini kitumikacho kama pambo (Kamusi ya Karne ya 21, 2011). Hivyo, mwandishi amemsawiri mhusika huyu kama mwenye thamani kubwa hasa kutokana na majukumu yake katika ukombozi wa jamii iliyosawiriwa. Licha ya kuwa yeye ni mke wa kiongozi Jumbe, anapinga utawala dhalimu uliotumbukiza jamii nzima katika janga la ukame. Anamkosoa Jumbe mara kwa mara huku akimkumbusha wajibu wake katika kutumikia umma. Katika mfano ufuatao, Lulu anamwamwambia mumewe:

Lulu: Kuna dukuduku.
Jumbe: La nini?
Lulu: Wameshaanza kulalamika kwamba umekwenda kinyume na ulivyowaahidi wakati wa uchaguzi. *Wanasema huyajali masilahi yao*.
Jumbe: Hayo ni maoni yao. Wana uhuru wa kujieleza. Ndiyo demokrasia hiyo.
Lulu: *Usiseme hivyo Jumbe. Watu wananung`unika na kukulaumu wewe.*
Jumbe: Kuhusu nini?
Lulu: Kuhusu mambo kadha. Moja kati ya hayo ni kwamba wewe na wenzako mmechukua sehemu za vyanzo vya maji na kuzigeuza kuwa vitega uchumi vyenu. *Kuna fununu kuwa nyinyi ndio mliosababisha kiangazi hiki…*(Uk 38)

Katika dondoo hili, Lulu anamweleza mumewe Jumbe kuhusu malalamishi ya wananchi. Wao wanalalamikia mambo mengi huku wakimlaumu Jumbe na wenzake

kwa kuchukua vyanzo vya maji na kuvigeuza kuwa vitega uchumi vyao, jambo ambalo limesababisha janga la kiangazi katika jamii. Kwa kufanya hivyo, Lulu anamkumbusha mumewe kwamba amekwenda kinyume na alivyowaahidi wananchi wakati wa uchaguzi kwa kutojali masilahi yao. Licha ya kuwa Jumbe anayapuuza mashauri ya mke wake, hatimaye wananchi wanafaulu kumfurusha pamoja na wenzake katika ardhi ya umma waliyotumia kwa ajili ya viwanda vya maua, sehemu za misitu zilizotumika na wanajamii kufanya matambiko. Uwezo wa wananchi wa kumwondoa Jumbe katika ardhi ya umma aliyonyakua, ndio Schatz (2012) anaorejelea anaposema kuwa, uhakiki wa kiekolojia unafaa kumwezesha binadamu kupiga vita uongozi dhalimu ambao unasababisha uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, ni wazi kwamba mchango wa mhusika Lulu katika ukombozi wa jamii yake dhidi ya dhuluma za muwewe hauwezi kupuuzwa kamwe.

### 5.6 Nyimbo

Waandishi wa tamthilia teule wametumia nyimbo kama mojawapo ya mbinu za kuzisawiri motifu mbalimbali za kimazingira. Katika *Janga la Werevu*, wimbo wa Mwendawazimu unafafanua dhiki na matatizo yanayowakumba wanajamii kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Sauti ya Mwendawazimu: | Pwani na bahari zinafura, ardhi zatishiwa kufunikwa, mafuriko yameenea na maafa yanatukamia, hewa imenajisiwa, nasi hatusikii, hatutaki kujua, hatumaizi wala kufikiria. U wapi ubinadamu tulioumbiwa? |
| Wachotamaji: | Uwapi ubinadamu tulioumbiwa? |
| Sauti ya Mwendawazimu: | U wapi utu tuliosimbikwa? |
| Wachotamaji: | U wapi utu tuliosimbikwa? |
| Mwendawazimu: | I wapi busara tuliyotunukiwa? |
| Wachotamaji: | I wapi busara tuliotunukiwa? (Uk 23). |

Katika wimbo huu, Mwendawazimu anayataja baadhi ya maafa yanayowasakama wanajamii. Moja kati ya maafa hayo ni tishio la mafuriko kutokana na kupita kiasi kwa maji ya bahari. Kama inavyobainika kutokana na maneno yake, haya yote yanatokana na uharibifu wa hewa. Isitoshe, Mwendawazimu anawalaumu wanajamii kwa jumla kwa kutojali, kumaizi wala kufikiria. Kama inavyodokezwa na Buell (1995), mawazo

ya dharura huwa yanahitajika panapotokea majanga ya kimazingira. Katika mfano uliotolewa, wananchi wanaonekana kutosheka tu na hali ya mambo badala ya kufikiria kuhusu hatua ambayo ingewasaidia ili kuepukana na madhara ya uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, Mwendawazimu anahitimisha kifungu cha wimbo huu kwa kuwakashifu wale wanaotekeleza uharibifu wa mazingira kwa kuwasawiri kama wasio na utu na kwamba ni watu wasiotumia busara waliotunukiwa. Kadhalika, mwandishi wa *Majira ya Utasa* anaiweka wazi hali ngumu inayowasibu wanajamii kutokana na uharibifu wa mazingira. Haya yanadhihirika kupitia wimbo wa Bi. Siwa kama ifuatavyo:

Bi. Siwa: Kupata dhiki na nyingi tabu, ni nini yake hasa sababu,
hali ngumu waja kutusibu, ni lipi kosa tulilotenda?
Kutufanya hivi kama ng`onda jana nyofu leo kuwa pinda
(Uk 9)

Bi. Siwa anaimba wimbo huu baada ya mazungumzo yake na bintiye Mbawazi, anayelalamika kuwa karibu umetimia mwaka tangu kufungwa shule kwa sababu ya njaa inayotokana na kiangazi. Kupitia kwa wimbo huu, mwandishi analeta taswira ya dhiki na hali ngumu ya kimaisha inayowakabili watu wengi katika jamii. Huenda mwandishi anadokeza kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi wakati Bi. Siwa anaposema `jana nyofu leo kuwa pinda`. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa wanajamii hawajui chanzo cha dhiki inayowakabili, ndiposa Bi. Siwa anauliza ni ipi sababu ya matatizo yanayowakumba na kushangaa iwapo huenda kuna kosa walilotenda. Kama inavyobainishwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, kuna haja ya kuwepo na elimu kwa umma ili kuwahamasisha wanajamii kuhusu chanzo cha uharibifu wa mazingira ili nao wachangie katika uhifadhi wa mazingira hayo (Heise, 2008). Jambo ambalo mwandishi wa tamthilia hii anasisitiza kiubunifu hasa kupitia wimbo wa Bi. Siwa.

Licha ya waandishi wa tamthilia teule kutumia nyimbo kusawiri matatizo yanayowakabili wanajamii kutokana na uharibifu wa mazingira, wameonyesha pia ya kwamba bado kuna matumaini ya hali kubadilika baada ya wote kuungana na kujitahidi katika harakati za kuhifadhi mazingira. Katika *Janga la werevu*, wimbo wa Kristy unashadidia:

Ama kweli, wahenga huweza kukasirika…

(Kiitikio) Kukasirika kukasirika huweza… Wakikasirika tunapata kipigo kikali.
(Kiitikio) Kipigo kikali, kipigo kikali lakini wahenga hufurahi na kuchangamka.
(Kiitikio) Hufurahi na kuchangamka, wakifurahi hufanya sherehe kunoga! (Uk 82)

Ujumbe unaojitokeza katika wimbo huu ni kwamba, huenda chanzo cha matatizo yaliyokumba jamii iliyosawiriwa na mwandishi ni kuasi ujadi. Hii ndio maana Kristy anasema kuwa wahenga huweza kukasirika watu wanapoasi ujadi hasa ule unaohusishwa na matambiko. Hivyo, kinachodhihirika ni kwamba janga la kiangazi kilichowakumba wanajamii kinaweza kuchukuliwa kama kipigo kikali kutokana na hasira za wahenga. Hata hivyo, Kupona kwa Kristy ni dhihirisho tosha la kuwa mazingira yaliyoharibiwa yanaweza kurejeshwa katika hali yake ya awali. Hii ndio maana anasema kwamba wahenga hufurahi na kuchangamka hasa baada ya wanajamii kuzingatia ujadi unaohusiana na matambiko. Hali hii inaweza kuthibitishwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia kwa kudokeza kuwa, utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Glotfelty, 1996). Hivyo, mwandishi anasisitiza nafasi ya utamaduni wa jamii katika uhifadhi wa mazingira, hasa ule ambao ulihusishwa na matambiko katika uhifadhi wa miti, misitu, mito, bahari na milima.

### 5.7 Kejeli

Kejeli ni namna ya kusema au kutenda kwa utani na dharau kinyume cha ukweli lakini kwa lengo la kuwasilisha ukweli fulani (Wangari, 2019). Naye Wamitila (2003) anafafanua kejeli ya kidrama kwa kusema kuwa ni aina ya kejeli inayohusishwa na tamthilia au drama. Hivyo, hutumiwa pale ambapo hadhira inaelekea kuifahamu maana au kidokezi cha hali fulani inayotokea jukwaani ilhali mhusika mmoja au baadhi ya wahusika hawaelekei kuifahamu maana hiyo. Watunzi wa tamthilia teule wametumia kejeli kwa mapana na marefu ili kusawiri baadhi ya motifu za kimazingira. Katika *Majira ya Utasa*, Arege anakejeli viongozi wa kidini ambao hawana uelewa wa uhalisia wa hali zinazowakabili waumini, kwa hivyo wanaweza kuwapotosha waumini hao. Dondoo lifuatalo linashadidia:

Bi Siwa: Wanasema eti haya yote yanatokana na mipango mibaya na ubinafsi. Lakini mimi nafikiri ni kwa sababu ya dhambi. Ulimwengu una dhambi nyingi na Mungu nionavyo amekasirika. Tukitubu tutaepukana na janga

hili! *Na juzi padre alipokuja hapa alisema hii ni moja kati ya mambo yanayoonyesha kuwa dunia inakwisha. Siku ya kiyama inakaribia!*

Mbawazi: Afadhali na iwe hivyo kuliko hivi tunavyoishi sasa!

Bi Siwa: Huenda ikawa kweli au isiwe kweli. Mwana wa Adamu aliumbwa kupambana na maisha… (Uk 7)

Haya ni mazungumzo baina ya Bi Siwa na mwanawe Mbawazi, wakizungumzia hali ya kiangazi inayowakabili. Licha ya kuwa Bi Siwa anafahamu kuwa yote hayo yanatokana na mipango mibaya ya utawala na ubinafsi wa viongozi, anabadili msimamo wake kuhusu chanzo cha matatizo yanayowakabili anapokumbuka maneno ya padre kuwa hali inayowakabili ni mojawapo ya ishara kwamba dunia inakwisha. Licha ya elimu kwa umma pamoja na dalili zote zinazoonyesha chanzo cha njaa inayosababishwa na kiangazi, bado kunao wanajamii ambao wanafuata viongozi wa kidini kikasuku bila kufikiria. Kilicho dhahiri ni kwamba, Arege anamtumia mhusika padre kama kielelezo cha viongozi wa kidini ambao hutumia dini kuwapotosha waumini badala ya kuwaeleza ukweli wa maisha katika ulimwengu halisi jinsi ulivyo.

Kadhalika, unafiki wa viongozi wa kidini unadhihirika wazi kupitia mhusika Mhubiri katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Meya wa baraza la mji wa Cheneo ni kiongozi dhalimu ambaye anatumia mbinu mbovu za utawala ili kujinufaisha mwenyewe pamoja na marafiki wake wa karibu. Hata hivyo, anamualika Mhubiri katika afisi yake mara kwa mara kwa lengo la kuombea uongozi wake, jambo ambalo mbubiri anakubali. Unafiki wa mhubiri unajitokeza katika dondoo lifuatalo:

Mhubiri: *Ndugu mpendwa akikuita unaitika. Hii ndiyo kazi ya watumishi wote wa Mungu. Kutowatii ni kutomtii Mungu.* Tulipoitwa kuhudumu tuliitika na hakuna kurudi nyuma. Itakuwa makosa Mtumishi wa Bwana kuivuta nyuma kazi yake.

Meya: Umenigusa ndugu mhubiri. Kila tukikutana kitu kutoka ndani kabisa hunisukuma kutaka nikufuate. Mara mbili hivi karibu naiacha kazi hii nije tushirikiane.

Mhubiri: Ameen! Hizo ni nguvu za Bwana. Ni mapenzi yake. Yote haya kwa utukufu wake. (Uk 41)

Mhubiri ni mwanajamii katika jamii iliyoangaziwa na mwandishi. Kwa hivyo, inatarajiwa kwamba anajua hali zinazowakumba wanajamii wenzake chini ya uongozi wa Mstahiki Meya. Hata hivyo, Mhubiri anapoitwa na Meya kuliombea baraza, anatii huku akimsifu Meya pamoja na uongozi wake. Sababu ya kusifu uongozi wa Meya ni

kuwa anaahidiwa kulipwa pesa nyingi kila mara anapoenda kuombea baraza. Katika hali ya kawaida, viongozi wa kidini wanatarajiwa kuwakosoa wanajamii wote pakiwemo viongozi wa kisiasa ili waongoze wananchi kwa njia inayowafaidi wanajamii wote.

Mhubiri katika tamthilia hii anawakilisha viongozi wengi wa kidini ambao ni wanafiki na wabinafsi wanaoenda kinyume na maadili kwa kutumia dini kujinufaisha wenyewe. Nadharia ya uhakiki wa kiekolojia hudai kwamba, kila binadamu ameathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira (Nabeta na Ongutte, 2014). Hii ina maana kwamba, ni wajibu wa kila mwanajamii kuhusika katika kuyaokoa mazingira yaliyoharibiwa, bila kujali umri, kabila jinsia, elimu, tabaka au hata dini. Kauli hii inawarejelea viongozi wa kisiasa na wale wa kidini ambao wanajitenga na uhalisia wa mabadiliko ya tabianchi, kama inavyobainika katika *Mstahiki Meya*.

Hali hii pia inaweza kuthibitishwa wa utafiti wa Ng`etich (2011) uliobaini kuwa kuna baadhi ya wahubiri ambao hutumia njia mbalimbali ili kuwavutia waumini wao. Aidha, wao hufanya chochote ili kujipatia sifa ambazo zinawafanya watu wengi kuwaamini na kujiunga na makanisa yao. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kunufaika na kujiendeleza kiuchumi bila kujali hali ya waumini wao. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba Arege anawakejeli viongozi wa kidini katika jamii ambao wametawaliwa na tamaa huku wakisahau wajibu wao wa kuielekeza na kuikosoa jamii.

## 5.8 Ushairi

Kwa mujibu wa Senkoro (1988), ushairi ni utungo ambao hutumia lugha ya mkato, yenye maneno yaliyoteuliwa kwa makini na kimakusudi ili yaibue taswira maalumu katika akili ya msomaji au msikilizaji. Aidha, ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo, wazo au tukio kwa namna inayovuta hisia kutokana na mpangilio maalumu wa maneno yaliyoteuliwa kimahususi. Mwandishi wa *Janga la Werevu* ametumia ushairi ili kueleza kiubunifu matatizo yanayokabili wanajamii pamoja na chanzo chake. Katika kufanya hivyo, Mwendawazimu anatongoa kishairi ifuatavyo:

> Jua la jahanamu linadanda, linapiga kuangamiza uhai, uhai wetu sisi na uhai wa dunia, maji yameshapeperushwa, hata wake mvuke hauko hewani, umebaki mwingi uangavu, ukavu na joto pia, vyakula

> vimetoweka na njaa ilojitawala inashikilia, kiu za mwili na roho sasa zaongoza. (Uk 21)

Kupitia ushairi wa Mwendawazimu, mwandishi analeta taswira ya uhalisia wa athari za uharibifu wa mazingira. Miongoni mwa athari hizi ni kuongezeka kwa viwango vya joto duniani, jambo ambalo linatishia kuangamiza uhai, uhaba wa maji na janga la kiangazi ambacho hatimaye kimesababisha njaa na kiu. Hivyo, inaelekea kuwa lengo la matumizi ya ushairi huu ni kufafanua chanzo cha madhila yaliyoikabili jamii iliyosawiriwa na mwandishi kwa namna inayoteka hisia, ili kuonyesha uzito wa suala la uharibifu wa mazingira. Akieleza kuhusu umuhimu wa uhakiki wa kiekolojia, Alia (2017) anasema kwamba fasihi inazingatiwa kuwa nyenzo iliyo na uwezo wa kuleta uelewa kuhusu masuala ya kiekolojia. Kwa kufanya hivyo, itasaidia katika kuhifadhi mazingira. Mtunzi wa *Janga la Werevu* ametumia ushairi ili kufafanua baadhi ya masuala muhimu yanayohusiana na mazingira. Kwa hivyo, jitihada katika uhifadhi wa mazingira ni jambo la dharura ili kuepuka majanga..

**5.9 Chuku**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), chuku ni mbinu inayotumiwa kuelezea hali ya kuikuza sifa ya kitu fulani kuliko kawaida. Kwa maoni yake, matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo na kwa kiasi kikubwa huchangia katika kuyachimuza masuala fulani katika kazi inayohusika. Watunzi wa tamthilia teule wametumia chuku katika kazi zao ili kuchimuza athari mbalimbali za uharibifu wa mazingira. Katika *Majira ya Utasa*, wahusika Hori na Kato wanazungumzia viwango vya joto vilivyozidi kama ifuatavyo:

> Kato: Joto hili halijawahi kushuhudiwa tangu tutie fahamu. Ndani hapakaliki na nje ni mfano wa tanuu. Huu ni mwaka wa hari.
> Hori: Kiangazi cha namna hii sijakiona mimi. Nimekuwa nikizisikia hadithi za mbali huko. Hadithi za Sahara na Kalahari. Si hapa kwetu. *Viwango hivi vya joto vinaweza kukuyeyusha ubongo ikiwa utalifanyia ushindani*. (Uk 65)

Ujumbe unaojitokeza kupitia mazungumzo haya ni kwamba viwango vya hali ya joto vimeongezeka kiasi cha kuwatia wanajamii wasiwasi. Hii ndio maana Kato anafananisha kukaa nje sawa na kukaa kwenye tanuu. Kutokana na maneno ya wahusika hao, ni dhahiri kwamba kuongezeka kwa viwango vya joto kumeathiri kila pembe ya dunia. Hii ina maana kwamba suala la kuhifadhi mazingira ni jukumu la kila

mtu kote duniani ili kupunguza athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira kama vile kuongezeka kwa viwango vya joto duniani. Kama anavyosema Iheka (2015), uhalisia wa ongezeko la joto duniani pamoja na mabadiliko ya tabianchi ni mambo ambayo yanawalazimu wahakiki wa kiekolojia kuangazia kwa umakini athari za kiekolojia kwa jumla. Hata ingawa viwango vya joto duniani vimeongezeka, mwandishi ameeleza hali hiyo kwa namna iliyotiliwa chuku, ili kuonyesha uzito wa suala hilo. Hori anaposema kuwa viwango hivyo vya joto vinaweza kuyeyusha ubongo wa mtu, ni chuku kwa kuwa huenda hali hiyo isiwezekane katika hali halisi. Kadhalika, mwandishi wa *Majira ya Utasa* amesawiri kuongezeka kwa viwango vya joto kwa namna iliyotiliwa chuku kama ifuatavyo:

Deka: Si mbaya sana hali. Wajua ni kwa sababu ya msimu huu mrefu wa kiangazi.
Bi Siwa: Hiki si kiangazi tena. Ni balaa hii. Sijawahi kuyaona haya maishani. *Joto kali hili. Linaweza kuzibambua ngozi.* Sasa imefikia hali ya watu kufa! Na ikiendelea hivi si ajabu tutakufa kama nzi! (Uk 9-10)

Bi Siwa anazungumza na Deka, mfanyikazi wa Jumbe kuhusu matatizo yanayowakabili wanajamii. Bi Siwa anakiri ya kwamba hajawahi kushuhudia joto la aina hiyo katika maisha yake. Ili kuonyesha kiasi cha kuongezeka kwa joto hilo, Bi Siwa anasema kwamba linaweza kuzibambua ngozi. Hii ni chuku iliyotumiwa na mwandishi ili kuonyesha uzito wa suala la kuongezeka kwa viwango vya halijoto duniani.

Kama anavyoeleza Sangili (2015), ongezeko la viwango vya joto duniani ni suala ambalo limeibua mijadala ya kitaifa na kimataifa hivi karibuni, ndiposa watunzi wa fasihi wamejihusisha katika kueleza hali hiyo kiubunifu kupitia kazi zao. Ili kudhibiti viwango vya joto hadi vipimo vinavyohitajika vya nyusi joto 1.5, wanasayansi wanashauri kuwa jamii inastahili kupunguza kwa kiwango kikubwa shughuli zake za viwanda na shughuli zingine za mazingira ambazo zinachangia kupanda kwa viwango vya joto duniani. Aidha, wanasayansi wanapendekeza mabadiliko katika mifumo ya nishati, mabadiliko ya njia za matumizi ya ardhi pamoja na mabadiliko ya mfumo wa usafiri (BBC News Swahili, 2018). Kwa hivyo, ni jukumu la kila mtu kuchukua hatua zinazohitajika ili kushiriki katika upunguzaji wa viwango vya halijoto vilivyo na athari kubwa kote duniani.

## 5.10 Tashbihi

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Aidha, tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungo kama mfano wa, mithili ya, kama vile na kadhalika (Wamitila, 2003). Kwa maoni ya Wamitila (keshatajwa), umuhimu wa matumizi ya tashbihi ni mchango wake katika kuwasilisha maudhui na mawazo ya mwandishi. Katika *Janga la Werevu*, mwandishi ametumia tashbihi kuonyesha hali ya uhaba wa maji kama ifuatavyo:

> Mwanamke II: Ebo! Itakuwaje sisi tumefika hapa alfajiri hata jua halijachomoza tukose maji. Na wewe uliyekuja hapa punde hivi upate maji. Unadhani sisi wapuuzi tuliokuja kupanga foleni mapema? Nyinyi mliofika hapa sasa hivi mnataka *kutukata bogi* na kuchukua nafasi zetu ili tukose hata tone moja la maji. *Mchirizi wa maji yenyewe unatiririka kama chozi la huzuni*. (Uk 18-19)

Kupitia mfano huu, mwandishi analeta taswira ya hali mbaya ya uhaba wa maji. Maji yamekauka kwenye chemchemi zote za misitu ya wananchi, na kubaki mchirizi mwembamba tu wa maji. Kwa sababu ya uhaba huu, umati wa watu umo katika vurugu la kutapia maji, ili mtu apate angalau matone machache. Ndiposa Mwanamke II anafananisha namna maji hayo yanavyotiririka na chozi la huzuni kutokana na uchache wake. Hali hii ya uhaba wa maji inaafikiana na ripoti ya Taasisi ya Rasilimali za Dunia kuwa, karibu watu bilioni 2.5 ulimwenguni wanaishi katika mikoa yenye upungufu mkubwa wa maji. Hivyo, ni dhahiri kuwa uhaba wa maji ulimwenguni ni tatizo ambalo linaongezeka kwa sababu ya kupungua kwa rasilimali na kuongezeka kwa mahitaji yake kadri idadi ya watu inavyoongezeka (FAO, 2013). Ili kupunguza uhaba wa maji, ripoti ya Taasisi ya Rasilimali za Dunia inapendekeza kuzuia uchafuzi wa maji kwenye mito, maziwa na maji ya chini ya ardhi pamoja na kuwa na matumizi bora ya maji katika kilimo na kwenye viwanda, mambo ambayo yatachangia katika kuongeza sehemu inayopatikana kwa matumizi ya binadamu. Kadhalika, mwandishi wa *Majira ya Utasa* ametumia tashbihi ili kusawiri athari za ukame. Uhalisia wa athari za ukame unaosababisha njaa unadhihirika katika dondoo lifuatalo:

> Deka: Watu wanakufa lakini hatuwezi kusema ni kwa sababu ya njaa wala kuvifananisha vifo vyao na vya nzi!

Bi Siwa: Kama watu wanakula mizoga ya wanyama ambayo haiwahakikishii nguvu na pumzi, *nini basi kama si kufa kama nzi?*
Deka: Mizoga? Una hakika?
Bi Siwa: Unafikiri mchezo? Nyinyi mlio na ajira kwa wenye navyo hamwezi kuelewa.
Deka: Ninajua kuwa umekuwepo ukame kwa muda sasa ambao umesababisha njaa ila sina habari kama watu wala mizoga. Si hapa kwetu! (Uk 10)

Kinachodhihirika katika dondoo hili ni kwamba ukame ambao umekuwepo kwa muda mrefu umesababisha njaa. Kama anavyoeleza Bi Siwa, njaa imeathiri watu kiasi cha kula mizoga ya wanyama, jambo ambalo lisababisha vifo vya watu wengi. Kwa hivyo, mwandishi anapotumia tashbihi ya `kufa kama nzi`, anarejelea hali ya idadi kubwa ya watu kufa ovyo ovyo hasa kwa sababu ya njaa. Kwa mujibu wa Heise (2008), kando na uhakiki wa kiekolojia kutazama jinsi mifumo mbalimbali inavyofanya kazi ili kukidhi maisha, huangazia pia jinsi mifumo hii inavyoharibiwa na kusababisha vifo vya binadamu, wanyama na hata kukauka kwa mimea. Hivyo, vifo vinavyosawiriwa katika mfano uliotolewa ni dhihirisho la athari za mifumo ya kiekolojia iliyoharibiwa. Vilevile, imebainika kwamba idadi kubwa ya wale walioathiriwa na njaa ni wananchi wa kawaida. Deka ambaye ni mfanyikazi wa Jumbe anaikana hali inayowakabili wananchi wa kawaida licha ya kuwa yeye ni mwenyeji wa jamii husika. Kwa hivyo, Deka anawakilisha watu wabinafsi ambao hufaidika kutokana na viongozi, ambao hawajali masilahai ya wanajamii wenzao.

Athari za ukame zilizoangaziwa na mwandishi wa *Majira ya utasa* zinaweza kushadidiwa na hali inayowakabili watu wengi katika sehemu nyingi kote ulimwenguni. Nchini Kenya, wakaazi katika jimbo la Marsabit wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu kufuatia hali ya ukame inayoendelea kushuhudiwa humo. Hali hii ya njaa kutokana na ukame imesababisha vifo vya watu na pia wanyama, pamoja na kuchochea mizozo kati ya binadamu na wanyamapori (Welle, 2022). Kando na juhudi za serikali za kuwanusuru watu dhidi ya makali ya njaa hasa kupitia vyakula vya misaada, ni wajibu wa serikali kuibua njia mbadala za kusitisha hali ya kiangazi. Njia hizo ni kama vile kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira pamoja na kutafuta njia nyinginezo za kilimo kisichotegemea maji ya mvua.

### 5.11 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo hueleza sifa za kitu fulani. Aidha, ni mbinu ya kiulinganishi lakini ulinganishi huo haujitokezi waziwazi. Kama anavyoeleza Wamitila (2003), sitiari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile. Katika msingi huu, sitiari imejengekea kwenye uhamishi wa maana. Hivyo, matumizi ya sitiari yanaweza kuwa yamelenga hisia au fahiwa fulani au kujenga taswira fulani. Watunzi wa tamthilia teule wameeleza motifu mbalimbali za kimazingira kwa kutumia sitiari. Katika *Majira ya Utasa*, Kato anasema:

> Kato: *Miungu wapo kuleta faraja kwetu, siyo kutufilisi. Labda miungu wa leo ni tofauti na wa jana.* Wa jana walijinyima kwa ajili ya watu. *Wa leo wapo kutunyonya damu* na kuvuruga njia za kuwasiliana na mizimu. Na wanajua tunawaogopa. Hivyo wanatuchezea shere. Hapana! Mtu huonyesha anapoumwa. Husema kinachomuuma. Hata bubu husema aonapo uchungu seuze mwenye sauti? (Uk 46)

Mhusika Kato anatumia neno `miungu` kuwarejelea viongozi katika jamii. Kulingana na mtazamo wake, viongozi wa aina yoyote katika jamii wanatarajiwa kuleta faraja kwa wanajamii kwa kuwajalia masilahi yao, huku wakiweka mahitaji ya wanajamii kabla ya mahitaji ya kibinafsi. Hata hivyo, inaelekea kuwa viongozi wanaorejelewa wamebadilika kiasi cha kwamba wanatumia njia zote za kujinufaisha binafsi huku wakiwasahau wananchi wanaowategemea.

Hivyo, Kato anaposema kwamba `miungu wa leo wapo kutunyonya damu`, anamaanisha kuwa viongozi hao wanawanyima haki zao kwa kuwakandamiza. Matokeo ni majanga kama vile ukame, njaa na umaskini. Katika hali halisi, `mungu` ni jina lenye asili ya kibantu ambalo hutumiwa kurejelea yeyote anayesadikiwa katika dini mbalimbali kuwa na uhai wa hali ya juu. Wirth (1945) anapoeleza kuwa mamlaka yote yamo mikononi mwa wachache, ambao huamua namna, wakati na ni nani ambaye anapaswa kufaidika kutokana na rasilimali, anawarejelea viongozi walio na mamlaka katika jamii, ambao hutumia mamlaka yao kujifaidi pamoja na marafiki wao wa karibu, huku wakiwanyanyasa wanajamii wengine. Jambo hili linabainika wazi katika mfano uliotolewa ambapo mhusika Kato anasema kuwa viongozi hao wapo kunyonya wanajamii damu. Hivyo, viongozi waliosawiriwa katika mfano huu wana uwezo

mkubwa. Hii ndio maana Kato anawalinganisha na `miungu` kwa kusema kuwa wanaogopwa.

Sifa hii ya viongozi kuwa wadhalimu na wenye tamaa inaweza kulinganishwa na unyakuzi wa msitu wa Mau uliotekelezwa na wanasiasa nchini Kenya. Aidha, ardhi iliyotengewa huduma muhimu kama vile hospitali na shule hunyakuliwa na wanasiasa huku wananchi wakiteseka kwa kukosa huduma muhimu (M`Ngaruthi, 2015). Hata ingawa mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anawalaumu viongozi wadhalimu wanaowanyanyasa wananchi, imebainika kuwa pia analenga kuwazindua wananchi kuhusu haja ya kuzungumzia madhila yanayowakabili bali si kunyamaza kwa kuwaogopa viongozi. Ushahidi zaidi wa udhalimu na unafiki wa viongozi hasa wa kiafrika unapatikana katika tamthilia ya *Janga la Werevu*, ambapo mtunzi anaonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyoendelezwa na viongozi wa kiafrika waliochukua nyadhifa za uongozi baada ya uhuru. Akifafanua suala hili, Mwendawazimu anasema:

> Mwendawazimu: Pia tuliambiwa *mashetani watarudi. Kwamba watarudi kwa `mlango wa nyuma*. Na hilo nalo tukalipuuza kwani hapana mpaka sasa anayefikiri na kufanya juhudi za kuzuia mashetani wasirudi. Hata wale werevu miongoni mwetu, hata wale tunaowadhania ni mashujaa. Hata wale tunaowaamini. Wale wenye macho na masikio makali nao wamebaki kutumbua macho na kuziba masikio yao. *Kazi kujaza mali mifukoni mwao. Wamo wamekaa kimya kuwafagilia njia mashetani wapite kunyang`anya bila ya kizuizi chochote kwa jina la utandawazi.*(Uk 13)

Katika mfano huu, mwandishi anawasawiri viongozi waliochukua nyadhifa mbalimbali serikalini baada ya uhuru kupatikana kama wadhalimu na wanafiki. Anatumia sitiari ya `mashetani` kuwasawiri viongozi wasio na utu kupitia matendo yao ya kuwanyanyasa wananchi kwa manufaa ya kibinafsi. Mwandishi anaposema kuwa `mashetani walirudi kwa mlango wa nyuma`, anarejelea jinsi viongozi wa kitaifa walivyobadilika na kuanza kuiga mbinu zilezile zilizotumiwa na wakoloni katika kuwanyanyasa wananchi. Kadhalika, mwandishi anawalaumu watu walio karibu na viongozi hao kwa kushirikiana nao kukandamiza umma badala ya kuwakosoa. Kwa hivyo, anasisitiza kuwa `wamo wamekaa kimya kuwafagilia njia mashetani wapite kunyang`anya bila

kizuizi chochote`. Sababu ya wao kukaa kimya ni kwa sababu pia nao wanafaidika kutokana na matendo ya viongozi hawa.

Hali hii ya ukoloni mamboleo katika mataifa mbaimbali inashadidiwa na madai ya Wamitila (2003) kuwa hata ingawa nchi za Asia, Afrika na Amerika ya Kilatini zina uhuru wa kisiasa, bado zinatawaliwa na kutegemea nchi za kizungu. Hii ni kwa sababu viongozi waliochukua hatamu za utawala baada ya ukoloni mkongwe waliendeleza uongozi wa kiimla na kuudhulumu umma. Bado kuna tamaa na ubinafsi ambapo viongozi wanatumia mbinu mbalimbali kujinufaisha binafsi bila kujali umma. Matokeo ni majanga kama vile ukame na njaa, mafuriko na vifo. Kwa mujibu wa Rigby (2002), mwanadamu anachangia katika kuharibu uhai asilia wa mimea na wanyama. Hivyo, wanatishia msingi wa uhai unaotegemewa na jamii za binadamu. Hata ingawa wanaorejelewa katika uharibu wa mazingira ni viongozi katika jamii, inaelekea kuwa mwandishi wa *Janga la Werevu* anaukosoa umma kwa kuwa na mapuuza kwani hakuna juhudi zinazoonekana za kuwazuia na kuwakomesha viongozi wadhalimu katika jamii.

### 5.12 Mbinu Rejeshi

Kulingana na TUKI (2013), mbinu rejeshi hutokea pale ambapo msanii hurejelea mambo yaliyotokea hapo awali lakini hayakutajwa wakati wa kutokea kwake, bali yanazungumziwa baadaye. Kwa upande wake, Wamitila (keshatajwa) anaeleza mbinu rejeshi kama mbinu anayoitumia mwandishi kuyaeleza matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi. Mwandishi wa *Janga la Werevu* ametumia mbinu rejeshi ili kusawiri umuhimu wa maji. Mfano ufuatao unashadidia:

> Mwendawazimu: Lakini kama tungeyatia maanani maneno yake tungejua kwamba ule si upuuzi. *Kwani maji ni kitu muhimu na kitakatifu kuliko kitu kingine chochote.* Kauli ya Kinjeketile ni kitendawili kilichofumba kikwelikweli. Fumbo linalotilia mkazo umuhimu na utakatifu wa maji. Pia *katika muktadha wa vita vya majimaji, maji yalikusudiwa kuchochea haja ya kuvinjari. Kuvinjari hata kama kuna kifo mbele ya wanaoonewa.* Haja ya kuthamini na kujiamini mtu mwenyewe na kuthamini baadhi ya fikra za kale ingawa ni fumbifu na tatizi. Fikra zinazoonekana hazina maana katika dunia hii ya werevu… (Uk 4-5)

Katika mfano huu, Mwendawazimu anayasawiri maji kuwa kitu kitakatifu kuliko kitu kingine chochote. Aidha, anarejelea muktadha wa vita vya majimaji ambapo Kinjeketile alipendekeza umuhimu wa maji ya uhai katika kupigana vita. Katika vita hivyo, maji yalikusudiwa kuchochea haja ya kujithamini na kujiamini mtu mwenyewe hata kama alikabiliwa na kifo. Kupitia mfano huu, mwandishi anapendekeza haja ya kuthamini baadhi ya fikra za kale hata zile ambazo zinaonekana kuwa hazina msingi. Hii ni kwa sababu si kila fikra za kale zimepitwa na wakati kwa kuwa zinaweza kuwa na manufaa mengi. Nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inashadidia kuhusu umuhimu wa kuthamini baadhi ya fikra za jadi kwa kudokeza kuwa, utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Glotfelty, 1996). Kwa hivyo, mwandishi anaangazia haja ya kuthamini tamaduni hasa zile zilizohusishwa na uhifadhi wa mazingira asilia kama vile misitu ili kuhakikisha kwamba uhaba wa maji umesitishwa.

## 5.13 Hitimisho

Sura hii imeangazia mbinu mbalimbali za kimtindo kama zilivyotumiwa na waandishi wa tamthilia teule za Said A. Mohamed na Timothy Arege katika kusawiri motifu za kimazingira. Mbinu zilizobainika zimetumika kufafanua masuala mahususi ya kimazingira kama yalivyosawiriwa na waandishi wa tamthilia teule, kama vile uharibifu wa mazingira na namna uharibifu huo umeathiri mfumo wote wa ekolojia. Kwa hivyo, utafiti huu umethibitisha kuwa, waandishi hawa wamefaulu katika kusawiri motifu za kimazingira kupitia kazi zao.

# SURA YA SITA

# MOTIFU ZA KIMAZINGIRA NA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA TIMOTHY AREGE

## 6.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alitathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira, kwa mujibu wa tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Uchanganuzi wa data ulibaini kwamba, lazima pawepo na mbinu za ukombozi wa mazingira kutokana na uharibifu uliosababishwa na mwanadamu ili kuokoa maisha yake pamoja na yale ya viumbehai wengine. Waandishi wa tamthilia teule wamesawiri motifu mbalimbali ambazo zimeangazia namna ya kuhifadhi mazingira. Motifu za kimazingira ambazo zililenga kuhifadhi mazingira zilizobainika katika utafiti huu ni pamoja na motifu ya safari, motifu ya ujadi, motifu ya elimu, motifu ya umoja, motifu ya uzalendo na motifu ya mapinduzi.

## 6.2 Motifu ya Safari

Kwa mujibu wa Senkoro (1997), roho ya kazi yoyote ya kifasihi iliyo bora ni safari. Kwa maoni yake, hii inaweza kuchangiwa na ukongwe wake, kama ilivyo fasihi yenyewe. Motifu ya safari ni mojawapo ya motifu zilizojitokeza kwa kiasi kikubwa katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Kama anavyoeleza Senkoro (keshatajwa), motifu ya safari na msako kwa kiishara zinahusiana na hatua za kukuza wahusika katika kazi hizo. Kwa msingi huu, wahusika mbali mbali katika tamthilia teule wamesafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kutafuta suluhisho la uharibifu wa mazingira uliowaathiri pamoja na jamii zao. Safari zilizobainika katika tamthilia teule ni safari ya Siki, Safari ya Mpya na safari ya wawakilishi wa Kijiji.

### 6.2.1 Safari ya Siki

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, daktari Siki ni mmoja kati ya wahusika waliojitolea katika utetezi wa haki za jamii yao. Yeye pamoja na wafanyikazi wenzake katika Cheneo wanafanya kazi katika mazingira duni. Miongoni mwa mambo yanayowaathiri ni ukosefu wa maji katika Cheneo nzima na uchafu unaotapakaa katika kila sehemu. Yote haya yamechangiwa na uongozi dhalimu wa Meya ambaye hayajali masilahi ya umma. Kutokana na hali hii, Siki anafunga safari kwenda kuzungumza na Meya ili amweleze kuhusu hali ya mambo Cheneo. Mfano ufuatao unathibitisha:

> Siki: Bwana Meya, mimi ninakwambia kama ndugu yako. Sisemi kwa sababu ya siasa. La! *Ukweli ni kwamba watu wetu wana tatizo. Watu wetu wana njaa. Wana kiu ambayo haikuzimwa…* Huenda isichukue muda mrefu…
>
> Meya: Umesema nini Siki? Huheshimu uongozi wangu? Huoni niliyoyafanya hapa Cheneo? (Uk 12)

Katika mazungumzo haya baina ya Siki na Meya, Siki anamkumbusha Meya kuhusu matatizo yanayowakabili wananchi kama vile njaa na kiu. Kutokana na maneno ya Siki, imebainika ya kwamba kumekuwa na hali ya ukame katika jamii, ambao umesababisha njaa na uhaba wa maji. Hii ni idhibati kwamba, Meya pamoja na marafiki wake wa karibu wamechangia katika matatizo yanayowakabili wanajamii, hasa kutokana na ubinafsi na mbinu mbovu za utawala wake. Hali ya viongozi kuwa chanzo cha matatizo yanayowakumba wanajamii inaafikiana na matokeo ya utafiti wa Sangili (2015). Alibaini kuwa viongozi katika serikali ya nchi wakati mwingine huchangia katika uharibifu wa mazingira kwa namna mbalimbali. Siki anatambua kuwa majanga yanayokumba watu wa jamii yake yamesababishwa na Meya. Hii ndiyo maana anamtahadharisha kuwa, ikiwa hali itaendelea hivyo, huenda uongozi wake usifike mbali.

Kadhalika, Siki anaamua kwenda kuzungumza na Diwani III ambaye alijulikana kwa kutetea masilahi ya wananchi katika mikutano ya madiwani. Lengo la kwenda kwa Diwani III lilikuwa kumshawishi ili aweze kumshauri Meya kuhusu namna ya kushughulikia wananchi wanaoangamia. Katika mazungumzo yafuatayo, Siki anamshawishi:

| | |
|---|---|
| Diwani III: | Kuona nimeona ulivyoona wewe. Lakini nitafanya nini? Mimi… |
| Siki: | *Unaweza kufanya jambo.* |
| Diwani III: | Lipi la kufanywa? |
| Siki: | Kheri, wewe ni diwani kama huyo Meya Sosi na mnakutana kila leo. Pili, wewe ndiye Bwana Hazina wa Baraza. *Ushauri wako kwa Meya unaweza kuwa na ushawishi mkubwa.* (Uk 46) |

Katika mfano huu, Siki anamwambia Diwani III kwamba ushauri wake kwa Meya unaweza kuwa na ushawishi mkubwa kwa kuwa yeye ndiye Mweka Hazina ya Baraza kando na kuwa diwani. Licha ya kuwa Meya huwa hatilii ushauri wa Diwani III maanani kama ilivyokuwa zamani, Siki anamshauri kwamba aendelee kuzungumza naye pasi kukata tamaa. Kutokana na hatua ya Siki ya kusafiri hadi nyumbani kwa Meya na vilevile kwa Diwani III ili kuzungumza nao kuhusu matatizo ya wanajamii, mwandishi anamsawiri kama mhusika mzalendo ambaye anafanya kila awezalo ili kuokoa wanajamii kutokana na matatizo yanayowakumba chini ya utawala dhalimu. Uzalendo huu ndio Buell (1996) anaorejelea anaposema kwamba, uraia wa kimazingira una misingi katika maadili ya kiekolojia. Hivyo, uhakiki wa kiekolojia unahimiza kila mtu kuwa raia wa kimazingira, ili kuhusika kikamilifu katika uhifadhi wake.

### 6.2.2 Safari ya Mpya

Katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, mhusika Mpya anasafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa nia ya kupata suluhu la majanga yanayokumba jamii yake. Katika mfano ufuatao, Mpya anasema:

> Mpya: Niko njiani wahenga. Hatua kwa hatua. Niko njiani. Nitajitumbukiza kisimani kichwa juu miguu chini au miguu juu kichwa chini. Lazima mmoja wetu aanze. Lazima mmoja wetu ajitolee. Lazima mtu mmoja ajitolee mhanga, ndipo usasa utatuheshimu na sisi kuuheshimu. (Uk 21)

Haya ni maneno ya Mpya akiijibu Sauti Ndani ya Kisima. Mpya ni kitindamimba wa kiongozi Bw. Binafsi ambaye ameongoza jamii yake kwa namna isiyowaridhisha. Hivyo, kuzaliwa kwa Mpya kunaleta matumaini ya ukombozi katika jamii hii. Katika mfano uliotolewa, Mpya anasafiri hadi kwenye kisima cha jadi palipoaminika kuwa na maji ya ujasiri. Lengo lake lilikuwa kupata ujasiri ili aanze kuhamasisha umma kuhusu

haja ya kusema wazi huku wakilalamikia matatizo yanayowakabili. Akieleza kuhusu umuhimu wa uhakiki wa kiekolojia katika kupiga vita uhalifu na majanga ya mazingira, Culler (2011) anasema kwamba ni lazima watu wahamasishwe kuhusu haja ya kuungana pamoja huku wakipinga uongozi dhalimu ili kuhakikisha kuwa maisha yao ya baadaye yameimarika. Uhamasishaji wa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira ndio mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* anaoangazia kupitia mhusika Mpya.

Baada ya kunywa maji ya kisima cha jadi, Mpya anapata ujasiri wa kupaza sauti yake ambayo inasikika kote. Anasafiri katika kila pembe ya nchi huku akiwazindua watu kuhusu ukombozi baada ya miaka mingi ya kunyanyaswa na viongozi. Miongoni mwa mambo ambayo Mpya anatetea ni ukataji ovyo wa miti na uchafuzi wa mazingira yao, mambo ambayo yanaathiri wanajamii wote kwa jumla. Haya yote yanatokana na ubinafsi wa Bw. Binafsi. Katika mfano ufuatao, Mpya anasema:

> Sauti ya Mpya: Sisi wananchi tumeamua kwamba *kesho tukutanike tena kulalamika na kutetea haki zetu.* Hatutaki fujo lakini. Tutasimama pamoja kuweka waziwazi kero zetu, maana tunaona hatusikilizwi. Sisi hatutaki fujo. Hatutaki fujo. (Uk 72)

Maneno haya yanarejelea sauti ya Mpya ambayo imeenea kote nchini. Inapenya majijini, vitongojini na viungani. Inatembea mitaani na viamboni vilevile. Katika mfano uliotolewa, Mpya anawahimiza wananchi kukutana tena ili kulalamikia haki zao. Vilevile, anawakumbusha kuwa watasimama pamoja kuweka wazi matatizo yao bila fujo. Kwa hivyo, jitihada za Mpya kusafiri katika kila pembe ya nchi huku akihamasisha wanajamii ni dhihirisho la kuwa yeye ni mtu anayependa nchi na watu wake. Maneno ya Mpya yanathibitishwa na Schartz (2012) anayedai kwamba, nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inahimiza kuwa, ni lazima watu wasimame kidete kudai kugeuza mwenendo wao wa kutojali maslahi yao ya kitaifa huku wakisaidia katika upatikanaji wa masilahi ya nchi na mataifa mengine. Madai haya yanarejelea suala la utandawazi ambapo mataifa makubwa ndiyo yanayotumia nguvu ili yang`ang`anie ustahiki wa kutetea na kupata masilahi yao wanayotaka. Isitoshe, kama anavyohimiza Mpya, ni lazima wananchi wawe tayari kupigana vita kwa ushujaa kuondoa ubinafsi na kugeuza hali ya nchi yao ili viongozi wasiigeuze mali ya kibinafsi.

### 6.2.3 Safari ya Wawakilishi wa Kijiji

Motifu ya safari inajitokeza katika tamthilia ya *Majira ya Utasa* kupitia safari ya wawakilishi wa kijiji. Katika mkutano wao, waliafikia uamuzi wa kutuma baadhi yao juu mlimani kuona hali ya madhababu yaliyotumiwa na wazee wao kutolea kafara, ili nao wazingatie mwenendo huo wa kutoa kafara kama suluhisho la hali mbaya ya kiangazi kilichowakabili. Katika mkutano wa wawakilishi wa kijiji, Hori anasema:

> Hori: Siwa ni mwakilishi wetu. Si wake yeye wala hawezi kutuchagulia nani wa kutuwakilisha. Naona aendelee bado kutuwakilisha. Ili kutuwakilisha vizuri, naona ajiunge na mimi na Dosho hiyo kesho twende juu mlimani kuangalia hali. Akijionea hali ilivyo ataweza kuieleza kwa Jumbe vizuri iwapo atahitajika kufanya hivyo. Mebo naye azunguke kijijini kuwaambia kuwaambia watu kusudi La kikao hiki. Wajiandae kuweka mwiko siku yenyewe itakapofika. Wewe utasubiri Kila kundi kuleta habari na kuzituma kwa watu. (Uk 48)

Mfano huu unaangazia kauli ya Mebo, mmoja wa wawakilishi wa Kijiji. Katika kikao chao kujadili kuhusu hali ya kiangazi cha muda mrefu kilichoelekea kuangamiza watu katika kila pembe ya nchi, waliafikia wazo la kuwa huenda wameghadhabisha mizimu hasa kwa kukosa kutoa kafara. Hii ndiyo maana walifanya uamuzi wa kwenda juu mlimani kuona hali ya madhabahu. Uamuzi huu ulitokana na fununu kwamba, madhabahu yenyewe yalishaharibiwa na Jumbe pamoja na wafanyakazi wake. Kama anavyoeleza mhusika Hori, kuona hali ya madhabahu kungemwezesha Siwa, mwakilishi wao kwa Jumbe kueleza jinsi alivyoshuhudia mwenyewe. Kwa mujibu wa Barry (2013), uhakiki wa kiekolojia huchunguza jinsi ambavyo binadamu, utamaduni na mazingira huhusiana na kuathiriana. Wawakilishi wa kijiji walipofanya uamuzi wa kusafiri hadi mlimani, walilenga kujua hali ya madhabahu ili waweze kutoa kafara. Waliamini kuwa wakifanya hivyo wazee watawasikiliza, jambo ambalo lingekuwa suluhisho la matatizo yao. Utoaji wa kafara ni sehemu ya utamaduni wa jamii, ambao ulilenga kuhifadhi mazingira hasa kupitia kunyesha kwa mvua. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba utamaduni wa jamii hauwezi kutenganishwa na ulimwengu halisi.

### 6.3 Motifu ya Ujadi

Suala la kudhamini fikra za jadi limekaririwa mara kwa mara katika tamthilia teule. Uchanganuzi wa tamthilia hizo umebaini kuwa, kuna baadhi ya fikra za jadi ambazo ni

muhimu katika uhifadhi wa mazingira. Hivyo, waandishi hawa wameangazia hali ambapo uasi wa baadhi ya fikra za jadi umesababisha majanga katika jamii kama vile kiangazi na njaa. Uchanganuzi wa tamthilia teule ulibainisha ujadi uliohusiana na itikadi na miiko na ule wa matambiko.

### 6.3.1 Itikadi na Miiko

Miiko ni makatazo makali ya matendo yaliyo katika imani ya tabia ambayo pengine ni takatifu au laana kwa mtu binafsi wa kawaida kufanya chini ya tishio la adhabu isiyo ya kawaida (Shongwe, 2015). Katika tamthilia ya *Janga la Werevu*, Mohamed anaangazia umuhimu wa miiko katika jamii kama njia ya kuhifadhi mazingira kupitia Mwendawazimu kama ifuatavyo:

> Mwendawazimu: Si kila siku fikra za kale ni mbovu lakini. *Bila ya shaka fikra za kale ziko nyingi nzuri na faafu*. Nazo hizo zinaweza kutusaidia kujilinda sisi wenyewe na kulinda mazingira yetu aina mbalimbali. *Na muhimu katika hizo ni zile zinazotuelekeza tuvinjari. Tupinge kuendelea kutawaliwa. Hasa kutawaliwa kimawazo*. (Uk 6).

Katika mfano huu, Mwendawazimu anasisitiza kwamba si kila fikra za kale mbovu kama zinavyopuuzwa na watu wengi katika dunia ya sasa. Hii ni kwa sababu kuna baadhi ya fikra hizo faafu ambazo zinaweza kusaidia katika kujilinda pamoja na kulinda mazingira. Kwa kusema hivyo, Mwendawazimu anarejelea hali ambapo watu wameasi mambo ya jadi yenye manufaa katika kulinda mazingira huku wakiiga yale ya kigeni. Kwa mujibu wa Alia (2017), Uhakiki wa kiekolojia hutoa nafasi ya kutathmini upya kuhusu uhusiano na ardhi ya baadaukoloni. Kwa kufanya hivyo, hujaza mapengo baina ya watu na mazingira, wenyeji na wageni na hivyo huwalazimu watu kujikita kwenye utamaduni wa kienyeji na kiasili pamoja na majukumu yao katika mazingira. Maoni ya Alia (keshatajwa) yanadhihirika katika mfano uliotolewa kupitia fikra za Mwendawazimu kuhusu umuhimu wa ujadi. Hivyo, anapendekeza kuwa watu wapinge kutawaliwa hasa kule kutawaliwa kimawazo. Kilicho dhahiri kupitia mfano huu ni kwamba, baadhi ya fikra za kale zina manufaa yake katika dunia ya sasa. Hivyo, ni wazi kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Janga la Werevu* anapendekeza kurejelea baadhi ya fikra za kale kama njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira.

Kando na kudhamini fikra za kale zinazopinga kutawaliwa kimawazo, mwandishi wa *Janga la Werevu* vilevile anasisitiza kuhusu manufaa ya kuendeleza tamaduni za kiafrika hasa zile zinazokumbatia itikadi na miiko katika kulinda mazingira. Katika mfano ufuatao, Busara anasema:

> Busara: Na hizo ndizo fikra zinazoelezea matabaka mnayosema hayo. Na sisi si wanamapinduzi kwa maana mnayofikiri nyinyi. Sisi tuna chembe ya *uhafidhina* tu. Sisi tunajali usasa ndiyo, *lakini hatusahau jadi. tuna chembechembe ya u-traditionalist, na u-conservative ambazo kila mzalendo wa kweli lazima awe nazo.* Kila mzalendo lazima awe mtazama nyuma na mbele… Nyuma natazama tulikotoka. *Tunahimiza busara za jadi, busara za wahenga. Na kwa hivyo tunasema misitu yote ni maeneo matakatifu tuliowachiwa na wahenga… maeneo ya sanctuary, yanayoambatana na itikadi, visaasili na miiko ya kijadiya kuyalinda*. Tusiache na kughairi mila bwana. Mwacha mila ni mtumwa. Lakini wale wanaojiita werevu miongoni mwetu tunayabeza hayo kwa *kufuata fikra za watu wengine zinazotangaza mfumo wa uroho duniani kote., mfumo unaomaliza kila kitu cha dunia hii*. (Uk 59-30)

Maneno ya Busara yanaonyesha kuwa watu wengi huchukulia wanamapinduzi kama waasi wa uongozi uliopo katika jamii. Kwa kutambua hivyo, Busara anamkosoa mamake Bimkuu kwa kumweleza ya kwamba kila mzalendo wa kweli lazima awe mtazama nyuma na mbele. Kwa kusema hivyo, Busara anahimiza hali ya kudhamini busara za jadi za wahenga, hasa zile zilizosisitiza kuwa misitu yote ni maeneo matakatifu hasa yaliyoambatana na miiko ya kijadi ili kuyalinda. Maoni ya mwandishi kupitia mhusika Busara yanaafikiana na mtazamo wa Falsafa ya Sankofa ambayo inasisitiza kwamba, ni lazima watu warudi kwenye mizizi yao ili kusonga mbele. Hii ina maana kwamba, watu wanapaswa kurejelea na kukumbatia mambo yao ya jadi mazuri na mafunzo yake ili kuafikia uwezo kamili wanaposonga mbele (Temple, 2010). Kwa hivyo, kupitia Busara, ni dhahiri kwamba mwandishi anawakashifu wanajamii ambao wameasi ujadi kwa kufuata fikra za watu wengine, hali ambayo anasisitiza kuwa ndiyo chanzo cha majanga yanayoangamiza dunia nzima.

### 6.3.2 Matambiko

Tambiko ni sadaka au ada inayotolewa kwa Mwenyezi Mungu, miungu, pepo au mizimu moja kwa moja au kwa Mungu kupitia kwa miungu (Kamusi ya Karne ya 21,

2011). Kama anavyoeleza Shemboko (2020), yapo matambiko ambayo yalitolewa na wazee waliokuwa wamepewa jukumu hilo. Hivyo, matatizo yaliyowakabili wanajamii yaliwasilishwa kwa miungu ili iwasaidie kuyatatua. Umuhimu wa matambiko katika uhifadhi wa mazingira umeshadidiwa na waandishi wa tamthilia teule. Katika *Majira ya Utasa,* Arege anasawiri hali ambapo ujadi uliohusiana na matambiko ulikusudiwa kuhifadhi mazingira. Haya yanajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Hori: Huelewi kuwa ni hayo ya madhababu? Utaelezwa vipi zaidi na huu si uvuvi?
> Dosho: Ulikuwa unasema madhababu hakuna?
> Siwa: Nilikuwa ninasema kuwa watu wameuvamia mlima wakavurugavuruga kila kitu.
> Hori: *Sheria ya Mzungu ilikataza watu kuingia msitunikule mlimani na hasa kwenye madhababu*. Ajabu leo hii watu kuingia mpaka mzimuni wakaiudhi mizimu. Ndiyo maana tunapata hiki kipigo(Uk 45)

Dondoo hili linaashiria kuwa matambiko kama shughuli ya kijadi ilikusudiwa kuhifadhi mazingira. Kwa kutambua umuhimu wa matambiko, wakazi wa jamii iliyosawiriwa na mwandishi wanajitahidi katika kutafuta madhabahu yaliyotumiwa na wazee wao kufanyia matambiko. Hata hivyo, inagunduliwa kuwa baadhi ya viongozi katika jamii waliuvamia mlima na kuvuruga madhabahu ili sehemu hizo zitumike kujengea viwanda vya maua. Kama anavyoeleza mhusika Hori, kuingia mzimuni kwenye milima kuliudhi mizimu, hali ambayo anaamini kwamba imesababisha majanga yanayowakabili kama vile kiangazi.

Umuhimu wa matambiko katika jamii unashadidiwa na King`ei na Kisovi (2010) wanaosema kwamba, matambiko katika jamii yalitokana na imani kuwa mababu ambao walifariki walikuwa na uwezo wa kutazama na kudhibiti matendo ya watoto wao ambao wako hai. Vilevile, iliaminiwa kuwa, mababu hao walipokasirika wakiwa kuzimu, wanao walio hai walikumbwa na matatizo na majanga kama vile magonjwa, vifo na kiangazi miongoni mwa majanga mengine. Kinachothihirika hapa ni kwamba sehemu za milimani zilihifadhiwa kwa ajili ya matambiko. Hivyo, sehemu hizo zilichukuliwa kuwa mahali patakatifu ambapo watu walikatazwa kuingia ovyo ovyo. Kwa kufanya hivyo, watu walijitenga na sehemu hizo, jambo ambalo lilichangia katika kuhifadhi misitu. Jambo hili pia limeshadidiwa na Mohamed katika *Kimya Kimya Kimya*. Katika

tamthilia hii, mwandishi anaangazia manufaa ya visima vya jadi ambapo wazee walikutana kwa ajili ya kujadili kuhusu matatizo yaliyowakabili na kutafuta njia za kuyaondoa matatizo hayo. Mfano ufuatao unashadidia:

> Kushoto: Aaaa, labda hiki ndicho *kile kisima cha jadi. Ndipo pahala patakatifu walipokutana wahenga kujadili mateso na kutafuta njia ya kuyaondoa*. Labda hapa ndipo baadaye palipochotwa maji kukata kiu na kuzima joto lililomo ndani ya nafsi zao. Labda hapa ndipo wazee wetu walipokuja kuinama kupiga kwenzi kusikiliza mwangwi wa sauti zao zilizowakejeli na kuwapa mori wa kusonga mbele… Au labda hiki ndicho kisima cha *Fumo Liongo alipotaka kufanya tambiko kuhifadhi nafsi yake*. Ndipo alipokimbilia kunywa maji ya kuokoa maisha yake baada ya kuchomwa *shazia* ya kitovu na mwanawe mwenyewe. (Uk 9-10)

Katika mfano uliotolewa, kisima cha jadi kinasawiriwa kuwa pahala patakatifu ambapo wahenga walikutana kila mara palipotokea matatizo katika jamii zao. Aidha, ni katika kisima hiki ambapo walipata matumaini na mori wa kusonga mbele kupitia kejeli za mwangwi wa sauti zao ndani ya kisima. Ili kuonyesha umuhimu wa maji ya kisima, mwandishi anadokeza kuwa ndipo pahali ambapo Fumo Liongo alitaka kufanya tambiko kuhifadhi nafsi yake ili kuokoa maisha yake. Ujumbe unaojitokeza ni kwamba, sehemu za visima zilichukuliwa kuwa mahali patakatifu palipotumiwa na wazee kwa ajili ya matambiko ili kupata suluhisho la matatizo yaliyowakabili wanajamii.

Kwa hivyo, sehemu hizi zilihifadhiwa kama mahali patakatifu kwa ajili ya shughuli hizo muhimu. Kinachodhihirika hapa ni kwamba, kukauka kwa visima vya jadi kuliweza kutatiza shughuli nyingi za kijamii. Hivyo, lilikuwa ni jambo muhimu kuhakikisha kuwa misitu ilihifadhiwa ili kuzuia kukauka kwa maji ya visima. Kama inavyodokezwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Glotfelty, 1996). Kwa msingi huu, waandishi wa tamthilia teule wanasisitiza kuwa utamaduni hasa wa kiafrika ulioambatana na matambiko unahusiana na ulimwengu halisi moja kwa moja. Hii ni kwa sababu tamaduni hizi zilikusudiwa kuhifadhi mazingira kwa kuchukulia sehemu zilizotumika kwa ajili ya shughuli hizo za kitamaduni kuwa mahali patakatifu. Hii ndio maana waandishi wa tamthilia hizo wanasawiri hali ambapo uasi wa tamaduni hizo

unasababisha majanga mengi katika jamii. Hivyo, uchanganuzi wa tamthilia teule umebaini kuwa, hali ya kurejelea fikra za kale ni muhimu katika uhifadhi wa mazingira, jambo ambalo wanasisitiza kupitia kazi zao.

### 6.4 Motifu ya Elimu

Uchanganuzi wa tamthilia teule umebaini kwamba, elimu kuhusu mazingira ni muhimu katika uhifadhi wa mazingira yaliyoharibiwa. Elimu iliyoangaziwa na waandishi hawa inaweza kuwasilishwa kwa jamii kupitia njia mbalimbali kama vile somo la mazingira katika mitaala ya elimu, vyombo vya habari, na elimu kwa umma.

#### 6.4.1 Somo la Mazingira katika Mitaala ya Elimu

Kujumuishwa kwa somo la mazingira katika mitaala ya elimu ni jambo lililosawiriwa na watunzi wa tamthilia teule kama njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira. Kupitia tamthilia ya *Janga la Werevu,* Mohamed anaangazia suala hili kupitia mhusika Busara kama ifuatavyo:

> Busara: *Lazima shuleni na vyuoni mwetu liwepo somo la mazingira linalojadili matatizo sugu yanayotokana na sisi watu tunaoharibu mahitaji ya maisha yetu*. Lazima tujifunze mambo yaliyo karibu na sisi kabla hatujajifunza yaliyo mbali na sisi. Lazima tupate elimu ya ujumla wa mambo. Si elimu ya kujazwa mawazo yaliyopitwa na wakati yanayotuzuia kudadisi. Tusiendelee kuifakamia mitaala ya mataifa mengine yanayojinaki *bora mimi* huku wao wakizidi kuzoa rasilimali zetu kupitia kwa makampuni yao ya kigeni. Nasi tumekaa tutwe tu, tukifisidi, tukidhulumu mazingira, tukilaumu wengine na kuibia umma hadharani. (Uk 32-33)

Ujumbe unaojitokeza katika mfano uliotolewa ni kwamba, mwandishi anaikosoa mitaala ya elimu ambayo imejikita katika mawazo yaliyopitwa na wakati, yanayozuia watu kudadisi mambo yanayotokea katika ulimwengu halisi. Kwa maoni yake, hii ni mitaala ya mataifa mengine inayosisitiza ubinafsi, na ambayo haina manufaa yoyote katika jamii husika. Kinachodhihirika hapa ni kwamba, mitaala ya elimu ya aina hii huwafanya watu kuwa watumwa kwa kufurahia mambo ya kigeni, huku wageni hao nao wakichukua nafasi hiyo kuzoa rasilimali za waafrika hasa kupitia makampuni yao ya kigeni. Kwa mujibu wa Thompson na Bendik (2012), urejesho wa ekolojia unahitaji maadili na elimu mpya ambazo pia huimarisha upatanisho miongoni mwa jumuiya

mbalimbali za watu na mataifa. Sababu ni kwamba, chanzo na athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga mengine ya kiekolojia yana misingi ya kibinafsi, kiushirika, kijamii na kilimwengu. Elimu hii mpya ambayo Thompson na Bendik (keshatajwa) wanayozungumzia ndiyo mwandishi wa *Janga la Werevu* anayorejelea kupitia mhusika Busara, anapopendekeza kuhusu haja ya kubadili mitaala ya elimu.

Aidha, viongozi wa kiafrika nao wanaiga mienendo hiyo ya wageni kwa kutekeleza kila aina ya maovu kama vile ufisadi, kudhulumu mazingira na kuibia umma. Kwa msingi huu, mwandishi wa *Janga la Werevu* anapendekeza mitaala ya elimu inayosisitiza elimu ya jumla ya mambo. Miongoni mwa masomo mengine muhimu ambayo lazima yajumuishwe katika mitaala ya elimu, ni somo la mazingira linalojadili matatizo sugu yanayotokana na wanajamii wenyewe wanaoharibu mahitaji ya maisha yao. Umuhimu wa kuhusisha somo la mazingira katika mitaala ya elimu unashadidiwa na Gachuru (2010) anayedai kwamba, kuhusisha somo la mazingira katika elimu huwa na athari chanya kwa wanafunzi kuhusu uhifadhi wa mazingira. Hivyo, ni dhahiri kwamba ufunzaji wa wanafunzi kuhusu masuala ya mazingira utawawezesha kuwa na uelewa wa chanzo na athari za uharibifu wa mazingira na jinsi ya kuchangia katika kuyahifadhi hayo mazingira. Ushahidi zaidi kuhusu manufaa ya somo la mazingira shuleni na vyuoni linajitokeza katika *Janga la Werevu* ambapo mhusika Kristy anaelezea wazazi wake kuhusu mijadala yao inayohusu hali ya mazingira katika chuo kikuu anakosomea. Katika mfano ufuatao, Kristy anasema:

> Kristy: Baba, baba, baba, mama, mama, mama, huu sasa ni mwezi wa sita maji hayapatikani chuoni kwetu. Yamekatika moja kwa moja. Yameyoyoma kabisa kabisa. Hayatoki tena mabombani. *Mjadala wetu chuoni unaelezea kuwa vianzo vya maji vimekauka. Na kisha tunatabiri kwamba litazuka balaa la watu kugombana na kupigana vita kwa nia ya kuhodhi peke yao maji ya taifa zima…*(Uk 31)

Kupitia maneno ya Kristy, ni dhahiri kwamba uhaba wa maji umeathiri hata wanafunzi katika shule na vyuo kwa muda mrefu. Maji hayatoki tena mabombani, jambo ambalo pia limezua mijadala yao kuhusu hali hiyo ya uhaba wa maji. Kutokana na mjadala wa wanafunzi katika chuo kikuu, sababu ya uhaba wa maji ni kuwa vyanzo vya maji vimekauka. Kwa kuwa hali ya uhaba wa maji imeathiri watu katika taifa nzima, wanafunzi hao wanatabiri kuwa huenda likazuka balaa la watu kugombana na kupigana

vita kwa sababu ya maji. Umuhimu wa kujumuishwa kwa somo la mazingira katika mtaala wa elimu unasisitizwa na Murikira (2019) anayeeleza kwamba somo la mazingira limejumuishwa katika Mtaala wa Kiumilisi wa Elimu (CBC) nchini Kenya. Ili kuonyesha uzito wa suala hili, somo la mazingira ni la lazima katika gredi ya kwanza hadi ya tatu, lengo lake kuu likiwa ni kuwapa wanafunzi maarifa ya kimsingi kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Jambo hili linaafikiana na maoni ya Mutahi (2021) anayedai kwamba suala la mazingira ni mojawapo ya masuala ibuka, ambalo linafaa kuangaziwa katika mtaala wa elimu, pakiwemo elimu katika shule za msingi.

Aidha, kuwepo na somo la mazingira katika mtaala wa elimu kunaambatana na malengo ya elimu shuleni nchini Kenya ambapo kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira, ni lengo la nane kati ya malengo manane ya kitaifa ya elimu (Ministry of Education, 2019). Kwa hivyo, imebainika kwamba kuwepo na somo la mazingira katika mtaala wa elimu ni jambo ambalo waandishi wa tamthilia teule wanapendekeza kiubunifu kama njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira.

### 6.4.2 Elimu kupitia Vyombo vya Habari

Uchanganuzi wa data katika tamthilia teule umebaini kuwa vyombo mbalimbali vya habari vina mchango muhimu katika uhifadhi wa mazingira. Vyombo hivi ni pamoja na redio, magazeti au majarida na runinga, ambavyo huwa na dhima ya kusihi, kuhimiza, kushauri, kutahadharisha na kukumbusha kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Katika *Janga la Werevu*, dhima ya magazeti katika uhifadhi wa mazingira inajitokeza kupitia dondoo lifuatalo:

> Bamkuu: Look! Tazama ukurasa wa tatu wa *gazeti la Mazingira… Wanasema watachukua ardhi, mashamba na viwanja vyetu vyote vya Msitu wa Uma bila ya fidia*. Kosa letu ni lipi lakini?
>
> Bimkuu: Kwani kuna kosa? Si basi tu. Eti wanasingizia kukatwa miti ndio chanzo cha kukauka maji! Wanasahau kwamba tulifyeka msitu kwa jasho letu na gharama zetu kwa maslahi ya nchi hii. Tukaanzisha mashamba makubwa ya chai, pareto na kahawa na kutoa ajira kwa wafanyakazi. Tukazalisha vyakula na mazao ya biashara. Kuna ubaya gani? (Uk 26)

Kinachojitokeza wazi katika dondoo hili ni unafiki na ubinafsi wa viongozi. Ni bayana kwamba Bamkuu na Bimkuu wamenyakua ardhi ya umma kwa masilahi ya kibinafsi. Aidha, unafiki wao unajitokeza wakati Bimkuu anapodai kuwa, wao walifyeka msitu kwa jasho na gharama yao kwa maslahi ya nchi yao. Hii ni kwa sababu walifanya hayo yote na kuanzisha mashamba makubwa ili kujitajirisha wenyewe pamoja na familia yao. Haya yanashadidiwa na Sangili (2015) anayedai kwamba, viongozi walio serikalini huchangia kwa kiwango kikubwa katika uharibifu wa mazingira hasa kupitia matendo yao ya kibinafsi. Hata hivyo, mchango wa vyombo vya habari unajitokeza kupitia gazeti la Mazingira, ambalo linaeleza kuhusu hali ya mazingira. Aidha, kupitia gazeti hilo, wanyakuzi wa ardhi ya umma wanashutumiwa na kutishiwa kuwa ardhi na viwanja vyote vya Msitu wa Umma vingechukuliwa bila fidia.

Hii ni hatua muhimu katika juhudi za kuokoa mazingira ambayo yameharibiwa kupitia ubinafsi na unafiki wa viongozi katika jamii. Kwa mujibu wa Buell (2005), msingi wa uraia wa kimazingira ni maadili ya kiekolojia, sera, na uharakati ambao unahusisha harakati za kimazingira, watafiti, waundaji wa sera na wadau wengine. Kama inavyobainika katika mfano uliotolewa, hatua ya kutwaa viwanja vya Misitu ya Umma bila fidia kwa wanyakuzi, inajumuisha wadau mbalimbali wa kimazingira ili kutekeleza jambo hilo, na hatimaye kuyaokoa mazingira. Kwa hivyo, ni muhimu wadau mbaimbali wa kitaifa na kimataifa wachukue hatua mwafaka ili kulinda mazingira yanayoendelea kuharibiwa kila uchao. Kando na magazeti katika kueleza mambo yanayohusiana na mazingira, mwandishi wa *Janga la Werevu* ameonyesha kuwa redio na runinga pia ni vyombo vya habari ambavyo vinaweza kutumika kuarifu umma kuhusu athari za uharibifu wa mazingira, kama njia ya kuwahamasisha kuhusu haja ya kuyahifadhi. Katika mfano ufuatao, Kristy anasema:

> Kristy: *Lakini hata kwenye redio kila siku habari za ukame tunazisikia. Na hata katika runinga tunajionea*. Ama ni ukame na watu, mimea na wanyama wanaoangamia kwa njaa na kiu, au mafuriko yanayofunika roho za watu na kila kitu chao. Au jinsi dunia inavyoharibiwa kwa moshi wa magari na madawa. Viwanda vinamwaga sumu mitoni, meli zinatumbukiza takataka baharini. Vadau vinatumiwa na wakubwa kumwaga uchafu maziwani. Kila kiumbe kinalilia maji, maji safi. Rasilimali ya maji imeleta cheche za moto duniani kote. Si mashariki ya kati si Uajemi si Afrika si Ulaya. Eti tunapalilia maendeleo! (Uk 31-32)

Katika mfano huu, mwandishi anaonyesha umuhimu wa redio na runinga kuhusu athari za uharibifu wa mazingira. Kutokana na habari kwenye redio na runinga, njaa na kiu zinazotokana na ukame ni dhahiri katika jamii, ambazo zimeathiri watu, wanyama na mimea. Aidha, uharibifu wa mazingira pia umesababisha mafuriko yanayoshuhudiwa katika sehemu mbalimbali duniani. Zaidi ya hayo, Kristy anaeleza kuhusu uchafuzi wa hewa unaosababishwa na moshi wa magari na madawa pamoja na uchafuzi wa maji unaosababishwa na umwagaji wa sumu mitoni kutoka kwenye viwanda, na meli kutumbukiza takataka baharini. Isitoshe, ni dhahiri kwamba kuna uhaba wa maji duniani kote, hasa kwa sababu ya uharibifu wa vyanzo vya maji. Haya yanaafikiana na matokeo ya utafiti wa Massey (2009) kwamba, matatizo ya kimazingira yanatokana na mahusiano baina ya binadamu na mazingira yake. Mahusiano hayo ndiyo mhusika Kristy anayowaeleza wazazi wake kama njia ya kuwafafanulia njia mbalimbali zinazochangia katika uharibifu wa mazingira pamoja na kuweka wazi athari zake. Hivyo, mwandishi amesawiri redio na runinga kama vyombo vya habari muhimu katika kueleza umma kuhusu athari na chanzo cha uharibifu wa mazingira. Ushahidi zaidi kuhusu mchango wa vyombo vya habari katika uhifadhi wa mazingira umeangaziwa na Arege katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*. Dondo lifuatalo linathibitisha:

> Jumbe: Eti mazingira… mazingira! Kwani hakuna Jambo la maana kuandikia? Waandishi siku hizi wamekosa ubunifu.
> Lulu: Kuna nini bwana? Kicheko hicho chote cha nini? Chatisha.
> Jumbe: *Ni haya magazeti*.
> Lulu: Yana nini magazeti?
> Jumbe: *Porojo yao nyingi. Eti mazingira yamo hatarini! Wanadai kuna chini ya asilimia kumi ya vegetation cover humu nchini!* Waliufanya lini utafiti hawa washenzi? Halafu la kuchekesha zaidi ni madai kuwa mabadiliko ya hali ya hewa duniani yataleta madhara makubwa duniani. Eti baadhi ya miji iliyo sehemu ya pwani itazama. Unawasikia washenzi hawa? Iwapo ukame unazidi, vipi maji yataongezeka kiasi cha kuzamisha miji? Wajinga ndio wa kudanganywa bwana. (Uk 78)

Dondoo lililonukuliwa linadhihirisha kwamba mazingira yamo hatarini ambapo inadaiwa kuwa, kuna chini ya asilimia kumi ya kifuniko cha uoto wa asili nchini. Aidha, inakisiwa kuwa mabadiliko ya hali ya anga huenda yakaleta madhara makubwa

duniani. Mojawapo ya madhara hayo ni mafuriko ambayo yanahofiwa kuwa yangezamisha miji. Kama anavyoeleza Ong`utte (2014), waandishi wa kazi za fasihi za kimazingira hulenga kuzindua, na kutabiri hali ya baadaye ya mazingira kwa jamii. Mfano uliotolewa unathibitisha madai haya ambapo mwandishi anatabiri kuwa mabadiliko ya tabianchi yatasababisha mafuriko, ikiwa watu hawatachukua tahadhari. Kadhalika, kutokana na dondoo hili, mwandishi anamsawiri mhusika Jumbe kama mwenye mapuuza, ambaye anawapuuza waandishi wa magazeti kwa madai kuwa wamekosa ubunifu hadi wakaamua kuandika mambo yanayohusu mazingira.

Kinachodhihirika hapa ni kwamba, vyombo vya habari kama vile magazeti yana nafasi muhimu katika kueleza umma kuhusu chanzo na madhara ya mabadiliko ya tabianchi. Hii ni njia mojawapo ya kuhamasisha umma kuhusu haja ya kuhifadhi mazingira ili kuepukana na madhara kama vile ukame na mafuriko. Hali hii inaweza kuthibitishwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia inayosisitiza kwamba, uhakiki wa kiekolojia unahusu uhamasishaji wa wanajamii kuhusu kubadilisha mielekeo na mienendo yao kuhusu mazingira (Culler, 2011).

Katiba ya Kenya (2010) inavipa vyombo vya utangazaji na vyombo vingine vya habari na vya kielektroniki uhuru wa kujiendeleza. Hii huwezekana kwa kuongozwa na taratibu za leseni ambazo zimeratibiwa kuhakikisha udhibiti wa mawimbi ya hewa na aina nyingine za usambazaji wa mawimbi, wala haviingiliwi na serikali, maslahi ya kisiasa au ya kibiashara. Kwa hivyo, vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuripoti taarifa zinazohusiana na masuala ya kijamii kama vile uhifadhi wa mazingira. Isitoshe, vyombo vya habari vina nguvu katika kuchambua na kutengeneza mustakabali wa taifa iwapo vitatumika vizuri badala ya kuwa chanzo cha matatizo na uchochezi, mambo ambayo yanaweza kulisambaratisha taifa. Kwa kutambua nafasi ya vyombo vya habari katika kuhamasisha wanajamii kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na namna ya kuyahifadhi, waandishi wa tamthilia teule wameangazia suala hili kwa lengo la kuonyesha kuwa vita dhidi ya uharibifu wa mazingira ni jukumu la kila mtu katika jamii.

### 6.4.3 Elimu kwa Umma

Suala la kuelimisha umma kuhusu uhifadhi wa mazingira limebainika kuwa muhimu ili kudhibiti madhara yanayotokana na uharibifu wa mazingira, ambayo yako dhahiri katika ulimwengu halisi. Haya yanaafikiana na mtazamo wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia kuwa, kazi za kimazingira zinahusu uhamasishaji wa wanajamii kuhusu kubadilisha mielekeo na mienendo yao kuhusu mazingira (Culler, 2011). Katika *Janga la Werevu*, mfano ufuatao unathibitisha:

> Busara: Kweli Kristy hili si suala la u-sisi sisi, ni suala la u-sisi wa ki-nchi na dunia nzima. Kwa ukaidi wetu tutamaliza haraka mahitaji yetu yam aji na mahitaji mengine ya maisha.
>
> Kristy: Hivyo ndivyo kila siku tunavyojadiliana sisi na walimu wetu, au sio dada Busara?
>
> Busara: *Ndivyo kabisa. Ndivyo inavyotakiwa. Matajiri na maskini, Watoto,vijana, na wazee lazima wafunzwe kuyaheshimu na kuyahifadhi mazingira.* (Uk 32)

Mfano uliotolewa unahusu mazungumzo kati ya Kristy na dadake Busara ambao kando na kuwa watoto wa Bamkubwa na Bimkubwa, viongozi wa jamii iliyoangaziwa, wao ni wanafunzi wa chuo kikuu. Wao wana mitazamo sawa kuhusu uhifadhi wa mazingira ambapo wanamweleza Bimkuu kuhusu haja ya kuacha ubinafsi na kujali maslahi ya jamii nzima. Kwa kufanya hivyo, kila mwanajamii atashiriki katika uhifadhi wa mazingira kwa manufaa ya jamii nzima. Kadhalika, Busara anahimiza kuwepo na mafunzo yanayosisitiza kuheshimu na kuhifadhi mazingira kwa kila mwanajamii bila kujali umri, cheo, jinsia au tabaka. Hii ndio maana Curry (2011) anaeleza kwamba, ulimwengu unahitaji elimu ya kiekolojia katika viwango vyote, ili maadili ya kimazingira yawekewe misingi katika mfumo wa chakula, mabadiliko ya tabianchi, majanga ya kimazingira na maendeleo endelevu. Manufaa ya kuwaelimisha wanajamii kuhusu uhifadhi wa mazingira pia umeangaziwa na Mohamed katika *Kimya Kimya Kimya* kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

> Bw. Naona: Naona sasa kundi linalojua na kutambua limekua, limejaa na kumiminika. Kila aina ya raia yumo humo. Wazee na vijana, wanawake na wanaume, wagonjwa na wazima, wa mjini, majijini na mashambani, waliosoma na wasiosoma, walimu, madaktari, wafanyabiashara, wakulima, mabingwa

> wa kilimo, wavuvi, mawakili, wanasheria na baadhi
> ya wanasiasa wa upinzani. (Uk 66-67)

Mfano uliotolewa unaangazia matokeo ya uhamasishaji wa umma kuhusu uhifadhi wa mazingira. Hivyo, ni wazi kwamba kila mwanajamii amepata mafunzo kuhusu haja ya kuyaheshimu na kuyahifadhi mazingira ili kuepuka athari za uharibifu wake. Kinachodhihirika hapa ni kwamba mafunzo ya kimazingira yanamhusu kila mwanajamii kwani matokeo ya uchafuzi wa mazingira yanaathiri kila mmoja wao vile vile. Mtazamo huu wa kuhamasisha na kuhusisha kila mwanajamii katika uhifadhi wa mazingira kama waandishi wa tamthilia teule wanavyosisitiza, unaafikiana na maoni ya Omollo (2013). Kutokana na maoni yake, ushirikishi wa umma katika uhifadhi wa mazingira kupitia kwa mwamko na elimu kuhusu mazingira huongeza uwezo wa umma kuheshimu sheria, maagizo na kanuni za uhifadhi wa mazingira. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa ushirikishwaji wa umma katika uhifadhi wa mazingira kupitia mafunzo kuhusu mazingira kutachangia kufikia malengo ya maendeleo endelevu kwa watu, sayari na ustawi.

### 6.5 Motifu ya Umoja

Suala la umoja katika kusuluhisha matatizo ya kimazingira ni jambo ambalo limeangaziwa kwa kina na watunzi wa tamthilia teule. Waandishi wa tamthilia hizo wameangazia hali ambapo umoja wa wananchi ni muhimu katika juhudi za kuhifadhi mazingira yaliyoharibika kutokana na vitendo vya kutojali vya viongozi wao. Kutokana na mitazamo ya waandishi, wananchi wanaweza kuungana na kushirikiana katika mambo mbalimbali yanayolenga kutoa suluhisho kwa mazingira yaliyoharibiwa. Hivyo, uchanganuzi wa tamthilia teule umebainisha hali ambapo wananchi wameshiriki katika maandamano, mijadala, uundaji wa sheria za mazingira na katika ufufuzi wa misitu.

#### 6.5.1 Kufanya Maandamano

Umoja wa wananchi katika utetezi wa mazingira umedhihirishwa na watunzi wa tamthilia teule kupitia maandamano. Maandamano hayo yalilenga kuwalazimisha viongozi kuwasikiliza na hatimaye kuyashughulikia masilahi yao. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Arege anaangazia hali ambapo wafanyakazi katika Jiji la Cheneo

wanaamua kufanya maandamano ya amani ili kumshurutisha Meya kuwasikiliza. Mfano ufuatao unathibitisha:

Sauti: Ndugu wafanyakazi wenzangu *tumefika hapa tukiwa kitu kimoja na umoja huu ndio nguzo yetu. Tushikamane hadi mwisho.* Mwisho wa madhila yanayotuzonga. Ndugu zangu katika vita hivi msisahau kuwa kwa muda sasa tumeonewa vya kutosha. Tumedhalilishwa vya kutosha…(Uk 57)

Katika mfano huu, kiongozi wa wafanyakazi anawahimiza wafanyakazi wenzake kudumisha umoja wao na kushikamana hadi watakapopata haki yao. Hivyo, wako tayari kuungana hadi watakapofika mwisho wa madhila yanayowazonga. Vilevile, anawakumbusha kuwa umoja wao ndio nguzo yao hasa katika vita dhidi ya dhuluma ya aina yoyote kutokana na viongozi. Hii ndiyo maana Carter (1999) anahimiza mbinu za kimahusiano katika kusuluhisha matatizo ya kimazingira hasa kwa kuwa watu binafsi huishi kwa ushirikiano na watu wengine pamoja na mazingira. Umoja huu ndio Arege anaosisitiza kama inavyodhihirika katika mfano uliotolewa. Katika *Majira ya Utasa,* mwandishi anasawiri umoja wa wananchi kama mojawapo ya njia za kusuluhisha matatizo ya jamii kama vile suala la uharibifu wa mazingira. Haya yanathibitika katika mfano ufuatao:

Hori: Nimesikia tayari wamebomoa ua uliozungushwa mlimani. Kufikia kesho wanataka kuwa kule shambani na kubomoa mabanda ya maua.
Kato: Ni nia nzuri lakini Jumbe atatuma askari kuja kufanya fujo.
Hori: Hilo la fujo hamna.
Kato: Litakuwapo. Nawaogopea watu wetu.
Hori: Hofu ya nini tena? *Tumeshikamana vya kutosha. Na mshikamano huo ndio ushindi wetu. Watu wanasema kwa kauli moja na wanatenda kama kundi moja.* Tayari Jumbe ameomba tuwatume watu wawili kwenda kushauriana naye.(Uk 68)

Dondoo hili linaangazia hali ambapo watu wamechoka kudhulumiwa na viongozi. Wanataka haki yao ya kurejeshewa ardhi ya umma iliyonyakuliwa na Jumbe akiwa na lengo la kujenga viwanda vya maua kwa manufaa ya kibinafsi. Kutokana na maneno ya Hori, ni wazi kwamba watu wameshikamana katika kusema na kutenda kwa kauli moja. Ni kutokana na umoja huu ambapo wanafanikiwa kubomoa ua uliozungushiwa mlima. Isitoshe, wana mpango wa kwenda shambani na kubomoa mabanda ya maua. Kwa mujibu wa Schartz (2012), uhakiki wa kiekolojia unahimiza matumizi ya siasa

zinazojishughulisha na uathiri wa sera ya umma na kufanya maamuzi muhimu kuhusu mazingira. Haya yatasaidia katika uundaji wa diskosi zinazolenga kupiga vita nguvu za serikali zinazosababisha uharibifu wa mazingira.

Mwandishi wa *Majira ya Utasa* anasawiri hali ambapo wanajamii wamekata shauri na kuchukua hatua ya kufanya maandamano huku wakibomoa mabanda ya maua ya Jumbe, kama njia ya kutumia nguvu kutetea haki yao. Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba, mwandishi anasisitiza kuhusu haja ya wanajamii wote kuungana ili kuokoa mazingira yaliyoharibiwa. Kwa upande wake, Mohamed katika *Kimya Kimya Kimya* anaangazia hali ambapo vijana wanafanya uamuzi wa kuungana na wazee ili kufaulu katika kuwaondoa viongozi dhalimu mamlakani. Dondoo lifuatalo linashadidia:

> Zanga: Sisi tuwe pamoja na umma kufanya nini?
> Mussa: Wewe vipi Zanga bwana? Unauliza jambo lililo wazi kabisa.
> Zanga: Yaani wewe umeshalijua siyo?
> Mussa: Naam, nimeshalijua kama jina langu, kama mchana wa mwangaza.
> Zanga: Liseme basi.
> Mussa: *Tujumuike nao kujifundisha kusema. Sisi vijana tuwafundishe wazee kusema. Ili tuseme pamoja. Tuseme kwa kauli moja.* (Uk 54)

Katika mazungumzo haya, Mussa anamshawishi nduguye Zanga kuhusu haja ya wao kama vijana kuungana na wazee ili kusema kwa kauli moja kuhusu madhila yanayowakumba wanajamii. Kinachodhihirika ni kwamba wazee wamekuwa wamenyamaza kimya kwa muda mrefu. Hivyo, vijana wametambua kuwa kuwafundisha wazee kuhusu manufaa ya kusema ili wote waseme kwa kauli moja kutawafaa katika vita dhidi ya uongozi dhalimu wa Bw. Binafsi. Kama inavyoelezwa na Mussa, huko kusema kunarejelea kuandama pamoja hadi kwa kiongozi wao Bw. Binafsi na kumweleza kuhusu matatizo yanayowakabili kama wanajamii.

Hatua ya vijana ya kuungana na wazee katika utetezi wa haki yao unashabihiana na matokeo ya utafiti wa Bulaya na Mhango (2020) waliobaini kuwa, mapambano dhidi ya uchafuzi wa mazingira yanapaswa kujumuisha kila mwanajamii bila kujali umri, jinsia, elimu au tabaka. Kama inavyodhihirishwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, kazi za kimazingira lazima zionyeshe njia mbadala za kuepusha jamii kutokana na

athari za uharibifu wa mazingira (Barry, 2013). Kwa msingi huu, watunzi wa tamthilia teule wameonyesha kuwa umoja wa wananchi ni njia mbadala ambayo inaweza kutumiwa katika kukabiliana na watu wanaochangia katika uharibifu wa mazingira, na kuungana pamoja katika kuyahifadhi mazingira hayo. Kwa kufanya hivyo, watunzi hawa wameonyesha kuwa hatimaye kunakuwa na mafanikio katika kurejesha mazingira katika hali yake ya awali.

### 6.5.2 Uundaji wa Sheria za Mazingira

Uchanganuzi wa tamthilia teule umebaini kwamba, uundaji wa sheria zinazolinda mazingira ni njia mwafaka ya kuzuia uharibifu wake. Arege anaangazia haya katika *Mstahiki Meya* kupitia dondoo lifuatalo:

> Waridi: Chakula gani hicho hasa ulichochukua kumpa mtoto?
> Mama: Wali na maharage yalolala.
> Siki: Wewe hukuyala?
> Mama: Sikuyala mie. Yalikuwa machache tu!
> Waridi: Wala hukukitokosa chakula hicho tena nyumbani?
> Mama: Moto utatoka wapi mwanangu? *Makaa siku hizi yamepanda bei tangu sheria ya misitu ishike kasi.* Nayo bei ya mafuta taa ndiyo hiyo inapanda kila uchao. (Uk 4-5)

Mazungumzo haya yanaendelezwa zahanatini baina ya Waridi ambaye ni nesi na mama mwenye mtoto aliyeugua tumbo kutokana na kula chakula kibovu. Taswira inayojitokeza hapa ni kwamba, watu katika jamii iliyoangaziwa na mwandishi wamekuwa wakitumia makaa katika upishi wao kwa muda mrefu. Hata hivyo, imebainika kwamba matumizi ya makaa yamepungua hasa kutokana na bei yake kupanda, jambo ambalo limewafanya baadhi ya wanajamii kushindwa kuimudu. Vilevile, imebainika kwamba kupanda kwa bei ya makaa kumetokana na hali ya kushika kasi kwa sheria ya misitu. Kama inavyoelezwa na Buell (1996), uraia wa kimazingira unajumuisha maadili ya kiekolojia na sera zinazohusisha harakati za kimazingira, watafiti, waundaji sera na wadau wengine. Hii ni kwa sababu kila mwanajamii ameathirika kutokana na uharibifu wa mazingira. Hivyo, mwandishi wa *Mstahiki Meya* ameangazia hali ambapo waundaji sera na sheria za mazingira pia nao wamejihusisha katika uhifadhi wa mazingira, kwa kudhibiti matendo ya wanajamii ambayo yanachangia katika kuyaharibu. Kwa hivyo, ni wazi kwamba sheria ya misitu imefaulu kudhibiti uharibifu wa misitu kupitia uchomaji wa makaa. Katika tamthilia ya

*Kimya Kimya Kimya*, Mohamed anaonyesha kuwa kuna haja ya kupitia upya sheria za nchi iwapo sheria zilizopo hazisaidii katika kushughulikia masilahi ya wananchi ipasavyo. Katika mfano ufuatao, Mpya anasema:

> Sauti ya Mpya: Muhimu kabisa katika yote, *kwanza ni kuipitia upya katiba yetu kwa mujibu wa matakwa ya sasa ya nchi yetu na matakwa ya kitaifa*. Pili, tutasimama kidete tudai kugeuza mwenendo wetu wa kutojali maslahi yetu ya kitaifa na kudhamini au kusaidia kupatikana kwa maslahi ya nchi na mataifa mengine…(Uk 73)

Kupitia mhusika Mpya, mwandishi anapendekeza kuhusu kuungana kwa wananchi katika marekebisho ya katiba. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa katiba iliyopo inaafiki matakwa yaliyopo ya wanajamii na nchi yao pamoja na matakwa ya kitaifa. Kando na kubadilisha katiba, Mpya anahimiza watu kusimama kidete kudai kugeuza mwenendo wao wa kutojali maslahi ya taifa lao huku wakidhamini maslahi ya mataifa mengine. Kwa kufanya hivyo, watakuwa na uwezo wa kushughulikia matatizo yanayowakabili kwanza kabla ya kujali ya wengine. Ili kufanikisha uhifadhi wa mazingira, Garrard (2004) anasisitiza kwamba, ni lazima watu waanze kufikiria kwa namna tofauti kuhusu mawazo, miili na utambulisho wao kwa sababu ya majanga ya kimazingira. Mageuzi haya ya namna ya kufikiria na kujitambulisha na mazingira ndiyo mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* anayosawiri katika mfano uliotolewa kupitia mhusika Mpya. Hapa, mwandishi anarejelea suala la utandawazi ambapo mataifa makubwa ndiyo yanang`ang`ania ustahiki wa kutetea na hatimaye kupata maslahi yao, ama ya kiuchumi au ya kijeshi na usalama au ya kiutamaduni.

Maoni ya waandishi wa tamthilia teule kuhusu umuhimu wa kuwepo na sheria za mazingira kama njia ya kuyahifadhi mazingira, kunaafikia na hatua ya kuundwa kwa NEMA nchini Kenya. Hii ni taasisi ya kitaifa iliyoanzishwa mwaka 2002 kwa lengo la kusimamia na kuratibu shughuli za mazingira pamoja na kutumika kama chombo kikuu cha kitaifa cha kutekeleza sera za mazingira katika sekta zote nchini. Aidha, sura ya tano katika katiba ya Kenya (2010) inahusu ardhi na mazingira ambayo inasisitizwa kwamba, serikali itaondoa michakato na shughuli zozote ambazo zinaweza kuhatarisha mazingira. Kadhalika, serikali ya Kenya kupitia taasisi ya NEMA ilibuni sheria mbalimbali kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira. Miongoni mwa sheria hizo

ni sheria ya kudhibiti ubora wa hewa ya mwaka wa 2015. Lengo la udhibiti huu ni kuzuia, kudhibiti na kupunguza uchafuzi wa hewa kutoka kwenye magari na viwanda. Zaidi ya hayo, hatua ya kupigwa marufuku kwa mifuko ya plastiki na shirika la NEMA nchini Kenya mwaka wa 2017 ilikuwa juhudi za serikali ya Kenya kupambana na uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba sheria za mazingira ni hatua mwafaka katika uhifadhi wa mazingira, kama inavyodokezwa na waandishi wa tamthilia teule.

### 6.5.3 Mijadala kuhusu Mazingira

Athari za mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la joto duniani zimekuwa dhahiri katika ulimwengu wa sasa, jambo ambalo limeibua mijadala kupitia makongamano ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kutafuta njia mbadala za kukomboa mazingira yaliyoharibiwa (Sangili, 2015). Watunzi wa tamthilia teule nao wameangazia hali ambapo athari za uharibifu wa mazingira zimeathiri wanajamii hadi wakaanza kutafuta njia za kuokoa wanajamii kutokana na majanga yanayowakabili. Mojawapo ya njia hizo ni kuandaliwa kwa mikutano katika jamii ili kujadiliana kuhusu hali inayowakabili, kwa lengo la kutafuta suluhisho. Katika *Janga la Werevu*, wito wa majadiliano kuhusu suala la mazingira linajitokeza kupitia Daktari wa Akili kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

> Daktari wa akili: Enhe, ewa! *Bora na wewe ushiriki katika majadiliano, maana hili si tatizo la mtu mmoja wala si tatizo la taifa moja.* Hata nyinyi mnastahiki kushiriki katika mjadala huu. *Dunia nzima lazima ishiriki… Leo maafa ya pahala Pamoja ni maafa ya pahala pengine*. Uchafuzi wa viwanda. Unajisi wa mazingira. Usafirishaji wa madawa ya sumu yanayokuja kumwagwa mbali na yanakotoka, haya si rahisikuzuilika siku hizi… (Uk 52)

Katika dondoo hili, Daktari wa akili anasisitiza kuwa, pana haja ya kila mwanajamii kushiriki katika majadiliano kuhusu athari za uharibifu wa mazingira. Hii ni kwa sababu matatizo ya kimazingira si tatizo la mtu mmoja wala taifa moja, bali ni tatizo la ulimwengu kwa jumla. Hivyo, anahimiza dunia nzima kushiriki katika mjadala huo kwa kuwa uharibifu wa mazingira si rahisi kuzuilika ikiwa ulimwengu mzima hautashiriki. Kutokana na matatizo ya kimazingira yaliyo na athari katika kila pembe

ya dunia, Buell (2005) anadokeza kuwa, juhudi za uhifadhi wa mazingira zinafaa kujumuisha binadamu wote pamoja na mashirika yasiyo ya kibinadamu. Kwa maoni yake, haya yanaweza kutimia kwa kwenda zaidi ya mawanda ya kitaaluma katika kuchunguza fasihi na mazingira. Kwa hivyo, hakuna taaluma, taifa, kabila, wakala au mtu binafsi ambaye anamiliki masuala ya kimazingira. Kwa kurejelea wazo hili, mwandishi wa *Janga la Werevu* anahimiza kila mtu kote ulimwenguni kushiriki katika mijadala inayohusu matatizo ya kimazingira.

Mwandishi wa *Majira ya Utasa* naye ameangazia hali ambapo wawakilishi wa Kijiji wanaitisha kikao ili kujadiliana kuhusu namna ya kusuluhisha matatizo yanayowakabili likiwemo tatizo la njaa iliyosababishwa na kiangazi cha muda mrefu. Majadiliano hayo yanadhihirika katika dondoo lifuatalo:

> Kato: Wanakijiji wenzangu mliofika hapa, leo tunakutana wakati wa hali ngumu inayowakabili watu wetu.
> Dosho: Kweli kabisa.
> Mebo: Hali ngumu hii.
> Kato: Sina haja kuielezea hapa maana kila mmoja wetu anaielewa vizuri. Tusipochukua tahadhari upesi yatakuwa hayasemeki tena. Wenye kusali, wamesali. Vivyo hivyo wenye kuswali. Bado hakuna dalili zozote. Lazima tuitafute suluhu. Nilipokutumieni habari za kikao hiki, niliwataka pia kufikiria kuhusu nini tufanye. Hatuwezi kungoja mauti yaje yatuzoe huku twaona… (Uk 40).

Kinachodhihirika hapa ni kwamba, watu wa jamii iliyosawiriwa wamekabiliwa na hali ngumu za kimaisha. Kutokana na hali hiyo, wawakilishi wa vijiji wameitisha kikao ili kujadiliana kuhusu hali hiyo. Kama anavyoeleza Kato, lengo la kikao hicho ni kuchukua tahadhari upesi hasa kwa kutafuta suluhu la matatizo hayo. Aidha, Kato anawataka wawakilishi hao kufikiria kuhusu jambo la kufanywa ili kuokoa maisha ya watu wao, pasi kukata tamaa. Kilicho wazi ni kwamba watu wote wanaelewa kuwa kiongozi Jumbe pamoja na marafiki wake wa karibu ndio wamesababisha tatizo la ukame. Hii ndio sababu ya watu kukutana ili kujadiliana jinsi ambavyo wanaweza kuwakabili. Vitendo vya binadamu ambavyo vimekuwa vikisababisha uharibifu wa mazingira vimeangaziwa na Bookchin (1980) anayedai kwamba, maangamizi ya dunia yanatokea kwa sababu ya vitendo vya binadamu. Tendo la ukataji wa miti na kuharibu

vyanzo vya maji ni miongoni mwa vitendo vya Jumbe ambavyo vimechangia katika uharibifu wa mazingira.

Haja ya kuandaa vikao vya majadiliano kuhusu masuala ya mazingira kama ilivyosawiriwa na waandishi wa tamthilia teule inashabihiana na maandalizi ya makongamano ya Umoja wa Mataifa ambayo hulenga kujadili kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Kongamano la 1972 mjini Stockholm ndilo lilikuwa la kwanza kujadili masuala ya mazingira ya binadamu. Aidha, ndilo lilipelekea kuanzishwa kwa UNEP na kuchagua Juni 5 kila mwaka kuwa siku ya mazingira duniani (Istvan, 2021). Kutokana na tishio la athari za mabadiliko ya tabianchi, Umoja wa Mataifa uliandaa kongamano mjini Rio de Janeiro mwaka 1992 lililoitwa `Kongamano la Sayari Duniani, ambapo mkataba wa mwongozo wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi (UNFCCC) ulipitishwa. Aidha, tangu mwaka 1994, ambapo mkataba huo ulianza kutekelezwa, Umoja wa Mataifa umekuwa ukizileta karibu nchi zote duniani kuhudhuria mikutano kuhusu tabianchi kila mwaka.

Kadhalika, awamu ya 26 ya Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, maarufu kama COP26 ilifanyika jijini Glasgow, Scotland ambalo liliwaleta viongozi wa ulimwengu pamoja katika juhudi za kutafuta suluhisho la kudumu dhidi ya athari hasi za mabadiliko ya tabianchi (Wangari, 2021). Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa waandishi wa tamthilia teule wanasisitiza kuwepo na makongomano ya kitaifa na kimataifa yanayolenga kujadili matatizo yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi, kama njia mbadala ya kutafuta suluhisho la matatizo hayo.

### 6.5.4 Kufufua Misitu

Mbinu nyingine ya uhifadhi wa mazingira ambayo imeangaziwa na watunzi wa tamthilia teule ni ufufuzi wa misitu**.** Katika *Janga la Werevu*, mwandishi ameeleza haya kiubunifu kupitia Mganguzi ambaye anatoa suluhisho la ugonjwa wa Kristy. Anapoeleza namna ya kupata maji matakatifu kutoka katika kisima cha umma ambayo ndiyo tiba ya ugonjwa wa Kristy, Mganguzi anasema:

Mganguzi: *Irejesheni misitu ya wananchi katika hali iliyokuwa*. Ndiyo,tutahitaji muda mrefu na fedha nyingi mpaka irudi na kutengenea tena. Lakini wahenga wamesema,

> kawia ufike. *Lazima tuifufue misitu yote ya wananchi na vyanzo vyake vya maji.* Na kabla ya hapo lazima muwaruhusu wananchi wachote maji kwenye visima mnavyoviita vyenu, kwani ni vyao si vyenu. Tangu lini vitu vyao vikawa vyenu? (Uk 65).

Kwa mujibu wa dondoo hili, Mganguzi anahimiza hatua ya wananchi kuungana pamoja katika ufufuzi wa misitu yote ya wananchi pamoja na vyanzo vyake vya maji ili kupata maji kwenye chemichemi za maji za umma. Kwa maoni yake, hii ndiyo njia ya pekee ya kupata maji matakatifu ambayo yalikuwa tiba ya ugonjwa wa Kristy. Ugonjwa wa Kristy unaweza kutafsiriwa kama jazanda ya majanga yanayowakabili watu kote duniani kutokana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na ongezeko la viwango vya joto duniani kama vile tatizo la ukame.

Hata ingawa Mganguzi anahimiza ufufuaji wa misitu, anaonya kwamba hatua hiyo ingechukua muda mrefu na kuhitaji fedha nyingi  mpaka misitu irudi katika hali yake ya awali. Kwa mujibu wa Quick (2004), mahitaji ya mazingira kwa jumla yanapaswa kutambuliwa na kutiliwa maanani na kwa umakini sawa na shughuli nyinginezo muhimu za kijamii kama vile siasa na uchumi. Kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, mwandishi wa *Janga la Werevu* anasisitiza kuwa ni lazima ufufuzi wa misitu utiliwe maanani, licha ya kuwa shughuli hiyo ingechukua muda na kugharimu pesa nyingi. Ndiposa Mganguzi anasema kuwa lazima viongozi waache ubinafsi kwa kutumia rasilimali ya umma kwa manufaa ya kibinafsi. Kwa kufanya hivyo, wananchi watafaidi kutokana na maji machache yanayopatikana kabla ya kuafikia urejeshi wa misitu katika hali yake ya awali.

Serikali za nchi mbalimbali kote duniani zinatambua manufaa ya kufufua misitu kama njia mojawapo ya kukomboa mazingira yaliyoharibiwa. Mnamo Julai 2019, Ethiopia ilivunja rekodi ambayo ilikuwa imeshikiliwa na India baada ya kupanda miti milioni hamsini mnamo 2016, kwa kupanda miti milioni 350 katika kipindi cha masaa kumi na mawili. Aidha, Kenya imekuwa ikilenga kupanda miti bilioni mbili kufikia mwaka 2022, kwa lengo la kuongeza maeneo yenye misitu kutoka asilimia saba hadi asilimia kumi. (Onyango, 2019). Isitoshe, hatua ya serikali ya Kenya ya kuwafurusha watu ambao waliishi kwenye msitu wa Mau kinyume cha sheria, ililenga kuchukua hekari elfu ishirini na tatu kwa minajili ya upanzi wa miti. (Mogambi, 2018). Hizi zilikuwa

juhudi za serikali ya Kenya za kufufua msitu huo ambao kwa miaka mingi, umekuwa chemchemi ya maji na nguzo muhimu kwa taifa la Kenya, hasa kwa kuwa watu wengi pamoja na wanyamapori wa kila aina hutegemea mito ambayo inatokana na msitu huu. Hata hivyo, kwa muda mrefu hatua hii imekuwa na utata kwa sababu ya tofauti za kisiasa kwa misingi ya kikabila.

Jitihada katika ufufuzi wa misitu kama njia ya kuhifadhi mazingira kama inavyoangaziwa na Mohamed katika *Janga la Werevu*, inaafikiana na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia kwamba, kazi za kimazingira lazima zionyeshe njia mbadala za kuponya jamii kutokana na athari za uharibifu wa mazingira (Buell, 2005). Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba mwandishi huyu amefaulu kuhamasisha na kuzindua utambuzi wa jinsi ya kuhifadhi mazingira kupitia upanzi wa miti ili kufufua misitu, ambayo ndiyo chemichemi ya vyanzo vya maji.

### 6.6 Motifu ya Uzalendo

Uzalendo ni hali ya mtu kuwa tayari kuifia nchi yake (TUKI, 2013). Suala la uzalendo limeangaziwa kwa mapana na marefu katika tamthilia teule. Waandishi wa tamthilia hizo wamesawiri baadhi ya wahusika hasa wanawake kama watu ambao wanaweza kufanya kila wawezalo ili kuokoa maisha ya wanajamii wenzao. Hivyo, wanawake mbalimbali wamejitokeza ili kutetea mazingira yaliyoharibiwa kupitia ubinafsi wa viongozi wao. Wanawake hawa ni pamoja na Busara na Kristy, Mpya na Bi Subira na Lulu.

#### 6.6.1 Busara na Kristy

Katika *Janga la Werevu*, wahusika Busara na Kristy ni wasichana walio katika chuo kikuu. Mwandishi wa tamthilia hii amewatumia wahusika hawa kuzindua utambuzi wa jamii iliyosawiriwa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na suala la mazingira kwa jumla.Tamthilia hii imeangazia hali ambapo vitendo vya viongozi vimesababisha uhaba wa maji kwa kuharibu vyanzo vya maji kupitia uharibifu wa misitu kwa manufaa ya kibinafsi. Hata hivyo, inaelekea kuwa wazazi wa Busara na Kristy ambao ndio wamesababisha uhaba huu wa maji hawatambui athari za vitendo vyao. Ndiposa Busara na Kristy wanachukua nafasi hiyo kuwaeleza kama ifuatavyo:

Bimkuu: Lakini sisi tunayo maji ya kutosha. Tuna yetu chemchemi ya kisima.
Kristy: *Mama, sasa umefika wakati wa kuacha u-sisi. Ni wakati wa kusisitiza u-kila-mtu.*
Busara: *Kweli Kristy hili si suala la u-sisi sisi, ni suala la u-sisi wa ki- nchi na dunia nzima*. Kwa ukaidi wetu tutamaliza haraka mahitaji yetu ya maji na mahitaji mengine ya maisha. (Uk 32)

Ujumbe unaojitokeza katika dondoo hili ni kwamba, Busara na Kristy wanahimiza kuasi ubinafsi na kusisitiza hali ya kujali kila mtu katika dunia nzima. Hii ni kwa sababu hatua ya ukataji misitu ambayo inaharibu chemchemi za maji inanufaisha watu wachache tu huku wao wakiwanyima watu wengine haki ya kufaidi rasilimali ya maji. Hivi ni miongoni mwa vitendo vya kibepari ambavyo Bennett (2001) anavyorejelea anaposema kwamba, uhakiki wa kiekolojia hujikita katika kushughulikia jamii ambayo imeharibika kutokana na shughuli za kibepari. Hizi ni shughuli za kiuchumi ambazo hunufaisha watu wachache katika jamii. Aidha, ubinafsi wa Bimkuu unadhihirika wazi anapodai kwamba, katika familia yake kuna maji ya kutosha, hasa kwa sababu wao wana uwezo wa kuchimba kisima cha maji kisichokauka. Bimkuu anawakilisha watu wachache wabinafsi katika jamii wasiojali maslahi ya watu wengine. Hivyo, Busara na Kristy wanatambua athari za vitendo vya kibinafsi hasa vile vinavyochangia katika kuharibu chemchemi za maji, na kuchukua hatua ya kuwazindua wazazi wao kutambua athari za vitendo vyao. Kwa kufanya hivyo, wanatetea watu walio wengi katika jamii ambao wananyimwa haki ya kufaidika kutokana na rasilimali ya umma.

### 6.6.2 Mpya na Bi Subira

Ushahidi zaidi wa mchango wa wanawake wazalendo katika uhifadhi wa mazingira umeangaziwa na Mohamed katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*. Katika tamthilia hii, mwandishi ameangazia hali ambapo watu wamepitia madhila mengi yanayosababishwa na kiongozi wao Bw. Binafasi. Licha ya kuwa watu wanatambua hivyo, wamekaa kimya kwa muda mrefu hasa kwa sababu hawana uhuru wa kusema waziwazi kuhusu matatizo yao. Hata hivyo, hali inabadilika wakati Mpya anapozaliwa. Mhusika huyu ni binti ya kiongozi Bw. Binafsi ambaye analeta mwamko mpya katika jamii yake kwa kumkosoa babake kuhusiana na ubinafsi. Zaidi ya hayo, anaanzisha harakati za mapinduzi kwa kuwahamasisha na kuchochea umma kuhusu haja ya kutetea

haki yao. Katika kuhamasisha umma kuhusu haja ya kufanya mapinduzi, Mpya anasema:

Sauti ya Mpya: Sisi wananchi tumeamua kwamba *kesho tukutanike tena kulalamika na kutetea haki zetu. Hatutaki fujo lakini. Tutasimama Pamoja kuweka waziwazi kero zetu, maana tunaona hatusikilizwi*. Sisi hatutaki fujo. Hatutaki fujo. Ingawa fujo zinaandaliwa upande mwingine ili tuambiwe sisi wapenda fujo. *Twakuombeni wananchi wenzangu tusimame na mabango yetu na kauli zetu ziwe ndio silaha zetu*…(Uk 72)

Katika mfano uliotolewa, Mpya anawahimiza wananchi wote kukusanyika kwa ajili ya kufanya maandamano. Aidha, anasisitiza kuwepo na maandamano ya amani bila fujo yoyote huku kauli zao zinazohusu masilahi yao zikiwa ndizo silaha zao. Kinachodhihirika hapa ni kwamba, wananchi wameamua kuungana pamoja kufanya maandamano ya amani kwa minajili ya kuweka wazi kero zao kwa kuwa wameona kwamba kiongozi hawajali wala kuyasikiliza malalamishi yao. Kwa hivyo, Mpya amesawiriwa kama mwanamke jasiri ambaye amejitolea kuongoza umma katika utetezi wa haki zao. Kando na mhusika Mpya, mwandishi wa *Kimya Kimya Kimya* amemsawiri mhusika Bi. Subira kama mwanamke shupavu na jasiri ambaye amesimama kidete kuhamasisha umma dhidi ya dhuluma kutokana na kiongozi wao. Aidha, anasisitiza haja ya kusema waziwazi ili kuweza kujikomboa kama ifuatavyo:

Bi. Subira: Mchakato ndio huu uliotuleta hapa. *Huwezi kujikomboa kama husemi. Lazima useme*. Siku hizi hapa petu watu wanafanya wapendavyo. *Miti inakatwa ovyo. Watu wanajenga nyumba au makazi bila ya vibali. Ardhi na viwanja vya watu vinachukuliwa kwa nguvu. Watu wanachafua mazingira katika kila eneo. Uchafu umejaa. Uchafu wa kila aina*. Makazi yetu machafu. Vijiji vyetu vichafu… Hisia za nchi zimepotea. Uzalendo umefifia. Tumekuwa wajinga kiasi cha kwamba tunauza nchi zetu kwa bei rahisi kabisa. Wajinga wa kukubali kuporwa raslimali zetu. ubinafsi ndio unaotutia ujinga (Uk 59)

Dondoo hili limeangazia jinsi Bi. Subira alivyo mwanamke shupavu. Kutokana na jinsi anavyoeleza umma kuhusu chanzo cha matatizo yao, ni wazi kwamba yeye ana maarifa

kuhusiana na umuhimu wa utunzani wa mazingira ili kuepuka madhara yanayotokana na uharibifu wake. Hivyo, anafichua maovu yanayofanywa na viongozi wao pakiwemo ukataji ovyo wa miti, ujenzi wa nyumba bila vibali, unyakuzi wa ardhi na uchafuzi wa mazingira. Kando na kuvikashifu vitendo vya viongozi vinavyoangamiza wananchi, Bi Subira pia anawalaumu wananchi wenzake kwa kuwa wajinga kiasi cha kukubali kuporwa rasilimali zao pasi kulalamika.

Wahusika Mpya na Bi Subira ni miongoni mwa wanawake ambao wamesimama kidete ili kupigania ukombozi wa mazingira ambayo athari za uharibifu wake ni dhahiri katika ulimwengu halisi. Usawiri wa wahusika hawa katika utetezi wa mazingira unashabihiana na utafiti wa Sabula (2014) kuhusu changamoto ambazo mwanamke alipitia katika kuhifadhi mazingira. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kwamba, mwanamke anayo nafasi kubwa katika uhifadhi wa mazingira hasa kwa kuhimiza jamii kubadili tabia na mielekeo yao kuhusu mazingira. Hivyo, mfano uliotolewa unadhihirisha kwamba, wahusika Mpya na Bi Subira wamefaulu katika kuhamasisha jamii kuhusu haja ya kutetea maslahi yao pakiwemo mazingira yaliyoharibiwa.

### 6.6.3 Lulu

Mchango wa mwanamke mzalendo katika utetezi wa mazingira pia umeangaziwa na Arege katika *Majira ya Utasa*. Haya yanajitokeza kupitia mhusika Lulu ambaye ni mke wa kiongozi Jumbe. Katika tamthilia hii, Lulu anajitokeza kama mkufunzi wa masuala ya kimazingira kwa mumewe ambaye anaonekana kuwa hatambui uhusiano uliopo kati ya ongezeko la joto duniani na mafuriko. Dondoo lifuatalo linashadidia:

> Jumbe: Unawasikia washenzi hawa? *Iwap ukame unazidi, vipi maji yataongezeka kiasi cha kuzamisha miji?* Wajinga ndio wa kudanganywa bwana.
> Lulu: Si uongo. *Sehemu za huko Arctic zenye theluji nyingi ajabu zimeanza kupoteza kiasi kikubwa cha theluji yake kutokana na global warming…*
> Jumbe: Arctic si maeneo ya huko Uzunguni?
> Lulu: Ni huko huko.
> Jumbe: Hayo yanatuhusu vipi?
> Lulu: Yanatuhusu kiasi chake. *Muyeyuko wa theluji utaleta ongezeko la maji baharini na hiyo hatari kwa wakazi wa pwani maana maji yatapasua kingo zake za kawaida na kuvuka nchi kavu.*
> Jumbe: Hizo ni porojo za wazungu. Ya kwao hayatuhusu Sisi.

| | |
|---|---|
| Lulu: | Si hivyo. |
| Jumbe: | Haya tuambie basi mtaalamu wetu. |
| Lulu: | Hata si suala la utaalamu. Ni suala la kila mmoja wetu kutoa mchango wake kuokoa mazingira. (Uk 79) |

Kutokana na ujumbe ulio katika dondoo hili, ni dhahiri kwamba mwandishi amemsawiri Lulu kama mwanamke aliye na maarifa ya masuala ya mazingira. Kutokana na maarifa haya, anamweleza mumewe Jumbe kuhusu uhusiano uliopo baina ya ukame na kuongezeka kwa maji kiasi cha kuzamisha miji. Hivyo, anamweleza kuwa kutokana na ongezeko la joto duniani, sehemu za *Arctic* zenye theluji nyingi zimeanza kupoteza kiasi kikubwa cha theluji yake. Aidha, Lulu anamfafanulia Jumbe kuwa muyeyuko huo wa theluji utasababisha kuongezeka kwa maji baharini, jambo ambalo ni hatari kwa wakazi wa pwani. Kama anavyoeleza Alia (2017), uhakiki wa kiekolojia unajihusisha na masuala ya sasa na jinsi yanavyohusiana na kuathiriana. Mahusiano haya ndiyo mhusika Lulu anayomweleza Jumbe ili aelewe jinsi ambavyo vitendo vyake, licha ya kuwa ni kwa njia isiyo ya moja kwa moja, vinaweza kuathiri jamii na ulimwengu kwa jumla. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba mwandishi amemtumia mhusika Lulu ili kuhamasisha jamii kuhusu haja ya kila mmoja katika dunia nzima kutoa mchango wake ili kuokoa mazingira.

Maarifa ya masuala ya mazingira pamoja na wito wa ukombozi wa mazingira unaotokana na wanawake walioangaziwa katika tamthilia teule, unashabihiana na wito wa Wangari Maathai wa kuboresha mazingira kupitia upanzi wa miti. Kando na hayo, Wangari Maathai ambaye alikuwa mwanaharakati wa mazingira aliibua wazo la kuanzisha shirika la `Greenbelt Movement` mnamo wa mwaka wa 1977 (Maathai, 2009). Lengo kuu la shirika hili lilikuwa kuwashirikisha wanawake wa vijiji katika uboreshaji wa mazingira kwa kupanda miti. Kwa kufanya hivyo, wanawake hawa walichangia katika upunguzaji wa taratibu za ukataji miti na kuenea kwa jangwa. Kwa hivyo, imebainika kuwa waandishi wa tamthilia teule wamewatumia wanawake wazalendo katika kazi zao kimakusudi ili kuibua mchango wao muhimu katika ukombozi wa mazingira, kutokana na uharibifu unaotekelezwa na vitendo mbalimbali vya binadamu.

### 6.7 Motifu ya Mapinduzi

Uchanganuzi wa tamthilia teule umebaini kuwa, iwapo njia nyinginezo za kukomesha uongozi dhalimu hazijafaulu, wananchi hawana budi kufanya mapinduzi ili kuwaondoa viongozi hao dhalimu mamlakani. Njia hizo ni kama vile kuitisha vikao vya mazungumzo na viongozi hao pamoja na kufanya maandamano ya amani. Watunzi wa tamthilia hizi wameangazia suala hili kwa namna mbalimbali hasa kupitia wahusika wa kimapinduzi ambao wanaanzisha harakati za kuzindua jamii kuhusu matatizo wanayopitia chini ya viongozi wa aina hiyo. Hivyo ujitokezaji wa suala la mapinduzi katika kila tamthilia teule kama njia ya kutetea masilahi ya jamii, ni dhihirisho la uzito wa hatua hii katika uhifadhi wa mazingira.

Katika *Majira ya Utasa*, Arege ameangazia hali ambapo juhudi za wawakilishi wa vijiji za kukutana na kiongozi wao Jumbe ili kujadili kuhusu matatizo yanayowakumba watu hazijafaulu kwa muda mrefu. Jambo hili limesababisha wanajamii wote kuafikia wazo la kufanya mapinduzi ili kumtimua Jumbe katika ardhi ya umma aliyonyakua. Dondoo lifuatalo linashadidia:

| | |
|---|---|
| Deka: | Nimeponea chupuchupu mzee. *Wametufukuza kazini*. |
| Jumbe: | Nani hao? |
| Deka: | Watu. Watu wengi kabisa. |
| Jumbe: | Askari wamekwenda wapi? |
| Deka: | *Watu walikuwa wengi ajabu. Walinzi walipowaona walikimbia na wafanyakazi wetu wakajiunga na wavamizi wakawa wanaimba nyimbo za ukombozi.* |
| Jumbe: | Ukombozi? |
| Deka: | Ndiyo. *Wanasema ni ukombozi wa ardhi*. Leo wameangusha vibanda vyote vya maua. |
| Jumbe: | *My God! What?* |
| Deka: | Watu ni wakali kama nyuki mzee. Wameonyesha ghadhabu kubwa. |
| Jumbe: | Najua hao vijana wanatumiwa kuniangusha. |
| Deka: | *Umma uliopo ni mchanganyiko. Hata watoto na wazee wapo*. (Uk 80) |

Katika dondoo hili, mwandishi analeta taswira ya uhalisia wa mapinduzi yanayotekelezwa na umma. Kutokana na ghadhabu za wanajamii, wanavamia sehemu za viwanda vya maua vya Jumbe na kuwafukuza wafanyakazi wake. Kilicho dhahiri ni

kwamba, wanajamii wote wameshiriki katika harakati za ukombozi. Jambo hili linathibitishwa na Deka anaposema kwamba walinzi na wafanyakazi wa Jumbe pia walikimbia na kujiunga na umma. Aidha, wazee na watoto pia wameshiriki katika mapinduzi haya. Kwa mujibu wa Njiru (2015), uhakiki wa kimazingira unasisitiza kuhusu mbinu za kidemokrasia na kiujumuishi. Kwa msingi huu, uhifadhi wa mazingira unadai ushiriki wa vijiji, wanaoishi katika makazi duni, wataalamu, waundaji sera, mashirika ya kidini, taasisi za elimu, jumuiya za wafanyabiashara, wanafunzi na vyombo vya usalama. Mtazamo huu unabainika katika mfano uliotolewa wakati kila mwanajamii anashiriki katika kufanya mapinduzi. Kama anavyosema Deka, lengo kuu la mapinduzi ni kuikomboa ardhi yao iliyonyakuliwa na Jumbe. Kwa hivyo, ujumbe unaojitokeza ni kwamba, harakati za ukombozi zinapoanza, hakuna yeyote anayeweza kuzikomesha, jambo ambalo linadokeza kuhusu nguvu za kuwepo na umoja miongoni mwa wanajamii.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mapinduzi yanajitokeza kupitia mgomo wa wafanyakazi wote wa Baraza la Mji. Kabla ya maamuzi ya kufanya mgomo, wawakilishi wa wafanyakazi wamefanya juhudi za kukutana na Meya ili kujadili kuhusu matatizo yanayowakumba. Hata hivyo, mikutano hiyo imeambulia patupu huku Meya akiendelea kuyapuuza masilahi yao. Hivyo, lililosalia ni wafanyikazi kutumia nguvu ili kudai haki yao. Mfano ufuatao unathibitisha:

| | |
|---|---|
| Meya: | Zimefika Habari… Habari gani? |
| Gedi: | *Wafanyakazi wa uwanja wa ndege.* |
| Diwani I: | Wameandamana nao? |
| Gedi: | La! *Wamegoma pia.* |
| Diwani II: | Wamegoma? |
| Gedi: | *Habari zinasema wamegoma. Kuwaunga wenzao waliogoma mkono.* |
| Meya: | Nd`o iweje? |
| Diwani II: | Alaa! |
| Gedi: | Habari zinasema wageni hawawezi kufika hapa maana ndege haziwezi kutua uwanjani. *Waelekezi hawapo kazini.* |
| Diwani I: | Lazima wawepo nd`o ndege zitue? Uwanja haukufungwa! |
| Diwani II: | Uwanja haukufungwa ndiyo lakini ndege haziwezi kutua zenyewe tu. Lazima rubani kuelekezwa. (Uk 76) |

Dondoo hili linadokeza kuwa wafanyakazi wote wa Baraza la Mji wamegoma, huku wakimtaka Meya wa Baraza la Mji wa Cheneo kuyashughulikia masilahi yao. Miongoni mwa mambo wanayolalamikia ni mishahara duni na mbinu mbovu za utawala, ambazo zimechangia katika uhaba wa maji na chakula pamoja na kutapakaa kwa uchafu katika Cheneo nzima. Ili kuonyesha umoja katika mapinduzi haya, wafanyakazi wa uwanja wa ndege pia wamegoma ili kuwaunga mkono wenzao waliogoma. Kutokana na hali hii, ni wazi kwamba wageni ambao Meya aliwatarajia kuwasili hawawezi kufika kwa sababu ndege haziwezi kutua bila waelekezi.

Ni kutokana na umoja huu ambapo wafanyikazi wote wanafaulu katika azma yao ya kutaka ukombozi, kwani hatimaye Meya analazimishwa kwenda hadi makao makuu ili kueleza kuhusu hali ya mambo katika Cheneo. Kwa mujibu wa Njiru (2015), uhakiki wa kiekolojia wa sasa unapaswa kukubali maono ya kujumuisha kila mtu katika uhifadhi wa mazingira. Kwa maoni yake, juhudi za kuhifadhi mazingira zitafaulu iwapo kila mtu kote ulimwenguni atawajibika katika kutetea mazingira yaliyoharibiwa. Hivyo, ujumuishaji na uwajibikaji wa kila mtu katika uhifadhi wa mazingira ndio mwandishi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* anayosawiri kupitia umoja wa wananchi katika kufanya mapinduzi ndidi ya uongozi dhalimu. Haja ya mapinduzi dhidi ya utawala dhalimu kama njia ya kukomboa mazingira yaliyoharibiwa pia ni jambo ambalo limeangaziwa na Mohamed katika tamthilia ya *Janga la Werevu*. Haya yanajitokeza katika dondoo lifuatalo:

Busara: Ole wao wote wanaouza maji safi na machafu, maskini au matajiri.
Sauti nyingi: Ole wao, ole wao, ole wao…
Mlinzi: Bwana na bibi, *wamevunja mlango na sasa wamo wanachota maji ya kisima chenu na kunywa.* Wanasema wana kiu ya miaka mingi. *Wanasema watakunywa na kuchukua maji hata kama watakabili kifo.*
Bimkuu: Hamkuwazuia?
Mlinzi: *Hawazuiliki. Umma kama huu unazuilikaje? Maelfu kwa maelfu ya watu wanaodai maji ni yao watasukumwaje?* Kisha wote wanaonekana wenye kiu kubwa sana. Kiu ya uhai na mauti. Wamepagawa hasa! Wanaimba ovyo: `maji, maji, maji`. Hili ni janga Bimkuu. (Uk 75)

Kwa mujibu wa dondoo hili, umma umekusanyika, maelfu kwa maelfu ya watu wanaodai haki ya kuchota maji katika kisima cha Bamkuu na Bimkuu. Kutokana na maneno ya Mlinzi, ni dhahiri kwamba watu wako tayari kunywa na kuchukua maji hata kama watakabili kifo. Aidha, ni wazi kwamba hawazuiliki kutokana na wingi na umoja wao, jambo ambalo limewawezesha kufaulu katika mapinduzi haya na kuzima kiu chao cha miaka mingi. Kadhalika, katika *Kimya, Kimya, Kimya*, Mohamed amesawiri hali ambapo wananchi wamechoshwa na matatizo mengi ambayo yamewakabili kwa miaka mingi. Haya yanatokana na vitendo vya Bw. Binafsi kama vile ukataji miti ovyo, ujenzi wa nyumba bila kibali, unyakuzi wa ardhi ya umma pamoja na uchafuzi wa mazingira. Kutokana na uhalisia wa tishio la mapinduzi ya wananchi, mkewe Bi. Shoo anamshauri ajiuzulu ili waepukane na balaa inayowakabili. Katika mfano ufuatao, Bi. Shoo anamwambia Bw. Binafsi:

| | |
|---|---|
| Bi. Shoo: | Nimeshakwambia |
| Bw. Binafsi: | Umeniambia nini? |
| Bi. Shoo: | *Kwamba ujiuzulu. Tutoke hapa tusije kukosa kaa na gando.* |
| Bw. Binafsi: | Muungwana hakimbii vita. |
| Bi. Shoo: | Hapana vita hapa, pana kushindwa tu. |
| BW. Binafsi: | Jeshi liko pamoja nasi. |
| Bi. Shoo: | *Jeshi kubwa zaidi ni la wananchi wenyewe.* |
| Bw. Binafsi: | Jeshi lisilo na silaha? |
| Bi: Shoo: | *Silaha zao ni umoja wao. Inasemekana kwamba wanajeshi wengine wamerukia upande wa wananchi*. |
| Bw. Binafsi: | Kakwambia nani? |
| Bi. Shoo: | Huoni kwamba sasa umeshapoteza dira? Husikii wala huoni. Kila unaloambiwa hulizingatii. |
| Bw. Binafsi: | Wewe sasa uko pamoja nami. |
| Bi. Shoo: | Unataka niwe pamoja na wewe vipi? *Huoni kwamba ninakuzindua kwamba hatari iko karibu nasi? Huoni kwamba mwisho wetu umefika*? (Uk 86-87) |

Katika dondoo hili, inaelekea kuwa Bi. Shoo ametambua ya kwamba mapinduzi ya wananchi hayana budi kutekelezwa. Hii inatokana na jinsi Bw. Binafsi anavyowadhulumu wananchi hao pamoja na kupuuza kila anachoambiwa. Kama anavyoeleza Garrard (2007), baadhi ya shughuli za wanajamii huharibu mazingira kwa namna ambayo husababisha wasiwasi mwingi wa umma. Athari hizi ni kama vile ukame, njaa na mafuriko miongoni mwa majanga mengine. Ni kutokana na wasiwasi walionao wanajamii ambapo wanaamua kumwondoa Bw. Binafsi katika uongozi. Aidha, Bi. Shoo anamweleza mumewe kuwa umoja wa wananchi ndizo silaha zao.

Vilevile, ni dhahiri kwamba wanajamii wote wameungana pamoja katika mapinduzi haya, jambo ambalo linaelezwa na Bi. Shoo anaposema kuwa hata baadhi ya wanajeshi wamejiunga na wananchi. Kadhalika, Bi. Shoo anakiri kwamba hata yeye anaunga wananchi mkono, kwa hivyo anamshauri mumewe ajiuzulu kwa kuwa mwisho wao umefika.

Hatua ya kufanya mapinduzi kama njia ya kuwaondoa viongozi dhalimu mamlakani inaweza kulinganishwa na mapinduzi yaliyofanyika Misri mwaka wa 2011, wakati wa uongozi wa aliyekuwa rais Hosni Mubarak. Katika mapinduzi hayo, mamilioni ya waandamanaji walijitokeza ili kutetea maslahi yao. Kama ilivyosawiriwa na waandishi wa tamthilia teule, malalamishi ya wananchi wa Misri yalilenga masuala ya kisheria na kisiasa. Miongoni mwa mambo waliyolalamikia ni ukatili wa polisi, uhuru wa kuzungumza, ufisadi, ukosefu wa ajira, kupanda kwa bei ya chakula na mishahara duni ya wafanyakazi. Kutokana na shinikizo la mapinduzi haya, hatimaye rais Mubarak alijiuzulu kama walivyofanya baadhi ya viongozi walioangaziwa katika tamthilia teule (Britannica, 2022).

## 6.8 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameangazia mchango wa motifu mbalimbali katika uhifadhi wa mazingira, kwa mujibu wa tamthilia teule za Said A. Mohamed na Timothy Arege. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, imebainika kwamba tamthilia ya Kiswahili ni mojawapo ya tanzu za fasihi ya Kiswahili ambayo inaweza kutumika kuonyesha namna ya kuhifadhi mazingira.

# SURA YA SABA
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 Muhtasari

Utafiti huu ulihakiki motifu za kimazingira katika tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege, kwa mtazamo wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia. Tamthilia zilizoteuliwa katika utafiti huu ni *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*), Janga la Werevu* (Mohamed, 2011), *Kimya Kimya Kimya* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). Motifu mbalimbali za kimazingira zilibainishwa kwa kuangazia jinsi ambavyo zimesawiriwa na waandishi wa tamthilia hizo teule, pamoja na kujadili namna mtindo ulivyotumika katika kusawiri motifu hizo. Katika ubainishaji huu, mtafiti alihakiki tamthilia teule ambazo zimeangazia masuala mbalimbali ya kimazingira.

Nadharia ya Uhakiki wa Kiekolojia iliyoasisiwa na Glotferty (1996) iliongoza utafiti huu. Uhakiki wa kiekolojia ni mkabala wa uhakiki wa kazi za fasihi ambao huchunguza uhusiano baina ya fasihi na mazingira. Aidha, mkabala wa kiekolojia katika uchambuzi wa kazi za kifasihi huchukulia mazingira kama suala la msingi katika kazi hizo. Kadhalika, nadharia hii inahusu uchanganuzi wa diskosi mbalimbali kuhusu mandhari, viumbe hai, maliasili na uzuiaji wa uchafuzi wa mazingira.

Mbali na kuangazia usawiri wa motifu za kimazingira, utafiti huu pia ulitambua mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira. Kama tanzu nyinginezo za fasihi ya Kiswahili, tamthilia ya Kiswahili pia imeanza kujitokeza kama utanzu unaoweza kutetea mazingira, hasa kutokana na namna ya uwasilishaji wake wa mazungumzo ya moja kwa moja unaotoa taswira halisi ya chanzo na athari za mabadiliko ya tabianchi na mwito wa uhifadhi wa mazingira. Kwa hivyo, tamthilia ya Kiswahili inaweza kutumiwa kuhamasisha, kukosoa, kutetea na kuelimisha jamii pana kuhusu uharibifu wa mazingira kwa lengo la kukomboa mazingira hayo.

## 7.2 Hitimisho

Sehemu hii inahusu hitimisho la matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Madhumuni ya kwanza katika utafiti huu yalikuwa kuhakiki jinsi motifu za kimazingira zilivyosawiriwa katika tamthila teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege. Madhumuni ya pili yalikuwa kujadili jinsi mtindo ulivyotumika katika kusawiri motifu za kimazingira kwa mujibu wa tamthila teule. Madhumuni ya tatu nayo yalikuwa kutathmini mchango wa motifu za kimazingira katika uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa tamthilia teule.

Uchunguzi wa tamthilia teule ulibainisha motifu mbalimbali za kimazingira ambazo zimesawiriwa na waandishi wa tamthilia hizo. Motifu zilizobainishwa ni pamoja na motifu ya maji, motifu ya ukame, motifu ya njaa, motifu ya magonjwa na motifu ya kifo. Katika kuangazia motifu ya maji, imebainika kwamba maji ni uhai hivi kwamba bila maji ni muhali uhai kupatikana. Kwa hivyo, maji ni muhimu kwa matumizi ya binadamu, mimea, wanyama pamoja na viumbehai kwa jumla. Kadhalika, imebainika kwamba kuna baadhi ya vifaa vitumiwavyo na binadamu ambavyo huhitaji maji. Vifaa

hivyo ni kama vile magari, ndege na roketi miongoni mwa vifaa vinginevyo. Hivyo, ni dhahiri kwamba waandishi wa tamthilia teule wanasisitiza kuhusu umuhimu wa maji katika takriban shughuli zote za binadamu.

Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa maji ni maliasili ya nchi. Kwa msingi huu, kila mwananchi anastahili kufaidika kutokana na maji hayo. Hata hivyo, imebainika kwamba vitendo mbalimbali vya viongozi vimechangia katika kusababisha uhaba wa maji. Vitendo hivyo ni kama vile ukataji wa miti na ufwekaji wa misitu unaochangia katika kuharibu vyanzo vya maji, pamoja na ubadilishaji wa mikondo ya maji. Kutokana na umuhimu wa maji, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba uhaba wa maji una athari nyingi katika jamii. Athari mojawapo ni milipuko ya magonjwa kama vile kipindupindu, ugonjwa unaotokana na uchafu. Aidha, ilibainika kwamba tatizo la uhaba wa maji limeathiri elimu ambapo wanafunzi huchukua muda mrefu kwenda mitoni kutafuta maji, au hata kusababisha baadhi ya shule kufungwa.

Mbali na athari za uhaba wa maji kwa elimu, ilibainika pia kuwa baadhi ya wanajamii hasa viongozi huchukulia uhaba wa maji kama nafasi yao ya kujinufaisha kutokana na biashara ya kuuza maji, jambo lililo dhahiri katika tamthilia teule. Kando na athari za kiuchumi zinazotokana na uhaba wa maji, ilibainika kwamba suala hili linaweza kuzua vita miongoni mwa wanajamii huku waking`ang`ania maji machache yanayopatikana. Motifu ya magonjwa kama suala la kimazingira iliangaziwa na waandishi wa tamthilia teule ambapo chanzo cha magonjwa kilibainishwa. Mambo yaliyojitokeza kama namna ya kusababisha magonjwa ya aina mbalimbali ni pamoja na kemikali kutoka kwenye viwanda, ambazo zinaweza kusababisha kikohozi pamoja na ugonjwa wa ngozi, na vilevile uchafu ambao husababisha ugonjwa wa kipindupindu. Aidha, mwandishi wa *Janga la Werevu* aliangazia aina nyingine ya ugonjwa uliojulikana kama ugonjwa wa wasiwasi na hofu, ambao uliwakumba hasa vijana kutokana na hofu ya athari za uharibifu wa mazingira.

Isitoshe, motifu ya ukame iliangaziwa na watunzi wa tamthilia teule kwa kuangazia chanzo na athari zake. Katika kuangazia chanzo cha ukame, ilibainika kuwa ukame unaweza kusababishwa na mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la joto duniani, hali ya kuasi baadhi ya mambo ya jadi na ukataji wa miti. Vilevile, ilidhihirika kwamba, ukame

ulisababishwa na tamaa ya viongozi iliyowafanya wajihusishe katika unyakuzi wa ardhi pamoja na kuharibu vyanzo vya maji. Aidha, ilibainika kwamba hali ya ukame huwa na athari nyingi kama vile kukauka kwa mimea, uhaba wa chakula, umaskini, kudidimia kwa maliasili na kuathirika kwa masomo.

Motifu nyingine iliyoangaziwa na watunzi wa tamthilia teule ni motifu ya njaa. Hivyo, ilibainika kwamba chanzo kikuu cha njaa ni kiangazi na umaskini unaotokana na mbinu mbovu za utawala katika jamii yoyote ile. Licha ya makali ya njaa kuwa tatizo sugu katika jamii, matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa si kila mtu ameathiriwa na njaa, bali ni wananchi wa kawaida tu, ambao wanaishi katika hali ya umaskini. Hali ambayo inawafanya wanajamii walioathirika kuishi kwa kutegemea tu misaada. Hata hivyo, ilibainika kwamba  waandishi wa tamthilia teule wanawalaumu wanajamii kwa kunyamaza kimya na kukubali viongozi wao kuwatumbukiza katika matatizo yanayowakabili.

Utafiti huu vilevile ulibainisha motifu ya kifo kama athari mojawapo inayotokana na uharibifu wa mazingira. Hivyo, matokeo ya utafiti yalibaini kuwa kifo kinaweza kusababishwa na mambo kadhaa kama vile ukosefu wa chakula au hata kula chakula kibovu, kiangazi na kemikali kutoka kwenye viwanda. Kemikali hizi zinaweza kusababisha vifo vya watu na wanyama au hata viumbe waishio majini. Hivyo, matokeo ya utafiti yalibaini kuwa baadhi ya vifo hivi hasa vinavyotokana na kemikali vinaweza kuzuiwa iwapo hatua mwafaka zitachukuliwa kama vile kuchukua tahadhari wakati wa matumizi ya kemikali pamoja na kuwepo na sheria zinazodhibiti matumizi ya kemikali hizo.

Kimtindo, mbinu mbalimbali za kimtindo zilizotumiwa na waandishi wa tamthilia teule katika kuwasilisha motifu za kimazingira zilibainishwa na kujadiliwa. Mojawapo ya mbinu za kimtindo zilizobainika ni matumizi ya jazanda. Matokeo ya utafiti yalibaini kwamba, kichwa cha tamthilia ya *Majira ya Utasa* na ile ya *Janga la Werevu* ni jazanda zilizotumiwa na waandishi wa tamthilia hizo kusawiri chanzo na athari za uharibifu wa mazingira. Jazanda nyinginezo zilizojitokeza ni jazanda ya mhusika Mpya, jazanda ya unajisi, jazanda ya jipu, jazanda ya ugonjwa wa mhusika Kristy na jazanda ya ndoto ya mhusika Kato. Mbali na jazanda, mbinu zingine za kimtindo zilizobainika katika utafiti

huu ni kinaya, taswira, majazi, nyimbo, kejeli, ushairi, chuku, tashbihi, sitiari na mbinu rejeshi.

Kadhalika, utafiti huu umethibitisha kuwa tamthilia ya Kiswahili ni mojawapo ya tanzu za fasihi ya Kiswahili ambayo inaweza kutumika katika kuangazia masuala ya mazingira. Haya yamedhihirika kwa mujibu wa tamthilia teule za Said Ahmed Mohamed na Timothy Arege, ambapo waandishi hawa wameangazia motifu mbalimbali za kimazingira ambazo zinaweza kutumika katika uhifadhi wa mazingira. Motifu ya kimazingira mojawapo iliyolenga kuhifadhi mazingira kama ilivyosawiriwa na watunzi wa tamthilia teule ni motifu ya safari. Wahusika mbalimbali walisafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine wakiwa na lengo la kutafuta suluhisho na matatizo yaliyowakumba wanajamii kama vile njaa, ukame, magonjwa na vifo.

Motifu ya ujadi ilibainika pia ambapo baadhi ya wahusika katika tamthilia teule walipendekeza haja ya kurejelea baadhi ya mambo ya jadi, ambayo yalinuiwa kuhifadhi mazingira. Hii ilitokana na msingi kuwa, si kila jambo la jadi mbaya, kwa sababu kuna baadhi ya mambo ya jadi yaliyo na manufaa katika jamii ya sasa, kama vile miiko na matambiko ambayo yalikusudiwa kuhifadhi sehemu za misitu kwa kuzichukulia kuwa mahali patakatifu.

Isitoshe, motifu ya elimu ilijitokeza kuwa suala la kimsingi katika uhifadhi wa mazingira. Kama ilivyobainika katika tamthilia teule, elimu inaweza kuwasilishwa kwa umma kupitia kujumuishwa kwa somo la mazingira katika mitaala ya elimu, elimu ya jumla kwa umma ambapo wanajamii huhamasishwa kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira, na vilevile elimu kupitia vyombo vya habari kama vile magazeti na majarida au runinga na redio. Hivyo vyombo hivi vilibainika kuwa na dhima muhimu katika kuelimisha, kushawishi kuzindua na kuhamasisha jamii pana kuhusu matatizo ya kimazingira.

Kando na kuwepo na elimu kwa umma, ambapo wanajamii wote wanastahili kuhamasishwa kuhusu namna ya kuhifadhi mazingira, ilibainika pia kwamba pana haja ya wananchi wote kuungana pamoja katika kukomboa mazingira yaliyoharibiwa kupitia njia mbalimbali. Kutokana na umoja wao, wananchi walishiriki na kufaulu

katika kufanya maandamano, uundaji wa sheria za nchi, mijadala kuhusu masuala ya mazingira na vilevile katika ufufuzi wa misitu. Hivyo, waandishi wa tamthilia teule walisisitiza kuwa umoja wa wananchi ndizo nguvu na silaha zao katika ukombozi wa mazingira.

Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa, baadhi ya wahusika hasa wanawake wamesawiriwa kama wahusika wazalendo ambao walisimama kidete kutetea haki za wanajamii. Kutokana na mchango wa wahusika hawa wazalendo, ilidhihirika kwamba, uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mtu, bila kujali jinsia, umri, kabila, elimu cheo au hata tabaka. Hivyo, ni dhahiri kwamba ushiriki wa kila mmoja katika jamii unaweza kuchangia katika ukombozi wa mazingira yaliyoharibiwa.

Hatimaye, matokeo ya utafiti huu yalithibitisha kwamba, ikiwa viongozi walio mamlakani hawawezi kujiunga na wanajamii katika harakati za kukomboa mazingira, basi wanajamii hawana budi  kufanya mapinduzi ili kuwaondoa mamlakani. Hivyo, ilibainika kwamba, wanajamii wana uwezo wa kuwaondoa viongozi wanaochangia katika kuharibu mazingira yao kwa manufaa ya kibinafsi, ikiwa wao ndio vikwazo vya kuyakomboa.

Kwa kuhitimisha, matokeo ya utafiti huu yalithibitisha kwamba, uhifadhi wa mazingira ni suala ambalo linahusu kila mwanajamii bila kujali umri, jinsia, cheo, viwango vya elimu au tabaka la mtu. Hata ingawa, kurejesha mazingira yaliyoharibiwa katika hali yake ya awali kunahitaji muda na fedha nyingi, ni wazi kwamba hili ni jambo ambalo haliwezi kuepukwa wala kupuuzwa ili kuokoa maisha ya vizazi vya baadaye, ambavyo viko katika hatari ya maangamizi yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba fasihi inaweza kuchukuliwa kama nyenzo iliyo na uwezo wa kuleta ufahamu na kuongeza busara kuhusu ekolojia. Hata ingawa ni kwa njia isiyo ya moja kwa moja, ufahamu huu unaweza kusaidia na kuchangia katika uhifadhi wa mazingira.

### 7.3 Mapendekezo ya Utafiti Kwa Jumla

Kutokana na matokeo ya utafiti huu kwamba viongozi wa kisiasa ndio wahusika wakuu katika ufyekaji wa misitu na ubadilishaji wa mikondo ya maji, inapendekezwa kuwa serikali za nchi mbalimbali kupitia vyombo ya kitaifa kama vile NEMA nchini Kenya,

zihakikishe ya kwamba sheria zinazolinda misitu zimezingatiwa na kila mtu bila kujali nafasi yake katika serikali. Aidha, inapendekezwa kuwa hatua mwafaka ichukuliwe kwa wote wanaohusika katika uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na kubadili mikondo ya maji kwa manufaa ya kibinafsi. Jambo hili litawezesha ufufuaji wa misitu pamoja na kupunguza uhaba wa maji.

Kwa kuwa shughuli ya uhifadhi wa mazingira inahitaji muda na pesa nyingi kama ilivyobainishwa na matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa serikali za kitaifa zitenge fedha za kutosha ambazo zitagharamia shughuli za uhifadhi wa mazingira, hasa kupitia upanzi wa miti. Aidha, inapendekezwa kuwa serikali ihakikishe kwamba pesa hizo zinatumika kama zilivyokusudiwa bila kuingiza masuala ya kisiasa katika harakati za uhifadhi wa mazingira.

Kadhalika, utafiti huu unapendekeza kujumuishwa kwa somo la mazingira katika mitaala ya elimu katika viwango vyote vya elimu. Hii inatokana na matokeo ya utafiti huu kwamba baadhi ya mitaala ya elimu ilijikita katika kuangazia na kutukuza utamaduni wa kigeni, badala ya kuangazia masuala yanayohusu jamii na ulimwengu halisi. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wote kutoka shule za msingi hadi katika vyuo watakuwa na uelewa wa namna ya kuhifadhi mazingira ili kuepuka athari zinazotokana na uharibifu wake.

Vilevile, inapendekezwa kuwa serikali ihakikishe kwamba umma umehamasishwa kuhusu uhifadhi wa mazingira hasa kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Hii inatokana na matokeo ya utafiti huu kwamba kuna baadhi ya wanajamii ambao bado hawana uelewa wowote kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake. Uhamasishaji huu utawezesha kila mwanajamii kuelewa na kuchangia katika juhudi za kukomesha uharibifu wa mazingira na vilevile kuhusika katika uhifadhi wa mazingira.

### 7.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Kumezuka haja ya utafiti zaidi kufanywa kutokana na matokeo ya utafiti huu. Kwanza, utafiti wa baadaye unaweza kufanywa kwa kuchunguza kwa kina mchango wa vijana katika uhifadhi wa mazingira. Hii ni kutokana na matokeo ya utafiti huu yaliyobaini kuwa vijana walikuwa na mchango na nafasi bora ambayo iliwezesha juhudi za

uhifadhi wa mazingira kufaulu. Pili, kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika motifu za kimazingira katika tamthilia ya Kiswahili kwa mkabala wa uhakiki wa kiekolojia, utafiti wa baadaye unaweza kufanywa katika tamthilia ya Kiswahili kwa mkabala wa nadharia ya uhalisia ili kuchunguza jinsi watunzi walivyosawiri motifu za kimazingira.

Kadhalika, inapendekezwa kuwa utafiti wa baadaye ufanywe katika tanzu nyinginezo za fasihi ya Kiswahili kama vile Ushairi wa Kiswahili kwa mtazamo wa Uhakiki wa Kiekolojia ili kuhakiki namna watunzi wa Ushairi wa Kiswahili wa kisasa wameangazia suala la mazingira.

## MAREJELEO


Abdallah, E.S (2013). *Athari za Viwanda katika Mazingira*. Available at https:/www.rfi.fr/sw/afya-mazingira/20130729-athari-za-viwanda-katika-mazingira: Accessed on 17/01/2022.

Abdallah, E.S (2014). *Uharibifu wa vyanzo vya maji na athari zake*. Available at https://www.rfi.fr/sw/afya-mazingira/20140317-uharibifu-wa-vyanzo-vya-maji-na-athari-zake: Accessed on 18/01/2022.

Adugna, A. (2014). Exploring Environmental Discourses in Oral Literature: Ecocritical Analysis of Oromo Proverbs. *Journal of Languages & Culture*. Vol 5 (2), pp 24-35.

Alia, A. (2017). Ecocritical Post-Colonial Studies on Humans, Land and Animals. Unpublished MA Thesis: University of Nothern Iowa.

Arege, T.M. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

Arege, T.M. (2015). *Majira ya Utasa*. Nairobi: Spotlight Publishers (E.A) Limited.

Assumpta, K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili.* Nairobi: Oxford University Press.

Barry, P. (2013). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester: Manchester University Press.

BBC New Swahili (10/10/2018). *Mabadiliko ya Tabianchi: Njia tano za kupunguza ongezeko la joto duniani-BBC News Swahili*. Availabe at https://www.bbc .com/swahili/habari-45794348.amp: Accessed on 02/02/2022.

BBC News Swahili (17/07/2021). *Mafuriko Ulaya: Wanasayansi Waelezea ni kwa Nini Hawawezi Kutabiri Mafuriko kama yale Yanayozikumba Ujerumani na Ubelgiji.* Available at https://www.bbc.com/swahili/habari-7872899. Accessed on 19/12/2021.

Bennett, M. (2001). From Wide Open Spaces to Metropolitan Places. The Urban Challenge to Ecocriticism: *Interdisciplinary Studies in Literature and Environment*. Vol 8(1), PP 31-52. doi:10.1093/isle/8.1.31

Bookchin, M. (1980). *Toward an Ecological Society*. Montreal: Blackrose Books.

Britannica, T. Editors of Encyclopaedia (2022, January 19). *Egypt Uprising of 2011. Encyclopaedia Britannica*. Available at https://www.britannica.com/event/ Egypt-Uprising-of-2011:Accessed on 21/02/2022.

Buell, L. (1995). *The Environmental Imagination: Thoreau, Nature Writing and the Formation of American Culture.* Cambridge Mass: Harvard University Press.

Buell, L. (2005). *The Future of Environmental Criticism: Environmental Crisis and Literary Study.* Malden: Malden blackwell Publishers.

Bulaya, J. & Mhango, P (2020). Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. *Mulika* no. (38), PP 105-125.

Carter, A. (1999). *A Radical Political Theory*. London and New York: Routledge.

Catrine, G. & Sylvia, M. (2006). *Nature in Literary and Cultural Studies: Transatlantic Conversations on Ecocriticism*. New York: Rodopi B. V, Amsterdam.

Culler, J. (2011). *Literary Theory: A Very Short Introduction*. New York: Oxford University Press.

Curry, P. (2011). *Ecological Ethics: An Introduction 2nd Edition*. Cambridge, UK&Malden, MA: Polity Press.

DeMott, N. (2018). *A Brief History of Ecocriticism: Where Literature and the Environment Cross Path*. Available at https://medium.com@Nick_DeMott/a-brief-history-of-ecocriticism-a120614d30fc. Accessed on 13/12/2020.

Dickens, C., & Fielding, K. (1988). *The Speeches of Charles Dickens. A Complete Edition.* Hemel Hempsted, Hertfordshire: Harvester Wheatsheaf.

Easterlin, N. (2012). *A Biocultural Approach to Literary Theory and Interpretation.* Baltimore:The John Hopkins University Press.

Etyang, H. (2021). *Students Trek 10kms in Search of Water as Turkana Draught Crisis Persists.* Available at https://www.the –star.co.ke/counties/rift-valley/2021-11-

02-students-trek-10km-in-search-of-water-as-turkana-drought-crisis-persisits/: accessed on 26/11/2021.

FAO (2013). *Uhaba wa Maji: Sababu, Matokeo, Suluhisho na Mifano*. Available at https://sw.warbletoncouncil.org/escasez-de-agua-822: Accessed on 04/02/2022.

Fortress, A., & Onwuka, E. (2014). Yoruba Eco-proverbs in English: An Eco-Critical Study of Osundare's Midlife and Horses of Memory. *Journal of Literary Society of Nigeria*. Vol 6(2014), PP 29-40.

Gachuru, K. (2010). The Influence of Environmental Education on Conservation among Secondary School Students in Nakuru Town Municipality. Unpublished MA Thesis: University of Nairobi.

Gakii, K. I. (2019). Mwingiliano matini katika Utenzi wa *Fumo Liyongo* na Tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Garrard, G. (2004). *Ecocriticism.* Oxfordshire: Routledge.

Garrard, G. (2007). Ecocriticism and Education for Sustainability. *In Pedalogy: Critica Approaches to Teaching Literature, Language, Composition & Culture*. Volume 7(3): 359-386. Duke University Press.

Gichure, R.W. (2017). Effects of Drought on Crop Production and Coping Mechanisms Undertaken by Small Scale Farmers: A Case Study of Makueni County, Kenya. Unpublished Masters Thesis (MA). University of Nairobi.

Glotfelty, C., & Fromm, H. (1996). *The Ecocriticism Reader: Landmark in Literary Ecology*. Georgia: University of Georgia Press.

Glotferty, C. (1996). *Introduction. The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. In Cheryll Glotferty and Harold Fromm. Athens: The University of Georgia Press.

Haji, M.I. (2018). Uhalisia wa Utabaka Katika Tamthilia za *Janga la Werevu* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Heise, K.U. (2008). Ecocriticism and the Transnational turn in American Studies. *American Literary History* Vol 20(1-2), PP 381-404.

Hitt, C. (2004). Ecocriticism and the Long Eighteenth Century. *College Literature.* Vol 31(3), PP 123-146.

Howe, C. (2009). The Role of Education as a Tool for Environmental Conservation and Sustainable Development. Unpublished PhD Thesis: Imperial College, London.

Iheka, C.N. (2015). African Literature and the Environment: A Study in Postcolonial Ecocriticism. Unpublished PhD Thesis: Michigan State University.

Istvan, F. (2021). *Uswidi kuwa Mwenyeji wa Siku ya Mazingira Duniani katika Mwaka wa 2022.* Available at https://www.unep.org/habari-na-matukio/toleo-la-habari/uswidi-kuwa-mwenyeji-wa-siku-ya-mazingira-duniani-katika-mwaka-wa:Accessed on 19/02/2022.

Kane, J. (2016). *Motifs in the Peal*. Available at https://prezi.com/nl;v6un9asyy/motifs-in-the-pearl/. Accessed on 21/04/2021.

Khamis, B.S (2018). *Ufahamu Ugonjwa wa Kipindupindu (Cholera)*. Available at https://tanzmed.co.tz/magonjwa/yanayoambukiza/item/314-ufahamu-ugonjwa-wa-kipindupindu-cholera.html: Accessed on 28/11/2021.

Khamis, B.S. (2015). Uhakiki wa Usimulizi katika Tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

King'ora, M. (2014). Utendaji katika Tamthilia ya *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.* Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

King`ei, K. na Kisovi, C. (2010). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kisanji, J.A. (2013). Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili: Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

M`Ngaruthi, T. (2015). Usawiri wa Mwanasiasa wa Afrika Katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu (PhD) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Chuka.

Maathai, W. (2006). *Unbowed*. United States: Alfred A. Knopf.

Maathai, W. (2009). *The Challenge for Africa*. Britain: William Heineman.

Maganga, A. (2019). *Umuhimu wa Maji katika Maisha ya Mwanadamu*. Available at http://alexmaganga.blogspot.com/2019/02/umuhimu-wa-maji-katika-maisha-ya-.html?m=1. Accessed on 12/10/2019.

Magharibi, L. (2017). *Athari za Ukame*. Available at https://sw.eferrit.com/athari-za-ukame: Accessed on 08/12/2021.

Maleya, S.L. (2016). Representation of Ecological Consciousness in Henry Ole Kulet *Vanishing Herds & The Hunter*. Unpublished M.A Thesis: Kenyatta University.

Malnati, A.M. (2017). Parallels in Environmental Justice: An Analysis of Literature and the Environment in the Pacific Northwest and Southern Italy. Unpublished Bachelor of Arts Thesis: Roberts D. Clark Honors College.

Maosi , R. (2020). *Magugumaji na Kemikali Kero Ziwa Naivasha-Taifa Leo*. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/magugumaji-na-kemikali-kero-ziwa-naivasha/: Accessed on 18/12/2021.

Marshall, S. (2011). The Water Crises in Kenya: Causes, Effects and Solutions. *Global Majority E-Journal*. Vol. 2 (1), PP 31-45.

Masoud, S.K. (2015). Matumizi ya Motifu katika Ngano za Ki-Pemba. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Massey, G. (2009). Reading the Environment: Narrative Constructions of Ecological Subjectivities in Australian Children's Literature. Unpublished PhD Thesis: Queensland University of Tecknology.

Massoi, A. (2021). *Mabadiliko ya Tabianchi na madhara yake Nchini Kenya*. Available at https://news.un.org/sw/audio/2021/04/1116642: Accessed on 17/01/2022.

Matheka, B. (2018). *Hatari Nchi Kugeuzwa Jangwa Kufuatia Ukataji wa Miti Kiholela-Taifa Leo*. Available at https:/taifaleo.nation.co.ke/hatari-nchi-kugeuzwa-jangwa-kufuatia-ukataji-miti-kiholela/. Accessed on 15/11/2021.

Matheka, B. (2021). *Serikali haifai Kupuuza Ripoti ya Human Rights.* Watch-Taifa Leo. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/benson-matheka-serikali-haifai-kupuuza-ripoti-ya-human-rights-watch/: Accessed on 13/12/2021.

Ministry of Education (2019). *Upper Primary Level Curriculum Designs*. Nairobi: Kenya Institute of Curriculum Development.

Mogambi, H. (2018). *Msitu wa Mau: Sababu zinazofanya eneo hilo kuzozaniwa Kenya-BBC News Swahili*. Available at https://www.bbc.com/swahili/habari-45070483: accessed on 20/02/2022.

Mohamed, S.A. (2011). *Janga la Werevu*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S.A. (2011). *Kimya Kimya Kimya*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es salaam: KAUTTU.

Mulwa, F. et al (2021). Water Scarcity in Kenya: Current Status Challenges and Future Solutions: *Open Access Library Journal*. Vol 8 (1), PP 1-15.

Murikira, J. (2019). *Can Kenya`s new Education System Address Climate Change?* Available at https://www.oneearth.org/can-kenyas-new-education-system-address-climate-change/: Accessed on 15/09/2020.

Murungi, J. M. et al (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Longhorn Publishers: Nairobi.

Mutahi, M. E. (2021). Ukiushi wa Kanoni katika Hadithi Teule za Watoto za John Kobia na Wadi Wamitila. Tasnifu ya Uzamifu (PhD) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Laikipia.

Mutua, P. (2020). "*Conserve Environment to Avoid Pandemics*". Daily Nation, page 18: 02/09/2020.

Nabeta, S. & Ongutte, N. (2014). Literary Environmentalism: An Ecocritique of Kiswahili Literature: *Internationa Journal of Ecology and Ecosolution*,Vol. 1(2), pp. 29-41.

Nabeta, S. (2011). Kenyan Universities and Environmental Studies: Advancing the Idea of Ecological Criticism in Kenyan Literature Departments. Paper presented in Catholic University International Conference on Idea of an African University, May 24-27.

Nankhuni, F. (2004). Environmental Degradation, Resource Scarcity and Children`s Welfare in Malawi: School Attendance, School Progress and Children`s Health. Unpublished PhD Thesis: Pennsylvania State University.

Nasong`o, S. (2018). *Environmental Policy and Practice in Kenya: Between Cornucopians and Neo-Malthusians*. Available at https://www.researchgate. net/publication/322530122-Environmental-policy-and-practice-in Kenya-Between- Cornucopians-and-Neo-Malthusians : Accessed on 20/09/2020.

Ng`etich, D.k (2011). Dini kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini: Mfano Kutoka Fasihi katika Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njeru, M.K. (2018). Suala la Ardhi katika Riwaya Teule za Kiswahili: Tathmini ya Kovu Moyoni na Kufa Kuzikana. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Chuka.

Njiru, H.M. (2015). Eco-Techno-Cosmopolitanism: Education, Inner Change and Practice in the Contemporary U.S. Eco-Disaster Novel. Unpublished PhD Thesis: Miami University.

Njoki, S.E. (2018). Motifu za Yatima katika Hadithi Teule za Watoto. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyamsenda, J.C. (2015). Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Tasnifu ya Uzamifu (PhD) Isiyochapishwa: Chuo kikuu cha Tanzania.

Obara, V. (2018). *Kutunza Mazingira ni Bora Kuliko Ajenda zote*. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/?p=9093: Accessed on 25/11/2019.

Odongo, F.O. (2014). Uchanganuzi wa Uwasilishaji wa Kifo katika Mashairi Teule ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Maseno.

Oiko, F.G. (2017). Uhakiki wa Mtindo Katika Tamthilia za Arege. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Ojomo, P. A. (2011). Environmental Ethics: An African Understanding. *African Journal of Environmental Science and Technology*. Vol 5(8), PP 572-578.

Omoga, R.G. (2018). Mwananchi wa Kawaida kama Mdhulumu wa Maslahi yake katika Tamthilia za *Kilio cha Haki, Amezidi* na *Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Omollo, E. (2013). *Toleo Maarufu ya Sera ya Kitaifa ya Mazingira*. Nairobi: The International Development Institute-Africa (IDIA).

Ongutte, R.N. (2014). *Uhakiki wa Suala la Uhifadhi wa Mazingira katika Tanzu Teule za Fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya*. Available at https://repository. maseno.ac.ke/handle/123456789/934.Accessed on 13/04/2021.

Onyango, L. (2019). *Wakenya wote Washirikishwe katika Upanzi wa Miti- Taifa Leo*. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/onyango-wakenya-wote-washirikishwe-katika-upanzi-wa-miti/: Accessed on 20/02/2022.

Public Service International (2020). *Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi*. Available at https://pop-umbrela..s3.amazonaws.com/uploads/105d8e43-efaa-4d91-aba4-f287453c0671_2020_SWAHILI_PSI-ClimateCrisisHandbook-master-web-01-56.pdf: Accessed on 15/12/2021.

Qatium, (2020). *How will water scarcity affect us*? Available at https://qatium.com/blog/how-will-water-scarcity-affect-us/: Accessed on 20/11/2021.

Quick, P.S (2004). An Ecocritical Approach to the Southern Novels of Cormac Mccarthy. Unpublished PhD Thesis: University of Georgia.

Reid, K. (2021). *Africa Hunger, Famine: Facts, FAQs, and How to Help*. Available at https://www.worldvision.org/hunger-news-stories/africa-hunger-famine-facts: Accessed on 12/12/2021.

Republic of Kenya (2010). *Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya (2015). *Corruption and Ethics Survey Report, 2014*. Nairobi: Government Printer.

Riccardo, R. (2017). *Ukame-Wikipedia, Kamusi Elezo Huru*. Available at https://sw.wikipedia.org/wiki/ukame: Accessed on 18/12/2021.

Rice, D. (2020). *Recent Global Warming Has Wiped out 6500 years of Cooling.* Available athttps://www.USAtoday.com/story/news/nation/2020/07/01/global-warming-has-wiped-out-6-500-years-cooling-study-says/5356154002/. Accessed on 10/12/2020.

Rigby, K. (2002). Ecocriticism in Julian Wolfreys (ed) Introducing Criticism in the twenty-first century. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Rueckert, W. (1978). *Literature and Ecology: An Experiment in Ecocriticism*. Athens: University of Georgia Press.

Sabula, M. (2014). Nafasi ya Mwanamke katika Uhifadhi wa Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto*: Mtazamo wa Fasihi ya Ufeministi wa Kiekolojia. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sabula, M. na Sangili, N. (2019). Fasihi Mazingira: Mtazamo wa Kinisai katika Riwaya ya *Nakuruto*. *Koja la Taaluma za Insia*. Vol 6(2019), PP 338-354.

Sangili, N. (2015). Nafasi ya Fasihi ya Kiswahili katika Uwanja wa Fasihi Mazingira. *CHAKAMA* (2015): 73-84.

Sarver, S. (1994). Defining Ecocritical Theory and Practice. What is Ecocriticism? ASLE: *Association for the Study of Literature and the Environment*. Available at http:www.asle.umn.edu/conf/other/wla/1994.html. Accessed on 30/03/2022.

Schartz, J. (2012). The Importance of Apocalypse: The Value of End of the Word Politics While Advancing Ecocriticism. *Journal of Ecocriticism*. Vol 4(2), PP 20-33

Scholerberg, D. (2007). *Defining Environmental Justice: Theories, Movements and Nature.* Oxford: Oxford University Press.

Senkoro, F. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Sera ya Kitaifa ya Mazingira (2012). *Toleo Maarufu ya Sera ya Kitaifa ya Mazingira*. Nairobi: The International Development Institute-Africa (IDIA).

Sexton, M.S. (2012). "An Aligned, Transformed Constructed World". Presenting Material Environments in American Literature 1835-1945. Unpublished PhD Thesis: University of Oregon.

Shemboko, L. (2020). *Matambiko katika Jamii ya Wasambaa*. Available at https://www.academia.edu/12037128/Matambiko_Katika_Jamii_yA_Wasambaa. Accessed on 15/12/2021.

Shongwe, M.D. (2015). Kulinganisha Miiko na Tasfida ya Waswahili (Wajomvu) na Warabai. Tasnifu ya Uzamili (MA) Isiyochapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Simel, A. (2015). The Effect of Drought and Famine on Agricultural Production, Living Standards and Education, Status of the People of Kitui County, Kenya. Unpublished MA Thesis: University of Nairobi.

Tan, C. (2019). An Ecocritical Study of J.G Ballard`s Climate Fiction Novels. Unpublished PhD Thesis. Pamukkale University.

Temple, C. (2010). The Emergence of Sankofa Practice in the United States: A Modern History. *Journal of Black Studies*: Vol 4(1), PP 127-150.

Thompson, A. & Bebdik, J. (2012). *Ethical Adaptation to Climate Change: Human Virtues of the Future*. Cambridge, MA & London: MIT Press.

TUKI (2013). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi: Oxford University Press.

Turton, A., & Henwood, R. (eds) (2002). *Hydropolitics in the Developing World; A Southern Africa Perspective, Africa*. Walter issues Research Unit: Pretoria.

UN (2006). *Water: A shared Responsibility; The United Nations World Water Development Report 2, Executive Sammary-UNESCO Digital Library*. Available at https://unesdoc.unesco.org/org/ark:/48223/pf000014409. Accessed on 10/11/2021.

UN (2010). *Afrika iko hatarini kupoteza vyanzo vya maji*: UNEP / Habari za UN. Available at https://news.un.org/sw/story/2010/11/267712-afrika-iko-hatarini-kupoteza-vyanzo-vya-majiunep: Accsssed on 23/01/2022.

UN (2019). *Maji Yaendelea Kuchafuliwa, Uhai wa Jamii, Uchumi wa Nchi Mashakani-Benki ya Dunia*: available at https:/news.un.org/sw/story /2019/08/1065631: Accessed on 05/12/2021.

UN (2020). *Maji ni Sehemu ya Tatizo, Lakini pia Sehemu ya Suluhisho la Mabadiliko ya Tabianchi*. Available at https://news.un.org/sw/story/2020/03/1085252. Accessed on 05/11/2021.

UN (2020). *Umuhimu wa Vijana wa Kiafrika katika Majadiliano ya Kimataifa Kuhusu Mazingira*. Available at https:/www.unep.org/habari-na-matukio/andika blogu/umuhimu-wa-vijana-wa-kiafrika-katika-majadiliano-ya-kimataifa kuhusu-mazingira. Accessed on 12/06/2021.

UN (2020). *Watu Wanaokabiliwa na Njaa Duniani Wanaendelea Kuongezeka*. Available at https://news.un.org/sw/story/2020/07/1094941: Accessed on 31/11/2021.

UN (2021). *Je, Wajua Uhaba wa Maji ni Silaha Hatari Zaidi Kuliko hata Mabomu*? Available at https://news.un.org/sw/audio/2021/05/1119542: Accessed on 24/11/2021/

UN (2021). *Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, COP26-/Vatican News*. Available at https://www.vaticannews.va/sw/pope/news/2021-10/mkutano-umoja-mataifa-mabadiliko-tabianchi-cop26-wito-vatican.html: Accessed on 23/12/2021.

UN Tanzania (2011). Mwongozo wa kufundishia Uhusiano kati ya Umaskini na Mazingira: Mwongozo wa Uwezeshaji. *Jarida la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*. Toleo la 7(2011).

UNDP. (1992). *Earth Summit Agenda 21*: The United Nations Programme of Action from Rio, United Nation: New York.

UNEP (2020). *Misitu Inapoendelea Kupungua Duniani, Hatua za Dharura Zinahitajika ili Kutunza Bayoanuai yake*. Available at https://www. unep.org/habari-na-matukio/toleo-la-habari/ripoti-ya-umoja-wa-mataifa-misitu -inapoendelea-kupungua-duniani: Accessed on 18/12/2021.

UNESCO (2006). *The United Nations World Water Development Report 2, 2006*. Available at www.unesco.org/water/wwap/wwdr2/pdf/wwdr2/ch4,pdf: Accessed on 18/11/2021.

UNFCC (2009). "The Copenhagen Accord",United Nations Framework Convention on Climate Change: Conference of the parties 15th Session, Bonn, 18th Becember.http://unfccc.int/files/meetings/cop15/application/pdf/cop15cpcauv.pdf.

Verma, P. (2016). *Youth Participation in Environment Protection*. Available at https://www.worldpulse.com/community/users/priya-verma/posts/65057: Accessed on 19/01/2022.

Vierke, C. (2007). Of Plants and Women. A Working edition of two Swahili Plants Poems. *Swahili forum* 14(2007): 27-80.

Voice of America, Swahili (31st December, 2021). *Maafa ya Ukame na Njaa*. Availabe at https://www.voaswahili.com/maafa-ya-ukame-na-njaa: Accessed on 15/12/2021.

Wafula, R.M (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wangari, M. (2019). *Ukumbi wa Lugha na Fasihi: Mbinu za Sanaa katika Kiswahili*. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/ukumbi-wa-lugha-na-fasihi-mbinu-za-sanaa-katika-kiswahili/: Accessed on 25/01/2022.

Wangari, M. (2021). *Kongamano Kuu la Mazingira Lizindue Viongozi Usingizini.- Taifa Leo*. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/kongamano-la-mazingira-lizindue-viongozi/: Accessed on 19/02/2022.

Wanjohi, A. (2010). *Effects of Draught in Kenya. KENPRO Publications Online Papers Portal*. Available at https://www.kenpro.org/paper/effects-of-draught-in-kenya.htm: Accessed on 19/12/2021.

Waweru, S. (2019). *Siku ya Maji Duniani: Hakuna Anayeachwa Numa*. Available at https:/taifaleo.nation.co.ke/siku-ya-maji-duniani-hakuna-anayeachwa-nyuma/. Accessed on 21/10/2021.

Welle, D. (2022). *Ukame waleta Athari Jimboni Marsabit Nchini Kenya*. Available at https://amp.dw.com/sw/ukame-waleta-athari-jimboni-marsabit-nchini-kenya/a-60464600. Accessed on 04/02/2022.

Wendorf, M. (2021). *"Water Wars:" The Fight For Earth`s Most Precious Resource*. Available at https://interestingengieering.com/water-wars-fights-over-a-precious-resource: Accessed on 14/12/2021.

Wesonga, E. (2020). Nafasi ya Fasihi katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule za K. W. Wamitila. *East African Journal of Swahili Studies.* Vol 2 (2020), PP 2707-3467.

WHO (2021). *The State of Food Security and Nutrition in the World*. Rome, Italy: FAO.

Wirth, L. (1945). *The Problems of Minority Groups. The Science of Man in the World Crisis*. New York: Columbia University Press.

Wu, C. (2016). Towards an African-Focused Ecocriticism: The Case of Nigeria. Unpublished PhD Thesis: University of Nevada.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Kibali cha Utafiti

**CHUKA UNIVERSITY**

CHUKA UNIVERSITY

Knowledge is Wealth (*Sapientia divitia est*) Akili ni Mali

CHUKA UNIVERSITY INSTITUTION ETHICS COMMITTEE

Telephones: 020-2310512/18
Direct Line:0772894438

P. O. Box 109-60400, Chuka
Website: www.chuka.ac.ke

REF: **CUIERC/ NACOSTI 188**

TO: **Mary Kanyua Njeru**

Dear Sir/Madam

**RE: Motifu Za Kimazingira Katika Tamthilia Teule Za Said A. Mohamed Na Timothy Arege ; Uhakiki Wa Kiekolojia**

This is to inform you that *Chuka University IERC* has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is *NACOSTI/NBC/AC-0812*. The approval period is 28th September 2021to 28th September 2022

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used
ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by *Chuka University IERC*.
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to *Chuka University IERC*.

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://research-portal.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely,

Chair, IERC

## Kiambatisho II: Idhini ya Utafiti

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 392034

Date of Issue: 28/October/2021

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Ms.. MARY NJERU KANYUA of Chuka University, has been licensed to conduct research in Tharaka-Nithi on the topic: MOTIFU ZA KIMAZINGIRA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA SAID A. MOHAMED NA TIMOTHY AREGE: UHAKIKI WA KIEKOLOJIA for the period ending : 28/October/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/13662**

**392034**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.